

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Sita – Tarehe 8 Aprili, 2020**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:-**

**HATI ZA ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU SPIKA:** Hati za kuwasilishwa mezani Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

Toleo Na. 05 la tarehe 31 Januari, 2020;

Toleo Na. 06 la tarehe 07 Februari, 2020;

Toleo Na. 07 la tarehe 14 Februari, 2020;

Toleo Na. 08 la tarehe 21 Februari, 2020;

Toleo Na. 09 la tarehe 28 Februari, 2020;

Toleo Na. 10 la tarehe 06 Machi, 2020;

Toleo Na. 11 la tarehe 13 Machi, 2020;  
Toleo Na. 12 la tarehe 20 Machi, 2020;  
Toleo Na. 13 la tarehe 27 Machi, 2020.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MHE.VENANCE M. MWAMOTO - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA):**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Bungeni Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:-**

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 45

**Elimu Juu ya Athari za Dawa za Kulevywa**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-**

Je, Serikali inatoa elimu gani kwa vijana waliopo mashuleni/vyuoni ili kujikinga na tatizo sugu la utumiaji wa dawa za kulevya nchini.

**WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga na imekuwa ikitoa elimu kwa vijana waliopo Mashuleni na vyuoni ili kujikinga na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Ikumbukwe, mwaka 2017, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alianzisha rasmi Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo licha ya kupambana na biashara hiyo, Mamlaka hii imejikita katika suala zima la utoaji wa elimu juu ya tatizo hilo kwa Umma wakiwemo vijana waliomo mashuleni na vyuoni kama moja ya vipaumbele vyake muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa, mamlaka imeweza kutoa elimu mashuleni na kutengeneza mwongozo wa uendeshaji wa vilabu vya kupinga matumizi ya dawa za kulevya mashuleni na wakati mwingine kutumia Vilabu vya UKIMWI mashuleni kuzungumzia pia suala la tatizo la Dawa za Kulevya. Sambamba na hilo, Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wanafanya utaratibu wa kuingiza suala la dawa za kulevya katika mitaala ya kufundishia wanafunzi wa mashuleni na vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, elimu imekuwa ikitolewa na Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Taasisi za Serikali, Asasi za kiraia pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo kupitia vyombo vya habari kama vile Televisheni, Redio, Magazeti na mitandao ya kijamii pamoja na matamasha. Aidha, Mamlaka imekuwa ikitumia hafla maalum za kitaifa kama vile siku ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani, Mbio za Mwenge wa Uhuru, Sikukuu ya

Sabasaba, Sikukuu ya Nanenane pamoja na siku ya UKIMWI Duniani ili kutoa elimu kwa Umma.

Na. 46

### **Utaratibu wa Kuvuna Viungo vya Binadamu**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikihimiza wananchi kuchangia damu na kuihifadhi katika benki za damu kwa ajili ya watu wenye uhitaji.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha utaratibu maalum wa kuvuna viungo kama vile figo na moyo kutoka kwa watu waliopata ajali na wapo kwenye hali ya kupoteza maisha au kutoka kwa watu walioridhia kutolewa viungo hivyo na kuvihifadhi kwa ajili ya Watanzania wenye uhitaji wa viungo hivyo?.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Muswada wa Sheria ya Uvunaji, Utunzaji, Usafirishaji na Upandikizaji wa viungo vya binadamu ikiwemo, Figo, Moyo, Maini, Mapafu, sclera ya macho, Uroto, IVF, pamoja na *Stem cells* itakayoweka utaratibu mzuri wa namna ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria itaelekeza vitu vya kuzingatia kwa mpokeaji na mtoaji wa viungo. Sheria hii itaweka utaratibu kwa watu wanaoridhia kutolewa viungo vyao pindi wanapokaribia kupoteza maisha ikiwa mchangiaji

(donor) huyo atakuwa ameridhia viungo vyake vitumike kwa ajili ya jamii inayohitaji viungo hivyo pindi akipoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inaheshimu haki za binadamu ikiwemo haki ya kuishi, mtu kupata ajali na kutolewa viungo vyake litafanywa pale ambapo mhusika atakuwa ameridhia akipata ajali na akawa hana uwezo wa kupona atolewe viungo, basi hatua za kisheria na kitabibu zitatumika ili kutoa viungo hivyo na kuvihifadhi kwa ajili ya matumizi ya mtu atakayehitaji.

Na. 47

### **Kuwasaidia Wazee Wanaoishi Katika Mazingira Magumu**

**MHE. JOYCE B. SIKOMBI** aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi kubwa la wazee ambao wanaoishi mtaani katika mazingira magumu.

Je, Serikali imejipanga vipi kuweza kusaidia wasiendeleo kuteseka?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Joyce Biti Sokombi (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuweka mikakati madhubuti kuhakikisha kuwa wazee wote nchini wanafurahia maisha ya uzee hasa tukizingatia kuwa wazee ni hazina ya Taifa. Katika kuhakikisha kuwa haki, ustawi, ulinzi na usalama wa wazee unaimarishwa, Serikali kupitia mamlaka za Serikali za Mitaa imekuwa ikifanya utambuzi na uandikishaji endelevu wa wazee wasiokuwa na uwezo wa kujimudu kimaisha katika jamii na kuwapatia huduma za msingi za ustawi ikiwemo vitambulisho vya matibabu bila

malipo, malazi katika makazi ya wazee wasiojiweza, pamoja na msaada wa kisaikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2020 kuna wazee wasiojiweza 349 (wanawake 149 na wanaume 200) wanahudumiwa na Serikali kwenye Makazi 13 ya wazee nchini. Wazee wale ambao hawana watoto, ndugu wala jamii wa karibu wa kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hakuna tathmini rasmi kitaifa iliofanyika kuwatambua wazee wanaoishi mitaani kwani miongoni mwao hutokea katika familia na jamii zao kuja mitaani kuomba mchana na kurudi makwao jioni au kulala pembezoni mwa maduka na katika masoko. Aidha, nitumie fursa hii kutoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuwatambua wazee na kuwaunganisha na huduma za msingi, pia familia na jamii kutekeleza wajibu wao wa kutoa matunzo kwa wazee hususan wale wasiojiweza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kutengeneza makazi ya hawa wazee lakini nasikitika kusema makazi hayo yapo kwenye hali mbaya sana hali inayo sababisha hata maana ya kuwasaidia wazee hawa isiwepo kutokana na makazi hayo kuwa na hali mbaya sana yaani mazingira siyo rafiki ni mabovu na hili swala la wazee siyo la leo wala jana ni la siku nyingi kwa nini Serikali isione ni wakati muafaka kuwawekea makazi rafiki na yaliyo bora na salama kwa maisha binadamu?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka Matibabu bure kwa wazee lakini nichelee kusema wazee bado wanapata shida sana ya matibabu bure na bado wapo mitaani wanazurura na kuombaomba mfano mzuri ni hapa Dodoma wazee bado wana randaranda hovyoyo ukizingatia Dodoma ni makao Makuu ya Serikali na ndio kioo cha Nchi yetu ya Tanzania.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kulifanyia kazi kinaga ubaga jambo hili ili kuondokana na

adha hii ya kudhalilisha wazee tukikumbuka kwamba wote sisi ni wazee watarajiwa?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha Makazi ya wazee nchini kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa Wizara imeboresha majengo ya makazi 3 ya Nunge-Dar es Salaam, Njoro-Kilimanjaro na Maguu-Manyara pamoja na kuunganisha makazi 4 ya Chaz - Morogoro, Mkaseka - Lindi, Nandanga - Lindi na Nge'he - Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la Msingi, Serikali imeendelea kuweka Mikakati ya kuwahudumia Wazee Wasiojiweza nchini, hususan kuwapatia matibabu bila malipo. Kuhusu wazee wanaozurura ni kwamba wajibu wa kuwatunza wazee ni wa familia, ndugu jamaa na marafiki. Nitoe rai kwa jamii husika kuendelea kutimiza wajibu wao wa kuwatunza wazee. Aidha, Serikali itaendelea kutoa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza ambao hawana ndugu kupitia makazi 13 ya wazee.

Na. 48

### **Elimu ya Afya ya Uzazi Kwa Vijana**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Elimu ya Afya ya Uzazi ni muhimu sana kwa vijana wa kike na kiume katika kuepuka mimba zisizo za lazima.

Je, Serikali imejipangaje kuwahabarisha vijana ili kupunguza mimba zinazozuilika?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa mitaala ya kuwafundishia watumishi wa afya pamoja na vijana kuhusu afya ya uzazi kwa vijana ili kuwajengea uwezo wa kujitambua hasa kuhusu hatua za makuzi wakati wa kubalehe na namna ya kuhimili mihemko ili wasijihusishe na masuala ya ngono katika umri mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo haya huwajengea weledi na stadi za maisha vijana wetu hivyo kuwasaidia kuzingatia masomo zaidi na kujipanga vizuri ili kufikia ndoto zao za maisha. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau, mwaka 2018 ilizindua Jukwaa la Vijana la SITETEREKI lenye maudhui mahususi ya kumuelimisha kijana awe na mtazamo chanya wenye kumuwezesha kupata taarifa na huduma muhimu za uhakika kuhusu afya ya Uzazi kwa Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Elimu pamoja na Wadau wa maendeleo imeandaa Agenda ya Kitaifa ya Afya kwa Vijana na Uwekezaji (NAIA) yenye afua mtambuka zinazowahusu vijana hasa wenye umri wa miaka 10 hadi 19. Ajenda hiyo ilikuwa izinduliwe mwezi Machi mwaka huu, lakini kutokana na tishio la ugonjwa unaotokana na virusi vya Corona zoezi hilo limeahirisha kwa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeona ni vema kuileta mikakati yote inalenga vijana pamoja na kuitengenezea ajenda moja. Ajenda hii imejikita katika maeneo sita ambayo ni eneo la kwanza ni Kuzuia maambukizi ya VVU, eneo la pili ni kuzuia mimba za utotoni na utoro wa shule, eneo la tatu ni Kuzuia unyanyasaji wa jinsia, kimwili na kisaikolojia, eneo la nne ni kuboresha lische ya vijana; eneo la tano ni kuhakikisha wavulana na wasichana wanabaki shuleni na eneo la sita ni kuwajengea stadi za maisha kupambana na mazingira yanayowazunguka, ni Imani yangu kuwa, tukitekeleza kwa ufanisi afua zilizomo kwenye nguzo hizi tutakuwa tumemwezesha kijana wa Kitanzania kupata elimu ya afya ya uzazi kwa kiasi kikubwa hivyo kuwafanya kuwa rasilimali muhimu katika kuujenga uchumi wa nchi na kuweza kufikia lengo letu la kuwa nchi yenye uchumi wa kati.



**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kufahamu Mradi wa SITETEREKI ulileta mafanikio kiasi gani wa kubadili mienendo ya vijana baada ya tathmini? Naipongeza Serikali kwa kuandaa ajenda ya Kitaifa ya afya kwa vijana na uwekezaji.

Je, utaratibu upoje katika kufanikisha elimu kwa vijana wenye Ulemavu wa akili kwani ni kundi ambalo lipo katika makundi yenye hatari kubwa ya kuathirika pia?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa SITETEREKI ulianza 2018-2019 ambao ni mradi wa miaka mitano 2018/2023 ni jukwaa la vijana ambalo linatumika kuwafikishia ujumbe vijana kuhusu elimu ya afya ya uzazi. Jukwaa hilo, sehemu kubwa umekuwa ukifadhiliwa na *USAID* kupitia Mradi wa Tulonge Afya lakini kitaalamu Wizara ndio ilikuwa inatekeleza katika Mikoa 20 ya Tanzania Bara ambayo ilileta mafaniko ya kupunguza mimba za utotoni na kusimamia malengo ya kishule. Tathmini ya kati ya mradi itafanyika kuanzia mwezi Juni, 2020 na tathmini kubwa itafanyika mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, tumefanya rejea ya waelimisha rika (*Pre Educators Manual*) kwenye mapitio ya rejea hiyo tumeweka sura ya kuwafikia vijana wenye ulemavu ambapo tunategemea kuukamilisha hivi karibuni. Kwa kushirikiana na wadau wa *Pathfinder* na UMATI kuna Mtaala unaotengezwa ili kuwafikia vijana wenye ulemavu.

Na.49

**Vyama vya Wasanii na Wanamichezo  
Vinayotambulika Kisheria**

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU** aliuliza:-

Kumekuwa na vyama vingi vinavyotambuliwa kama vyama vya wasanii na wanamichezo nchini.

(a) Je, kuna jumla ya vyama vingapi halali vya wasanii na wanamichezo ambavyo vinatambuliwa kwa mujibu wa sheria?

(b) Serikali imechukua hatua gani dhidi ya vyama visivyo na usajili vya Sanaa na Michezo?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru Viti Maalum lenye sehemu A na B kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Disemba mwaka 2019 vipo vyama 69 ambavyo vinatambuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) Na. 23 ya mwaka 1984, ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019. Kwa upande wa michezo vipo jumla ya vyama 11 kwa ngazi ya kata vyama 28 vya Wilaya, Vyama 193 vya Kimkoa na Vyama 74 vya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya BASATA namba 23 ya mwaka 1984; ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019 na BMT ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kujihusisha na shughuli za Sanaa na Michezo pasipo na usajili na vibali halali vya Serikali. Vyama vya Michezo visivyosajiliwa haviruhusiwi kushiriki kwenye michezo yoyote rasmi inayofanyika kwenye ngazi za Wilaya, Mkoa au Taifa.

Na. 50

**Hitaji la Maji Kata za Jimbo la Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata za Kwai, Kilole, Kwekanga na Makanya katika Jimbo la Lushoto.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua tatizo la maji katika Wilaya ya Lushoto, Serikali tayari imekamilisha miradi ya Maji katika vijiji vya Mlalo/Mwangoi, Mlalo/Lwandai, Malibwi na Ngulu. Wananchi katika vijiji hivyo tayari wanapata huduma ya majisafi na salama na miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, Kata ya Kwai kuna mradi wa maji unaotoa huduma katika Kijiji cha Kwai. Aidha, Kata ya Kwai na Makanya zipo kwenye mpango wa muda wa kati wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji utakaotoa huduma ya maji katika vijiji 16 ambapo usanifu wake ulikamilika na kupata kibali cha utekelezaji. Mradi huo, umepangwa kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha wa 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kata ya Kilole, Kwekanga na Makanya Wizara imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 57 kwa ajili ya kufufua visima vifupi vilivyopo ambavyo havifanyi kazi. Kazi hii itafanyika kupitia mpango wa malipo kwa matokeo (*Payment by Results*). Tayari vifaa vya ujenzi wa miradi hiyo vimenunuliwa na utekelezaji wa mradi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwaondolea adha ya upatikanaji wa maji wananchi, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.18 kwa Halmashauri ya Lushoto ili kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa katika vijiji vya Shume,

Manolo, Madala, Gologolo, Ngwelo ambayo itahudumia jumla ya watu 48,781.

Na. 51

### **Kuhifadhi Vyanzo Vya Maji**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wadau wote wanaotumia rasilimali ya maji katika shughuli zao wanashiriki pia kikamilifu kuhifadhi vyanzo vya maji ikiwemo misitu, mabonde na ardhi?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Jimbo la Kaliua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha vyanzo vya maji vinahifadhiwa, Wizara imeweka utaratibu mbalimbali ili kuhakikisha wadau wote wanaotumia rasilimali ya maji katika shughuli zao wanashiriki kikamilifu kuhifadhi vyanzo vya maji ikiwemo misitu, mabonde na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu hizi ni pamoja na kuweka muundo wa kitaasisi wa usimamizi wa rasilimali za maji ambao unashirikisha watumia maji kupitia vyama vya watumia maji, utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya 2009 sambamba na sheria ya nyingine zinazohusika katika utunzaji wa vyanzo vya maji na kuandaa na kutekeleza mipango ya pamoja ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

Na. 52

### **Umeme Jazilizi Katika Jimbo la Lulindi**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Serikali iliahidi kusambaza umeme katika Vijiji vya Matogolo na Nagaga.

(a) Je, ni lini vijiji hivyo vitasambaziwa umeme?

(b) Je, ni lini umeme jazilizi katika Jimbo la Lulindi utasambazwa?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi Mbunge wa Lulindi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inatekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini katika vijiji vyote vya Tanzania Bara. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwenzoni Juni, 2021. Mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza unaoendelea utapeleka umeme katika vijiji 67 katika Wilaya ya Masasi kupitia Mkandarasi *JV Radi Services Ltd.*, *Njarita Contractors Ltd* na *Anguila Contractors Ltd*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Matogolo na Nagaga vimeshapatiwa huduma ya umeme kupitia Shirika la Umeme nchini - *TANESCO* mwezi Februari, 2020. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni maandalizi ya kusambaza umeme katika vitongoji vyote vya vijiji hivyo na kuunganishia umeme wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujazilizi katika Jimbo la Lulindi Mkoani Mtwara utanza kutekelezwa kupitia Mradi wa Ujazilizi Fungu la Pili (IIB) ambapo jumla ya Mikoa 16 itanufaika ikiwamo Mtwara. Mradi ya Ujazilizi IIB itawezesha kupeleka umeme katika vitongoji 2,400 na kuunganishiwa umeme wateja wa awali 95,000. Gharama na mradi ni Dola za Marekani milioni 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu utaanza mwezi Mei, 2020 na kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 9.

Na. 53

### **Kupeleka Umeme – Sekondari ya Lanzoni**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Kijiji cha Segoma Wilayani Mkinga ni miongoni mwa vijiji vitakavyopata umeme wa *REA III*.

Je, kwa nini Serikali isitumie fursa hiyo kuunganisha umeme katika Sekondari ya Lanzoni iliyopo karibu na Kitongoji cha Darajani?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) pamoja na Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) inatoa kipaumbele kupeleka umeme katika Taasisi za umma na za kijamii ikiwa ni pamoja na Shule za Awali, Msingi na Sekondari, Vyuo vya Ufundi Stadi, Vituo vya Afya, Zahanati, Visima vya Maji na Nyumba za Ibada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika Mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea na kazi ya kusambaza umeme katika Vijiji vya Mgamboshashui, Kumbamtoni na Mpale. Kazi hiyo inahusisha kupeleka umeme katika Shule za Sekondari Duga na Lanzoni zilizopo katika Jimbo la Mkinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gharama ya kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo vitatu pamoja na shule hizo za Sekondari ni Shilingi Milioni 91. Utekelezaji wa kazi hiyo

ulianza mwezi Machi, 2020 na utakamilika mwezi Mei, 2020. Jumla ya wateja wa awali zaidi ya 175 wataunganishiwa umeme.

Na. 54

### **Kero Zinazokabili Zao la Pamba**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Zao la pamba linakabiliwa na kero nyingi kutokana na kukosekana uhakika wa bei yake.

Je, Serikali inawaambia nini wakulima wa pamba?

**WAZIRI WA KILIMO** aliuza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni Mbunge wa Jimbo la Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la kuyumba kwa bei ya pamba katika soko la Kimataifa. Aidha, kufuatia tatizo hilo, Serikali ili ingilia kati ununuzi wa pamba katika msimu wa ununuzi wa 2019/2020 ili kuhakikisha mkulima anapata bei yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Suluhisho la kudumu kuhusu bei ya pamba ni kuongeza kiasi cha pamba inayochakatwa ndani ya nchi ili kuzalisha bidhaa zitakazotumika hapa nchini na hivyo kupunguza utegemezi wa soko la nje. Ili kutekeleza Mpango huo, Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje kujenga Viwanda vya kuongeza thamani ya zao la Pamba kwa kufuta tozo na kodi mbalimbali, kuzalisha umeme wa uhakika na bei nafuu, kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kuongeza tija na uzalishaji ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza bei na kipato kwa wakulima wa pamba, kuendelea kuongeza mitaji katika Taasisi za kifedha na maendeleo kama vile Benki ya Maendeleo ya kilimo na

Benki ya Rasilimali ili ziweze kutoa mkopo ya muda mrefu na kati kwa Viwanda vya Pamba ili kuongeza soko na mahitaji ya soko la ndani la Pamba na kupandisha uhitaji na Bei ya Pamba kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo imekipatia Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*) kazi ya kuandaa taarifa ya kina ya uwekezaji katika viwanda vya pamba ili kukuza soko la pamba. Taarifa hiyo ittoa dira ya namna ya kuanzisha viwanda vikiwemo vya kusindika pamba na inatarajiwa kukamilika kabla ya Julai, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha huduma za ugani na upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza kipato kwa wakulima.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimuite sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemani Jafo.

**WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na kuomba hoja kwamba, Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Mpango wa Makadirio ya Mapato



na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba taarifa yangu yote, hotuba yangu yote ambayo ina *page* 418 iweze kuingia katika kumbukumbu za Bunge kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii ili kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao madhubuti ambao umekuwa dira katika utekelezaji majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika wetu pamoja na Wenyeviti wote wa bunge kwa umahiri wenu katika kuongoza Mhimili huu wa Bunge kwa staili ya kipekee.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati hii ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kuyapitisha kwa kauli moja. Aidha, Kamati imekuwa ikitoa ushauri ambao umesaidia kuboresha utendaji wa kazi ya Ofisi ya Rais kwa kipindi chote kwa lengo la kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Januari, 2020, Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mheshimiwa Rashidi Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijijini. Naungana na wenzangu wote kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu na ndugu wote walioguswa na msiba huo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa Taarifa ya Utekelezaji kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/2020, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miaka minne kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesimamia ujenzi na ukarabati wa hospitali za halmashauri 98, Vituo vya Afya 433 na Zahanati 368. Aidha, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umekuwa wa uhakika kwa asilimia 92.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba 2015 hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya shilingi trilioni 1.01 kugharamia Mpango wa Elimu bila Ada. Kwa upande wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari, Serikali imejenga na kukamilisha vyumba vya madarasa 19,808, maabara 227 zimejengwa. Shule za sekondari 1,258 zimepatwa vifaa vya maabara na matundu ya vyoo 7,922 yamejengwa na shule kongwe za sekondari takribani 73 zimekarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imesimamia ukarabati na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 74,940.06, madaraja 232 na makalvati 7,168 yamejengwa katika maeneo mbalimbali na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejenga majengo ya utawala 86 ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2019/2020, halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 2.99. Hadi Februari 2020, makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri yalikuwa shilingi trilioni 2.54 sawa na asilimia 85 ya lengo. Aidha, shilingi bilioni 93.3 imewezesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata mikopo isiyokuwa na riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za maendeleo zilizotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kipindi cha miaka minne zimegharimu jumla ya shilingi trilioni 6.31 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imebuni, kusanifu na kujenga miundombinu na mifumo ya TEHAMA inayotumika katika maandalizi ya bajeti na mpango, ukusanyaji wa mapato na matumizi, usimamizi wa fedha za umma na utawala na bora. Mifumo hii imechangia katika kuimarisha katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, usimamizi wa fedha za Serikali, kupunguza gharama za mawasiliano na uendeshaji wa Ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi bilioni 802.6. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 36.46 ni za Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake, shilingi milioni 213.3 ni za mikoa na shilingi bilioni 765.48 ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hadi Februari 2020, jumla ya shilingi bilioni 491.59 zimekusanywa sawa na asilimia 61.28 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 6.20 kwa ajili ya kutekeleza majukumu

yake. Katika fedha hizo shilingi trilioni 3.81 ni kwa ajili ya Mishahara, shilingi bilioni 707.95 ni Matumizi Mengineyo, na shilingi trilioni 1.69 ni miradi ya maendeleo. Hadi Februari 2020 shilingi trilioni 3.89 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 62.59 ya bajeti iliyoidhinishwa. Hadi Februari 2020, jumla ya shilingi trilioni 3.36 sawa na asilimia 61 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi trilioni 2.87 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 494.96 ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa shughuli zilizofanyika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imefanya shughuli zifuatazo hadi ilipofika mwezi Februari, 2020:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumenunua mashine za mashine za kielektroniki (POS) 7,227 na kuzigawa katika halmashauri zote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; tumekamilisha zoezi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 ambapo Chama cha Mapinduzi kilipata ushiri wa wastani wa asilimia 99.9 kwa nafasi zote zilizoshindaniwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesimamia utoaji wa mikopo ambapo hadi Februari, 2020 mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 25.38 sawa na asilimia 33.3 ilishatolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulema; Kupitia kampeni ya Mkoa wetu Viwanda vyetu, viwanda vikubwa, vya kati na vidogo na vidogo sana 4,876 vilikuwa vimeshakamilika; na Wafanya biashara 1,551,126 walipatiwa vitambulisho vya ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vibali 11,737 vya ujenzi vimetolewa hadi Februari, 2020 ikilinganishwa na vibali 2,425 vya ujenzi vilivyotolewa hadi Februari, 2019. Mafanikio haya makubwa yametokana na mwongozo mpya uliotolewa ambapo kwa sasa kibali kinatolewa ndani ya siku saba ikilinganishwa na siku 180 zilizokuwa zikitolewa hapo awali; ujenzi wa miradi mkakati unaendelea katika maeneo ya Halmashauri ya Ruangwa, Chato, Kakonko, Nanyumbu,

Ilemela, Kinondoni, Ilala, Moshi, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Maswa, Momba, Songwe, Buhigwe, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya magari 155, pikipiki 484 na baiskeli 2,689 zilinunuliwa kwa ajili ya viongozi na watendaji wa ngazi mbalimbali katika ngazi za mikoa, wilaya, halmashauri na tarafa hadi ngazi ya kata kwa lengo la kuboresha usimamizi na utendaji wa kazi; Matumizi sahihi ya *Epicor* na mifumo mingine ambayo ni ya ukusanyaji mapato ambapo katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015, usimamizi wa fedha za umma umeimarika kutoka kuongezeka kwa halmashauri zinazopata hati zinazoridhisha toka asilimia 81 mwaka wa fedha 2015/2016 hadi asilimia 95 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hati zenye mashaka zimepungua kutoka asilimia 19 katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi asilimia tano katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi waliokiuka sheria na kanuni, utaratibu za utumishi wa umma ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai mpaka Februari 2020, jumla ya watumishi 26 wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanikisha ujenzi wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI Makao Makuu kwa utaratibu wa *Force Account* katika eneo la Mji wa Mtumba kwa kupunguza gharama kutoka mradi wa wastani wa shilingi bilioni 3.6, ambapo mkandarasi angetumika mpaka bilioni 1.5. Viongozi Wakuu sita (6) pamoja na Wakurugenzi na Watendaji mbalimbali wapatao 100 wote wamepata sehemu ya kufanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekamilisha ujenzi wa Ofisi ya *TARURA* Makao Makuu katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba kwa gharama ya shilingi bilioni 2.1 kwa kutumia utaratibu wa *Force Account*. Hivi sasa tumeokoa takribani shilingi milioni 552.64 kwa mwaka ambazo zilikuwa zikitumika kwa ajili ya kulipia kodi ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea na ujenzi wa majengo ya utawala na nyumba za viongozi katika ngazi za mikoa, wilaya, halmashauri, tarafa katika maeneo mbalimbali yaliyoainishwa ambayo yote yanapatikana katika kitabu changu cha bajeti. Tumeendelea kusimamia ujenzi wa hospitali za Halmashauri 71 na kuanza ujenzi wa hospitali mpya 27 za halmashauri. Tumeendelea na zoezi la ujenzi wa vituo vya afya 81 katika halmashauri mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kupunguza msongamano wa wagonjwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma ya afya. Tumefanya ununuzi wa madawa na vifaa ambao umeendelea katika maeneo mbalimbali, mapambano dhidi ya malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na masuala yote ya ustawi wa jamii yote yamepewa kipaumbele katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeainisha na kuviandaa vituo vipatavyo 182 kwa ajili ya kuwatenga na kuwahudumia washukiwa na watakaothibitika kuwa na ugonjwa wa *corona*. Vilevile, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto tumezitambua hoteli na hosteli zitakazotumika katika kutenga wageni na wenyeji watakaolingia nchini ili kuzuia kuenea kwa virusi vya ugonjwa wa *corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya elimu kuanzia mwaka 2016 - 2020 katika kipindi hiki tulichokifanya, kwa kipindi cha miaka minne uandikishaji wa rika lengwa la watoto wa darasa la elimu ya awali wameongezeka kutoka wastani wa asilimia 45 mwaka 2015 hadi asilimia 86.2 mwezi Machi, 2020. Maboma 364 ya nyumba za Walimu yaliyokuwa yamejengwa kwa nguvu za wananchi sasa tumeyakamilisha. Shule nne za mfano ambazo tumejenga katika Mkoa wa Dodoma, Geita, Mtwara pamoja na Kigoma ambayo imegharimu shilingi bilioni 2.82 tumezikamilisha. Shule ya Msingi Mwisenge shule ambayo Baba wa Taifa alisoma pale iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imefanyiwa ukarabati mkubwa kwa jumla ya shilingi milioni 706.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wanafunzi bilioni moja, mia tano thelathini na moja elfu mia moja na ishirini sawa na asilimia 91.6 walifaulu mtihani wa upimaji wa darasa la nne. Kati ya wanafunzi milioni moja laki sita sitini na tano elfu mia nane na sitini na tatu waliofanya mtihani huo. Ufaulu wa mtihani wa darasa la saba umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 57 iliyokuwa mwaka 2015 hadi asilimia 81.5 kwa mwaka 2019; jumla ya matundu ya vyoo 2,601 yamejengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 2.87 na mabweni 253 yamejengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 8.22; na Ujenzi wa nyumba za Walimu 153, majengo ya utawala 64 na ujenzi wa daharia 55 kwa gharama ya shilingi bilioni 10.69 umefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa shule za sekondari kongwe tisa (9) umeendelea kwa gharama ya shilingi bilioni 6.71. Aidha, katika kipindi cha miaka minne jumla ya shule kongwe 73 zimekarabatiwa kati ya shule 89 kwa gharama ya shilingi bilioni 84.3 hadi Februari, 2020. Ukarabati huu wa shule umewezesha kusaidia uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia pamoja na idadi ya wanafunzi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne ufaulu wa mitihani wa kidato cha nne umeongezeka kutoka asilimia 69.8 mwaka 2015 hadi asilimia 80.65 mwaka 2019. Kwa upande wa mtihani wa Taifa wa kuhitimu kidato cha sita katika mwaka 2019 jumla ya wanafunzi 78,666 sawa na asilimia 98.6 ya wanafunzi 79,770 walifanya mtihani huo na kufaulu. Mafanikio haya makubwa yametokana kwa kiasi kikubwa kwa juhudi kubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kushirikiana na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la michezo, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeratibu na kusimamia michezo katika Shule za Msingi na Sekondari kuanzia ngazi ya shule mpaka ngazi ya taifa; mashindano ya michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA yamefanyika katika Mkoa wa Mtwara mwaka huu. Mashindano haya yamekuwa chachu ya ukuzaji na kuibua vipaji vya watoto wetu wenye umri mdogo ambapo

mfano timu yetu ya UMISSETA ya *Copa Coca Cola* Tanzania ilishiriki mashindano ya *Copa Coca Cola* Afrika yaliyofanyika mwaka 2019 nchini Kenya na kutwaa ubingwa wa Afrika kati ya nchi 11 zilizoshiriki mashindano hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*). Hadi Februari 2020, *TARURA* ilikuwa imekamilisha matengenezo ya jumla ya kilomita 4,998.6, madaraja 57 na makalvati 238 kwa gharama ya shilingi bilioni 154.19. Pia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami chenye urefu wa kilometa 64 kwa fedha za ndani katika Halmashauri 64 ulifanyika kwa gharama ya shilingi bilioni 33 unaendelea. Hata hivyo, mvua nyingi zinazoendelea kunyesha nchini zimesababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara za mijini na vijijini. Aidha, *TARURA* inaendelea kufanya matengenezo katika maeneo korofi katika kipindi cha mvua ili barabara hizo zilizoharibika ziweze kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara katika Mji wa Serikali katika eneo la Mtumba zenye urefu wa kilometa 40. Kati ya barabara hizo, barabara zenye urefu wa kilometa 11.2 zitakuwa za njia nne zitakazopitisha magari mawili kila upande. Pia tutajenga barabara za watembea kwa miguu, barabara za baiskeli, vituo vya abiria 50, taa za barabarani 739, taa za kuongozea magari na mifereji ya zege ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 98. Mradi huo mkubwa umeanza kutekelezwa Februari, 2020 kupitia Mkandarasi *China Henan International Group (CHICO)* ambapo mradi huo umepangwa kukamilika katika kipindi cha miezi 18 utakaogharimu shilingi bilioni 89.13

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salam (*DMDP*) katika mwaka wa fedha 2019/2020 kazi zifuatazo zimefanyika. Ujenzi wa jumla ya kilomita 47.59 za barabara za lami, masoko 6, vizimba 33, vituo vya mabasi viwili, kituo cha afya Buza na kiwanja cha mpira katika Jiji la Dar es Salaam kwa gharama ya shilingili bilioni 85.69.



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mradi wa Mji Mkakati (*TSCP na ULGSP*) katika Miji 18, hadi Februari 2020, *TARURA* ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 213.05 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami; ujenzi wa mifereji mikubwa ya maji ya mvua; ujenzi wa madaraja ya waenda kwa miguu; ujenzi wa masoko ya kisasa matano ya Dodoma, Mtwara, Morogoro, Iringa na Njombe; vituo vya mabasi sita ikiwemo stendi kuu ya mabasi ya Dodoma; ununuzi wa maroli 10 ya kubebea taka ngumu na maandalizi ya Mpango Kapambe yaani *General Planning Scheme (GPS)* katika Miji 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zilizoko chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia taasisi zake zingine zikiwemo Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salam (*DART*), Tume ya Utumishi wa Walimu, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Shirika la Elimu Kibaha, Shirika la Masoko Kariakoo na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imefanikiwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2019/2020. Hakika tunajivunia mafanikio makubwa hayo yaliyopatikana katika kipindi chote tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia marakani. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Kawaida wa Maendeleo katika mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zake, Mikoja pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea na usimamizi wa shughuli za utawala bora (*D by D*); uratibu na ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya utawala ya Mkoa, Wilaya, Halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri 30 ambazo zimeelekezwa na Serikali kuhamia katika maeneo yake ya utawala.

(ii) Kufanya matengenezo ya barabara za Wilaya vijijini na mijini zenye urefu wa kilometa 23,175.11.

(iii) Ujenzi na ukarabati wa madaraja 80, makalvati 2,052 na mifereji yenye urefu wa kilometa 79.9.

(iv) Kufanya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 35.3 kwa kiwango cha lami na ukarabati na ujenzi wa kilometa 321 kwa kiwango cha changarawe,

(v) Kukamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu kilometa 47.59 kwa kiwango cha lami chini ya mradi wa *DMDP*.

(vi) Kuanza ujenzi wa barabara ya Nzasa – Kirungule – Buza; Ulongoni – Bangulo - Kinyerezi na Magomeni Mapipa - Urafiki.

(vii) Kuanza ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 11.7 kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

(viii) Kukamilisha ujenzi wa masoko sita ya Kilakala, Kigilagila, Bombom, Minazi Mirefu, Mbagala na Bwawani.

(ix) Kuanza utekelezaji wa mradi katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara kwa kiwango cha lami katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Morogoro, Rukwa, Katavi, Songwe, Tanga, Pwani, Dodoma, Mtwara, Ruvuma na Lindi.

(x) Kuanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi mpya ujulikanao kama *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness* katika Halmashauri 45 za Majiji, Manispaa na Miji.

(xi) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Jiji Dodoma.

(xii) Kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250 katika Kampasi ya Hombolo.

(xiii) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Hospitali ya Tumbi.

(xiv) Kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu katika maeneo mbalimbali ya Shirika la Masoko Kariakoo ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

(xv) Kuendelea na ujenzi wa soko la jumla katika eneo la Mbezi Beach Makonde.

(xvi) Kujenga wodi tatu katika kila hospitali zote 67 za Halmashauri zinazoendelea kujengwa.

(xvii) Kuendelea na ujenzi mpya wa hospitali 27.

(xviii) Kuanza ujenzi wa zahanati tatu katika kila Halmashauri. Hii ni *message* kwa Waheshimiwa Wabunge kila Halmashauri tutakuwa na ujenzi wa zahanati tatu. (*Makofi*)

(xix) Ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali 67 za Halmashauri ili kuziwezesha kutoa huduma.

(xx) Kukamilisha ujenzi wa maboma vya vyumba vya madarasa katika shule za msingi kwenye halmashauri zote 184. Tunaenda kujenga maabara zisizopungua saba (7) katika kila Halmashauri kwa ajili ya masomo ya sayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Halmashauri tunaenda kujenga maabara zisizopungua saba (7) za sayansi katika kila Halmashauri ili kuwezesha ufundishaji wa masomo ya sayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni machache miongoni mwa mengi ambayo yako katika kitabu changu. Sasa naomba niwashukuru, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kukushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika wetu na Mwenyekiti wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wote wa Bunge la Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli zake. Vilevile naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini na Makamu Mwenyekiti, mama yetu

Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum kwa kazi nzuri sana ya kuisimamia Kamati ya TAMISEMI na kazi mahiri iliyofanywa na Wajumbe wa Kamati hii ndani ya miaka minne. Maoni na ushauri wao umetusaidia kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na ndiyo maana tunasema TAMISEMI ni Wizara ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wadau wote wa maendeleo kutoka Mashirika ya Kimataifa na kitaifa katika utekelezaji wa programu, miradi na shughuli mbalimbali katika Ofisi ya TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ofisi ya Rais TAMISEMI itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza umaskini kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kipekee nimshukuru Manaibu wangu ndugu yangu Mheshimiwa Kandege, Mbunge wa Kalambo na ndugu yangu Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Ukonga kwa msaada mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph Nyamhanga, Naibu Katibu Mkuu Dorothy Gwajima na mwenzio Gerald Mweli pamoja na Katibu wa Tume wa Utumishi wa Walimu Bibi Winifrida Rutaindurwa. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wakurugenzi katika Ofisi ya TAMISEMI na Wakurugenzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, wananchi wote kwa ujumla, Maafisa Tarafa na Watendaji wa Kata kwa kufanya kazi ya pamoja iliyotufikisha hapa tulipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais wakiongozwa na Waziri mkongwe *Senator*, Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Rais (Manajimenti ya Utumishi ya Umma), Mheshimiwa George Huruma Mkuchika na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwachuche Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa ushirikiano mzuri. Aidha, nawashukuru sana Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na Naibu Katibu Mkuu ndugu yangu Dkt. Francis kwa ushirikiano walionipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote wakiongozwa na mkuu wa kazi dada yangu Jenista Mhagama hapa kwa kazi kubwa wanayofanya na kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha miaka minne kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo langu la Kisarawe kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Nawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuboresha utoaji wa huduma kiuchumi na kijamii. Aidha, naishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu muda wote walipokuwa mbali nami katika kutekeleza majukumu haya ya kitafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizochini Ofisi ya Rais - TAMISEMI yaani Mikoa 6 na Halmashauri 185, inaomba idhini ya kukusanya maduhuli ya mapato ya ndani ya Sh.860,683,049,427. Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho ya masurufu na mishahara na kodi na ushuru mbalimbali zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria yetu Sura 290.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Sh.7,019,800,353,000) kwa ajili ya Ofisi ya Rais - Fungu Na. 56,

Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na. 02, Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 185. Kati ya fedha hizo zinazombwa, Sh.4,729,880,457,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara ya Sh. 3,878,738,058,000 na Sh.851,142,399,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya Sh.2,289,919,896,000 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya hizo Sh.1,296,949,390,000 ni fedha za ndani na Sh.992,990,506,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba yangu hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi, Mikoa na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa ambayo ni sehemu ya hotuba yangu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hutoba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambayo ni [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA SELEMANI SAIDI JAFO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili

Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi kwa mwaka wa fedha 2019/20 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais-TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**2. Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo.

**3. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao madhubuti ambao umekuwa dira katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**4. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri katika kuongoza Mhimili wa Bunge. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/21. Kamati hii ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na kuyapitisha kwa kauli moja. Aidha, Kamati imekuwa ikitoa ushauri ambao umesaidia kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kuwahudumia wananchi.

**5. Mheshimiwa Spika**, tarehe 15 Januari, 2020, Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mheshimiwa Rashidi Ajali Ahkbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini. Naungana na wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu na wote walioguswa na msiba huo. Tunamuomba

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

**6. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kutoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilivyotekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miaka minne iliyopita. Kwa mujibu wa Ibara ya 48 ya llani ya CCM, Ofisi yangu ina jukumu la kusimamia utoaji wa huduma bora za kiuchumi na kijamii ili kuchangia jitihada za kuondoa umaskini na kuharakisha maendeleo ya wananchi. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni katika sekta za afya, elimu, ujenzi wa majengo ya utawala, miundombinu ya barabara, na kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara.

**7. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesimamia ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Halmashauri 98, Vituo vya Afya 433 na Zahanati 368. Aidha, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umekuwa wa uhakika kwa **asilimia 92**.

**8. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba 2015 hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi trilioni 1.01** kugharamia Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kwa upande wa miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari, Serikali imejenga na kukamilisha vyumba vya madarasa **19,808** na vyumba **1,313** vipo katika hatua za ukamilishaji, maabara za masomo ya sayansi **227** zimejengwa na Shule za Sekondari **1,258** zimepatiwia vifaa vya maabara, matundu ya vyoo 7,922 yamejengwa na kukamilika na matundu ya vyoo **571** yanaendelea kukamilishwa. Aidha, madawati **5,070,896** yametengenezwa na shule Kongwe za Sekondari **73** zimekarabatiwa.

**9. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesimamia ukarabati na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa **74,940.06** ambapo kati ya hizo kilometa **485** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, jumla ya madaraja 232 na makalvati **7,168** yamejengwa na kukamilika.



**10. Mheshimiwa Spika**, Serikali imejenga majengo ya utawala 86 ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri. Kati ya majengo hayo, majengo 29 yamekamiliika na 57 yapo katika hatua za ukamilishaji.

**11. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2019/20, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 2.99**. Hadi Februari 2020, makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri yalikuwa **Shilingi trilioni 2.54** sawa na **asilimia 85** ya lengo. Aidha, jumla ya **Shilingi bilioni 93.3** imewezesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

**12. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imebuni, kusanifu na kujenga miundombinu na mifumo ya TEHAMA inayotumika katika maandalizi ya bajeti na mipango, ukusanyaji wa mapato na matumizi, usimamizi wa fedha za umma na Utawala na Bora. Mifumo iliyosanifiwa na kujengwa ni mtandao kiambo (LAN) na mtandao mpana (WAN) ambayo imeunganisha Mikoa 26, Halmashauri 185 za Tanzania Bara na Taasisi za Ofisi ya Rais- TAMISEMI. Mifumo hii imechangia katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, usimamizi wa fedha, kupunguza gharama za mawasiliano na uendeshaji wa Ofisi.

**13. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne, jumla ya ajira za kudumu na za muda **2,347,334** zimezalishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa. Wananchi wamenufaika na upatikanaji wa ajira hizo na kuboresha maisha yao.

**14. Mheshimiwa Spika**, shughuli za maendeleo zilizotekelezwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimegharimu takriban **Shilingi trilioni 6.31** katika kipindi cha miaka minne.

**B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA OFISI YA RAIS- TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2015.**

**15. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi

ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake iliendelea kutekeleza vipaumbele vyake kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kusimamia na kuratibu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019; uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya msingi na elimu katika Shule za Msingi na Sekondari; kusimamia mpango wa utoaji Elimumsingi Bila Ada, usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha; kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi; uwezesaji wananchi kiuchumi; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kujenga miundombinu ya kiuchumi na kijamii ili kufungua fursa za kiuchumi mijini na vijijini na kuziwezesha Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais- TAMISEMI kutekeleza majukumu yake.

### **Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**16. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya **Shilingi bilioni 802.6**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 36.46** ni za Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, **Shilingi milioni 213.30** ni za Mikoa na **Shilingi bilioni 765.48** ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi bilioni 491.59** zimekusanywa sawa na **asilimia 61.28** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**17. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa **Shilingi Trilioni 6.20** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 3.81** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 707.95** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi trilioni 1.69** ni za miradi ya maendeleo. Hadi Februari 2020, **Shilingi trilioni 3.89** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 62.59** ya bajeti iliyoidhinishwa.

## Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI

**18. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake iliidhiniwa jumla ya **Shilingi bilioni 563.29**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 496.56** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi bilioni 66.73** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi bilioni 413.65** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 73** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 35.91** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 377.73** ni Fedha za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake imekusanya maduhuli ya **Shilingi bilioni 25.06** sawa na **asilimia 80** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 31.23**. Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, mauzo ya huduma, ada za wanafunzi na tozo mbalimbali.

## Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu

**19. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya Utumishi wa Walimu iliidhiniwa jumla ya **Shilingi bilioni 15.90** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 9.89** zilikuwa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 6.00** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi Februari, 2020, Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 7.04** sawa na **asilimia 44** ya bajeti. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha Shilingi bilioni 4.41 za Mishahara na **Shilingi bilioni 2.63** za Matumizi Mengineyo.

## Bajeti za Mikoa

**20. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Tawala za Mikoa ziliidhiniwa jumla ya **Shilingi bilioni 196.20** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 128.87** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 67.33** zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi bilioni**

**100.04** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 51** ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi bilioni 84.97** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 15.06 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Mikoa imekusanya maduhuli ya **Shilingi milioni 77.29** sawa na **asilimia 35.29** ya lengo la kukusanya **Shilingi milioni 219.30**. Makusanyo ya maduhuli yametokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu.

### **Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

**21. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha, 2019/20, Halmashauri ziliidhinishwa kukusanya mapato ya ndani jumla ya **Shilingi bilioni 765.48** kutokana na ushuru, tozo na vyanzo mbalimbali vya mapato kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Hadi Februari 2020, Halmashauri zilikuwa zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 466.45** sawa na **asilimia 61.28** ya lengo la mwaka wa fedha 2019/20 (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.1*). Makusanyo haya ni ongezeko la **Shilingi bilioni 73.54** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 392.90** zilizokusanywa hadi Februari 2019, kwa mwaka wa fedha 2018/19.

**22. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imeendelea kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kununua mashine za kielektroniki (POS) **7,227** ambazo zimetolewa kwenye Halmashauri zote ambapo Halmashauri zenye makusanyo madogo ya mapato ya ndani zimepatiwa kipaumbele kwenye mgao. Lengo ni kuzisaidia Halmashauri hizo kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

### **Ruzuku ya Serikali Kuu**

**23. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishwa kutumia jumla ya Shilingi trilioni 5.48. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 4.32** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zikijumuisha Mishahara **Shilingi trilioni 3.66** na **Shilingi bilioni 650.92** ni kwa

ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa maendeleo, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.16** ambazo zinajumuisha fedha za ndani **Shilingi bilioni 669.55** na **Shilingi bilioni 492.48** fedha za nje. Hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi trilioni 3.36** sawa na **asilimia 61** zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi trilioni 2.87** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 494.96** ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

## Matumizi

**24. Mheshimiwa Spika**, fedha zilizopokelewa na kukusanywa zimetumika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais- TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia misingi ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019; ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na elimu katika Shule za Msingi na Sekondari; Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi kwenye Mikoa, Wilaya, Tarafa na Halmashauri; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa majukumu kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; uwezeshaji wananchi kiuchumi; uboreshaji mazingira ya biashara na uwekezaji; usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha, huduma za utawala, ujenzi wa miundombinu ya barabara, na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Taasisi.

## Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019

**25. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 uliofanyika tarehe 24 Novemba, 2019 kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288 kwa mafanikio makubwa. Uchaguzi wa mwaka 2019 ni wa sita (6) tangu ulipofanyika kwa mara ya kwanza chini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1994.

**26. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la maeneo ya utawala Na. 536 na 537, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulihusisha Mitaa **4,263**, Vijiji **12,319** na Vitongoji **64,384**. Uchaguzi huo ulihusisha Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vitongoji, Wajumbe wa Serikali za Vijiji na Wajumbe wa Kamati za Mitaa. Katika uchaguzi huo, Chama cha Mapinduzi kilipata ushindi kwa wastani wa **asilimia 99.9** kwa nafasi zote zilizoshindaniwa yaani za Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vitongoji na Wajumbe.

**27. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliowezesha na kufanikisha uchaguzi kufanyika kwa usalama na amani wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Vyama vya Siasa, Asasi za Kiraia (AZAKI) na Taasisi za Serikali. Kazi iliyobaki ni kuendelea kushirikiana na viongozi waliochaguliwa ili kutimiza azma ya kuwaletea wananchi maendeleo wanayotarajia.

### **Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**28. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kukuza ajira na kipato kwa wananchi. Hadi Februari 2020, mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 25.38** sawa na **asilimia 31.3** ya malengo ya mwaka wa fedha 2019/20 ilikuwa imetolewa kati ya lengo la kutoa mikopo ya **Shilingi bilioni 62.2**. Mikopo hiyo ilitolewa kutokana na **asilimia 10** ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

**29. Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 12.92** zimetolewa kwa vikundi **8,207** vya Wanawake, **Shilingi bilioni 9.54** zimetolewa kwa vikundi **4,266** vya Vijana na **Shilingi bilioni 2.91** zimetolewa kwa vikundi **915** vya Watu Wenye Ulemavu. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya **Shilingi bilioni 9.39** zilirejeshwa kutoka kwenye mikopo ya vikundi **10,530**.

**30. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka zaidi ya minne kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020, Serikali imefanikiwa

kutoa mikopo ya jumla ya **Shilingi bilioni 93.3** ambayo imenufaisha vikundi **32,553** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Kati ya mikopo hiyo, **Shilingi bilioni 54.08** zilitolewa kwa vikundi **20,542** vya Wanawake, **Shilingi bilioni 34.98** zilitolewa kwa vikundi **10,741** vya Vijana na **Shilingi bilioni 4.24** zilitolewa kwa vikundi **1,270** vya Watu Wenye Ulemavu. Mikopo hiyo imechangia kukuza uwekezaji mdogo na mkubwa na kuongeza kipato cha wananchi.

**31. Mheshimiwa Spika**, mikopo hiyo imewekezwa kwenye viwanda vidogo, kilimo na ufugaji wa kisasa, biashara, utunzaji wa mazingira, huduma za kifedha na huduma za usafiri. Baadhi ya Vikundi vimeanza kuwekeza katika miradi mikubwa yenye tija ya kuongeza kipato na ajira ikiwemo mradi wa kuwezesha Wajasiriamali katika Halmashauri ya Mji Kahama ambapo ekari 500 zimetengwa na kuendelezwa. Mradi huo umewezesha utoaji wa mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.29** kwa vikundi 403 vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu vinavyoendesha shughuli zao katika kituo kimoja cha Zongomela ambapo ajira 1,692 zimezalishwa; mradi wa Vijana wa kike wa ushonaji nguo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga wenye gharama ya **Shilingi milioni 100** na wanufaika **30**, mradi wa kilimo cha mboga mboga katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala wenye uwekezaji wa Shilingi milioni 150, mradi wa kuzalisha sabuni (*Mafinga Soap*) ambao umewekeza zaidi ya **Shilingi milioni 70** katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, mradi wa kiwanda cha kuchakata kokoto katika Halmashauri ya Mji wa Makambako wenye uwekezaji wa zaidi ya **Shilingi milioni 45**, mradi wa ununuzi wa mashine ya kuchanganya malighafi wenye uwekezaji wa **Shilingi milioni 30.0** katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, mradi wa kiwanda cha uhomeleaji cha *Five Youth Innovators* katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wenye mtaji wa **Shilingi milioni 20** na mradi wa usafirishaji katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke uliogharimu **Shilingi milioni 229**.

**32. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilifanikiwa kufuta malimbikizo ya fedha za mikopo ya miaka ya nyuma yaliyotokana na uwezeshaji wa **asilimia 10** ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa vikundi

vya Wanawake na Vijana kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Malimbikizo yaliyofutwa yalitokana na fedha ambazo Halmashauri hazikuchangia kabla ya kutungwa kwa Sheria ya kusimamia mikopo hiyo.

### Maeneo ya Uwekezaji

**33. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (BLUEPRINT) ambao lengo lake ni kuhakikisha vikwazo na kero mbalimbali za biashara na uwekezaji zinaondolewa ili kurahisisha mazingira ya kufanyia biashara. Hadi Februari 2020, tozo mbalimbali zimeondolewa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo ushuru wa huduma kwa biashara za nyumba za kulala wageni, ushuru wa mabango yanayoelekeza mahali huduma inapopatikana, ushuru kwa wafanyabiashara wadogo, marekebisho ya ushuru wa mazao kati ya asilimia 3 hadi 5 wa awali hadi asilimia 3 kwa mazao ya biashara na chakula yasiyopungua tani moja (1). Tozo na ushuru huo umeondolewa kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2017. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini ili kuondoa kodi zenye kero zinazokwamisha ufanyaji wa biashara na uwekezaji zikiwemo tozo zinazotowza na Taasisi zaidi ya moja.

**34. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya hekta **854,821.59** zimetengwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uwekezaji zikiwemo hekta **403,784.92** kwa ajili ya viwanda vikubwa, vidogo na vya kati. Aidha, hekta **45,231.33** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa masoko, minada, hoteli, ujenzi wa stendi za mabasi, maduka na biashara. Vilevile, hekta **405,805.34** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika sekta za kilimo, misitu, ufugaji, umwagiliaji, madini na gesi. Hivyo, wadau mbalimbali wanahamasishwa kutumia fursa hiyo ya uwekezaji.

**35. Mheshimiwa Spika**, kupitia kaulimbiu ya **Mkoa Wetu, Viwanda Vyetu**, iliyoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia na kutoa hamasa kwa wadau na wananchi kwa ujumla kushiriki



kikamilifu katika mkakati wa ujenzi wa viwanda ili kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Hadi Februari 2020, viwanda **4,876** vimeanzishwa na kuvuka lengo la kuanzisha viwanda **2,600** lililowekwa sawa na viwanda **100** katika kila Mkoa kwa Mikoa yote 26 Tanzania Bara. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa ni **108**, viwanda vya kati ni **236**, viwanda vidogo **2,522** na viwanda vidogo sana **2,010**.

**36. Mheshimiwa Spika**, Mikoa **8** ya Tabora, Ruvuma, Simiyu, Mtwara, Geita, Songwe, Morogoro na Dodoma imefanikiwa kuandaa wasifu wa kiuchumi (*Regional Economic Profile*) ili kubainisha fursa za kiuchumi na uwekezaji. Mikoa hiyo iliandaa makongamano ya uwekezaji yaliyotumika kuwatangazia wadau fursa za uwekezaji zinazopatikana katika Mikoa hiyo ili waweze kuzitumia. Hivyo, nawahamasisha wadau mbalimbali watumie fursa hiyo ili kuwekeza katika miradi itakayochangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

**37. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, wafanyabiashara wadogo **1,551,126** wamepatiwa vitambulisho ambavyo vimewezesha kukusanywa kwa **Shilingi bilioni 31.02** katika Mikoa yote **26**. Lengo la azma hii ni kuwatambua wafanyabiashara wadogo na kuwawekea mazingira rafiki ya ufanyaji biashara. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa Kanuni za kusimamia wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo ili kutambua mchango wa biashara hizo katika ukuaji wa uchumi.

**38. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi ulioanza kutekelezwa mwaka 2018 kwenye Halmashauri 184 Tanzania Bara. Mwongozo umesaidia kupunguza muda wa kushughulikia kibali cha ujenzi kutoka wastani wa siku **180** hadi wastani wa siku **7**. Hadi Februari 2020, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa zimetoa vibali **11,737** vya ujenzi ikilinganishwa na vibali **2,425** vya ujenzi vilivyotolewa hadi Februari 2019.

**39. Mheshimiwa Spika**, mafanikio hayo yametokana na uwepo wa Kamati ya pamoja ya wataalam inayoshughulikia utoaji wa vibali katika Halmashauri. Hadi Februari 2020, Halmashauri zimekusanya ada ya vibali vya ujenzi jumla ya **Shilingi bilioni 3.20** sawa na **asilimia 57** kati ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 5.64**. Ufanisi katika utoaji wa vibali vya ujenzi umesaidia kuboresha mazingira ya uwekezaji kutokana na kuondolewa kwa urasimu na kupungua kwa muda uliokuwa unatumika awali kutoa vibali vya ujenzi.

### **Miradi ya Kimkakati**

**40. Mheshimiwa Spika**, Miradi ya kimkakati inajenga dhana ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kujitegemea na kupunguza utegemezi kutoka katika ruzuku ya Serikali Kuu na Wadau wa Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2019/20, ziliidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 70** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi **38** ya Kimkakati. Hadi Februari 2020, **Shilingi bilioni 25.36** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 36.24** ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi **13** katika Halmashauri **11** za Wilaya za Ruangwa, Chato, Kakonko na Nanyumbu; Halmashauri za Manispaa za Ilemela, Ubungo, Kinondoni, Ilala, Moshi; Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam; na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Aidha, miradi mingine **9** ya kimkakati inaendelea kutekelezwa katika Halmashauri **8** za Wilaya za Maswa, Momba, Songwe, Kakonko, Buhigwe, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwa gharama ya **Shilingi bilioni 22.41** kwa kutumia fedha za bakaa ya mwaka wa fedha 2018/19.

### **Usimamizi wa Watumishi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**41. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya watumishi 7,280 wameajiriwa katika ajira za kudumu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya hao, walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walikuwa **4,945**, watumishi wa kada za afya walikuwa 765 na Watendaji wa Kata walikuwa **1,570**. Ajira hizo zinafanya watumishi walioajiriwa katika Mamlaka za Serikali

za Mitaa kufikia **28,673** katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020 wakiwemo walimu **18,181**, watumishi wa afya **8,922** na Watendaji wa Kata **1,570**. Ajira hizo zimesaidia kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, nafasi **88** za Wakuu wa Idara na Vitengo zilizokuwa zinakaimiwa zimejazwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ili kuboresha utendaji na uwajibikaji.

**42. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne kuanzia Novemba, 2015 hadi Februari 2020, jumla ya ajira **2,347,334** za mikataba/muda zimezalishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sekta zilizoongoza kwa kuzalisha ajira nyingi ni uwezeshaji wananchi kiuchumi (**ajira 1,551,126**), ujenzi wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini (**ajira 729,160**), elimu (**ajira 53,578**), afya (**ajira 12,820**) na ujenzi wa majengo ya utawala ya Mikoa na Halmashauri (**ajira 650**). Watanzania wamenufaika na ajira hizo kupitia utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi na matumizi ya utaratibu wa *Force Account* katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### **Kuzijengea Uwezo Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**43. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, mafunzo ya kuboresha utendaji yametolewa kwa watumishi **880** katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Kilimanjaro, Manyara, Dar es Salaam, Pwani, Iringa, Mbeya, Njombe, Katavi, Ruvuma, Lindi, Mtwara na Rukwa kuhusu Mfumo wa Upimaji wa Wazi wa Utendaji Kazi wa Watumishi wa Umma (OPRAS). Mafunzo hayo yamesaidia kuimarisha utendaji na ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Serikali. Aidha, mafunzo mengine yametolewa kwa Kamati za Kudhibiti Uadilifu katika Halmashauri **185** ili kuimarisha weledi na kupunguza viashiria vya rushwa katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Vilevile, Wakurugenzi, Maafisa Utumishi na Wakaguzi wa Ndani kutoka Halmashauri **185** wamepatiwa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha ili kuimarisha shughuli za

kiutumishi na mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**44. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, wahudumu wa afya **2,689** kutoka Mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro na Rukwa wamepatiwa mafunzo kuhusu masuala ya lishe. Aidha, Maafisa Ugani **297** na wakulima wadogo **1,761** wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji wa mboga mboga na matunda kupitia mashamba darasa yapatayo **111** yaliyoanzishwa Vilevile, wakulima na wafugaji **71,091** wamepatiwa mafunzo kuhusu kilimo bora na ufugaji endelevu ili kuongeza tija ya uzalishaji na kudhibiti migogoro inayotokana na mwingiliano katika matumizi ya ardhi.

**45. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari 2020, Maafisa Ustawi wa Jamii **711** wamejengewa uwezo wa namna ya kushughulikia mashauri ya watoto wanaokinzana na Sheria na waliofanyiwa vitendo vya ukatili. Aidha, makabati **1,500** yamenunuliwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 765.23** na kusambazwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuimarisha utunzaji wa nyaraka za huduma za ustawi wa jamii. Lengo ni kuwawezesha Maafisa hao kusimamia haki za watoto na kuelimisha jamii kushiriki katika kuwalinda watoto na kuwapa haki yao kikatiba ya kupata elimu.

**46. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya walimu **31,824** sawa na **asilimia 98** kati ya walimu **32,314** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu za ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika Shule za Msingi hususan Darasa la Kwanza na Darasa la Nne. Aidha, walimu **14,275** wa Shule za Sekondari sawa na **asilimia 77** ya walimu **18,540** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu za ufundishaji wa masomo ya Lugha, Hisabati na Elimu ya Viumbe. Vilevile, walimu 1,500 wamepatiwa mafunzo ya namna ya kutumia Kompyuta na kufanya matengenezo madogo ya vifaa vya TEHAMA.

**47. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya magari **155**, yamenunuliwa kwa ajili ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya magari hayo, magari

**15** yametolewa kwa Wakuu wa Mikoa, magari manne **(4)** kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, magari **26** kwa Makatibu Tawala Wasaidizi (Elimu), magari **24** kwa Wakuu wa Wilaya, magari **55** kwa Makatibu Tawala wa Wilaya na magari **13** yamenunuliwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri. Aidha, magari **20** yamenunuliwa kupitia Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya usimamizi wa taka na kuhudumia dampo na gari moja **(1)** limenunuliwa kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii.

**48. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya pikipiki **484** zimenunuliwa ambapo pikipiki **448** zimetolewa kwa ajili ya Maafisa Tarafa, pikipiki **20** zimetolewa kwa ajili ya Maafisa Ugani wa kilimo na pikipiki **16** zimetolewa kwa Maafisa Ustawi wa Jamii. Aidha, baiskeli **2,689** zimetolewa kwa Maafisa Ustawi wa Jamii zikiwemo jaketi **2,805** zinazoakisi mwanga kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za lishe kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### **Ushughulikaji wa Malalamiko ya Wananchi**

**49. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imeendelea kuimarisha na kusimamia madawati ya malalamiko katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2020, malalamiko **317** kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali yalikuwa yamepokelewa na kushughulikiwa. Malalamiko hayo yameshughulikiwa kupitia Kamati zilizoundwa kila Mkoa na Halmashauri kwa usimamizi wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri. Aidha, ziara za Viongozi wa Kitaifa, Mikoa na Wilaya zimetumika kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi. Utaratibu huu ni utekelezaji wa Ibara ya 8 (1)(C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayoelekeza Serikali kuwajibika kwa wananchi.

### **Usimamizi wa Fedha Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**50. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa fedha kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria

ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; na Kanuni zake pamoja na miongozo mingine ya Serikali. Lengo ni kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ili kuhakikisha kazi zinazotekelezwa zinalingana na thamani ya fedha iliyotumika (*Value for Money*).

**51. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamia matumizi ya fedha za Serikali kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma wa *Epicor* ambao umeunganishwa kwenye Halmashauri zote **185** ili kuleta uwazi, uwajibikaji na utawala bora katika matumizi ya fedha za umma. Kwa sasa mfumo wa *Epicor* umeunganishwa na Mfumo wa Mipango na Utoaji Taarifa (*PlanRep*) ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa ya mapato na matumizi.

**52. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI pia imefanikiwa kuandaa Mwongozo wa Uhasibu na Usimamizi wa Mapato ambao umesambazwa kwenye Halmashauri zote **185**. Hadi Februari 2020, Waweka Hazina na Wahasibu **370** wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya miongozo hiyo pamoja na ufungaji wa hesabu za mwisho za Halmashauri. Sambamba na utoaji wa miongozo, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unaofanywa kwa pamoja kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na wataalam umesaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**53. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 usimamizi wa fedha za umma umeimarika kutokana na kuongezeka kwa Halmashauri zinazopata Hati zinazoridhisha kutoka **asilimia 81** mwaka wa fedha 2015/16 hadi **asilimia 95** kwa mwaka wa fedha 2018/19, Hati zenye mashaka zimepungua kutoka **asilimia 19** katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi **asilimia 5** katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2018/19.

**54. Mheshimiwa Spika**, hatua za kinidhamu zimeendelea kuchukuliwa kwa watumishi wanaokiuka Sheria na Kanuni za utumishi wa umma. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020, jumla ya watumishi **26** wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu. Hatua hizo zimechukuliwa kwa lengo la kuimarisha maadili na nidhamu ya watumishi katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

### **Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Viongozi**

**55. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imekamilisha ujenzi wa Ofisi katika eneo la Mji wa Serikali-Mtumba. Mradi umetekelezwa kwa utaratibu wa *Forcé Account* na kupunguza gharama za mradi kutoka wastani wa **Shilingi bilioni 3.6** endapo Makandarasi wangetumika kutekeleza mradi hadi Shilingi bilioni 1.5. Viongozi Wakuu wote sita (**6**) wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI wamepata mahali pa kufanyia kazi pamoja na Wakurugenzi na watumishi wengine wapatao **100**.

**56. Mheshimiwa Spika**, vilevile katika mwaka wa fedha 2019/20, TARURA imekamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya TARURA Makao Makuu katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.1** kwa kutumia utaratibu wa *Force Account* katika kiwanja chenye ukubwa wa **ekari 3**. Kukamilika kwa Ofisi hizo kutaiwezesha TARURA kuokoa jumla ya **Shilingi milioni 552.64** kwa mwaka zilizokuwa zinatumiwa kama kodi ya pango. Aidha, watumishi wa TARURA watakuwa na mazingira yaliyoboreshwa ya kufanyia kazi.

**57. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Songwe na Njombe na Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Kigamboni na Nyamagana zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha, Ofisi **48** za Tarafa zimejengwa katika Mikoa ya Mtwara (5), Shinyanga (14), Kigoma (**5**) na Tanga (**24**). Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hiyo kutawezesha Mikoa na Wilaya hizo kuwa na Ofisi kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na wadau mbalimbali.

**58. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, nyumba nne (**4**) za Wakuu wa Mikoa zimejengwa katika Mikoa ya Mwanza,

Simiyu, Songwe na Njombe. Aidha, nyumba tatu (3) za Makatibu Tawala wa Mikoa zimejengwa katika Mikoa ya Simiyu, Songwe na Njombe. Vilevile, nyumba tatu (3) za Wakuu wa Wilaya zimejengwa katika Wilaya ya Malinyi, Gairo na Momba. Kadhalika nyumba 21 za Maafisa Waandamizi zimejengwa katika Mikoa ya Simiyu (nyumba 7), Singida (nyumba 2), Katavi (nyumba 10) na Songwe (nyumba 2).

**59. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Ofisi na nyumba hizo za viongozi ambao umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 4.18** umewezesha viongozi na watumishi wa Tawala za Mikoa kuwa na mahali pa kuishi na kufanyia kazi katika kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.

**60. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Halmashauri 10 za Wilaya za Mpanda, Wanging'ombe, Kibaha, Magu, Itigi, Pangani, Bumbuli, Ruangwa na Halmashauri za Miji za Tarime na Mbinga zilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 3.76** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa majengo ya utawala. Aidha, jumla ya Halmashauri 21 ziliendelea na ukamilishaji wa majengo ya utawala kwa kutumia bakaa ya mwaka wa fedha 2018/19 zikiwemo Halmashauri za Wilaya za Buchosa, Busokelo, Chalinze, Handeni, Kibiti, Madaba, Malinyi, Mbulu, Misungwi, Mpimbwe na Songwe; Halmashauri za Miji za Bunda, Ifakara, Kasulu, Kondo, Mafinga, Nanyamba, Newala na Nzega na Halmashauri za Manispaa za Kigamboni na Ubungo.

## **Huduma za Afya ya Msingi**

**61. Mheshimiwa Spika**, huduma za afya ya msingi ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa maisha ya watu kwa kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka kipaumbele katika uboreshaji wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya kwa kuweka mkazo katika kuimarisha afya ya mama na mtoto, kudhibiti magonjwa sugu kama vile Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na magonjwa yasiyoambukiza ambayo ndiyo chanzo kikuu cha vifo na kuchukua hatua za kutatua tatizo la uhaba wa miundombinu na watumishi wa sekta ya afya.



**62. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kusimamia ujenzi wa Hospitali za Halmashauri **71** na kuanza ujenzi wa Hospitali mpya **27** za Halmashauri. Ujenzi huo utakapokamilika utawezesha kuwa na Hospitali mpya **98** za Halmashauri ambazo zimejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 155.45**. Ujenzi huu umefanyika sambamba na ukarabati wa Hospitali 13 za Halmashauri uliogharimu **Shilingi bilioni 5.4**.

**63. Mheshimiwa Spika**, ujenzi huo utakapokamilika utaongeza idadi ya Hospitali za Halmashauri kutoka Hospitali **77** zilizokuwepo mwaka 2015 hadi Hospitali **175** kufikia Juni, 2020. Uboreshaji wa Hospitali za Halmashauri umesaidia kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi na kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa za Mikoa.

**64. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali inaendelea na ujenzi wa Vituo vya Afya **81**. Kati ya vituo hivyo, vituo **52** vinaendelea kujengwa na Serikali kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10.4 (Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.2)** na vituo **29** vinaendelea kujengwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa gharama ya **Shilingi bilioni 12.4**.

**65. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne, idadi ya Vituo vya Afya vya Serikali imeongezeka kutoka **535** mwaka 2015 hadi **968** Februari 2020. Hivyo, katika kipindi hicho cha miaka minne Serikali imefanikiwa kujenga na kukarabati Vituo vya Afya **433**. Mpango huo umesogeza huduma karibu zaidi kwa wananchi na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ya msingi ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga hususan maeneo ya vijijini.

**66. Mheshimiwa Spika**, Zahanati zilizoengwa na kukarabatiwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ni **38** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 5.40**. Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, Zahanati za Serikali zimeongezeka kutoka Zahanati **4,554** za Serikali mwaka 2015 hadi Zahanati **4,922** hadi Februari, 2020. Mkakati wa uboreshaji

wa Zahanati umesaidia kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi na kuwapunguzia wagonjwa umbali mrefu kufuata huduma.

### Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

**67. Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya unafanyika sambamba na kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Upatikanaji wa dawa umeongezeka kutoka **asilimia 30** mwaka 2015 hadi **asilimia 92** hadi Februari, 2020. Ufanisi huo umechangiwa na matumizi ya Mfumo wa Mshitiri (*Prime Vendor System*) katika Mkoa **26** ya Tanzania Bara ikiwa ni utaratibu wa kuondoa upungufu wa dawa pale unapotokea katika Bohari ya Taifa ya Dawa (MSD). Utaratibu wa mshitiri umewezesha vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali kununua dawa na vifaa tiba kutoka wauzaji binafsi walioteuliwa katika kila Mkoa pale inapothibitika dawa hizo kukosekana MSD. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 53.11** zinazojumuisha **Shilingi bilioni 27.11** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba na **Shilingi bilioni 26** kwa ajili ya ununuzi wa dawa muhimu.

### Afya na Usafi wa Mazingira

**68. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za Afya na Usafi wa Mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Lengo la mpango huu ni kuikinga jamii na magonjwa ya mlipuko ya kipindupindu, kuhara, kuhara damu, minyoo, kichocho, matende, trakoma na Polio. Hadi Februari 2020, idadi ya Kaya zenye vyoo bora imeongezeka kutoka **asilimia 51** hadi asilimia 62 na Kaya zisizokuwa na vyoo zimepungua kutoka **asilimia 2.6** hadi **asilimia 1.9** katika kipindi hicho. Mkoa iliyofanya vizuri katika utekelezaji wa Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira ni Njombe, Kilimanjaro, Iringa, Katavi na Dodoma. Serikali imetumia jumla ya **Shilingi milioni 350.0** kwa ajili ya kuboresha afya na usafi wa mazingira kupitia Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira.

**69. Mheshimiwa Spika**, mafanikio haya yamechangia kupunguza magonjwa ya mlipuko kama Kipindupindu ambapo kutoka Julai, 2019 hadi Februari, 2020 hakuna Halmashauri yoyote iliyoripoti kuwa na mlipuko wa Kipindupindu. Aidha, idadi ya wagonjwa wa kuhara imepungua kutoka wagonjwa **4,550** waliokuwepo Julai 2019 hadi wagonjwa **2,037** kufikia Februari 2020, kichocho kimepungua kutoka wagonjwa **4,112** hadi wagonjwa **2,204** na homa ya matumbo (Typhoid) imepungua kutoka wagonjwa **21,291** hadi wagonjwa **11,368**.

### **Huduma za Chanjo**

**70. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wadau wengine iliendesha kampeni ya utoaji wa chanjo ya Surua na Rubella iliyofanyika Oktoba, 2019 ambayo imegharimu **Shilingi bilioni 8.93** na kuwafikia watoto **4,410,095** sawa na **asilimia 113** ya watoto **3,920,040** waliolengwa. Kampeni hii ni moja ya mkakati wa kuwakinga watoto wenye umri chini ya miaka mitano dhidi ya magonjwa ya Rubella na Surua.

**71. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI vilevile imeendelea kutoa huduma za chanjo nyingine kwa kufuata utaratibu wa huduma tembezi, mkoba na kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari 2020, jumla ya watoto **8,663,356** wenye umri kati ya miezi 9 hadi 59 walipatiwa chanjo kati ya lengo la watoto **8,082,838** sawa na **asilimia 107.1**. Chanjo hizi hutolewa ili kuwalinda watoto wasipatwe na magonjwa nyemelezi yakiwemo nimonia, ngozi, macho na masikio ambayo yasipodhibitiwa mapema huchangia udumavu na vifo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

### **Udhibiti wa Magonjwa ya Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI**

**72. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria, Serikali imetoa mgao wa viaadudu vya kibailojia **lita 96,000** zenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.26**

na kusambazwa kwenye Mikoa yenye maambukizi makubwa ya malaria ambayo niKagera (**Lita 12,308**), Mtwara (**lita 11,536**), Dar es Salaam (**lita 11,400**), Lindi (**lita 9,048**), Geita (**lita 8,092**), Kigoma (**lita 7,616**). Aidha, Mikoa iliyokuwa na maambukizi ya ugonjwa wa Dengue ilipewa kipaumbele na kupatiwa dawa za kudhibiti ugonjwa wa Dengue ikiwemo Mikoa ya Tanga (**lita 7,040**), Mwanza (**lita 6,640**), Morogoro (**lita 6,240**), Dodoma (**lita 5,960**), Ruvuma (**lita 5,320**) na Tabora (**lita 4,800**). Mkakati huu umesaidia kudhibiti mazalia ya mbu wanaosababisha magonjwa ya Malaria na Dengue.

**73. Mheshimiwa Spika**, mikakati mingine iliyotekelezwa ni pamoja na kugawa vyandarua **5,681,712** vyenye dawa kwa mama wajawazito waliohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza na watoto wenye umri wa miezi **9** walioandikishwa na kupatiwa chanjo ya Surua Rubella katika vituo vya kutolea huduma za afya. Utekelezaji wa mikakati hiyo umepunguza kiwango cha maambukizi ya malaria Tanzania Bara kutoka **asilimia 14** mwaka 2015 hadi **asilimia 7.3** mwaka 2020. Aidha, vyandarua vingine 7,095,565 vinategemewa kusambazwa katika Mikoa 10 ya Dodoma (**1,508,754**), Tanga (**1,336,926**), Mbeya (**1,124,024**), Rukwa (**719,254**), Singida (**695,188**), Iringa (**573,400**), Songwe (**412,264**), Manyara (**304,673**), Kilimanjaro (**298,665**) na Njombe (**123,417**) kabla Juni, 2020. Mikoa hiyo imepewa kipaumbele kutokana na kuwa na vyandarua chini ya **asilimia 85** ya mahitaji.

**74. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imeendelea kutekeleza malengo ya kimkakati ya kudhibiti UKIMWI ya **asilimia 90** ya wanaoishi na UKIMWI wawe wanafahamu hali zao, **asilimia 90** ya watu wanaofahamu hali zao wapate dawa za kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (ARV) na **asilimia 90** ya wanaotumia ARV kutoambukiza wengine ifikapo mwaka 2020. Hadi Februari, 2020 Tanzania imefanikiwa kufikia **asilimia 77** ya lengo la kwanza, **asilimia 98** ya waliopima UKIMWI wanatumia dawa (ARVs) na **asilimia 91** wamefubaza virusi vya UKIMWI. Lengo la Mpango huu unaosimamiwa na Umoja wa Mataifa ni kuhakikisha maambukizi mapya ya UKIMWI yanadhibitiwa na watu wanaoishi na maambukizi wanapatiwa huduma ili kuzuia maambukizi mapya.

**75. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKI) zimeendelea kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ili kujenga uelewa miongoni mwa jamii kupima ili kutambua hali zao za kiafya na kwa walioambukizwa kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kupata ushauri wa wataalam na dawa. Aidha, utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na UKIMWI umeboreshwa kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyoko katika Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya. Elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI imesaidia kupunguza unyanyapaa katika jamii na kuongeza idadi ya wagonjwa wanaojitokeza kupima afya zao. Vilevile, elimu imesaidia kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa Mama kwenda kwa mtoto.

**76. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona (COVID – 19), Ofisi ya Rais TAMISEMI imeweza kuainisha na kuviandaa vituo **182** kwa ajili ya kuwatenga na kuwahudumia washukiwa na waliothibitika kuwa na ugonjwa wa Corona. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zimetambuliwa hoteli zinazotumika katika kutenga wageni na wenyeji wanaoingia nchini ili kuzuia kuenea kwa virusi hivyo vya Corona.

**77. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imetumia jumla **Shilingi milioni 184.85** kwa ajili ya mafunzo kwa watoa huduma za afya **200** kuhusu utambuzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu. Lengo la Serikali ni kuendelea kuwatambua wagonjwa wenye vimelea vya Kifua Kikuu na kuwapa matibabu kwa kuzingatia miongozo ya tiba ya Kifua Kikuu ili kuzuia maambukizi mapya hapa nchini

## **Huduma za Lishe**

**78. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKI) inasimamia afua za uboreshaji wa lishe kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kupunguza kiwango cha udumavu. Kwa mujibu wa takwimu zinazotokana na Utafiti wa Lishe wa Taifa wa mwaka 2018

hali ya udumavu imepungua kutoka **asilimia 34** hadi **asilimia 31.8** kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano.

**79. Mheshimiwa Spika**, ili kutatua changamoto hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeongeza rasilimali fedha za kutekeleza afua za lishe kutoka **Shilingi bilioni 15** kwa mwaka wa fedha 2018/19 hadi **Shilingi bilioni 16.8** kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, Ofisi yangu imeendelea kusaini mikataba ya utendaji na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kila mwaka kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika kutekeleza shughuli za lishe.

**80. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mkakati unaohakikisha wananchi wanatumia chumvi iliyowekewa madini joto. Jumla ya mashine **70** za kupima chumvi zimesambazwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika Wilaya ya Wete na Chakechake. Mashine hizo zimenunuliwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 97.24** sawa na wastani wa **Shilingi 1,389,200** kwa kila mashine. Vilevile, Serikali imesambaza vifaa vya kupimia chumvi (*Rapid Test Kits*) ambapo kiasi cha boksi **124** zenye vifaa **62,000** vimesambazwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini.

#### **Huduma za Watu Wenye Ulemavu**

**81. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Watu Wenye Ulemavu wapatao **10,035** wametambuliwa ambapo wanawake ni **6,100** na wanaume **3,935**; Watu Wenye Ualbino ni **2,400** wanawake **1,300** na wanaume **1,100**; Watu Wenye Ulemavu wa Viungo ni **5,233** wanawake **3,133** na wanaume **2,100**; Wasioona ni **510** Wanawake **203** na Wanaume **307**; Viziwi ni **1,500** wanawake **785** wanaume **715**; na Wenye Ulemavu wa Akili ni **392** wanawake **281** wanaume **111**. Watu hao Wenye Ulemavu wamepatiwa vifaa kama miwani, miamvuli, mafuta ya ngozi, fimbo nyeupe na baiskeli za miguu mitatu ili kuwawezesha kujimudu. Aidha, Kamati **5,024** za Watu Wenye Ulemavu zimeundwa katika Vijiji na Kamati **2,284** katika Mitaa. Lengo la Kamati hizo ni kusimamia masuala ya Watu Wenye Ulemavu na kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili katika maeneo yao.

## Huduma za Ustawi wa Jamii

**82. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha huduma na haki kwa makundi maalum, hadi Februari 2020, Serikali imefanikiwa kuwatambua jumla ya watoto **2,398,354** walio katika mazingira hatari wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 2.31** kwa kuwapatia huduma mbalimbali ikiwemo ujuzi kupitia vyuo vya VETA, chakula, ada, vifaa vya shule, mavazi, huduma za msaada wa kisaikolojia na kuwaunganisha na familia zao.

**83. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya mashauri **22,060** ya watoto waliofanyiwa ukatili na watoto **3,892** wanaokinzana na Sheria yamepokelewa na kushughulikiwa ambapo kati ya hayo mashauri **13,342** yametolewa hukumu. Aidha, jumla ya watoto **25,979** waliofanyiwa vitendo vya ukatili na watoto wanaokinzana na Sheria walipatiwa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii na kuunganishwa na familia zao. Vilevile, Kamati za Ulinzi na Usalama wa mwanamke na watoto zimeundwa katika Halmashauri.

**84. Mheshimiwa Spika**, Wazee **1,540,435** pia wametambuliwa na kati yao, Wazee **856,052** sawa na **asilimia 55.6** wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bila malipo na Wazee **684,383** sawa na **asilimia 44.4** wamepatiwa kadi za bima ya afya. Aidha, jumla ya mabaraza **171,655** ya Ushauri ya Wazee yameundwa kwa ajili ya usimamizi wa masuala ya wazee katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, jumla ya watu **4,338,752** wamepatiwa msamaha wa matibabu kutoka makundi mengine ambapo kati yao wanaume ni **1,424,891** na wanawake ni **2,913,861**. Jumla ya **Shilingi bilioni 6.33** zimetumika kugharamia matibabu bila malipo kwa makundi maalum yanayohusisha wazee wenye umri wa miaka zaidi ya **60** na wasio na uwezo, wafungwa, watoto chini ya miaka mitano, wajawazito, wasiojiweza kiuchumi, watu wenye magonjwa sugu na Watu Wenye Ulemavu.

## Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

**85. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020 wanachama **milioni 9.6** wameandikishwa sawa na kaya **milioni 1.6** katika Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa katika Mikoa 26. Kaya hizo zimechangia jumla ya **Shilingi bilioni 1.3** kupitia malipo yaliyofanyika kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya. Kati ya fedha hizo, Hospitali za Halmashauri zimekusanya **Shilingi milioni 407.06** na **Shilingi milioni 910.45** zimekusanywa kwenye Vituo vya Afya na Zahanati. Katika kipindi cha miaka minne kuanzia Novemba, 2015 hadi Februari, 2020 jumla ya wanufaika **milioni 28.08** katika Kaya **milioni 6.73** wanatumia kadi za CHF.

**86. Mheshimiwa Spika**, asilimia **80** ya fedha zinazokusanywa zinatumika kununua dawa, vifaa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Kupitia CHF iliyoboreshwa mapato yote yanakusanywa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (*Government Electronic Payment Gateway - GePG*) na fedha hizo zinatunzwa katika akaunti iliyoko Benki Kuu.

## Sekta ya Elimu

**87. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina jukumu la kusimamia utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini. Jukumu hilo linahusisha utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada, uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari. Lengo ni kuwa na jamii iliyoelimika yenye maarifa, uzalendo, ujuzi na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa viwanda uliofungamanishwa na maendeleo ya watu.

## Elimu ya Msingi

**88. Mheshimiwa Spika**, idadi ya Shule za Msingi imeongezeka kutoka **16,857** (Shule **15,802** za Serikali na Shule **1,055** za binafsi) mwaka 2016 hadi 17,771 (shule za Serikali **16,155** na shule za binafsi **1,616**) hadi Februari, 2020 sawa na ongezeko la shule



**914** katika kipindi cha miaka minne. Idadi ya wanafunzi pia imeongezeka kutoka **10,201,972** mwaka 2016 hadi **12,034,599** mwezi Februari, 2020 katika shule za Serikali na binafsi. Ongezeko la idadi ya wanafunzi linatokana na utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ulioanza kutekelezwa Desemba, 2015.

### **Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Msingi**

**89. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2020, wanafunzi **1,196,278** sawa na **asilimia 86.2** walikuwa wameandikishwa katika elimu ya awali ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanafunzi **1,389,913**. Kati ya hao, wanafunzi **1,018** ni wenye mahitaji maalum (***Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.3***). Katika kipindi cha miaka minne uandikishaji wa rika lengwa la watoto wa darasa la Elimu ya Awali umeongezeka kutoka **asilimia 45** mwaka 2015 hadi **asilimia 86.2** mwezi Machi, 2020.

**90. Mheshimiwa Spika**, wanafunzi wa Darasa la Kwanza walioandikishwa hadi Machi, 2020 ni **1,557,453** sawa na **asilimia 97.5** ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanafunzi **1,597,612**. Kati ya hao, wanafunzi 2,897 ni wenye mahitaji maalum (***Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.4***). Uandikishaji wa rika lengwa la watoto wa Darasa la Kwanza umeongezeka kutoka **asilimia 95** mwaka 2015 hadi **asilimia 97.5** mwezi Machi, 2020.

### **Uboreshaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi**

**91. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, vyumba **3,232** vya madarasa vimejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 30.32** katika Shule za Msingi na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa vilivyopo kutoka **122,487** mwaka 2019 hadi **125,719** hadi Februari, 2020. Aidha, **vyumba 224** vya madarasa vinaendelea kujengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi na Wadau wa Maendeleo. Ongezeko la vyumba vya madarasa limefanyika sambamba na ongezeko la madawati kutoka madawati **2,994,266** yaliyokuwepo mwaka 2019 hadi madawati **3,052,541** hadi Februari 2020. Miundombinu hiyo

ya madarasa na madawati imechangia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa vilivyokuwepo.

**92. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne, vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi vimeongezeka kutoka **108,504** mwaka 2016 hadi **125,719** mwezi Februari 2020, sawa na ongezeko la **asilimia 13.7**. Ongezeko la vyumba vya madarasa limefanyika sambamba na ongezeko la madawati kutoka madawati **3,024,311** yaliyokuwepo mwaka 2016 hadi madawati **8,095,207** kufikia Februari, 2020. Miundombinu hiyo ya madarasa na madawati imechangia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa vilivyokuwepo.

**93. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya matundu ya vyoo **7,922** yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10.62** katika Shule za Msingi na kuongeza idadi ya matundu ya vyoo yaliyopo kutoka **197,741** hadi **205,663** yakijumuisha vyoo vya wanafunzi wenye mahitaji maalum na vyumba maalum kwa ajili ya wanafunzi wa kike. Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusisitiza umuhimu wa kunawa mikono kwa kutumia vibuyu chirizi na vyanzo vingine vya maji vinavyopatikana. Aidha, matundu ya vyoo **571** yanaendelea kujengwa na yanatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2020. Ujenzi wa miundombinu ya vyoo umesaidia kuboresha afya na mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule.

**94. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusisitiza umuhimu wa kuwa na vyumba maalum kwa watoto wa kike na usambazaji wa taulo za kike. Aidha, shule zimeelekezwa kutumia sehemu ya fedha ya ruzuku ya uendeshaji wa shule iliyotengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa baridi itumike kununua taulo za kike. Vilevile, miundombinu ya shule inayojengwa inazingatia kuwa na chumba maalum cha wasichana ili kuboresha mazingira ya wanafunzi wa kike kupata muda kuhudhuria shule kwa siku zote za masomo.

**95. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetoa **Shilingi bilioni 9.1** kwa ajili ya ukamilishaji wa

maboma **364** ya nyumba za walimu yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi katika Shule za Msingi (***Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.5***) na kuongeza idadi ya nyumba za walimu zilizopo kutoka nyumba **161,007** mwaka 2015 hadi nyumba **161,371** hadi Februari, 2020. Ujenzi wa nyumba hizo umechangia kuboresha mazingira ya kuishi walimu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa lengo la kuinua kiwango cha taaluma. Aidha, mabweni matatu (**3**) ya Shule za Msingi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **80** kila moja yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 225** katika Mikoa ya Arusha, Iringa na Tanga kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**96. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia ujenzi wa shule nne (**4**) za Msingi katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Mtwara na Kigoma kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.82** sawa na **Shilingi milioni 706** kwa kila shule. Aidha, Shule ya Msingi Mwisenge iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imefanyiwa ukarabati mkubwa kwa jumla ya **Shilingi milioni 706**. Shule hizo za mfano zimejengwa na kuwekewa miundombinu yote muhimu ili zive mfano wa shule bora zitakazojengwa kila Mkoa kwa lengo la kuboresha mazingira ya shule.

**97. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya vituo shikizi **164** kati ya vituo **251** vimesajiliwa kuwa Shule za Msingi baada ya kukidhi vigezo. Vituo hivyo vilijengwa ili kuwaondolea wanafunzi kero ya kutembea umbali mrefu katika maeneo ambayo Vijiji viko mbali na shule. Mtihani wa Upimaji wa Darasa la Nne na Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba

**98. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **1,531,120** sawa na **asilimia 91.9** walifaulu Mtihani wa Upimaji wa Taifa wa Darasa la Nne kati ya wanafunzi **1,665,863** waliofanya mtihani huo. Aidha, wanafunzi **759,737** sawa na **asilimia 81.5** walifaulu Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba uliofanyika Septemba 2019, kati ya wanafunzi **933,369** waliofanya mtihani huo. Ufaulu wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba umeongezeka kutoka **asilimia 57** mwaka 2015

hadi **asilimia 81.5** mwaka 2019. Ongezeko la ufaulu limetokana na jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano za kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

### **Elimu ya Sekondari**

**99. Mheshimiwa Spika**, Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka **4,773** (shule za Serikali **3,601** na shule za binafsi **1,172**) mwaka 2016 hadi shule **5,001** (shule za Serikali **3,742** na shule za binafsi **1,259**) hadi Februari 2020. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la shule 228 katika kipindi cha miaka minne. Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka **1,806,955** mwaka 2016 hadi **2,023,457** hadi Februari 2020. Ongezeko la Shule za Sekondari limetoa fursa zaidi kwa wanafunzi wote wanaofaulu kuchaguliwa kujiunga na elimu ya Sekondari.

### **Usajili wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza**

**100. Mheshimiwa Spika**, jumla ya wanafunzi **759,737** sawa na **asilimia 100** ya waliofaulu walichaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza Januari, 2020. Kati ya hao, wanafunzi **666,206** sawa na **asilimia 87.7** wameripoti katika shule walizopangiwa. Kati ya wanafunzi walioripoti shuleni, wanafunzi wenye mahitaji maalum ni **1,341** (***Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 6***). Idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza imeongezeka kutoka **asilimia 60** ya waliofaulu mwaka 2015 hadi **asilimia 87.7** kufikia Machi 2020.

### **Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Shule za Sekondari**

**101. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuboresha miundombinu ya Shule za Sekondari ili kuwezesha wanafunzi waliochaguliwa kuendelea na masomo. Hadi Februari 2020, vyumba vya madarasa **2,593** vilikuwa vimejengwa na kukarabatiwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 27.73** katika mwaka wa fedha 2019/20. Idadi hiyo inajumuisha vyumba vya madarasa **273** vilivyojengwa kuanzia Desemba, 2019 hadi Februari, 2020 ili kuwawezesha wanafunzi **58,699** waliokosa nafasi ya kujiunga

na Kidato cha Kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa kupata nafasi. Aidha, vyumba vingine **1,089** vya madarasa vinaendelea kukamilishwa.

**102. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya matundu ya vyoo **2,601** yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.87** na mabweni **253** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **80** kila moja yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 8.22**. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni ujenzi wa nyumba za walimu **153**, ujenzi wa majengo ya utawala **64** na ujenzi wa Daharia (Hosteli) (**55** zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 kila moja ambapo miradi hiyo imegharimu **Shilingi bilioni 10.96**).

**103. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, ukamilishaji wa vyumba vya maabara za masomo ya sayansi **227** umefanyika kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.63**. Ujenzi huo, umeongeza idadi ya vyumba vya maabara kutoka **4,237** mwaka 2015 hadi **4,464** hadi Februari 2020, sawa na ongezeko la vyumba vya maabara **227**. Aidha, Shule **1,258** za Sekondari ambazo zimekamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara zimepatiwa vifaa vilivyogharimu **Shilingi bilioni 3.13** kwa ajili ya masomo ya Baiolojia, Fizikia na Kemia. Ujenzi wa vyumba vya Maabara na usambazaji wa vifaa vya maabara umewezesha wanafunzi wa Shule za Sekondari kusoma kwa vitendo masomo ya sayansi.

**104. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Shule za Sekondari Kongwe **9** zinaendelea kukarabatiwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.71** (**Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 7**). Aidha, katika kipindi cha miaka minne jumla ya Shule za Sekondari Kongwe **73** zimekarabatiwa kati ya shule **89** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 84.3** hadi Februari 2020. Ukarabati huo umefanyika kwa kuboresha miundombinu iliyokuwepo na kuongeza miundombinu mipya ili kuzirejesha katika hali ya awali. Ukarabati wa Shule za Sekondari Kongwe umesaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia pamoja na idadi ya wanafunzi.

## Mtihani wa Upimaji wa Kidato cha Pili na Mtihani wa Taifa Kidato cha Nne na Sita

**105. Mheshimiwa Spika**, katika Mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **514,251** walifaulu kati ya wanafunzi **571,137** waliofanya mtihani huo sawa na **asilimia 90.04**. Aidha, wanafunzi **340,914** kati ya wanafunzi **422,722** waliofanya mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne sawa na **asilimia 80.65**. Katika kipindi cha miaka minne, ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne umeongezeka kutoka **asilimia 69.8** mwaka 2015 hadi **asilimia 80.65** mwaka 2019.

**106. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Kidato cha Sita katika mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **78,666** sawa na **asilimia 98.6** ya wanafunzi **79,770** waliofanya Mtihani huo walifaulu ikilinganishwa na wanafunzi **34,787** waliofaulu sawa na **asilimia 98.9** ya wanafunzi **35,188** waliofanya mtihani huo mwaka 2015.

## Utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada

**107. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 169.67** kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 81.68** zimetumika katika Shule za Msingi (**Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.8**) na **Shilingi bilioni 87.99** kwa Shule za Sekondari (**Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.9**). Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 53.91** zimetumika kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji, **Shilingi bilioni 52.61** kwa ajili ya chakula cha wanafunzi, **Shilingi bilioni 21.82** kwa ajili ya fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na wa bweni na **Shilingi bilioni 41.33** kwa ajili ya posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi, Wakuu wa Shule za Sekondari na Maafisa Elimu Kata. Mpango wa Elimumsingi Bila Ada umewezesha ongezeko la wanafunzi hasa wanaotoka katika Kaya zenye kipato cha chini.

**108. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba, 2015 hadi Februari 2020, Serikali imetumia

jumla ya **Shilingi trilioni 1.01** kwa ajili ya kugharamia utoaji wa Elimumsingi Bila Ada kwa Shule za Msingi na Sekondari. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 460.63** zimetumika kwa Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 549.07** zimetumika kwa Shule za Sekondari. Mpango huu umewawezesha watoto wa Kitanzania kupata fursa ya masomo ya Shule za Msingi na Sekondari kutokana na kuondolewa kwa vikwazo vilivyokuwepo awali hasa michango kwa wanafunzi na ada. Aidha, Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ni utekelezaji wa Lengo la Nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) linalosisitiza "*Kuhakikisha elimu bora yenye usawa na kutoa fursa kwa watu wote kujiendeleza*".

### **Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

**109. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi 2020, wanafunzi **11,777** wameandikishwa kupitia mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Idadi hiyo imepungua kutoka wanafunzi **69,492** waliondikishwa mwaka 2016 hadi wanafunzi **11,777** mwezi Machi 2020, kunatokana na mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ambao umewawezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kila mwaka.

### **Elimu ya Watu Wazima**

**110. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Serikali kupitia Programu ya Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo Rasmi wa Shule, imewawezesha vijana **28,220** kupata mafunzo ya ujasiriamali ikilinganishwa na vijana **36,055** waliosajiliwa mwaka 2016. Aidha, vijana wenye umri wa miaka **14** hadi **19** wamewawezeshwa kupata mafunzo ya ujasiriamali, stadi za maisha pamoja na masomo ya ufundi yakiwemo ufugaji nyuki, samaki na kuku; ufundi seremala na uashi, utengenezaji mishumaa, sabuni, batiki, mafuta ya kujipaka, usindikaji vyakula pamoja na ushonaji. Walimu wapatao **216** wamejengewa uwezo wa utoaji wa mafunzo kwa kundi hilo la vijana ili kuwawezesha kupata ujuzi. Vilevile, jumla ya wanafunzi **9,939** wamesajiliwa na kuanza kusoma katika vituo **72** kwenye Mikoa nane (**8**) ya Kigoma, Tabora, Iringa, Njombe,

Mbeya, Songwe, Dar es Salaam, na Dodoma. Lengo la mpango huu ni kuwawezesha vijana kupata elimu ya ujasiriamali ili waweze kujajiri na kujipatia kipato.

## Elimu Maalum

**111. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI inasimamia pia utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hadi sasa, tunazo Shule **46** na Vitengo **682** kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hadi Machi 2020, shule na vituo hivyo vimeandikisha jumla ya wanafunzi **55,185** wa Shule za Msingi na wanafunzi **920** wa Shule za Sekondari. Idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum imeongezeka kutoka **49,655** walioandikishwa mwaka 2019 kutokana na kuongezeka kwa uelewa miongoni mwa jamii kuhusu haki za watoto wenye mahitaji maalum na kuboreshwa kwa miundombinu.

**112. Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi na Sekondari, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/20 imechapa na kusambaza rimu **7,664** katika Shule **416** za Sekondari. Aidha, karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu zimesambazwa kwa wanafunzi wasioona kwa gharama ya **Shilingi milioni 54.12** na nakala **53,104** ya vitabu vya kiada kwa Darasa la Kwanza hadi la Tano vilivyoandikwa kwa maandishi ya nukta nundu na vilivyoandikwa kwa maandishi makubwa (*large print*) zilisambazwa katika Shule za Msingi.

## Michezo Shuleni

**113. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeratibu na kusimamia michezo katika Shule za Msingi na Sekondari kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa. Katika mwaka 2019, mashindano ya michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA yalifanyika kitaifa katika Mkoa wa Mtwara na kuhusisha wanafunzi **2,662** na walimu **1,047** wa Shule za Msingi na wanafunzi **2,728** na walimu **965** wa Shule za Sekondari. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeshiriki mashindano ya Michezo ya Shule za Msingi na Sekondari kwa Nchi za Afrika Mashariki



yaliyofanyika mwezi Agosti, 2019 katika Mkoa wa Arusha. Michezo hiyo ilishirikisha jumla ya wanafunzi **4,448** kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (FEASSA) za Kenya, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na Tanzania yenyewe. Michezo iliyoshindaniwa ni pamoja na soka, netiboli, mpira wa wavu, mpira wa kikapu, mpira wa mikono, mpira wa magongo, raga, mpira wa meza, tenisi, kuogelea na riadha.

**114. Mheshimiwa Spika**, mashindano hayo yamekuwa chachu ya kukuza na kuibua vipaji vya watoto wetu katika umri mdogo ambapo kwa mfano timu ya UMISSETA Copa Coca Cola Tanzania ilifanikiwa kushiriki fainali za mashindano ya Copa Coca Cola Afrika yaliyofanyika mwaka 2019 nchini Kenya na kutwaa ubingwa wa Afrika kati ya nchi **11** zilizoshiriki fainali za mashindano hayo. Aidha, zaidi ya **asilimia 80** ya wachezaji wanaounda timu za soka kwa vijana wenye umri chini ya miaka **19** kwa wasichana na wavulana wametokana na mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA.

## **Matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari**

**115. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imeweka msisitizo wa matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ambayo ni muhimu katika uchumi wa viwanda. Hadi Februari 2020, jumla ya Shule **153** za Sekondari zinafundisha somo la TEHAMA kwa wanafunzi 36,101 wakiwemo wasichana **17,108** na wavulana **18,993**. Aidha, Shule za Sekondari zimejengewa uwezo wa kufundisha TEHAMA kwa kupatiwa Kompyuta **92,667** za Mezani, meza **5,346** za Kompyuta, Kompyuta Mpakato (*Laptops*) **46,207**, mashine za kudurufu **7,209**, *printer* **8,927**, *Projectors* **11,132**, Luninga (*Television*) **7,863** na Simu Janja (*Smart Phones*) **58,879**. Aidha, Shule za Msingi zimepatiwa Kompyuta za Mezani **3,148**, Kompyuta Mpakato (*laptops*) **3,570**, Mashine za Kudurufu **478**, *Printers* **603**, *Projectors* **891**, Televisheni **478** na Simu Janja (*Smart Phones*) **10,082**.

## Huduma za Kiuchumi na Uzalishaji Sekta ya Kilimo

**116. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, mashamba darasa **357** yalikuwa yameandaliwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 458.0** ili kuelimisha wakulima kwa vitendo kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya kilimo katika Halmashauri za Wilaya za Chunya, Geita, Hai, Iringa, Kilolo, Kiteto, Mbarali, Mufindi, Mbinga, Rombo, Sumbawanga, Ulanga, Mbozi; Halmashauri za Miji ya Mafinga, Njombe na Tarime na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani.

**117. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia ujenzi na ukarabati wa vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata katika Halmashauri za Majiji ya Arusha (katika Kata ya Themi) na Mbeya (katika Kata ya Igeyo) kwa gharama ya **Shilingi milioni 28.553**. Aidha, vituo vingine vimekarabatiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa (katika Kata ya Kibakwe) kwa gharama ya **Shilingi milioni 2.3** na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (katika Kata ya Kinyamwezi) kwa **Shilingi milioni 35**. Vituo hivyo vinatumika kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za kilimo kwa wakulima na wadau wengine wanaojihusisha na kilimo ili kuimarisha matumizi ya mbinu bora za kilimo.

**118. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya miche **3,115,240** ya mazao ya biashara ilikuwa imesambazwa kwa wakulima kwa gharama ya **Shilingi milioni 100.2**. Miche iliyosambazwa ni pamoja na miche **275,150** ya kahawa kwa gharama ya **Shilingi milioni 33.02** ambayo imesambazwa katika Halmashauri za Wilaya za Rombo, Karagwe, Mbozi na Halmashauri ya Mji wa Mbulu; miche **859,500** ya mikorosho imesambazwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 11.895** katika Halmashauri za Wilaya za Mbarali, Kongwa na Mpwapwa; miche **1,955,536** ya pareto kwa gharama ya **Shilingi milioni 19.4** katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu; na miche **25,384** ya Miparachichi imeandaliwa na kusambazwa katika Halmashauri za Wilaya ya Ileje na Ukerewe kwa gharama ya **Shilingi milioni 35.920**.

**119. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, maghala sita (**6**) ya kuhifadhia mazao yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Nyang'hwale, Ruangwa, Kiteto, Kilombero na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa gharama ya **Shilingi bilioni 7.39**. Aidha, masoko matano (**5**) ya mazao yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Geita, Ulanga, Muheza na Halmashauri ya Mji wa Kibaha ambayo yamegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 1.35**.

**120. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imezijengeta uwezo Halmashauri 7 za Wilaya za Hanang, Babati, Karatu, Meru, Siha, Hai na Kilindi kuhusu uandaaji wa mipango bora ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Wilaya kwa gharama ya **Shilingi milioni 48.9**. Lengo la mipango hiyo ni kuboresha mazingira wezeshi katika uwezekezaji, uzalishaji na tija katika sekta hizo kwa kuzingatia malengo ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini.

**121. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, jumla ya viwanja **11,903** vimepimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo uwekezaji na makazi katika Halmashauri za Manispaa za Ilemela (**viwanja 1,200**), Shinyanga (**viwanja 308**), Sumbawanga (**viwanja 254**), Iringa (**viwanja 253**), Halmashauri za Miji za Kahama (**viwanja 2,300**), Bariadi (**viwanja 1,446**), Nzega (**viwanja 779**), Kondoza (**viwanja 172**), Halmashauri za Wilaya za Msalala (**viwanja 400**), Busega (**viwanja 1,186**), Misungwi (**viwanja 71**), Magu (**viwanja 1,535**), Ukerewe (**viwanja 1,434**) na Halmashauri ya Jiji la Mbeya (**viwanja 565**).

**122. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe (*Master Plan*) wa Uendelezaji wa Jiji la Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mpango huo umekamilika na kuzinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuhakikisha uendelezaji wa Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya Nchi unafanyika kwa kuzingatia mpango huo. Aidha, Halmashauri nyingine **13** zikiwemo Majiji ya Mwanza na Arusha; Halmashauri za

Manispaa za Singida, Musoma, Mtwara/Mikindani, Iringa, Kigoma/Ujiji, Tabora na Songea; na Halmashauri za Miji za Bariadi, Korogwe, Kibaha na Tunduma zimekamilisha maandalizi ya Mipango Kabambe na kuitangaza kwa ajili ya uendelezaji wa ardhi katika maeneo hayo.

### C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI

#### Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

**123. Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) umeendelea kusimamia matengenezo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2020, TARURA ilikuwa imekamilisha matengenezo ya jumla ya kilomita **4,998.60** za barabara kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili ziweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka. Kati ya barabara hizo, kilomita **1,396.38** zimefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi, kilomita **730.19** zimefanyiwa matengenezo ya muda maalum na kilomita **2,872.03** zimefanyiwa matengenezo ya kawaida. Kazi nyingine zilizotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni ujenzi wa kilomita **31** za barabara za lami, madaraja **57**, makalvati **238** pamoja na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **9.3**. Ujenzi na matengenezo haya umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 154.13**

**124. Mheshimiwa Spika**, matengenezo, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya barabara umesaidia kuboresha usafiri na usafirishaji pamoja na utoaji huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Hata hivyo, mvua nyingi zinazoendelea kunyesha nchini zimeharibu sana miundombinu ya barabara za vijijini na mijini. Barabara hizo zilizoharibiwa na mvua zitafanyiwa matengenezo baada ya msimu wa mvua kumalizika. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini unaendelea kufanya matengenezo katika maeneo korofi katika kipindi hiki cha mvua ili barabara zilizoharibika ziendelee kupitika.

**125. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne, Serikali imetumia **Shilingi bilioni 799.37** kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara kupitia fedha za Mfuko wa Barabara. Fedha hizo zilitumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa **72,916.94**. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometa **1,538.12** zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na barabara zenye urefu wa kilometa **485** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Vilevile, madaraja makubwa **7**, madaraja madogo **225**, makalvati **7,168** yamejengwa na kukamilika.

### **Ujenzi wa Barabara Katika Mji wa Serikali Mtumba**

**126. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara katika Mji wa Serikali katika eneo la Mtumba zenye urefu wa kilometa **40**. Kati ya barabara hizo, barabara zenye urefu wa kilometa **11.2** zitakuwa za njia nne zitakazopitisha magari mawili kila upande na barabara zenye urefu wa kilometa **28.8** zenye njia mbili zitakazopitisha gari moja kila upande. Kwa mantiki hiyo, urefu halisi wa barabara zinazojengwa ni kilometa **51.2**. Miundombinu mingine itakayojengwa ni pamoja na: Makalvati makubwa **20**, makalvati madogo **52**, njia za watembea kwa miguu zenye upana wa **mita 1.5** kila upande wa barabara, njia za waendesha baiskeli zenye upana wa **mita 2.71** kila upande wa barabara, vituo vya kupakia na kushusha abiria **50**, taa za barabarani **739**, maeneo **mawili (2)** yenye taa za kuongoza magari, mifereji ya maji ya mvua yemye **kilometa 98** iliyojengwa kwa zege na makutano ya barabara ya mzunguko (*Roundabout*) **mbili (2)**. Mradi huo umeanza kutekelezwa Februari, 2020 kupitia Mkandarasi *China Henan International Group Co. Ltd (CHICO)* kwa gharama ya **Shilingi bilioni 89.13** zinazojumuisha ujenzi na usimamizi wa mradi. Kati ya fedha hizo, Serikali imekamilisha malipo ya awali ya kiasi cha **Shilingi bilioni 13.21** na mradi unaendelea kutekelezwa. Mradi umepangwa kukamilika katika kipindi cha miezi **18** kulingana na mkataba. Mradi huu unasimamiwa na Mhandisi Mshauri *Afrisa Consulting* kwa gharama ya **Shilingi milioni 998.55**. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuboresha eneo la Mji wa Serikali kwa miundombinu ya barabara na kuvutia

uwekezaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa **asilimia 100**.

**127. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, TARURA imeanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa **64** kwa fedha za ndani katika Halmashauri **64** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 33** ikiwa ni utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Miradi hii itakapokamilika itawezesha Makao Makuu ya Halmashauri na Miji Midogo kuwa na barabara za kiwango cha lami na kuboresha usafiri na usafirishaji pamoja na utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii.

#### **Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

**128. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya kilomita **47.59** za barabara ziliendelea kujengwa kwa kiwango cha lami katika Halmashauri za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam kwa gharama ya **Shilingi bilioni 85.67**. Kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa masoko **6** ya kisasa, ujenzi wa vizimba **33** vya kukusanyia taka ngumu na ujenzi wa vituo viwili (**2**) vya mabasi katika maeneo ya Kijichi na Mbagala.

**129. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Tano, mradi wa DMDP umepokea jumla ya **Shilingi bilioni 357.26** ambazo zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kilomita **187.59** za barabara kwa kiwango cha lami, kati ya lengo la kujenga kilomita **210**. Aidha, madaraja mawili ya Tuangoma na Mwanamtoti yamejengwa na kukamilika katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **14**, ujenzi wa masoko **9** ya kisasa maeneo ya Kijichi, Makangarawe, Mbagala Kuu, Kilakala, Kigilagila, Bomubom, Minazi Mirefu, Mbagala na Bwawani katika Halmashauri za Manispaa ya Temeke, Ilala na Kinondoni. Aidha, umeandaliwa Mpango Kabambe wa Mfumo wa Maji ya Mvua na Maji Taka katika Jiji la Dar es

Salaam kwa ajili ya kutatua changamoto ya mafuriko. Mpango huo utatekelezwa katika kipindi cha miaka **17** na ulianza kutekelezwa mwaka 2018 hadi mwaka 2035.

### **Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)**

**130. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, TARURA ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 92.57** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Miji ya Kimkakati (TSCP) katika Halmashauri za Majiji ya Tanga, Dodoma, Mbeya, Arusha na Mwanza na Halmashauri za Manispaa za Mtwara/Mikindani, Ilemela na Kigoma/Ujiji. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kilomita **89.22** za barabara kwa kiwango cha lami ambapo kilomita **85.82** zimekamilika, mifereji mikubwa ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **16.47** na ujenzi wa madaraja **6** ya waenda kwa miguu ambao umekamilika.

**131. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, ujenzi wa masoko mawili ya kisasa umekamilika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani. Utekelezaji wa mradi wa soko la kisasa katika Jiji Dodoma umefanyika katika kiwanja chenye ukubwa wa **ekari 27** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 14.64**. Mradi huo utanufaisha watoa huduma na wafanyabiashara **400**. Aidha, soko hilo litakuwa na uwezo wa kuegesha magari binafsi **600**, magari madogo ya abiria (daladala) **348** na malori **18**. Mradi huo utasaidia Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**132. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, TARURA imesimamia ujenzi wa Kituo Kikuu cha mabasi cha kisasa katika Jiji la Dodoma ambacho kitagharimu **Shilingi bilioni 24.03**. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia mabasi **100** na abiria **6,000** kwa wakati mmoja, kuegesha magari madogo **850**, bajaji **100** na pikipiki **150**. Aidha, kituo hicho kitakuwa na sehemu maalum kwa ajili ya abiria mahsusi (VIP) **80** kwa wakati mmoja. Aidha, kwa kipindi cha miaka mitatu, mradi wa TSCP umepokea jumla ya **Shilingi bilioni**

**211.39** kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara katika Miji minane (8) ya kimkakati.

### **Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Miji 18 (ULGSP)**

**133. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia TARURA imetekeleza Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Miji 18 (*Urban Local Government Strengthening Programme - ULGSP*) katika Halmashauri za Miji **6** ya Babati, Bariadi, Geita, Kibaha, Njombe na Korogwe na Manispaa **12** za Bukoba, Lindi, Iringa, Morogoro, Moshi, Mpanda, Musoma, Shinyanga, Singida, Songea, Sumbawanga na Tabora kwa fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi bilioni 120.35** zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa **kilometa 49.3**, ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya mabasi **5**, masoko **3** katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Iringa na Njombe; machinjio ya kisasa **matano (5)**; kituo kimoja cha malori katika Halmashauri ya Mji Bariadi na kituo kimoja cha daladala katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na maandalizi ya Mpango Kabambe (General Planning Scheme - GPS) katika miji **10**, ununuzi wa malori **10** ya kubeba taka ngumu, ununuzi wa mitambo ya kuchakata taka ngumu **2**, ununuzi wa vifaa vya kukusanya taka ngumu **31** na ukarabati wa madampo **mawili (2)** katika Halmashauri za Manispaa za Moshi na Shinyanga.

**134. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne Mradi wa ULGSP umetumia jumla ya **Shilingi bilioni 419.44** kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenye urefu **kilometa 175.34** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa vituo **11** vya mabasi, ujenzi wa masoko manne **(4)** katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Iringa na Miji ya Njombe na Korogwe; machinjio ya kisasa **matano (5)**, vituo **viwili (2)** vya malori katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Mji Bariadi; vituo **viwili (2)** vya daladala katika Halmashauri ya Manispaa za Singida na Morogoro, maandalizi ya Mpango Kabambe (General Planning Scheme-GPS) katika Miji **18**, ununuzi wa malori **34** ya kubeba taka ngumu, ununuzi wa mitambo **10**



ya kuchakata taka ngumu, ununuzi wa vifaa **231** vya kukusanyia taka ngumu, ukarabati wa madampo **matatu (3)** katika Halmashauri za Manispaa za Lindi, Moshi na Shinyanga na ujenzi wa bustani moja ya kupumzikia katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

### **Mradi wa Kimkakati Katika Maeneo ya Uzalishaji wa Kilimo (Agri-Connect Programme)**

**135. Mheshimiwa Spika**, TARURA kupitia mradi wa kimkakati wa kuboresha maeneo ya uzalishaji wa kilimo kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya inajenga barabara zenye urefu wa kilomita **87.6** kwa kiwango cha lami katika Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mufindi, Rungwe na Mbeya. Hadi Februari, 2020 jumla ya **Shilingi bilioni 40.7** zilikuwa zimetolewa ili kuanza utekelezaji wa mradi huo. Lengo la mradi huu ni kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yanayozalisha mboga mboga, chai na kahawa ili kuimarisha mnyonyoro wa thamani wa mazao ya kilimo na upatikanaji wa masoko. Hadi Februari 2020, taratibu za ununuzi zilikuwa zimekamili na mikataba ilikuwa imesainiwa. Makandarasi wapo hatua ya kupeleka vifaa vya ujenzi maeneo ya kazi. Kazi za ujenzi wa barabara hizo zinategemewa kukamilika ifikapo mwezi Mei 2021.

### **Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam (DART)**

**136. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam (DART) umeendelea kusimamia utoaji huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) inayohusisha barabara za Kimara-Kivukoni; Magomeni-Morocco na Fire-Kariakoo zenye urefu wa kilometa **20.9**. DART pia imeendelea na maandalizi ya kumtafuta mtoa huduma wa kudumu atakayekuwa na uwezo kutoa huduma ya mabasi **305** ikilinganishwa na mtoa huduma wa sasa ambaye ana uwezo wa kutoa huduma ya mabasi **140**. Zabuni ya kumpata mtoa huduma imetangazwa na taratibu za ununuzi zinaendelea. Vilevile, DART imeshughulikia ulipaji wa fidia na uhamishaji wa miundombinu

ya kijamii ambapo hadi Februari 2020, **Shilingi bilioni 28.84** zilitumika katika Awamu ya Pili ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) wenye urefu wa kilometa **20.3** ambao unahusisha barabara za Kilwa, Gerezani, Sokoine, Bandari, Chang'ombe na Kawawa.

**137. Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya Awamu ya Tatu ya mradi wa BRT utakaohusisha barabara za Azikiwe, Maktaba, Lindi, Shaurimoyo, Uhuru, Bibi Titi, Nyerere kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto zenye urefu wa kilometa **23.6** yanaendelea. Hadi Februari, 2020 malipo ya fidia ya **Shilingi bilioni 5.29** yalikuwa yamefanyika kwa wananchi **77** waliopisha utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya BRT. Miradi hii itakapokamilika itapunguza msongamano wa magari, kupunguza muda wa kusafiri, kuboresha mandhari na kuongeza tija katika utoaji wa huduma ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam.

**138. Mheshimiwa Spika**, DART imeimarisha usimamizi na matengenezo ya miundombinu katika vituo vikuu vitano (**5**) vya Kimara, Ubungo, Morocco, Gerezani na Kivukoni, vituo vidogo ishirini na saba (**27**) na madaraja ya waenda kwa miguu matatu (**3**). Vilevile, Ofisi ya Rais –TAMISEMI kupitia DART kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Serikali Mtandao inaendelea na usanifu wa mfumo wa ukusanyaji nauli (*Automatic Fare Collection System - AFCS*) na ununuzi wa vifaa vya mfano yakiwemo mageti sita (**6**) na kadi janja (*smart cards*) kwa ajili ya ukusanyaji wa nauli na kudhibiti upotevu wa mapato.

## Tume ya Utumishi wa Walimu

**139. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya Utumishi wa Walimu imepokea na kushughulikia rufaa **106** zinazohusu masuala ya utumishi wa walimu. Aidha, vikao vya Kamati **208** vya kisheria vimefanyika katika ngazi ya Wilaya na kuwezesha walimu **2,591** kuthibitishwa kazini, walimu **112** walibadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza, walimu **123,444** wamepandishwa vyeo na mashauri ya nidhamu **399** yalitolewa uamuzi. Mafanikio haya yamesaidia

kuongeza ari ya utendaji kazi wa walimu ili kuinua kiwango cha taaluma katika Shule za Msingi na Sekondari.

**140. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Makatibu **139** wa Wilaya wamejengewa uwezo kuhusu masuala ya utumishi wa walimu, upandishwaji vyeo na usimamizi wa nidhamu. Mafunzo hayo yataongeza ufanisi katika kuimarisha usimamizi wa walimu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, watumishi **80** wa Tume ya Utumishi wa Walimu wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa vihatarishi katika utendaji wa kila siku wa kazi za Tume. Mkakati huo utawezesha Tume kuchukua hatua za haraka za kuondoa vihatarishi hivyo ili kufikia malengo ya utekelezaji wa majukumu yake.

### **Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo**

**141. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo kimekamilisha ujenzi wa kumbi mbili za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **1,008** kwa kutumia mapato ya ndani ya Chuo. Aidha, viti **504** visivyohamishika vimefungwa katika darasa moja lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **504**. Ujenzi wa miundombinu hiyo umeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa wanachuo. Vilevile, hadi kufikia Februari 2020, Chuo cha Serikali za Mitaa kimevuka lengo kwa kudahili wanafunzi **7,484** kati ya lengo la kudahili wanafunzi **5,000** sawa na **asilimia 149.68**.

**142. Mheshimiwa Spika**, Chuo kimefanikiwa kuanzisha Shahada ya Kwanza ya Menejimenti ya Utawala katika Serikali za Mitaa ambayo imepokea wanafunzi **20** katika mwaka wa masomo wa 2019/20 ili kukidhi mahitaji wa wataalam wa Menejimenti na Utawala katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mkakati huo unalenga kukitangaza Chuo ndani na nje ya nchi ili watu wengi zaidi wavutiwe kusoma katika Chuo cha Serikali za Mitaa ambacho ni cha kipekee katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**143. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Chuo kimefanikiwa kupeleka masomoni jumla ya watumishi **55** kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Kati ya hao, watumishi **14** wamekwenda kusoma Shahada ya Uzamivu; Watumishi **tisa (9)** Shahada ya Uzamili; Watumishi wanne **(4)** Shahada ya Kwanza na watumishi **28** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi **724** kutoka katika Halmashauri **14** za Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Iringa, Singida, Dar es Salaam na Dodoma wamepatiwa mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango na bajeti, usimamizi wa mazingira, usimamizi wa fedha za Serikali za Mitaa na masuala ya utawala bora.

### **Shirika la Elimu Kibaha**

**144. Mheshimiwa Spika**, malengo ya kuanzishwa kwa Shirika la Elimu Kibaha ni kupambana na maadui watatu wa maendeleo ambao ni **Ujinga, Umaskini** na **Maradhi**. Hivyo, Shirika linasimamia utoaji wa huduma za elimu kupitia Shule za Msingi na Sekondari na huduma za afya na maendeleo ya jamii kupitia Hospitali ya Rufaa Tumbi na Chuo cha Maendeleo ya Jamii.

**145. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika la Elimu Kibaha limewezesha kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi **2,796** na kutoa huduma za maktaba kwa wadau **16,050** wa ndani na nje. Shirika limefanikiwa kukarabati miundombinu ya Shule ya Sekondari Kibaha uliohusisha ujenzi wa uzio, ukarabati wa mabweni matatu yenye uwezo wa kulaza jumla ya wanafunzi **660**, ujenzi wa jengo la utawala, jengo la maktaba, jengo la maabara, jengo la kilimo, jiko na bwalo na madarasa mawili ya Kidato cha Kwanza uliogharamu **Shilingi bilioni 1.18**. Ukarabati uliofanyika umesaidia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi.

**146. Mheshimiwa Spika**, kitaaluma, Shule zinazomilikiwa na Shirika zimeendelea kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa. MATHALANI, Shule ya Sekondari Kibaha imefanya vizuri katika Mtihani wa Taifa wa mwaka 2019 kwa kufaulisha **asilimia 100**

ya wanafunzi **172** waliofanya mtihani wa Kidato cha Sita. Aidha, jumla ya wanafunzi **59** walifaulu Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Kidato cha Nne kwa mwaka 2019 sawa na takribani **asilimia 87** ya wanafunzi **68** waliofanya mtihani huo. Vilevile, wanafunzi **119** sawa na asilimia **99** wa Shule ya Msingi Tumbi wamefaulu Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba wa mwaka 2019 kati ya wanafunzi **120** waliofanya mtihani huo.

**147. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika limetoa elimu ya ujasiriamali kwa wanufaika **695** katika fani za ufugaji, kilimo, ufundi wa umeme wa majumbani, uungaji na uundaji vyuma, uashi na useremala, ufundi wa mitambo na magari, hoteli na ushonaji. Mafunzo hayo yametolewa kupitia Chuo cha Maendeleo ya Jamii kinachomilikiwa na Shirika. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana kupata elimu ya ujasiriamali ili waweze kutekeleza miradi itakayokuza kipato na ajira.

**148. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Shirika lilikuwa limetoa huduma za afya kwa wagonjwa **36,500** kupitia Hospitali ya Rufaa ya Tumbi. Kati ya hao, wagonjwa **18,592** walitibiwa na kuondoka na wagonjwa **17,908** walilazwa na kutibiwa. Aidha, Hospitali imehudumia majeruhi **1,336** kutokana na ajali wakiwemo wanawake **364** na wanaume **972**.

**149. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Shirika limefanikiwa kufunga mtambo mpya wa *X-Ray* wenye thamani ya **Shilingi milioni 428** kwa ufadhili wa nchi ya Korea Kusini. Aidha, mashine mbili za kutolea dawa ya usingizi zimesimikwa ili kuboresha huduma za upasuaji na matibabu ya dharura. Vilevile, Shirika limekarabati jengo la watoto na wodi Daraja la I na II kwa gharama ya **Shilingi milioni 42.56**.

**150. Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha upatikanaji wa dawa, Shirika limeanzisha duka la dawa la Hospitali kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa. Kwa sasa hali ya upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa Hospitalini hapo ni **asilimia 90**.

## Shirika la Masoko ya Kariakoo

**151. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato ya Shirika ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato. Matumizi ya mifumo hiyo yamechangia kuimarisha makusanyo kutoka **Shilingi milioni 263.04** kwa mwezi hadi **Shilingi milioni 285.89** kwa mwezi sawa na **Shilingi bilioni 3.43** kwa mwaka.

**152. Mheshimiwa Spika**, mapato yanayokusanywa yamewezesha Shirika kuimarisha uwekezaji ambapo wafanyabiashara **1,673** wamepata vibanda vya biashara na wanaliingizia Shirika mapato. Wafanyabiashara hao wanajumuisha wapangaji wa Ofisi na maeneo ya wazi **121**, wapangaji wa maduka **205**, wapangaji wa mbao katika soko dogo **231**, wafanyabiashara katika soko la wazi **575** na eneo la shimoni ndani ya soko wafanyabiashara wadogo **541**. Aidha, Shirika limefanya mapitio ya Mpango wa Biashara ili kupanua fursa za uwekezaji ndani na nje ya Jiji la Dar es Salaam.

**153. Mheshimiwa Spika**, Shirika limefanikiwa kuimarisha hali ya usafi na mazingira ndani na nje ya soko kwa kutekeleza mikakati ya uondoshaji wa taka. Aidha, ukarabati mdogo wa soko umefanyika kwa gharama ya **Shilingi milioni 64.5** hasa sehemu ya shimoni kwa kufunga mifumo ya hewa (viyoyozi) kwa kuzingatia idadi kubwa ya watu wanaotumia soko hilo. Mikakati hiyo imesaidia kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa watumiaji.

## Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

**154. Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2020, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imefanikiwa kukusanya marejesho ya mikopo kiasi cha **Shilingi milioni 227.58** kutoka kwenye Halmashauri zilizokopeshwa mikopo kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, michango ya akiba kiasi cha **Shilingi milioni 97.26** imekusanywa kutoka kwenye Halmashauri ili kujenga uwezo wa Bodi kutoa mikopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**155. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imefanikiwa kutoa mkopo wa **Shilingi milioni 550.00** kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la biashara ambalo litakuwa na ukumbi wa mikutano na biashara nyingine na **Shilingi milioni 520.0** zimekopeshwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa ajili ya kuendeleza uwanja wa michezo wa Halmashauri.

**156. Mheshimiwa Spika**, utoaji wa mikopo umefanyika sambamba na utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wataalam wa Halmashauri **22** za Mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam na Pwani kuhusu uandaaji wa maandiko ya miradi ya maendeleo na kuimarisha usimamizi wa miradi iliyopatiwa mikopo ili kudhibiti viashiria vinavyoweza kukwamisha malengo ya miradi. Lengo la Bodi ni kujenga uwezo wa Halmashauri ili ziweze kuandaa maandiko ya miradi yatakyokidhi gizeo vya kupata mkopo.

#### **D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

**157. Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa kuzindua Bunge mwaka 2015 na maelekezo ya viongozi wengine wa Kitaifa, Sera, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati ya Taasisi.

#### **Ofisi ya Rais-TAMISEMI**

**158. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatujaji wa Madaraka kwa Umma (*D by D*);
- ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Ada;
- iv) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- v) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;
- vi) Kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kuwaongezea ujuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi;
- vii) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya Biashara na Uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;
- viii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ix) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais–TAMISEMI ikiwa ni pamoja na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;



x) Kuratibu shughuli za utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI;

xi) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, elimu inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

xii) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, na Halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri 30 ambazo zimeelekezwa na Serikali kuhamia katika maeneo yao ya utawala; na

xiii) Kusimamia matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

### **Tawala za Mikoa**

**159. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tawala za Mikoa zitatekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;

ii) Kuratibu utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan katika usimamizi wa afya ya msingi, elimu ya msingi na sekondari, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, lise na ustawi wa jamii;

iii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa majengo ya Ofisi na nyumba za makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya , Makatibu Tawala Wasaidizi, Maafisa Tarafa na watumishi waandamizi;

iv) Kuratibu zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 wa Rais, Wabunge na Madiwani uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2020;

v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi na Sera nyingine za kisékta ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi;

- vi) Kusimamia rasilimaliwatu na fedha katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vii) Kuratibu mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- viii) Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ix) Kuratibu uanzishwaji wa viwanda kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara mijini na vijijini, uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati, na vikubwa kwa kutumia malighafi zilizopo;
- x) Kutatua migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xi) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali za uchumi katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xii) Kuendelea kusimamia na kuimarisha Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xiii) Kuratibu uanzishaji wa viwanda vya kuchakata/kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo;
- xiv) Kufanya mapitio ya mipango mikakati ya Tawala za Mikoa na kuratibu mapitio ya mipango mikakati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xv) Kuratibu uendelezaji wa maeneo maalum ya shughuli za kiuchumi na uwekezaji;
- xvi) Kuratibu utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake (4%), Vijana (4%) na Watu Wenye Ulemavu (2%);
- xvii) Kuhamasisha na kusimamia kilimo cha mazao ya kipaumbele; na

Kuandaa na kuboresha wasifu wa uwekezaji (*Investment Profile*) na Miongozo ya Uwekezaji (*Investment Guide*).

## Mamlaka za Serikali za Mitaa

**160. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- i) Kusimamia ulinzi na usalama;
- ii) Kushiriki katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2020;
- iii) Kuimarisha na kubuni mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani;
- iv) Ukamilishaji na kuanza ujenzi wa majengo ya Ofisi, nyumba za makazi ya viongozi na watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo **Halmashauri 30** zilizohamia katika maeneo yao ya utawala;
- v) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi katika sekta zote hususan kujenga na kuboresha Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya, Zahanati, maabara za masomo ya sayansi, nyumba za watumishi, matundu ya vyoo, na yumba vya madarasa;
- vi) Kusimamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Ada katika Shule za Msingi na Sekondari;
- vii) Kukamilisha ujenzi wa miradi viporo ya miundombinu mbalimbali ya huduma za kijamii;
- viii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji kwa kuhakikisha mikutano ya kisheria inafanyika na taarifa za mikutano hiyo zinawekwa katika maeneo ya wazi na katika tovuti za kila Halmashauri hasa taarifa za mapato na matumizi.

- ix) Kubuni na kutekeleza miradi ya kimkakati itakayosaidia kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri;
- x) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuimarisha utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xi) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa na maeneo ya wafanyabiashara wadogo (Machinga);
- xii) Kusimamia na kuratibu shughuli za uendelezaji Miji na Vijiji; na
- xiii) Kusimamia utunzaji wa mazingira na shughuli mtambuka.

## E. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OR-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

*161. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA kupitia Mfuko wa Barabara umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i) Matengenezo ya barabara za Wilaya zilizopo vijijini na mijini zenye urefu wa kilometa **23,175.11**. Kati ya hizo, kilometa **14,104.86** ni matengenezo ya kawaida, kilometa **6,094.52** ni matengenezo ya maeneo korofi na kilometa **2,975.73** ni matengenezo ya muda maalum.

ii) Ujenzi na ukarabati wa madaraja **80**, makalvati **2,052** na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa **79.9**. Ujenzi wa barabara urefu wa kilometa **35.3** kwa kiwango cha lami na ukarabati urefu wa kilometa **321** kwa kiwango cha changarawe.

Katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi bilioni 275.03** zimetengwa kupitia Mfuko wa Barabara kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo pamoja na kazi za ufuatiliaji na utawala.

## Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu Katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP)

**162. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam umetengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 186.8** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa **47.59** kwa kiwango cha lami kwa mikataba na Makandarasi inayoendelea;

ii) Kuanza ujenzi wa barabara ya Nzasa-Kilungule-Buza (kilomita **7.6**),Ulongoni-Bangulo-Kinyerezi (kilomita **7.5**) na Magomeni Mapipa- Urafiki (kilomita **7.31**);

iii) Kuanza ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa **11.7** kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni;

iv) Kuendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa **26**;

v) Kukamilisha ujenzi wa masoko sita (**6**) ya Kilakala, Kigilagila, Bomubom, Minazi Mirefu, Mbagala na Bwawani;

vi) Kuandaa Mpango wa Uendelezaji Ukanda wa Mabasi Yaendayo Haraka (*Intergrated Transport and Land Use Planning along BRT Corridor*);

vii) Kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani (*Local Government Revenue Collection Information System*) uliunganishwa na mfumo wa kijiografia wenye taarifa muhimu za vyanzo vya mapato; na

viii) Ununuzi wa vifaa vya kufanyia usafi wa miundombinu ya barabara na mifereji ya maji ya mvua.

### **Mradi wa Kuboresha Barabara Katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (*Agri-Connect Programme*)**

**163. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, TARURA imetengewa **Shilingi bilioni 35.5** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuboresha Barabara katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo utakaohusisha ujenzi wa barabara katika baadhi ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Maeneo ambayo barabara hizo zitajengwa yatakuwa ni yale yenye miradi mingine ya uendelezaji wa kilimo inayofadhiliwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya na kuratibiwa na Wizara ya Kilimo. Lengo la mradi huu ni kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yanayozalisha mboga mboga, chai na kahawa ili kuimarisha mnyonyoro wa thamani wa mazao na upatikanaji wa masoko.

### **Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (*Roads to Inclusion and Socio-Economic Opportunities - RISE*)**

**164. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaanza utekelezaji wa Mradi mpya wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii. Mradi utatekelezwa katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara ambapo kazi za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zitafanyika katika Mkoa wa Iringa na kazi ya matengenezo ya maeneo korofi na matengenezo ya kawaida yatafanyika kwenye Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Morogoro, Rukwa, Katavi, Songwe, Tanga, Pwani, Dodoma, Mtwara, Ruvuma na Lindi. Mradi huu utagharimu jumla ya **Shilingi bilioni 817.25** sawa na **Dola za Marekani milioni 350** kwa kipindi cha miaka sita (6) kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2025/26 ambazo Serikali inatarajia kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu una vipengele vinne ambavyo ni ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini, uimarishaji wa Taasisi, usimamizi wa rasilimaliwatu na ufuatiliaji wa miradi na ushirikishwaji wa jamii. Lengo la mradi huu ni kuboresha ujenzi na upitikaji wa barabara ili kusaidia kuinua kipato cha watu wanaoishi vijijini katika maeneo yaliyoteuliwa na kujenga uwezo wa usimamizi

endelevu wa barabara za vijijini. Katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi bilioni 28.0** zimetengwa ili kuanza utekelezaji wa mradi.

**165. Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukuaji wa miji nchini unaoenda sambamba na uhitaji wa miundombinu ya msingi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika mwaka wa fedha 2020/21 itaanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi mpya ujulikanao kama *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness Project* (TACTIC). Mradi huu utahusisha Halmashauri **45** za Majiji, Manispaa na Miji. Lengo la mradi huu ni kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ya uwekezaji katika maeneo ya mijini. Mradi huu ni muendelezo wa Mradi wa Miji ya Kimkakati (TSCP) na Mradi wa Kuimarisha Miundombinu katika Halmashauri za Miji (ULGSP) ulioharamiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

### **Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Katika Jiji la Dar es Salaam (DART)**

**166. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam utatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kusimamia utoaji wa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) katika Jiji la Dar es Salaam;

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa mpango kazi juu ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa miundombinu ya barabara Awamu ya Tatu;

(iii) Kuanza taratibu za kuwapata Wazabuni wa kutoa huduma za kusafirisha abiria, Mkusanyaji wa Nauli na Meneja wa Mfuko wa Fedha kwa Awamu ya Pili na ya Tatu ya mradi;

(iv) Kuimarisha makusanyo ya mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(v) Kufanya mapitio ya michoro kwa ajili ya usimikaji wa mtandao wa mawasiliano wa Wakala (DART – net);

(vi) Kuhuisha Kanuni na Sheria Ndogo ili ziendane na mahitaji ya uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka; na

(vii) Usimamizi, uendeshaji na ufuatiliaji wa mashauri mahakamani na usimamizi wa mikataba ya Wakala.

### **Tume ya Utumishi wa Walimu**

**167. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kusimamia maadili na kutoa uamuzi wa mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko ya walimu katika Shule za Msingi na Sekondari;

(ii) Kusimamia upangaji na msawazo wa Walimu kwa Shule za Msingi na Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Tume Makao Makuu Jijini Dodoma;

(iv) Kuratibu upandishwaji wa madaraja kwa walimu;

(v) Kuimarisha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusimamia masuala ya walimu nchini;

(vi) Kuelimisha wadau kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu;

(vii) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wa Tume Makao Makuu na kwenye Wilaya pamoja na kuendeleza rasilimaliwatu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi; na

(viii) Kufanya mapitio na kuandaa Mpango Mkakati wa Tume kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2024/25.



## Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo

**168. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kudahili wanafunzi **7,000** wakiwemo wanafunzi **5,800** Kampasi ya Hombolo na wanafunzi **1,200** katika Kampasi iliyoko Dodoma Mjini;
- ii) Kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **250** katika Kampasi ya Hombolo;
- iii) Kukamilisha ujenzi wa daharia (hostel) ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **200** kwa kuweka samani;
- iv) Ujenzi wa darasa na Ofisi Awamu ya Kwanza katika Kampasi ya Dodoma Mjini; na
- v) Ujenzi wa jengo la utawala Awamu ya Kwanza katika Kampasi ya Hombolo.

## Shirika la Elimu Kibaha

**169. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kuendelea kutoa huduma za afya, kinga na tiba katika Hospitali ya Tumbi;
- ii) Kuendelea kutoa elimu ya uuguzi na utabibu kwa wanafunzi **430** katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;
- iii) Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi **1,758** wa Sekondari na wanafunzi **926** wa Shule ya Msingi;

- iv) Kuendelea kutoa huduma za maendeleo ya jamii ili kupunguza umaskini kwa kutoa mafunzo ya ufundi, ujasiriamali, kilimo na mifugo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha na shamba darasa la mifugo na mazao;
- v) Kuongeza uzalishaji wa maji tiba kwa ajili ya matumizi ya Hospitali;
- vi) Kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa jamii;
- vii) Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa Hospitali ya Tumbi;
- viii) Kujenga maabara ya Baiolojia, Maarifa ya Nyumbani (*Home Economics*) na mabweni katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha; na
- ix) Kukarabati madarasa ya Shule ya Msingi Tumbi.

### **Shirika la Masoko ya Kariakoo**

**170. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Masoko ya Kariakoo litatekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu katika maeneo mbalimbali ya Shirika ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara;
- ii) Kuendelea na ujenzi wa Soko la jumla katika eneo la Mbezi *Beach* (Makonde); na
- iii) Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ndani ya Shirika la Masoko ya Kariakoo.

### **Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**171. Mheshimiwa Spika**; katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo;
- ii) Kuendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu kuandaa maandiko ya miradi ya maendeleo itakayokidhi vigezo vya kukopesheka;
- iii) Kuimarisha ufuatiliaji wa urejeshwaji wa mikopo na uwasilishwaji wa michango kutoka Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi; na
- iv) Kubuni vyanzo vipya vya mapato.

## **F. MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

### **Sekta ya Afya**

**172. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika sekta ya afya:-

- i) Ujenzi wa wodi tatu (**3**) katika kila Hospitali **67** za Halmashauri zinazoendelea kujengwa ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 32.50** kwa kazi hiyo. Kukamilika kwa ujenzi wa wodi hizo kutawezesha Hospitali hizo kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa;
- ii) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali mpya **27** za Halmashauri ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 27.00**. Hospitali hizo zinajengwa katika Halmashauri za Wilaya za Karatu, Chalinze, Kondoa, Kongwa, Mbogwe, Biharamulo, Nsimbo, Kigoma, Kakonko, Liwale, Serengeti, Sengerema, Mbeya, Kilombero, Kaliua, Babati, Mvomero, Newala, Madaba, Kwimba, Msalala, Ikungi, Handeni, Mkinga, Halmashauri ya Mji wa Tunduma na Halmashauri za Manispaa za Sumbawanga na Tabora;
- iii) Ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati **3** katika kila Halmashauri ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 27.75**,

Kipaumbele kitakuwa ni kukamilisha maboma ya Zahanati zilizoanza kujengwa kwa nguvu za Wananchi;

iv) Ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali **67** za Halmashauri ili kuziwezesha kuanza kutoa huduma. Katika mwaka wa fedha 2020/21, zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 32.50** kwa kazi hiyo;

***Mchanganuo wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya na upatikanaji wa vifaa tiba umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 10.***

v) Mpango wa Uimarishaji wa Huduma za Afya ya Msingi kwa Matokeo umetengewa **Shilingi bilioni 128.91** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya afya, ununuzi wa vifaa tiba, ajira za watumishi wa afya kwa mkataba, kujenga uwezo wa watumishi wa sekta ya afya na usimamizi wa mradi.

### **Sekta ya Elimu**

**173. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika sekta ya elimu:-

i) Ugharamiaji wa Elimu msingi Bila Ada ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 298.13** kwa Shule za Msingi na Sekondari. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 137.63** zitatumika kwa Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 160.49** zitatumika kwa Shule za Sekondari. Bajeti hiyo ni sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 9.6** ikilinganishwa na Bajeti ya **Shilingi bilioni 288.48** iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Ongezeko la Bajeti limetokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika Shule za Msingi na Sekondari (***Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 11***);

ii) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi kwenye Halmashauri **184** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 26.10** zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo (***Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 12***). Miradi itakayokamilishwa ni ile iliyoanza kutekelezwa kwa nguvu za wananchi ili ianze kutoa huduma;

iii) Ukamilishaji wa ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi **1,411** katika Shule za Sekondari kwenye Halmashauri **184** ambapo zimetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 42.33** (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 13*). Lengo ni kuwezesha ukamilishaji wa maabara hizo ili zianze kutumika kwa ajili ya masomo ya sayansi katika Shule za Sekondari; na

iv) Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu umetengewa **Shilingi bilioni 73.6** kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari kwenye Halmashauri 184 nchini (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 14*). Aidha, Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LANES) imetengewa **Shilingi bilioni 9.34** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **150** kwa ajili ya elimu ya awali, ujenzi wa mabweni **10** katika Shule zenye watoto wenye mahitaji maalum, kujenga uwezo wa Walimu kufundisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, ununuzi wa vifaa vya watoto wenye mahitaji maalum na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA.

### **Sekta ya Miundombinu**

*174.Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeweka kipaumbele cha ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambao utahusisha utekelezaji wa kazi zifuatazo:-

i) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita **23,531**, madaraja **80**, makalvati **2,052** na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **79.9** ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 275.03** kupitia Mfuko wa Barabara;

ii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP) ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 186.8** kwa ajili ya ujenzi wa kilomita **70** za barabara kwa kiwango cha lami;

iii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Barabara Katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo

(*Agri-Connect Programme*) ambao umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 35.5**;

iv) Kuanza utekelezaji wa Mradi mpya wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (*Roads to Inclusion and Socio-Economic Opportunities - RISE*) ambao umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 28.0**. Mradi utatekelezwa katika Mikoa 13 ya Iringa, Njombe, Mbeya, Morogoro, Rukwa, Katavi, Songwe, Tanga, Pwani, Dodoma, Mtwara, Ruvuma na Lindi.

v) Kuanza maandalizi ya mradi mpya wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness Project* (TACTIC) ambao utahusisha ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri 45 za Majiji, Manispaa na Miji.

### **Maeneo ya Utawala**

**175. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeweka kipaumbele na kutenga **Shilingi bilioni 49.29** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya utawala ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tarafa na nyumba za viongozi katika Mikoa, Wilaya na Tarafa (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 15*).

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetenga fedha za kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri na nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara kama ifuatavyo:- Ujenzi wa majengo ya utawala ya Ofisi za Halmashauri **100** ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 80.42** kwa ajili ya kutekeleza ujenzi huo. Aidha, ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara umepangwa kufanyika katika Halmashauri **9** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 1.35** zimetengwa (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 16*).

### **Ununuzi wa Magari**

**176. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya magari **54** yatanunuliwa katika Mikoa na

Halmashauri. Kati ya magari hayo, magari **16** yatanunuliwa kwa ajili ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambapo zimetengwa **Shilingi bilioni 4.48** na magari **38** yatanunuliwa kwa ajili ya Halmashauri **38** zenye makusanyo madogo ya mapato ya ndani ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 8.36** (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.17*).

### **Miradi ya Kimkakati**

**177. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambapo Halmashauri **16** zimetengwa jumla **Shilingi bilioni 50.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.18*). Miradi hiyo ina lengo la kuongeza wigo wa mapato ya Halmashauri ili kuziwezesha kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa ufanisi na kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali Kuu.

### **Kiinua Mgongo cha Madiwani**

**178. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 61.76** kwa ajili ya kulipa kiinua mgongo cha Madiwani watakapomaliza muda wao wa uongozi kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

### **Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**179. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itasimamia utoaji wa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 64.46** zimetengwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 25.78** zitatumika kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, **Shilingi bilioni 25.78** zitatumika kwa ajili ya vikundi vya Vijana na **Shilingi bilioni 12.89** zitatumika kutoa mikopo kwa vikundi vya Watu Wenye Ulemavu (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 19*).

## **Programu ya Maboresho ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*Regional and Local Government Strengthening Programme-RLGSP*)**

**180. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaanza utekelezaji wa programu mpya ya Maboresho ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo itatekelezwa kwa muda wa miaka 10 kwa kipindi cha miaka mitano mitano kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2029/30. Malengo ya programu hii ni kuimarisha ugatuaji wa majukumu na mahusiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kuimarisha utoaji wa huduma kwa kuboresha usimamizi wa rasilimali watu na fedha, kuimarisha ushiriki wa jamii katika kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo, kukuza uchumi katika ngazi ya jamii (*Local Economic Development*) na kujunga uwezo wa usimamizi na ufuatiliaji na tathmini.

**181. Mheshimiwa Spika**, Programu hii imeandaliwa kwa kuzingatia uzoefu na mafunzo yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Awamu ya Kwanza na Pili pamoja na maboresho mengine yanayoendelea ndani ya Serikali. Programu hii itasaidia kuimarisha utawala bora, usimamizi wa rasilimali katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii na ushiriki wa jamii katika kujiletea maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2020/21, programu imetengewa **Shilingi bilioni 1.5**.

### **Tume ya Utumishi wa Walimu**

**182. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu imetengewa **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Tume katika Jiji la Dodoma.

### **G. SHUKRANI**

**183. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, naomba kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu



Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mwenyekiti wa Kamati na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Maoni na ushauri wa Kamati yamesaidia kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**184. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa programu, miradi na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hao wa Maendeleo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya Ulaya (EU), *Global Partnership for Education*, Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Nchi zote zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya.

**185. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji huduma na kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru Wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sehemu kubwa ya mafanikio ambayo Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepata katika uboreshaji huduma za afya, elimu na sekta nyingine za kiuchumi yametokana na ushirikiano wa wananchi na Wadau mbalimbali.

**186. Mheshimiwa Spika**, napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji

wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Kipekee nawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb) kwa msaada mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph M. Nyamhanga, Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Dorothy O. Gwajima na Bw. Gerald G. Mwelu pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Bibi Winifrida G. Rutaindurwa. Aidha, ninawashukuru Wakuu wa Mikoja, Makatibu Tawala wa Mikoja, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**187. Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika (Mb) na Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais. Aidha, ninawashukuru sana Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Dkt. Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao.

**188. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI.

**189. Mheshimiwa Spika**, kipekee ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kisarawe kwa ushirikiano wanaonipa wakati wote ninapotekeleza majukumu haya ya Kitaifa. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote

ili kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii. Aidha, naishukuru familia yangu kwa uvumilivu muda wote nilipokuwa mbali nao katika utekelezaji wa majukumu haya ya Kitaifa.

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani

**190. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 185 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya **Shilingi Biloni Mia Nane na Sitini, Milioni Mia Sita Themanini na Tatu, Elfu Arobaini na Tisa, Mia Nne Ishirini na Sita (Shilingi 860,683,049,426.00)**. Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho ya masurufu na mishahara na kodi na ushuru mbalimbali unaotowza na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

### Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa mwaka wa fedha 2020/21

OFISI/TAASISI	MAKADIRIO
Ofisi ya Rais – TAMISEMI	11,520,000.00
Taasisi	45,500,839,514.00
Mikoa	209,698,912.00
Halmashauri	814,960,990,076.00
<b>JUMLA KUU</b>	<b>860,683,049,426.00</b>

**191. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi Trilioni Saba Bilioni Kumi na Tisa Milioni Mia Nane Laki Tatu Hamsini na Tatu Eflu (Shilingi 7,019,800,353,000.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 02 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 185.

**192. Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zinazombwa, **Shilingi 4,729,880,457,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara **Shilingi 3,878,738,058,000.00** na **Shilingi 851,142,399,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,289,919,896,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya hizo **Shilingi 1,296,949,390,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 992,970,506,000.00** ni fedha za nje (*Mchanganuo wa fedha zinazombwa katika mwaka wa fedha 2020/21 umeoneshwa katika Jedwali Na. 2*).

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Makisio katika Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/21**

AINA YA MATUMIZI	BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21
Matumizi ya Kawaida Ofisi ya Rais - TAMISEMI	
<b>Mishahara</b>	
Mishahara Mako Makuu	11,298,245,000
Mishahara ya Taasisi	42,148,645,000
<b>Jumla Mishahara Ofisi TAMISEMI</b>	<b>53,446,890,000</b>
<b>Matumizi Mengineyo</b>	
Mako Makuu	70,634,361,155
Taasisi	1,318,869,845
Jumla ya Matumizi Mengineyo	71,953,231,000
<b>Jumla Matumizi ya Kawaida</b>	<b>125,400,121,000</b>
<b>TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)</b>	
Mishahara	8,165,271,000
Matumizi Mengineyo	6,108,202,000
<b>Jumla ya Matumizi ya Kawaida TSC</b>	<b>14,273,473,000</b>
<b>MIKOA NA HALMA SHAURI</b>	
MIKOA:	
Mishahara	76,896,293,000
Matumizi Mengineyo	58,998,656,000
<b>Jumla ya Matumizi ya Kawaida</b>	<b>135,894,949,000</b>

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

<b>HAL MASHA URI</b>	
<b>AINA YA MATUMIZI</b>	<b>BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21</b>
Mishahara	3,740,229,604,000
Matumizi Mengineyo (SK)	232,212,477,000
Matumizi Mengineyo (MSM)	481,869,833,000
<b>Jumla Matumizi ya Kawaida</b>	<b>4,454,311,914,000</b>
<b>MIRADI YA MAENDELEO</b>	
<b>OFISI YA RAIS -TAMISEMI</b>	
Fedha za Ndani	276,534,159,000
Fedha za Nje	301,513,025,000
<b>Jumla Maendeleo</b>	<b>578,047,184,000</b>
<b>TUME YA UTUMISHI WA WALIMU</b>	
Fedha za Ndani	500,000,000
<b>Jumla</b>	<b>500,000,000</b>
<b>MIKOA</b>	
Fedha za Ndani	57,724,000,000
Fedha za Nje	28,268,688,000
<b>Jumla Maendeleo</b>	<b>85,992,688,000</b>
<b>HAL MASHA URI</b>	
Fedha za Ndani (SK)	629,100,064,000
Fedha za Ndani (MSM)	333,091,167,000
Fedha za Nje	663,188,793,000
<b>Jumla Maendeleo Halimashauri</b>	<b>1,625,380,024,000</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>7,019,800,353,000</b>

*SK – Serikali Kuu na MSM – Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*

**193. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI,

Taasisi, Mikoa na Halmashauri ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

**194. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)

**195. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu, lakini niwakumbushe Waheshimiwa tujitahidi sana kukumbuka sehemu tunazokuwa tumekaa siku yetu ya kuingia Bungeni ili kupunguza yale yanayoendelea ambayo wote tunayafahamu. Kwa namna hiyo nitoe fursa kwa upande wa Upinzani kwa sababu wakati mwingine *Chief Whip* anabadilika tutakuwa tunaletewa tu taarifa hapa mezani kwamba *Chief Whip* sasa ni nani kuliko *microphone* moja kuwa inatumiwa na watu wengi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuzingatie kadri inavyowezekana kwa sababu hata mimi hapa mezani jamani mambo yote yamebadilishwa Mheshimiwa Spika yuko makini sana na haya mambo. Kwa hiyo, hata mimi ya kwangu hapa mezani yamebadilika ya kwake yote yamesogea. Kwa hiyo, hata sisi tulichukulie jambo hili kwa umuhimu huo huo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mheshimiwa Rweikiza. (*Makofi*)

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Januari 2016, naomba kuwasalisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilizingatia masharti ya kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kufanya ziara za kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa siku zisizozidi saba kabla ya kuanza uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla wa mafungu 28 kama yanavyoonekana kwenye ukurasa wa 2 na 3 wa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha unaoanza ulifanyika kuanzia tarehe 16 hadi tarehe 27 Machi 2020. Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais - TAMISEMI imejikita katika maeneo manne yafuatayo:-

(i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati.

(ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

(iv) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi hii ya maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa mwaka fedha 2018/2019. Ufafafanuzi wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi trilion 1.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ili kuzingatia Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati



ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2019/2020. Miradi hiyo iliyotembelewa na Kamati ni pamoja na Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali za Mwenge (Singida) na Nangwa (Manyara); Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) katika Manispaa ya Singida; na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu. Ufafanuzi zaidi kuhusu miradi hiyo na maoni ya jumla ya utelekezaji wake unapatikana katika ukurasa wa 5 - 14 wa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya utelekezaji wa miradi na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Fungu 56 pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 31.2 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Februari 2020 kiasi cha shilingi bilioni 25 kilikuwa kimekusanywa sawa na asilimia 80.2 ya malengo yaliyowekwa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa sehemu kubwa makusanyo hayo yalichangiwa na taasisi zifuatazo:-

(i) *TARURA* ambayo ilikusanya kwa asilimia 110.4 kutokana na ongezeko la eneo la makusanyo na uwezo wa kukusanya.

(ii) Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ambacho kilikusanya jumla ya asilimia 83.5 kutokana na ongezeko la udahili wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha kwamba kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa asilimia 33.2 ikilinganishwa na asilimia 44 iliyoshuhudiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, uchambuzi umebaini kwamba makusanyo yamekuwa yakiongezeka mfululizo katika kipindi cha miaka minne ya fedha iliyopita. Vilevile Halmashauri zillidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 765.5 na hadi kufikia Februari 2020 zilikuwa zimekusanya asilimia 61 ya lengo ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI umebaini kwamba:-

(i) Fedha zilizotolewa ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (*cash floor plan*) uliowekwa umeongezeka ukilinganisha na miaka mingine.

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wingi ikilinganishwa na matumizi na maendeleo.

(iii) Fedha za maendeleo za ndani kwa kiasi kikubwa zinatolewa ikilinganishwa na fedha za maendeleo ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2020, Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea shilingi bilioni 413.7 kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 73.4 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii. Kiasi hicho kimeongezeka kwa asilimia 28.2 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa fedha 2018/2019 ambapo kiasi kilichopatikana kilikuwa ni asilimia 45.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Kamati ilibaini kwamba hadi kufikia Februari 2020, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya shilingi bilioni 377.7 sawa na asilimia 76 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimeongezeka kwa takribani asilimia 31 ikilinganishwa na asilimia 44.5 ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishwa bajeti ya shilingi trilioni 5.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2020 shilingi trilioni 2.9 zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 66, na takribani shilingi bilioni 500 zilipokelewa kwa ajili ya maendeleo sawa na asilimia 43.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba fedha za maendeleo ya ndani zilitolewa kwa kiwango kikubwa (asilimia 52) ikilinganishwa na fedha za nje ambazo zilipatikana kwa asilimia 20 tu. Hii ni ishara njema kwamba miradi ya maendeleo inaweza kutekelezwa kwa uhakika zaidi kuliko kutegemea fedha za nje ambazo hazina uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati katika uchambuzi na mapitio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo kumi 14 ili ofisi hii iweze kuyazingatia katika kutekeleza vipaumbele vya bajeti kwa lengo la kuleta ufanisi na tija. Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 22 hadi 25 wa Taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, imepanga kutekeleza malengo yake kwa kuzingatia vipaumbele 13. Baadhi ya vipaumbele hivyo ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 25 hadi 27 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, ziliomba kuidhinishwa jumla ya Shilingi trilioni saba. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi trilioni 2.3 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, shilingi trilioni 3.9 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 851 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika jedwali Na. 3 la taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 860.7.

Mapato hayo ni ongezeko la shilingi bilioni 63.8, sawa na 8% ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati, makusanyo yote yanatarajiwa kuongezeka kwa shilingi bilioni 63.8 ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaomalizika. Ongezeko hilo limechangiwa na Wakala wa Barabara Vijijini (*TARURA*) kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani na Chuo cha Hombolo kuongeza udahili wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao 2020/2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa pamoja zinaomba kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi trilioni saba kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyopangwa. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 4.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 2.3 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha hizo zinazooombwa kuidhinishwa na Bunge, shilingi bilioni 14.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Tume ya Utumishi wa Walimu (*TSC*) – Fungu 02.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti inayoombwa kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeongezeka kwa shilingi bilioni 811.8 sawa na asilimia 11.5 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la asilimia 35.2 kutoka shilingi trilioni 1.7 katika mwaka wa fedha 2019/2020 hadi shilingi 2.3 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Uchambuzi zaidi umebaini kwamba ongezeko la bajeti kwa ujumla wake, limetokana na Serikali kuongeza fedha za maendeleo kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu, afya na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma katika sekta hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulinganisha Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa

fedha 2020/2021, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kulikuwa na ongezeko kwa pande zote mbili. Aidha, bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni sawa na asilimia 20.13 ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeongezeka kwa asilimia 1.39 ikilinganishwa na uwiano katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambao ulikuwa ni asilimia 18.7. Ufafanuzi zaidi ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 5 la taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa umefafanuliwa zaidi kupitia jedwali Na.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati:-

(i) Kamati inapongeza hatua ya Serikali kununua na kugawa mashine za kukusanyia mapato 7,227 (POS) kwa Halmashauri zote nchini, kwani hatua hii imesaidia kuongeza makusanyo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi mwezi Februari, 2020 Halmashauri zilikuwa zimekusanya asilimia 61 ya lengo lililokusudiwa. Kamati inashauri Serikali iweke msisitizo zaidi katika matumizi ya mashine hizo ili kuongeza na kudhibiti ufujaji wa mapato ya Halmashauri;

(ii) Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo zinadaiwa na benki mikopo ya Waheshimiwa Madiwani iliyotokana na dhamana ya posho za kila mwezi, zinakamilisha ulipaji wa madeni hayo kabla ya tarehe 30 Mei, 2020. Hatua hiyo itasaidia kuondoa usumbufu ambao Madiwani wanaweza kukumbana nao kutoka kwenye benki hizo iwapo watamaliza kipindi chao cha uongozi bila ulipaji wa madeni hayo. Mfano, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Halmashauri Sita za Mkoa wa Singida pekee zilikuwa zinadaiwa jumla ya shilingi milioni 688.7, deni ambalo hata hivyo, uongozi wa Mkoa uliahidi kulipatia ufumbuzi;

(iii) Kamati inapongeza hatua ya baadhi ya Halmashauri nchini kutumia fedha za vyanzo vya ndani na kushirikiana na wahisani kutoa taulo za kike kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari ili kuwawezesha kushiriki

kikamilifu katika masomo. Miongoni mwa Halmashauri zilizofanya vizuri ni za Mkoa wa Mara ambazo katika mwaka wa fedha 2018/2019 zilitoa taulo 33,617; kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi Februari, 2020 taulo 25,429 na zimepanga kutoa taulo 43,950 katika mwaka wa fedha ujao. Kamati inashauri Halmashauri nyingine nchini kubuni namna ya kuwasaidia watoto wa kike kutoka familia masikini kupata taulo za kike ili waweze kuhudhuria masomo bila matatizo;

(iv) Kamati inapongeza kazi nzuri inayotekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini (*TARURA*) katika kujenga na kuboresha miundombinu ya barabara nchini. Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Wakala huu ni kidogo sana ikilinganishwa na mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) zinazohudumiwa.

Kamati inashauri *TARURA* iongezewe fedha hasa katika mwaka huu wa fedha ili kukabiliana na uharibifu mkubwa uliosababishwa na mvua ambazo zimekuwa zikinyesha nchini tangu mwishoni mwa mwaka 2019. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa kuongeza mgawo wa fedha wa asilimia 30 ambao *TARURA* inapewa kutoka Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) hadi kufika asilimia 50;

(v) Kamati imebaini kwamba, baadhi ya Halmashauri zinakiuka kifungu cha 37 A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kuhusu utengaji na utoaji wa fedha za 10% ya mapato ya ndani ili kuwezesha kiuchumi wanawake, vijana na wenye ulemavu, kwa kushindwa kutenga na kutoa fedha hizo kikamilifu.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, Mikoa ya Kagera, Tabora na Singida ilifanya vizuri zaidi kwa kutoa Halmashauri tatu zilizoongoza katika utengaji wa fedha hizo. Aidha, Mikoa ya Simiyu na Manyara ilifanya vibaya kwa kutoa asilimia tatu zilizofanya vibaya zaidi. NB:- mchanganuo wa namna Halmashauri zilivyotenga na kutoa asilimia 10 ya mapato hiyo imeonekana kupitia jedwali Na. 8;

(vi) Halmashauri zisaidie vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu kutumia fedha za 10% ya mapato ya ndani kuanzisha miradi mikubwa ya maendeleo na hivyo kutoa ajira na kuchangia mapato ya Serikali, badala ya wanachama wa vikundi hivyo kugawiwa fedha hizo. Baadhi ya Halmashauri zimesaidia vikundi kuanzisha miradi hii mikubwa ya kiuchumi.

Mfano, Manispaa ya Temeke, imesaidia Kikundi cha Jukwaa la Wanawake la Mibulani kinachojihusisha na utunzaji wa mazingira kwa kuwanunulia gari la uzoaji taka na vifaa vingine kwa thamani ya shilingi milioni 189. Kupitia mkopo huo wanawake 102 wanaounda kikundi hicho wamepata ajira na kila mwezi wanarejesha shilingi milioni sita za mkopo huo ambao utalipwa ndani ya miaka mitatu;

(vii) Serikali ihimise Halmashauri nchini kutenga na kupeleka kikamilifu asilimia 60 (Majiji na Manispaa) na asilimia 40 (Wilaya na Miji) ya mapato ya ndani kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya Halmashauri zinafanya vizuri katika eneo hili, huku baadhi zikifanya vibaya na hivyo kuathiri miradi hiyo.

Mikoa mitatu iliyoongoza katika utoaji wa fedha za maendeleo kutokana na mapato ya ndani ni Geita (wastani wa asilimia 96); Njombe (asilimia 95) na Mara (asilimia 92). Aidha kwa upande wa mikoa mitatu iliyofanya vibaya zaidi ni Rukwa (asilimia 30); Dodoma (asilimia 42) na Tanga (asilimia 53);

(viii) Serikali isimamie kikamilifu na kuhakikisha Halmashauri zinapeleka kikamilifu fedha zinazotokana na asilimia 60 au 40 ya mapato ya ndani katika Halmashauri hizo kwenda miradi ya maendeleo iliyokusudiwa na siyo kutumika kwenye shughuli za uendeshaji wa ofisi;

(ix) Serikali ielekeze Halmashauri zishirikiane na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kuanzisha katika Halmashauri Kituo Kimoja cha Urasimishaji wa Biashara (*One Stop Business*

*Centre*) ili kurahisisha, kuharakisha na kupunguza gharama za mfanyabiashara.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kituo cha aina hiyo katika Manispaa ya Singida ambacho kinafanya vizuri sana kwani kimesaidia kuondoa kero kwa wananchi pale wanapotaka kuanzisha au kurasimisha biashara zao na kuchochea maendeleo. Aidha, ni muhimu kushirikisha wadau wengine muhimu kama Benki, *TRA*, *BRELA*, *SIDO*, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi. Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati yangu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati katika Bunge hili la Kumi na Moja, nitumie fursa hii kuwatakia Wajumbe wa Kamati pamoja na Wabunge wengine wote kila la kheri katika uchaguzi ujao na panapo majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, sote turejee humu ndani katika Bunge lako la Kumi na Mbili ili kuendeleza gurudumu la ujenzi wa Taifa letu kwa kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuwakilisha wananchi na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wake, ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa



Selemani Saidi Jafo, kwa ushirikiano mkubwa sana aliouonesha kwa Kamati ambao umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Utendaji wake na Naibu wake Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Mwita Waitara umedhihirisha zaidi walivyo hazina kubwa kwa ustawi wa Taifa letu.

Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph Nyamuhanga, akisaidiana na Naibu Makatibu Wakuu, Dkt. Dorothy Gwajima na Ndg. Gerald Mwelu kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya Kamati hii. Aidha, shukrani za Kamati ziwaendee Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini kwa utekelezaji makini wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima, Ndg. Asmin Kihemba na Ndg. Prosper Minja wakisaidiwa na Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii ya TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA  
SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU  
YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI  
YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii imepewa jukumu la kuisimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR - UUB) pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) (a), Kamati imepewa jukumu mahususi la kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kwa kufanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa siku zisizozidi saba (7), kabla ya kuanza uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla ya mafungu ishirini na nane (28) yafuatayo: -

- i. Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- ii. Fungu 02 - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC);
- iii. Fungu 36 – Mkoa wa Katavi;
- iv. Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu;
- v. Fungu 54 – Mkoa wa Njombe;
- vi. Fungu 63 – Mkoa wa Geita;
- vii. Fungu 70 – Mkoa wa Arusha;
- viii. Fungu 71 – Mkoa wa Pwani;
- ix. Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma;
- x. Fungu 73 – Mkoa wa Iringa;
- xi. Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma;
- xii. Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro;
- xiii. Fungu 76 – Mkoa wa Lindi;
- xiv. Fungu 77 – Mkoa wa Mara;
- xv. Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya;
- xvi. Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro;
- xvii. Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara;
- xviii. Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza;
- xix. Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma;
- xx. Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga;
- xxi. Fungu 84 – Mkoa wa Singida;
- xxii. Fungu 85 – Mkoa wa Tabora;
- xxiii. Fungu 86 – Mkoa wa Tanga;
- xxiv. Fungu 87 – Mkoa wa Kagera;
- xxv. Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam;
- xxvi. Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa;
- xxvii. Fungu 90 – Mkoa wa Songwe; na
- xxviii. Fungu 95 – Mkoa wa Manyara.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha unaoanza, ulifanyika kuanzia tarehe 16 hadi 27 Machi, 2012. Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne (4) yafuatayo: -

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati hii ndiyo yenye dhamana ya kuisimamia Serikali katika masuala ya Serikali za Mitaa, nigusie kidogo kuhusu dhana ya ugatuzi wa madaraka au upelekaji wa madaraka kwa wananchi (*Devolution by Decentralization – D by D*) ambayo msingi wake ni Ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Ibara ya 146 (1) inasisitiza kwamba, vyombo vya serikali za mitaa (Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji) vitakuwa na haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla.

Utekelezaji wa dhana hiyo ya kikatiba kupitia sera iliyotungwa mwaka 1998 umekuwa na manufaa kadhaa ikiwa ni pamoja na kusogezwa kwa huduma karibu na wananchi, na ushiriki wa wananchi katika kutathmini, kupanga, kuamua na kutekeleza mipango mbalimbali kwa kuzingatia matatizo yanayowakabili kwa kutumia mbinu ya fursa na vikwazo kwa maendeleo.

Ni kwa mantiki hiyo wananchi kwa nguvu zao na uungwaji mkono wa Serikali wamefanikiwa kujenga shule za msingi, shule za sekondari za kata, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, miradi ya maji, uhifadhi endelevu wa misitu na mazingira, n.k

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi za Serikali za kuzingatia dhana hii ya ugatuzi na kuunga mkono nguvu za wananchi. Hata hivyo, inashauri Serikali iendelee kujikita katika kujenga mfumo imara wa kumhudumia mwananchi ambao utazingatia misingi ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi ambao Ibara ya 8(a) ya Katiba inawataja kuwa wao ndiyo msingi wa madaraka yote na Serikali, na itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi. Aidha, Serikali ihakikishe inagatua rasilimali fedha za kutosha na kuzipeleka kikamilifu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa

ambako utekelezaji unafanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

## **2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

### **2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ziliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,692,937,354,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ili kuzingatia Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2019/2020. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, kama ifuatavyo: -

#### **2.1.1 Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali**

Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari ni utaratibu unaotekelezwa na Serikali kwa lengo la kurejesha shule hizo katika hali nzuri itakayowezesha Walimu kufundisha na Wanafunzi kujifunzia katika mazingira bora. Mpango huo ulioanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 unajumuisha shule Kongwe za Sekondari zipatazo 89 na unatekelezwa kwa awamu.

##### **(a) Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Mwenge**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Shule ya Sekondari ya Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Mei, 2017 na Mkandarasi ambaye ni National Housing Corporation (NHC) kwa ufadhili wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Mradi ulipaswa kukamilika ndani ya miezi mitano tangu kuanza kwake, hata hivyo ilishindikana kutokana na kazi ya

ukarabati kufanyika wakati ratiba za shule zikiendelea, na mabadiliko ya kazi ambavyo viliathiri kasi ya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, awali upembuzi yakinifu ulianisha gharama za mradi kuwa ni **shilingi 7,924,063,872** kiasi ambacho kilikuwa kikubwa ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa ya **shilingi bilioni moja (1,000,000,000)**.

Kutokana na ufinyu wa bajeti iliamuliwa kuwa ukarabati utekelezwe kwa awamu, na awamu ya kwanza ilitengewa **shilingi 939,187,027** na kuhusisha ukarabati wa mabweni ya Azimio, Jamhuri, Ujamaa, Nyerere I,II,& III, vyoo vya mabweni, maeneo ya kufulia na miundombinu ya umeme.

Aidha, wakati wa utekelezaji wa mradi huu ziliibuka kazi nyingine ambazo zilisababisha ongezeko la gharama za ukarabati kwa kiasi cha **shilingi 333,769,679**. Kazi hizo ni ujenzi wa mfumo wa kisasa wa maji taka " *anaerobic baffled reactor*", ujenzi wa sakafu " *aprons*" kuzunguka maeneo yaliyokarabatiwa, ujenzi wa kubadilisha matumizi ya Karakana ya Nyerere kuwa vyoo, na ukarabati wa bweni la Umoja. Kazi zilizoongezeka zilisababisha gharama za mradi kufikia **shilingi 1,272,956,707**.

**Mheshimiwa Spika**, ukarabati wa miundombinu ya shule hii kwa awamu ya pili ambao utahusisha ukarabati wa mabweni mawili ya Umoja na Ujamaa umepangiwa shilingi milioni 196.7 na utekelezaji wake utanza muda wowote.

#### **(b) Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Nangwa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Shule ya Sekondari ya Nangwa iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Mkoani Manyara. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ilianza mwaka 2016 na kutekelezwa hasi 2018 na Wakala wa Majengo wa Serikali (TBA) ambaye alikarabati vyumba 10 vya madarasa, ofisi nne za walimu na maabara mbili za masomo ya kemia na biolojia. Aidha, kazi nyingine ambazo zimetekelzwa ni pamoja na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kubeba wanafunzi 160,

madarasa mawili na matundu sita ya vyoo. Jumla ya gharama ambazo zimetumika katika ukarabati na ujenzi huo wa awamu ya kwanza ni **shilingi 759,136,573**.

Aidha, awamu ya pili ya ukarabati ambayo ilipaswa kuanza mwaka 2019 na ikashindikana kutokana na kuchelewa kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Hazina kutokana na fedha kupokelewa nje ya mpango wa bajeti ya halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019.2020, ilianza mwezi februari na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020 na itatekelezwa kwa awamu mbili kutokana na kukosekana kwa majengo ya kuwahifadhi wanafunzi pamoja na vifaa.

Miongoni mwa kazi zitakazofanyika ni ukarabati wa maabara za Fizikia na Jiografia, bwalo la chakula, ukumbi na vyoo katika awamu ya kwanza ambayo itagharimu **shilingi 302,967,000**. Awamu ya pili itahusisha ukarabati wa mabweni ya Jakaya Kikwete, Mary Nagu, Ngorongoro, Tarangire pamoja na vyoo vya vya ndani na nje.

### 2.1.2 **Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 na kuanza kutekeleza majukumu yake tarehe 2 Julai, 2017. Kuanzishwa kwa wakala huu ni muendelezo wa utekelezaji wa mabadiliko (*reforms*) kwenye sekta ya ujenzi na barabara yaliyoanza mwaka 1998 ambayo ni pamoja na marekebisho ya Road Tolls Act, kuanzishwa kwa Mfuko wa Barabara (RF), TANROADS na sasa TARURA.

TARURA ambayo inahudumia mtandao wa barabara wenye zaidi ya kilomita 108,946 nchi nzima ina majukumu makubwa ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za Vijijini na Mijini pamoja na madaraja na mpango mkakati wa kuondoa vikwanzo ili barabara ziweze kupitika muda wote. Aidha, TARURA inatarajiwa kuimarisha barabara zinazopita kwenye maeneo muhimu yenye viwanda na kilimo na hivyo kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhidha na utekelezaji wa shughuli za TARURA Kamati ilitembelea Halmashauri ya Manispaa ya Singida Mkoani Singida ambapo Wakala inahudumia mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 9.85 ambazo kati ya hizo kilomita 8.75 zimeishakamilika na kilomita 1.1 ni mradi unaoendelea kutekelezwa.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Septemba, 2019 kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.78** na unatekelezwa na Mhandisi Harising & Sons Ltd JV na BML na kusimamiwa na Mhandisi Mshauri (Mhandisi Jv na Luptan).

Barabara zinazohusika na mradi huu ni Karume Jct Semali – Singida Road (0.4 Km), Salmin Road (0.6) na Majengo – Mungumaji (0.1 km). Awali mradi ulitarajiwa kukamilika Februari, 2020 hata hivyo ilishindikana kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Mradi unahusisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ngumu, njia za waenda kwa miguu, mifereji ya maji ya mvua, uwekaji wa taa za barabarani za solar, na ujenzi wa vivuko kuruhusu watu kuingia katika makazi yao.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inafanya ziara katika mradi huu, utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 90.

### 2.1.3 Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa hospitali hii ni sehemu ya ujenzi wa hospitali za halmashauri 67 nchini ambao unatekelezwa na Serikali kwa Wilaya ambazo hazina Hospitali za Halmashauri. Mradi huu unaotekelezwa katika awamu ya kwanza ulitengewa **shilingi bilioni 1.5** na utahusisha majengo saba ambayo ni jengo la utawala, wagonjwa wa nje, maabara, mionzi, madawa, kufulia nguo na mama na mtoto. Utekelezaji wa mradi huu unahusisha nguvu za wananchi na unafanyika kwa utaratibu wa *force account*, ambapo kwa ujumla umefikia wastani wa asilimia 91.

Kukamilika kwa hospitali hii kutasaidia Wananchi wa Wilaya ya Mbulu kupata huduma za matitabu ambazo hulazimika



kuzifuata katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu, eneo ambalo ni mbali sana na wakati wa msimu wa mvua kunakuwa na changamoto ya usafiri.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo hiyo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika mwaka wa fedha 2019/2020, naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tufuku kuhusu mambo ambayo Kamati iliyabaini kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Halmashauri ya wilaya ya Hanang ambako Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu wa ukarabati wa shule kongwe za Sekondari, mambo yafuatayo yalibainika: -

#### a) Mafanikio;

i) Kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia kwa Walimu na kujifunzia kwa Wanafunzi kutokana na ofisi na madarasa kurejeshwa katika hali nzuri;

ii) Kuboreshwa kwa mabweni ya Wanafunzi na hivyo kuwafanya kuishi katika mazingira bora;

iii) Kuongezeka kwa ari ya Walimu kufanya kazi kwani wanaona Serikali imejali na kuboresha mazingira yao ya kazi;

iv) Kurejesha majengo na mazingira ya shule katika ubora wa awali uliokuwepo katika shule za Sekondari za Serikali;

#### b) Changamoto;

i) Kuchelewa kupokelewa kwa kibali cha kuruhusu kufanya ukarabati uliokusudiwa (kwa shule ya Nangwa – Hanang);

ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa ukarabati kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha;

iii) Uhaba wa majengo ya wanafunzi kwa ajili ya kupisha shughuli za ukarabati;

iv) Bajeti ndogo ikilinganishwa na ukarabati unaohitajika kufanyika kwani miundombinu na majengo vimekaa muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati;

### **2.2.2 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA)**

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli za TARURA katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida ulibaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

#### **(a) Mafanikio;**

i. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami hadi kufikia kilomita 9.85 katika Manispaa ya Singida;

ii. Kuimarika usalama nyakati za usiku kutokana na kuwepo kwa taa za mitaani na hivyo kuhamasisha wananchi kuongeza shughuli za kiuchumi na hivyo kuongeza mapato ya manispaa;

iii. Usalama kwa watumiaji wa barabara kutokana na kujengwa kwa njia za waenda kwa miguu (walk ways) na vivuko vya kuruhusu watu kuingia katika makazi;

iv. Kuongezeka kwa thamani ya majengo na ardhi kando ya barabara zinazojengwa kwa kiwango cha lami; na

v. Kurahisisha mawasiliano kwa wananchi kwa kupunguza umbali kati ya eneo la stendi kuu ya mabasi na eneo la kati ya mji.

#### **(b) Changamoto;**

i. Kuchelewa kukamilika kwa kazi za ujenzi kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha;

ii. Baadhi ya Wananchi waishio kando ya mradi kutozingatia usafi kwa kutupa taka katika mifereji ya maji iliyojengwa kando ya barabara; na

iii. Upungufu wa wataalam wa ujenzi kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

### 2.2.3 Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa Kamati kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ulibaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo: -

#### (a) Mafanikio;

(i) Wananchi wana matumaini ya kupata huduma za Hospitali ya Halmashauri katika maeneo yao badala ya kufuata huduma hiyo katika maeneo mengine; na

(ii) Kupatikana kwa huduma hizo kutasaidia Wanawake Wajawazito na Watoto kupata msaada wa haraka wa matibabu;

#### (b) Changamoto;

i. Upungufu wa Watumishi wa ujenzi kwani Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ina Mhandisi ujenzi mmoja;

ii. Kukosekana kwa bajeti ya ujenzi wa nyumba za Watumishi jambo linaloweza kuchelewesha kuanza kwa huduma ya matibabu baada ya majengo ya awali kukamilika; na

iii. Kukosekana kwa miundombinu ya barabara kuingia katika eneo la Hospitali.

### 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mikoa ya Singida na Manyara, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na ingependa kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

i. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) unahitaji kuongezewa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara kutokana na

kuwa na mtandao mkubwa wa barabara. Aidha, msimu mrefu wa mvua umechangia uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na madaraja, hivyo gharama zaidi zitahitajika ili kurejesha miundombinu hiyo katika hali nzuri;

ii. Hazina itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa na hivyo kuendelea kuwakosesha wananchi huduma zilizokusudiwa;

iii. Serikali iandae utaratibu wa kupata Watumishi wa afya ili hospitali za Halmashauri zinapokamilika ziweze kuanza kutoa huduma ya matibabu mara moja;

iv. Kukosa umakini katika usanifu wa awali (*feasibility study*) wa miradi ya maendeleo kunaathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama kutokana na kuongeza kazi;

v. Serikali iweke utaratibu wa kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha ili kuepusha ubadhilifu unaoweza kutokea;

vi. Serikali itoe fedha ili kukamilisha miradi inayotekelezwa ili kupunguza gharama za miradi hiyo na hivyo kupatikana kwa thamani halisi ya fedha katika miradi hiyo, badala ya kuanza miradi mipya.

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

#### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa.

Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kwa kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Kwa ufafanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake (LGTI, KEC, DART na LGLB) ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 31,237,895,252** kutoka vyanzo vya ndani. Mapato hayo yanatokana na kuuza vifaa chakavu na zabuni kwa upande wa makao makuu (Fungu 56) na ada za wanafunzi, ukusanyaji wa madeni, tozo, ushuru na mauzo ya bidhaa mbalimbali kwa upande wa taasisi.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 kiasi cha **Shilingi 25,048,538,365.20** kilikuwa kimekusanywa, sawa na **asilimia 80.2** ya malengo yaliyowekwa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa sehemu kubwa makusanyo hayo yalichangiwa na taasisi zifuatazo ambazo zilikusanya kwa kiwango cha juu:-

i. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ambao ulikusanya kwa asilimia 110.4 kutokana na ongezeko la eneo la makusanyo na uwezo wa kukusanya; na

ii. Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo ambacho makusanyo yake yalifikia asilimia 83.5 kutokana na ongezeko la udahili wa wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa **asilimia 36.2** ikilinganishwa na **asilimia 44** iliyoshuhudiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Kiwango hicho cha makusanyo kinaonesha kwamba, wastani wa makusanyo kwa kila robo ulifikia **asilimia 26.73** ikiwa ni juu kidogo ya wastani wa **asilimia 25** ambao unapaswa kufikiwa kwa kila robo ya mwaka wa fedha. Aidha, uchambuzi umebaini kwamba, makusanyo yamekuwa yakiongezeka mfululizo katika kipindi cha miaka minne ya fedha (2016/17, 2017/18, 2018/19 na 2019/2020).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mikoa hadi kufikia mwezi Februari, 2020 makusanyo yalikuwa ni **shilingi 77,692,255** kiasi ambacho ni sawa na **asilimia 39** ya lengo lililowekwa. Kiasi hicho kimepungua kwa **asilimia 46** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019 kutokana na mikoa kushindwa kuuza mali chakavu kwa kukosa kibali kutoka Hazina. Aidha, Halmashauri ziliidhinishwa kukusanya **shilingi 765,483,375,122** na hadi kufikia mwezi Februari, 2020 zilikuwa zimekusanya **asilimia 61** ya lengo lililokusudiwa.

Wastani wa makusanyo kwa TAMISEMI Makao Makuu na Taasisi zake, Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi hicho ulifikia **asilimia 60.1** kiwango ambacho ni takribani sawa na wastani uliofikiwa katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Pamoja na ukweli kwamba, TAMISEMI Makao Makuu na taasisi zake ilikuwa na asilimia kubwa ya makusanyo, bado Halmashauri zimeendelea kuwa na makusanyo mengi ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na wigo mkubwa wa vyanzo vya mapato na idadi kubwa ya watu, ambavyo ni muhimu katika ukusanyaji wa mapato.

### 3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI umebaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2019/20 na kiasi kinachotolewa na Hazina.

Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba: -

- i. Fedha zinazotolewa ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (*cash flow plan*) uliowekwa zimeongezeka ikilinganishwa na miaka mingine;
- ii. Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wingi ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na
- iii. Fedha za Maendeleo za Ndani zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo za nje.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **Shilingi 413,655,352,910/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 73.4** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kwamba, kiasi hicho kimeongezeka kwa takribani **asilimia 28.2** ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo kiasi kilichopatikana kilikuwa ni **asilimia 45.2**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2020 Ofisi hiyo na taasisi zake ilikuwa imepokea **shilingi 35,915,538,575** sawa na **asilimia 53.8** ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimeongezeka kwa **asilimia 3.2** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo Kamati ilibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi 377,739,814,335**, sawa na **asilimia 76.1** ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimeongezeka kwa takribani **asilimia 31** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2018/19 ambacho kilikuwa ni **asilimia 44.5**.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na.02) katika mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishwa kiasi cha **shilingi 14,901,157,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Kati ya fedha hizo, **shilingi 8,889,012,000/=** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 6,002,145,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea **shilingi 7,936,816,489/=** sawa na **asilimia 53** kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi 4,409,399,480/=** ni kwa ajili ya mishahara, na **shilingi 3,527,417,009/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2019/2020 ziliidhinishwa bajeti ya **shilingi 5,482,300,354,950/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

Kati ya fedha hizo **shilingi 3,669,329,614,000/=** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 650,930,095,453/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **1,162,040,645,497/=** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 **shilingi 2,851,371,408,238** zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 66**, wakati fedha za maendeleo zilikuwa zimepokelewa **shilingi 499,677,477,563** sawa na **asilimia 43**.

Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba fedha za maendeleo za ndani zilitolewa kwa kiwango kikubwa (**asilimia 52**) ikilinganishwa na fedha za nje ambazo zilipatikana kwa **asilimia 20** tu. Hii ni ishara njema kwamba, miradi ya maendeleo inaweza kutekelezwa kwa uhakika zaidi kuliko kutegemea fedha za nje ambazo hazina uhakika.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini kwamba kwa wastani upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake katika mwaka wa fedha 2019/2020 ulikuwa ni **asilimia 64.95**, kiwango ambacho kimeongezeka ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 47.55** katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Aidha, ongezeko hilo la wastani wa upatikanaji fedha katika kipindi kama hicho cha bajeti, ikiwa ni takribani robo ya tatu



ya mwaka wa fedha, liko chini ya kiwango cha angalau asilimia 25 ambacho kinatakiwa kwa kila robo katika mwaka wa fedha. Kwa ongezeko hilo wastani ni asilimia 21.65 kwa robo mwaka wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, uchambuzi umebaini kwamba, wastani wa upatikanaji wa fedha ulikuwa ni kwa **asilimia 54.5**. Aidha, bado fedha za matumizi ya kawaida zimeendelea kupatikana kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo.

Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamkala za Serikali za Mitaa na kiasi kilichopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2020, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Miradi ya Maendeleo. Ufafanuzi zaidi kwa baadhi ya maeneo hayo umeoneshwa kupitia **Jedwali Na. 01 & Jedwali Na.02**

**Jedwali Na.01:** Bajeti iliyoidhinishwa kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana hadi Februari, 2020

Mgawanyo wa Bajeti	Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20	Kiasi kilichopokelewa hadi Februari, 2020	Asilimia ya kiasi kilichopokelewa
OC	22,509,217,291	18,403,175,965	81.8
Mshahara	44,221,769,000	17,512,362,610	39.6
Maendeleo	496,563,123,910	377,739,814,335	76.1
<b>Jumla</b>	<b>563,294,110,201</b>	<b>413,655,352,910</b>	<b>73.4</b>

**Jedwali Na.02:** Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana hadi Februari, 2020

Mgawanyo wa Bajeti	Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20	Kiasi kilichopokelewa hadi Februari, 2020	Asilimia ya Kiasi kilichopokelewa
Mishahara	3,699,329,614,000	2,353,110,121,869	64
OC (SK+OS)	650,930,095,453	516,945,711,295	88.5
Maendeleo	1,162,040,645,497	494,968,372,552	43
<b>Jumla</b>	<b>5,482,300,354,950</b>	<b>3,365,024,205,716</b>	<b>61</b>

**Chanzo Jedwali Na 01 & 02:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mwaka wa Fedha 2020/2021.

### 3.1.3 Mapito ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi na mapitio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo kumi na nne (14) ili ofisi hii iweze kuzingatia katika utekelezaji wa vipaumbele vya bajeti kwa lengo la kuleta ufanisi na tija.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa baada ya kupitia majibu yaliyowasilishwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Kamati imeridhishwa na jitihada zilizooneshwa katika kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati kwa kutatua changamoto zilizobainishwa. Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati umechangia katika uboreshaji wa huduma za msingi kwa wananchi na maendeleo ya jamii. Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanyia kazi maoni na ushauri kwa baadhi ya maeneo yaliyosalia ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na: -

i. Maandalizi ya Kanuni za utekelezaji wa Kifungu cha 37 A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kinachosimamia ya utoaji asilimia kumi (10) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, ambapo Kanuni hizo zilikamilika na kuanza kutumika Aprili, 2019;

ii. Serikali iendeele kuhimiza Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, ambapo Halmashauri 40 zimeweza kubuni miradi ya kimkakati na kuandaa maandiko 50 na kuyawasilisha Serikalini kwa lengo la kupatiwa fedha za utekelezaji. Iwapo maandiko hayo yatapatiwa fedha za utekelezaji, idadi ya Halmashauri zitaongezeka kutoka 30 za awali hadi 70 sawa na asilimia 37.84 ya Halmashauri zote nchini; na

iii. Serikali ikamilishe ujenzi wa wodi maalum (Mama Ngojea) katika Mikoa sita iliyosalia kati ya 26 ya Tanzania Bara ili kuwezesha Wajawazito kutoka maeneo ya mbali na huduma za afya, kupata uangalizi wa karibu kutoka kwa Wataalam wa afya hasa wanapokaribia kujifungua. Hatua hiyo itasaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua (*maternity motarity deaths*) ambavyo huchangiwa na kukosa huduma za msingi za afya kama vile upasuaji (*operation*). Serikali imeongeza wodi hizo katika mikoa miwili ya Mtwara na Tanga, na hivyo kufikisha idadi ya mikoa 22. Mikoa iliyosalia ni Katavi, Rukwa, Mara na Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya baadhi ya maoni kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na: -

i. Ofisi ya Rais, TAMISEMI isimamie na kuhakikisha halmashauri ambazo zilidhamini Waheshimiwa Madiwani kukopa katika benki kwa kutumia posho za mwezi lakini zikakiuka utaratibu wa urejeshaji wa fedha kwa mujibu wa makubaliano, zinalipa madeni hayo. Bado halmashauri nchini zinadaiwa madeni ya Madiwani;

ii. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu fedha za asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri na kuzipeleka kwenye Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. Aidha, Halmashauri ziandae na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na idadi ya vikundi, ukopeshaji na urejeshaji wa fedha hizo; na

iii. TARURA iongezewe fedha na Serikali ili kuweza kuhudumia mtandao wa zaidi ya kilomita 108,000 inaohudumia nchini. Aidha, mgawo wa fedha wa asilimia 30 ambao TARURA inapata kutoka Mfuko wa Barabara (Road Fund) uongezwe hadi asilimia 50.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

##### **4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

i. Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

ii. Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21;

iii. Vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020;

iv. Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030 (*Sustainable Development Goals 2030*);

v. Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye uzinduzi wa Bunge la 11; na

vi. Maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa, Sera, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati ya Taasisi;

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI), imepanga kutekeleza malengo yake kwa kuzingatia vipaumbele kumi (13). Baadhi ya vipaumbele hivyo ni hivi vifuatavyo:-

i. Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuuji wa madaraka kwa umma (D by D);

ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu msingi bila ada; afya ya msingi, lisho na ustawi wa jamii katika mamlaka za serikali za mitaa;

iii. Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;

iv. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, programu na miradi katika ngazi ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

v. Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya ya msingi, elimu ya msingi na sekondari inayotekelezwa katika mamlaka za serikali za mitaa;

vi. Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika mamlaka za serikali za mitaa; na

vii. Kusimamia matumizi ya rasilmali na TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 7,019,800,353,000/=**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,729,880,457,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na

**Shilingi 2,289,919,896,000/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 3,878,738,058,000/=** sawa na asilimia 55.25 ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 851,142,399,000/=** sawa na asilimia 12.12 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Bajeti ya maendeleo ni sawa na asilimia 32.62 ya bajeti yote ya ofisi hii. Ufafanuzi zaidi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 03**.

**Jedwali Na. 03** Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mgawanyo wa Bajeti	Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021	Asilimia ya Makadirio (%)
Mishahara	3,878,738,058,000	55.25
Matumizi Mengineyo	851,142,399,000	12.13
Maendeleo	2, 289, 919, 896,000	32.62
<b>Jumla</b>	<b>7, 019,800, 353,000</b>	<b>100</b>

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2020/2021)

#### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 860,678,914,502/=**. Mapato hayo ni ongezeko la **Shilingi 63,758,435,216/=** sawa na **asilimia 8** ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2019/2020. Ulinganisho wa makusanyo kati ya mwaka wa fedha 2019/2020 na 2020/2021 umefafanuliwa zaidi katika **Jedwali Na. 04**.

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, faini

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mbalimbali, ada, tozo, marejesho ya masurufu na mishahara kwa makao makuu. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivyopo kwa mujibu wa sheria.

### Jedwali Na.4 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya Ndani

Ofisi/ Taasisi	Bajeti 2019/2020	Bajeti 2020/2021	Tofauti	Asilimia
OR – TAMISEMI na Taasisi	31,237,893,252	45,508,225,514	14,270,332,262	45.68
Mikoa	199,210,912	209,698,912	10,488,000	5.26
Halmashauri	765,483,375,122	814,960,990,076	49,477,614,954	6.46
<b>Jumla</b>	<b>796,920,479,286</b>	<b>860,678,914,502</b>	<b>63,758,435,216</b>	<b>8</b>

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI (2020/2021)

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati makusanyo yote yanatarajiwa kuongezeka kwa **shilingi 63,758,435,216/=** ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaomalizika. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 8. Kumekuwa na ongezeko la makusanyo kwa upande wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na taasisi zake na kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, huku makadirio ya makusanyo yakishuka kwa upande wa Mikoa.

Kwa upande wa Taasisi ongezeko la makusanyo ya maduhuli katika mwaka wa fedha 2020/2021 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/2020 linatokana na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kuongeza ukusanyaji wa wa mapato ya ndani katika vyanzo vya adhabu za makosa ya barabarani, tozo za maegesho ya magari, uuzaji wa nyaraka za zabuni na malipo ya matumizi ya maabara kwa ajili ya kupima vifaa vya ujenzi wa barabara. Aidha, Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo kimechangia ongezeko hilo kwa kuongeza udahili wa Wanafunzi.

Hata hivyo, bado Halmashauri zinatarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kutokana na maduhuli yake kuongezeka kwa takribani **shilingi 49,758,435,216** sawa na asilimia 6.5 ikilinganishwa na makusanyo ya Halmashauri katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, huenda ongezeko hilo limechangiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, na kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato.

#### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha ujao 2020/2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa pamoja zinaomba kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 7,019,800,353,000/=** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 4,729,880,457,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,289,919,896,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha hizo zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge, **Shilingi 14, 273,473,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) – Fungu 02.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla wake bajeti inayoombwa kuidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeongezeka kwa **Shilingi 811,807,573,231** sawa na asilimia 11.56 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaomalizika wa 2019/2020.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la asilimia 35.26 kutoka **shilingi 1,692,937,354,769/=** katika mwaka wa fedha 2019/2020 hadi **shilingi 2,289,919,896,000/=** kwa mwaka wa fedha ujao wa 2020/2021.

Uchambuzi zaidi umebaini kwamba, ongezeko la bajeti kwa ujumla wake, limetokana na Serikali kuongeza fedha za



maendeleo kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu nchini na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma katika sekta hizo. Hali hiyo inatoa taswira kwamba, katika kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia 2016/2017 hadi 2020/2021 bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeongezeka katika kipindi cha miaka minne isipokuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo ilipungua kwa asilimia 5.92.

**Mheshimiwa Spika**, katika kulinganisha Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kulikuwa na ongezeko katika pande zote mbili. Hata hivyo, ongezeko la bajeti ya Taifa ni dogo kwani lilikuwa ni **asilimia 5.4** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/2020, wakati ongezeko la Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika kipindi hicho lilikuwa ni **asilimia 11.56**.

Aidha, bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni sawa na asilimia 20.13 ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeongezeka kwa asilimia 1.39 ikilinganishwa na uwiano katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambao ulikuwa ni asilimia 18.74. Aidha, uwiano huu unabadili mwenendo wa uwiano uliokuwepo ambao ulipungua katika kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka mwaka wa fedha 2016/17 (asilimia 24) hadi mwaka wa fedha 2019/2020 (asilimia 18.74). Ulinganisho zaidi wa Uwiano wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Bajeti ya Taifa umefafanuliwa zaidi kupitia **Jedwali Na. 05**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuongeza bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwani inaonesha kutambua umuhimu wa Ofisi hii ambayo ina jukumu la kusimamia sekta nyingi katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohudumia na kugusa wananchi moja kwa moja ikiwa ni pamoja na kuunga mkono juhudi za wananchi katika shughuli za maendeleo.

Ni wazi kuwa ongezeko la bajeti ya ofisi hii litachangia kuunga mkono juhudi za wananchi kujiletea maendeleo kwa kusaidia ukamilishaji wa maboma mbalimbali yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

Aidha, ongezeko hilo la fedha linadhihirisha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujikita katika kujenga mfumo imara wa kuwahudumia wananchi ambao ndiyo msingi wa madaraka yote ya Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977. Njia madhubuti ya kujenga mfumo huo ni Serikali kuhakikisha inagatua rasilimali fedha za kutosha (kuongeza bajeti) na kuzipeleka kikamilifu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa umefafanuliwa zaidi kupitia **Jedwali Na. 06.** ambalo ni Kiambatisho “A” cha Taarifa hii ya Kamati.

**Jedwali Na. 05:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa mwaka wa fedha 2020/2021

BAJETI KUJ YA TAIFA 2020/2021			BAJETI YA OFISI YA RAIS – TAMISEMI 2020/2021		
Mgawanyo	Bajeti Kuu (Tsh. Milioni)	Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu	Mgawanyo	Bajeti ya Wizara (Tsh. Milioni)	Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara
OC	3,741,137	10.73	OC	851,142	12.13
Deri la Taifa	10,476,834	30.04	-	-	-
Mshahara	7,762,389	22.25	Mshahara	3,878,738	55.25
Maendeleo	12,899,433	36.98	Maendeleo	2,289,919	32.62
<b>Jumla</b>	<b>34,879,793</b>	<b>100</b>	<b>Jumla</b>	<b>7,019,800.4</b>	<b>100.00</b>

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya maendeleo na kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

i. Kamati inapongeza hatua ya Serikali kununua na kugawa mashine za kukusanyia **mapato 7,227 (POS)** kwa Halmashauri zote nchini, kwani hatua hii imepunguza mzigo kwa halmashauri ambazo zilikuwa na uwezo mdogo wa kununua mashine hizo, lakini pia kuongeza makusanyo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hadi mwezi Februari, 2020 Halmashauri zilikuwa zimekusanya **asilimia 61** ya lengo lililokusudiwa. Kamati inashauri Serikali iweke msisitizo zaidi katika matumizi ya mashine hizo ili kuhakikisha lengo lililokusudiwa linatimizwa kwa Halmashauri kuongeza na kudhibiti ufujaji wa mapato;

ii. Serikali ihakikishe halmashauri ambazo zinadaiwa na benki mikopo ya Waheshimiwa Madiwani iliyotokana na dhamana ya posho za kila mwezi, zinakamilisha ulipaji wa madeni hayo kabla ya tarehe 30 Mei, 2020. Hatua hiyo itasaidia kuondoa usumbufu ambao Madiwani wanaweza kukumbana nao kutoka kwenye benki hizo iwapo watamaliza kipindi cha uongozi bila ulipaji wa madeni hayo kukamilika. Mfano, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa halmashauri Sita (6) za Mkoa wa Singida pekee zilikuwa zinadaiwa jumla ya **shilingi milioni 688.75**, deni ambalo hata hivyo, uongozi wa mkoa uliahidi litakuwa limelipwa hadi mwishoni mwa mwezi Mei, 2020.

iii. Kamati inapongeza hatua ya baadhi ya halmashauri nchini kutumia fedha za vyanzo vya ndani na kushirikiana na wahisani kutoa taulo za kike kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika masomo. Miongoni mwa Halmashauri zilizofanya vizuri ni za mkoa wa Mara ambazo katika mwaka wa fedha 2018/19 zilitoa **taulo 33,617**; mwaka wa fedha 2019/2020 (hadi Februari, 2020) **taulo 25,429** na zimepanga kutoa **taulo 43,950**

katika mwaka ujao wa fedha. Kamati inashauri halmashauri nyingine nchini kubuni namna ya kuwasaidia watoto wa kike kutoka familia maskini kupata taulo hizo bure ili waweze kuhudhuria masomo kikamilifu wakati wote na kutimiza ndoto zao.

iv. Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya afya vikiwemo vituo vya Afya zaidi ya 350 na Hospitali za Wilaya 67 na kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo na hospitali zaidi katika mwaka ujao wa fedha. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuanza maandalizi ya kupata watumishi wa sekta ya afya na vifaa tiba ili miundombinu hiyo itakapokamilika wananchi waanze kupata huduma za matibabu;

v. Kamati inapongeza kazi nzuri inayotekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) katika kujenga na kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja katika maeneo inayoyasimamia. Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wakala huu ni kidogo sana ikilinganishwa na mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) inazohudumia. Kamati inashauri TARURA iongezewe fedha hasa katika mwaka huu wa fedha ili kukabiliana na uharibifu uliosababishwa na mvua ambazo zimekuwa zikinyesha nchini tangia mwishoni mwa mwaka jana. Aidha, Kamati inaendelea kusesitiza juu ya umuhimu wa kuongeza mgawo wa fedha wa asilimia 30 ambao TARURA inapata kutoka Mfuko wa Barabara (Road Fund) hadi asilimia 50.

vi. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya Halmashauri zinakiuka kifungu cha 37 A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kuhusu utengaji na utoaji wa fedha za 10% ya mapato ya ndani ili kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu, kwa kushindwa kutenga na kutoa fedha hizo kikamilifu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, Mikoa ya Kagera, Tabora na Singida ilifanya vizuri zaidi kwa kutoa Halmashauri tatu zilizoongoza katika utengaji na utoaji wa fedha za 10%. Aidha, Mikoa ya Simiyu na Manyara ilifanya vibaya kwa kutoa Halmashauri tatu zilizofanya vibaya zaidi. **Jedwali Na. 07** linafafanua zaidi.

**Jedwali Na.07** Mikoa na Halmashauri zilizofanya vizuri/vibaya utoaji wa asilimia 10 ya Mapato ya Ndani

Mkoa	Mikoa na Halmashauri zilizofanya vizuri			Mikoa na Halmashauri zilizofanya vibaya		
	Kagera	Tabora	Singida	Simiyu	Manyara	
Halmashauri	Karagwe	Tabora(M)	Singida(M)	Meatu	Kiteto	Babati (M)
Asilimia (%)	143	136	127	9	11	21
Nafasi	1	2	3	1	2	3

**Chanzo:** Randama za Mikoa kwa Mwaka wa fedha 2020/2021

**NB:** Aidha, mchanganuo wa namna halmashauri zilivyotenga na kutoa asilimia 10 ya mapato ya ndani umefafanuliwa zaidi kupitia **Jedwali Na. 08.** ambalo ni Kiambatisho “**B**” cha Taarifa hii ya Kamati.

vii. Halmashauri zisaidie Vikundi vya Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu kutumia fedha za 10% ya mapato ya ndani kuanzisha miradi mikubwa ya maendeleo na hivyo kutoa ajira na kuchangia mapato ya Serikali, badala ya wanachama wa vikundi hivyo kugawana fedha hizo. Baadhi ya Halmashauri zimesaidia Vikundi kuanzisha miradi mikubwa ya kiuchumi.

Mfano; Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, imesaidia Kikundi cha Jukwaa la Wanawake wa Mibulani kinachojihusisha na utunzaji wa mazingira kwa kuwanunulia gari la uzoaji taka na vifaa vingine kwa thamani ya **shilingi milioni 189**. Kupitia mkopo huo Wanawake 102 wanaounda kikundi hicho wamepata ajira, na kila mwezi wanarejesha **shilingi milioni 6** za mkopo huo ambao utalipwa ndani ya miaka mitatu. Aidha, Halmashauri hiyo imewezesha Kikundi cha Jukwaa la Wanawake wa Temeke (JUWATE) kuanzisha kiwanda cha ushonaji wa sare za viwandani kwa kuwanunulia

vyerehani na mashine nyingine zenye thamani ya **shilingi milioni 126**. Mbali na kuwezesha kiuchumi Wanachama wake wapatao 75, mradi huo umeajiri wafanyakazi 33 (mafundi 30, Mhasibu, Katibu Muhutasi na Meneja). Mkopo huo utalipwa ndani ya miaka minne kwa rejesho la **shilingi milioni 2.6** kwa mwezi.

viii. Serikali ihimize halmashauri nchini kutenga na kupeleka kikamilifu asilimia 60 (Majiji na Manispaa) na asilimia 40 (Wilaya na Miji) ya mapato ya ndani kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya Halmashauri zinafanya vizuri katika eneo hili, huku baadhi zikifanya vibaya na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi. Mikoa mitatu iliyoongoza katika utoaji wa fedha za maendeleo kutokana na mapato ya ndani ni Geita (wastani wa asilimia 96); Njombe (wastani wa asilimia 95) na Mara (wastani wa asilimia 92). Aidha kwa upande wa mikoa mitatu iliyofanya vibaya zaidi ni Rukwa (Wastani wa asilimia 30); Dodoma (wastani wa asilimia 42) na Tanga (wastani wa asilimia 53). Aidha, Jedwali Na. 9 linafafanua zaidi kuhusu Halmashauri zilizofanya vizuri na Halmashauri zilizofanya vibaya.

**Jedwali Na.9:** Halmashauri zilizofanya vizuri/vibaya katika utoaji wa fedha za maendeleo kutokana na makusanyo ya ndani.

Halmashauri	Halmashauri zilizofanya vizuri			Halmashauri zilizofanya vibaya		
	Ruangwa	Magu	Tarime	Kakonko	Chamwino	Chemba
Asilimia (%)	120	110	108	10.4	13.25	13.28
Nafasi	1	2	3	1	2	3

ix. Halmashauri ziendelee kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza wigo wa mapato katika halmashauri hizo na hivyo kuzifanya kuepuka kuongeza kodi mara kwa mara ambazo ni kero kwa wananchi. Miongoni mwa njia za kuongeza mapato ni kubuni miradi ya kimkakati na kuandaa maandiko na kuyawasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ajili ya kuomba

fedha za utekelezaji. Aidha, ofisi hiyo ipunguze urasimu katika kupitia maandiko hayo ili kuwezesha Halmashauri kutekeleza miradi hiyo;

x. Serikali isimamie kikamilifu ili kuhakikisha halmashauri zinapeleka kikamilifu fedha zinazotokana na asilimia 60/40 ya mapato ya ndani katika halmashauri hizo kwenye miradi ya maendeleo iliyokusudiwa na siyo kutumika kwenye shughuli za uendeshaji wa ofisi;

xi. Serikali ielekeze halmashauri zishirikiane na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kuanzisha katika kila halmashauri Kituo Kimoja cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara (***One Stop Business Formalization and Development Centre***) ili kurahisisha, kuharakisha na kupunguza gharama kwa mfanyabiashara. Kamati inapongeza Serikali kwa kituo cha aina hiyo katika Manispaa ya Singida, ambacho kinafanya vizuri sana kwani kimesaidia kuondoa kero kwa wananchi pale wanapotaka kuanzisha au kurasimisha biashara zao na kinachochea maendeleo. Aidha, ni muhimu kushirikisha wadau wengine muhimu kama Benki, TRA, BRELA, SIDO, n.k;

xii. Ofisi ya Rais – TAMISEMI ifuatilie na kuchunguza ukusanyaji wa mapato unaotekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke katika eneo linalomilikiwa na EPZA Kurasini ili kubaini iwapo hakuna ufujaji wa mapato ya Serikali; na

xiii. Serikali iboreshe usimamizi wa masuala ya Watumishi wa Halmashauri ili kuhakikisha upandaji wa madaraja na kubadilishiwa mishahara, uhamisho na stahiki nyingine zinatolewa kikamilifu na kwa wakati na hivyo kuondoa malalamiko miongoni mwa Watumishi;

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa Taarifa hii. Kwa kutambua kuwa hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati katika Bunge hili la Kumi na Moja, nitumie fursa hii kuwatakiwa Wajumbe wa Kamati pamoja na Wabunge wengine wote kila lakheri katika uchaguzi ujao na panapo majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, turejee sote katika Bunge lijalo ili kuendeleza gurudumu la ujenzi wa Taifa letu kwa kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuwakilisha wananchi na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii inashughulikia mafungu ya bajeti 36 ambayo ni mengi kuliko Kamati nyingine ya Bunge, na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa muda mrefu na wakati mwingine hadi jioni kabisa. Licha ya mazingira hayo Wajumbe walitekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, hii ikiashiria utayari wao wa kuitumikia Bunge, Taifa na Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb
5. Mhe.George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba,Mb
7. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
8. Mhe.Hamad Salim Maalim, Mb
9. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
10. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
11. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum,Mb



12. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
13. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
14. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
15. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
16. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
17. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
23. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
24. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb
25. Mhe. Mansoor Hirani Shanif, Mb
26. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Seleman Said Jafo (Mb) kwa ushirikiano mkubwa aliouonesha kwa Kamati ambao umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake. Utendaji wake na Naibu Mawaziri wake, Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mhe. Waitara Mwita Mwikwabe (Mb) umedhihirisha jinsi walivyo hazina kubwa kwa ustawi na maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini na maendeleo ya Taifa hili.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph Nyamuhanga, akisaidiana na Naibu Makatibu Wakuu, Dkt. Dorothy Gwajima na Ndg. Gerald Mweli kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, shukrani za Kamati ziwaendee Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa utekelezaji makini wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha, na uwasilishaji mzuri wa Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndg. Gerlad Magili, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima, Ndg. Asmin Kihemba na Ndg. Prosper Minja wakisaidiwa na Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Jasson S. Rweikiza (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA**

**NA SERIKALI ZA MITAA**

08 Aprili, 2020

## KIELELEZO "A"

**Jedwali Na 6:** Mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya OR - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Eneo la Matumizi	Makadirio 2019/2020 (Tsh. 000)	Makadirio 2020/2021 (Tsh. 000)	Tofauti Ongezeko/ Upungufu (Tsh. 000)	Asilimia (%)
<b>Matumizi ya Kawaida</b>				
<b>Mishahara:</b>				
OR - TAMISEMI (HQ)	10,836,663	11,298,245	461,582	4.23
Taasisi	33,385,105	42,148,645	8,763,540	26.25
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)	9,899,012	8,165,271	-1,730,741	17.48
Mikoa	83,654,030	76,896,293	-6,757,737	8.08
Halmashauri	3,669,329,614	3,740,229,604	70,889,990	1.93
<b>Jumla Mishahara</b>	<b>3,807,104,425</b>	<b>3,878,738,058</b>	<b>71,633,633</b>	<b>1.88</b>
<b>Matumizi Mengineyo:</b>				
OR - TAMISEMI (HQ)	7,896,530	70,643,361	62,746,831	794.61
Taasisi	1,318,870	1,318,870	0	0
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)	6,002,155	6,108,202	106,047	1.77
Mikoa	41,803,829	58,998,656	17,194,827	41.13
Halmashauri	650,929,615	714,082,310	63,152,695	9.7
<b>Jumla Matumizi Mengineyo</b>	<b>707,951,000</b>	<b>849,832,529</b>	<b>141,881,529</b>	<b>20.04</b>
<b>Jumla Matumizi ya Kawaida</b>	<b>4,515,055,425</b>	<b>4,729,880,457</b>	<b>214,825,032</b>	<b>4.76</b>
<b>Fedha za Maendeleo:</b>				
OR - TAMISEMI	463,563,123	578,047,184	114,484,061	24.7
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)		500,000	500,000	100
Mikoa	67,333,480	85,992,688	18,659,208	27.71
Halmashauri	1,162,040,750	1,625,380,024	463,339,274	39.87
<b>Jumla ya Maendeleo</b>	<b>1,692,937,354</b>	<b>2,289,919,896</b>	<b>596,982,542</b>	<b>35.26</b>
<b>JUMLA KJU</b>	<b>6,207,992,779</b>	<b>7,019,800,353</b>	<b>810,497,704</b>	<b>17.1</b>

**Chanzo:** Randama ya OR - TAMISEMI (2020/2021)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Japhary ambaye ni Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**MHE. JAPHARY J. MICHAEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KATIKA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na pia kuangalia utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa nitoe pongezi kwa vyama vyote vya ushindani kwa kuendelea kuwepo na kuendelea kutimiza jukumu kubwa la kuiwajibisha Serikali kwa wananchi kwa vile uwepo wao umesababisha baadhi ya mambo kufanyika hata kama siyo kwa weledi na ufanisi ambao ungetamalaki kama nchi hii ingekuwa imeongozwa na Serikali ya Chama tofauti na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pole na hongera nyingi sana kwanza kwa Viongozi Waandamizi wa CHADEMA kwa madhila ambayo wamekutana nayo kwa kipindi cha takriban miaka miwili na nusu wakiwa katika Mahakama kwa kesi ambayo tunaamini ilikuwa na lengo la kudhalilisha Sheria ya Vyama vya Siasa. Pili, ni kwa Watanzania wote kwa umoja wao kuhakikisha kwamba wanachangia Viongozi wote wa CHADEMA ambao walipatikana na hatia na hivyo kuamuliwa kulipa faini ya shilingi milioni 350. Mungu awabariki sana Watanzania wote waliofanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Moshi Mjini kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote ambacho nimekuwa Mbunge, sambamba na kipindi ambacho nilikuwa *Mayor* wa Halmashauri ya Manispaa ya

Moshi. Nawaomba waendelee na mshikamano katika kuhakikisha Moshi inaendelea kuwa mahali salama katika kuendeleza uchumi wa wananchi wake na pia sehemu ya kutoa uongozi uliotukuka kwa wananchi wake. Hilo wananchi wa Moshi mnaliona na siyo jambo la kushawishiwa ila linaonekana kwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu ambayo imenivumilia sana kwa kipindi chote ambacho nimekuwa nje ya familia kwa ajili ya kutimiza wajibu wangu kwa Chama changu cha CHADEMA na kwa Bunge. Nasema asanteni sana, tuendeleo kuvumiliana katika hilo na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi, naomba sasa kuanza kupitia utendaji wa Wizara hii kwa kadri ambavyo inawezekana kutokana na ukweli kwamba Wizara hii ni Serikali ambapo kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania Ibara ya 145 na 146 inatakiwa kutekeleza majukumu yake kufuatana na maelekezo ya Katiba na pia kwa sheria zilizotungwa na Bunge, bila hila ya kupoka mamlaka za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara tajwa za Katiba ndiyo kichocheo kikubwa cha uanzishwaji wa Sera ya Ugatuuji wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa na sheria zikatayarishwa na maboresho yakafanyika kwa fedha za wananchi, lakini sasa kinachoendelea ni hila za kupoka mamlaka hayo na kuyarejesha Serikali Kuu. Jambo hili siyo jema na litaelezwa baadaye katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote Serikali za Mitaa zina majukumu makubwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kulingana na taratibu, kanuni na sheria zinazoiongoza jamii husika. Kwa Tanzania sheria ndogo hutungwa na Baraza la Madiwani ambacho ndicho chombo cha uwakilishi wa wananchi kwenye Halmashauri husika. Ili Halmashauri zitimize wajibu wake wa kutoa huduma kwa jamii, zinahitajika kuwa na uwezo wa kukusanya rasilimali, fedha pamoja na rasilimaliwatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya majukumu hayo ya utoaji wa huduma za msingi, pia katika nchi yetu Halmashauri zinaongezewa wigo wa majukumu kama vile kupunguza umasikini katika jamii, kupunguza vifo vya mama na mtoto, kupambana na UKIMWI pamoja na virusi vyake. Sasa tungetegemea Halmashauri zetu ziwe na uwezo wa kupambana na mlipuko wa *Corona* na kuhakikisha njaa katika jamii inakuwa ni historia. Mbali na ongezeko la majukumu kwa Serikali za Mitaa, bado Halmashauri zetu hazina uwezo wa kifedha kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama ambavyo imeonyeshwa katika nukuu tuliyoonyesha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu huo wa rasilimali kwa Halmashauri zetu, inalazimu kutegemea uwezeshwaji kutoka Serikali Kuu jambo ambalo linaathiri sana utendaji wa Halmashauri zetu katika kukabiliana na mahitaji ya wananchi. Uendeshaji au uhuru wa Mabaraza ya Madiwani katika kupanga na kuamua mgawanyo wa rasilimali zao kwa mujibu wa vyanzo vya mapato ambavyo vipo kisheria, siyo jambo la hisani, bali ni jukumu lao kisheria, na hivyo kitendo cha kupoka madaraka hayo ni kutowatendea haki wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ni vyema tukafahamu vizuri uhusiano, haki na sheria katika uendeshaji wa nchi. Msingi mkubwa wa kuendesha nchi au taasisi yoyote ni haki, sheria zinakuja baadaye. Kwani kuna wakati sheria zetu zinatungwa kwa hila ili kutimiza matakwa ambayo siyo ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kama ilivyoainishwa kwenye Hati Idhini ya mgawanyo wa majukumu ya Wizara za Serikali ni kusimamia utekelezaji wa Sera za Ugatuuji Madaraka (*D by D*) na kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, katika ugatuuji wa madaraka hatuwezi kuongelea jambo hilo bila ya

kuangalia uwezo wa Halmashauri zetu kifedha na nguvu ya kujitegemea katika muktadha mpana ambao msingi wake mkuu ni uwezo wake wa kujitegemea kifedha. Katika hili ni vyema tuangalie sheria zinatoa mwanya wa kupata fedha na kwa jinsi gani uwezo wa kujitegemea unafifishwa kwa makusudi ili wananchi waendeleo kuwa masikini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimeainishwa katika vifungu 6 na 9 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (*The Local Government Finance Act, No. 9 of 1982*). Kulingana na Sheria ya Fedha Na. 9 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na. 15 ya mwaka 2003 (*The Finance Act No. 15 of 2003*), Serikali za Mitaa hazitozi kodi za mapato, bali kodi hiyo hutozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Ni muhimu sana, tupewe hiyo tathmini ya hali za Halmashauri zetu katika kutimiza majukumu yake ya msingi kama ambavyo tumeainisha hapo awali tangu Serikali ya Awamu ya Tano iinge madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, thathmini hiyo ni lazima ijibu swali la nia njema ya kupeleka madaraka kwa wananchi (*d by d*) iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu na kuendelezwa na ile Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya Mapato kwa Mujibu wa Sheria. Maelezo au ufafanuzi wa utendaji kazi wa Serikali za Mitaa umetolewa katika sheria iliyotungwa na Bunge yaani Sheria ya *“The Local Government (District Authorities) Act, and The Local Government (Urban Authorities) Act”* ya mwaka mwaka 1982.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya utafiti wa utekelezaji wa sheria hiyo, unaonyesha Serikali Kuu imeshindwa kuweka mkakati uliowazi na makini wa kufanikisha matakwa ya Kikatiba na Kisheria. Katika uchambuzi huo kwa ngazi ya mkakati wa utekelezaji umeeleza kuwa hakuna mpango mahususi unaohusiana na ugatuaji madaraka unaonesha majukumu na mipaka ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vigezo au viashiria vilivyoonyesha mkanganyiko kwa Sera ya Ugatuuji wa Madaraka kwa mujibu wa andiko hilo ni *Transfer of competencies and sector-based policies*, Serikali za Mitaa hapa nchini sio taasisi inayojitegemea kama inavyotakiwa kuwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Uhawilishwaji wa raslimali watu katika Serikali za Mitaa ni matakwa ya Serikali Kuu na si matakwa ya Serikali za Mitaa, pili uteuzi na ajira kwa watumishi hufanywa na Serikali Kuu kupitia kwa kilinachoitwa- "*Local Government Service Commission*". Hivyo jambo hilo husababisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokuwa na uwezo wa kuajiri au kufukuza mtumishi hadi pale Mamlaka iliyofanya uteuzi au uajiri kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mojawapo ya sababu za kushindwa kufanya vizuri katika utoaji wa huduma za msingi kwa wananchi kwa Halmashauri nyingi hapa nchini inatokana na kukosa au kutokuwa na uwezo kwenye utawala na fedha katika kutoa maamuzi yanayohusu maendeleo ya Halmashauri zao. Badala yake maamuzi mengi ya kiutawala na kifedha yanatolewa na Serikali Kuu, na utendaji wa Halmashauri nyingi kwa sehemu kubwa unaingiliwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali ya Awamu ya Tano ikatazama juhudi iliyofanywa na Serikali za awamu zilizotangulia hususani awamu ya tatu na ya nne ambazo zilifanikiwa kukaribia lengo na dhana nzima la ugatuuji wa madaraka kama linavyoelezwa katika Ibara ya 154 na 156 lakini kwa bahati mbaya tumerudi nyuma miaka takriban 25 iliyopita. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyenzo muhimu inayotumiwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa inazidi kuhodhi madaraka ya Serikali za Mitaa ni kuhodhi watumishi waandamizi *senior staffs* wa Serikali za Mitaa walio kwenye sekta za utawala, afya, fedha, kilimo na kadhalika, wote hawa huteuliwa kutoka Serikali Kuu.



Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Serikali za Mitaa baadhi ya majukumu yake ya msingi ili kuimarisha demokrasia na utawala bora ni pamoja na kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuuji wa Madaraka kwa Umma *D by D*, kuwezesha maandalizi na Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kusimamia matumizi ya rasilimali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, lisho na ustawi wa jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli hizo haziwezi kufanikiwa ikiwa kila kitu kinategemea kutoka Serikali Kuu, kutokana na ukweli kwamba Halmashauri zetu hazina vyanzo vya mapato vya uhakika kwani vimepokwa na Serikali Kuu. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa uwezeshaji wa kweli utatokana na mapinduzi ya kidemokrasia yanayohusiana na nguvu ya umma, uwezeshaji utaletwa na watu kwa ajili ya watu. Uwezeshaji hapa utaanzia kwa watu wenyewe kwa kuangalia watu wanataka nini na sio dola kuamua kwa niaba ya wananchi. Misaada toka kwenye taasisi na asasi za Serikali itasaidia pale tu ambapo jamii itakuwa tayari kwa misaada hiyo na tayari ina mipango yake ya maendeleo. Kinyume na hapo ni kupoteza rasilimali nyingi bila ya kuwepo matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa ielewe kwamba vyanzo ilivyovipora kutoka halmashauri ndio vilikuwa vyanzo vikubwa na nguzo imara ya kuzifikisha halmashauri nyingi kufikia malengo ya kuondokana na utegemezi wa Serikali Kuu katika kutimiza majukumu yake ya msingi ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa ardhi ndiyo rasilimali pekee ambayo kila halmashauri katika nchi inaimiliki. Ardhi ndiyo chanzo cha mapato cha uhakika kwa kila halmashauri ya nchi hii, hivyo basi Serikali Kuu kujaribu

kufifisha uwezo wa makusanyo ya chanzo hiki ni kuifanya halmashauri kushindwa kabisa kutoa huduma za msingi kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zinatakiwa kuchukua 30% ya kodi ya ardhi, hivyo inapotokea kuwa Serikali Kuu inachukua fedha hizo na urejeshaji wake unakuwa ni pale itakapojiridhisha kuwa zinahitajika, hilo sio sahihi kwa maendeleo ya wananchi. Chanzo cha mapato ya halmashauri kinachotokana na kodi ya ardhi kama makusanyo ya ndani ni muhimu sana katika kuzifanya halmashauri zikabiliane na changamoto mbalimbali za kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ukusanyaji ufanywe na halmashauri kama ambavyo ilikuwa inafanyika miaka yote na ziada au hitaji la fedha la Serikali lipelekwe na halmashauri na sio kinyume chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala wa Mabaraza ya Madiwani, dhana nzima ya ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa inatoa madaraka kwa utawala na upangaji wa mipango kwenye Wilaya kwa Baraza la Madiwani. TAMISEMI ndio mlezi wa halmashauri ikihusishwa na Mabaraza ya Madiwani pia, lakini imeshindwa kukemea mambo ambayo yameshika kasi kwa siku za karibuni ya kuhakikisha wale wote waliopewa ridhaa na wananchi ya kuendesha halmashauri hizo katika uchaguzi wa Oktoba 2015, hasa wale kutoka vyama nje ya CCM wanafanyiwa hila na kuondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kubwa kwa Serikali inayojinasibu kuwa ni ya kidemokrasia na inafuata misingi ya utawala bora, kwa makusudi kushindwa hata kuona au kutekeleza dhana ndogo ya madaraka kwa umma, pale ambapo wananchi wanatoa ridhaa kwa chama cha Upinzani kutoa Mwenyekiti wa kuongoza halmashauri, mara tu anaondolewa kwa hila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kweli kati ya Halmashauri takriban 134 zilizopo hapa nchini ni Wenyeviti au Mameya wanaotoka Vyama vya Upinzani tu ndio wenye shida na hivyo kuondolewa? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hizo hila zinazofanywa na Wakuu wa Mikoa za kuwaondoa Mameya au Wenyeviti wa Halmashauri ni kipimo kwa Waziri mwenye dhamana kama kweli anawajibika kwa jamii na kufuata utekelezaji wa sera ya *D by D*. Tukumbuke kwamba Meya sio mtendaji kwa nafasi yake na stahili zake zote anazipata kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, hivyo kwa hali ya kawaida ubadhirifu wa Meya unatoka wapi na Mkurugenzi kubakia akiwa ni msafi na mchapa kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, kwa mfumo huu ambao umeibuka katika Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha inasigina Katiba na sheria zake ni ishara mbaya sana katika kufikia lengo la kuwa na Serikali za Mitaa zenye nguvu. Tukumbuke kwamba toka mfumo wa vyama vingi uanze hapa nchini, kuna halmashauri kama vile Karatu, Kigoma, Ujiji, Bariadi, Moshi Mjini, Musoma Mjini, Tarime ambazo zilikuwa chini ya Upinzani katika Serikali za Awamu ya Tatu na ya Nne lakini hatujawahi kusikia hiki kinachoitwa kuondolewa kwa Wenyeviti wa Halmashauri hizo eti kwa matumizi mabaya ya ofisi halafu Wakurugenzi wakibaki salama. Ni muhimu sana Serikali ya Awamu ya Tano iheshimu maamuzi ya wananchi hata wanapochagua wawakilishi wao kutoka vyama vya upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwezo wa Halmashauri zetu Kukabiliana na Janga la Corona. Halmashauri ndizo zenye watu, na shughuli nyingi za kijamii na za kiuchumi zinafanyika zaidi kwenye maeneo yao. Shughuli za kiuchumi kama vile usafirishaji wa abiria kwa boda boda, bajaji, daladala, masoko katika maeneo mbalimbali na kadhalika na vituo vya kuabudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhibitaji wa ugonjwa huu kwa kiasi kikubwa kinga yake tunaambiwa ni usafi na kujitenga, kuzuia misongamano ya watu katika maeneo mbalimbali ya kijamii na kibiashara. Hoja yetu ya msingi ni

kutaka kupata maelezo ni kwa vipi halmashauri zetu zimejipanga kwa uwezo wa kifedha wa kuzuia maambukizi kuenea katika maeneo takribani yote yenye mkusanyiko wa watu.

Mhesimiwa Naibu Spika, ni kwa vipi pale itakapohitajika kuwapo na vituo vya "isolation", matayarisho yake kwa sasa yako vipi na kwa kila halmashauri ina mkakati gani kuhakikisha inakabiliana na maambukizi badala ya kutegemea Serikali Kuu ambayo nayo uwezo wake wakati mwingine ni mdogo. Ni kwa kiasi gani kila halmashauri ina uwezo wa kuhakikisha vyakula kwenye masoko yake vinauwezo wa kuhimili msukosuko wa kipindi endapo jambo hili litakuwa limekuwa janga kubwa watu wakawa katika karantini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa Serikali kwamba, ni vyema kujiandaa vilivyo kupambana ili kuepusha madhara makubwa pale mapambano yatakapoanza. Hivyo kinga ni bora kuliko tiba. Naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, ni ukweli uliowazi kuwa TAMISEMI ni Wizara ambayo inahudumia Watanzania wote ikiwa na lengo la kuifanya kuwa na mamlaka kamili kwa mujibu wa Ibara ya 145 na 146 sambamba na sera ya ugatuaji wa madaraka. Kitendo chochote kitakachofanyika cha kuiondolea TAMISEMI hasa Mabaraza ya Halmashauri uhuru wao katika kuhakikisha yanatoa huduma kwa wananchi, ni kitendo ambacho hakitoleta maendeleo kwa wananchi wengi, na hivyo kinapingana na dhana nzima ya wananchi kuwa ndio wenye Mamlaka ya kuamua, kupanga na kushiriki katika mchakato mzima wa kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani mara zote imekuwa ikishauri na kutahadharisha juu ya azma ya Serikali inayopoka madaraka ya wananchi na kuyarudisha Serikali Kuu kuwa ni kuharibu kabisa mfumo wa kuipeleka nchi yetu kuwa nchi ya uchumi wa kati na nchi inayotegemea

viwanda. Kwa bahati mbaya sana Serikali ya CCM imeshindwa kuelewa dhana hiyo ya wananchi kuwa wamiliki na wasimamizi wa mipango na miradi yao ya maendeleo. Jambo hilo la kupoka uhuru na vyanzo vikubwa vya mapato kwa halmashauri, limesababisha halmashauri nyingi kushindwa kujendesha na hivyo kushindwa kutoa huduma za msingi kwa wananchi. Hivyo basi kuwa tegemezi na ombaomba kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, tunawataka wananchi ambao wametuelewa hasa katika dhana nzima ya kutoa uhuru kamili kwa Serikali za Mitaa kupitia Mabaraza ya Madiwani, tuungane wote kurejesha kile ambacho Serikali ya awamu ya tatu ilikianzisha cha kufanya maboresho ya Serikali za Mitaa ili kuwa imara katika kutetea maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha ahsante sana. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI, MHESHIMIWA  
JAPHARY RAPHAEL MICHAEL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI  
MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA OFISI HIYO,  
KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021- KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za  
Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu hivyo kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na pia kuangalia utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**2. Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa nitoe pongezi kwa vyama vyote vya ushindani kwa kuendelea kuwepo na kuendelea kutimiza jukumu kubwa la kuiwajibisha Serikali kwa wananchi kwa vile uwepo wao umesababisha baadhi ya mambo kufanyika hata kama sio kwa weledi na ufanisi ambao ungetamalaki kama nchi hii ingeongozwa na Serikali ya chama tofauti na CCM.

**3. Mheshimiwa Spika**, nitoe pole na hongera nyingi sana kwanza kwa viongozi waandamizi wa CHADEMA kwa madhila ambayo wamekutana nayo, kwa kipindi cha takriban miaka miwili na nusu kuwa katika mahakama kwa kesi ambayo tunaamini ilikuwa na lengo la kudhalilisha Sheria ya Vyama vya Siasa. Pili ni kwa Watanzania wote kwa umoja wao kuhakikisha wanachangia viongozi wote wa CHADEMA ambao walipatikana na hatia na hivyo kuamuliwa kulipa faini ya shilingi milioni 350. Asanteni sana Watanzania kwa kuifanya demokrasia na utawala bora kushinda majaribu.

**4. Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Moshi Mjini kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote ambacho nimekuwa Mbunge sambamba na kipindi ambacho nilikuwa Mayor wa Halmashauri hiyo. Nawaomba tuendelee kushikamana katika kuhakikisha MOSHI inaendelea kuwa mahali salama katika kuendeleza uchumi wa wananchi wake na pia sehemu ya kutoa uongozi uliotukuka kwa wananchi wake, hilo wana-MOSHI mnaliona na sio jambo la kushawishiwa ili kuliona.

**5. Mheshimiwa Spika**, Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu ambayo imenivumilia sana kwa kipindi chote ambacho nimekuwa nje ya familia kwa ajili ya kutimiza wajibu wangu kwa Chama na kwa Bunge, nasema asanteni sana na tuendelee kuvumiliana katika hilo.

## **B. MAPITIO YA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**6. Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba sasa kuanza kupitia utendaji wa Wizara hii kwa kadri ambavyo itawezekana kutokana na ukweli kwamba Wizara

hii ni Serikali ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania Ibara ya 145 na 146 inatakiwa kutekeleza majukumu yake kufuatana na maelekezo ya Katiba na pia kwa sheria zilizotungwa na Bunge, bila ya hila ya kupoka mamlaka za wananchi.

**7. Mheshimiwa Spika**, Ibara tajwa za Katiba ndio kichocheo kikubwa cha uanzishwaji wa Sera ya Ugatujaji wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa (kwa wananchi) na sheria zikatayarishwa na maboresho yakafanyika kwa fedha nyingi za wananchi wenyewe, lakini sasa kinachoendelea ni hila za kupoka mamlaka hayo na kuyarejesha Serikali Kuu, jambo hili litaelezwa hapo baadae.

**8. Mheshimiwa Spika**, Duniani kote Serikali za Mitaa zina majukumu makubwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kulingana na taratibu, kanuni na sheria zinazoiongoza jamii husika. Kwa Tanzania sheria ndogo (by laws) hutungwa na Baraza la Madiwani ambalo ndicho chombo cha uwakilishi wa wananchi kwenye Halmashauri husika. Ili Halmashauri zitimize wajibu wake wa kutoa huduma kwa jamii zinahitajika kuwa na uwezo wa kukusanya rasilimali mali, fedha pamoja na rasilimali watu.

**9. Mheshimiwa Spika**, Mbali ya majukumu hayo ya utoaji wa huduma za msingi, pia katika nchi yetu Halmashauri zimeongezewa wigo wa majukumu kama vile kupunguza umasikini katika jamii, kupunguza vifo vya mama na mtoto, kupambana na UKIMWI pamoja na virusi vyake, na sasa tungetegemea Halmashauri zetu zinakuwa na uwezo wa kupambana na mlipuka wa Corona, kuhakikisha njaa katika jamii inakuwa ni historia. Mbali na ongezeko la majukumu kwa Serikali za Mitaa, bado Halmashauri zetu hazina uwezo wa kifedha kuweza kutekeleza majukumu yake kwa kikamilifu (PMO-RALG, 2013; Repoa, 2008; URT, 2016 and LGCDP, 2010).

**10. Mheshimiwa Spika**, Kutokana na ufinyu huo wa rasilimali kwa Halmashauri zetu inazilazimu kutegemea uwezeshwaji kutoka Serikali Kuu jambo ambalo linaathiri sana utendaji wa Halmashauri zetu katika kukabiliana na mahitaji ya wananchi.

**11. Mheshimiwa Spika**, uendeshaji au uhuru wa Mabaraza ya Madiwani katika kupanga na kuamua mgawanyo wa rasilimali zao kwa mujibu wa vyanzo vya mapato ambavyo vipo kisheria sio jambo la hisani, bali ni jukumu lao la kisheria, hivyo kitendo cha kupoka madaraka hayo ni kutokuwatendea haki wananchi. Aidha ni vyema tukafahamu vizuri uhusiano wa HAKI na SHERIA katika uendeshaji wa nchi, na msingi mkubwa wa kuendesha nchi au taasisi yoyote ni HAKI, sheria zinakuja baadae, kwani kuna wakati sheria zetu zinatungwa kwa hila ili kutimiza matakwa ambayo sio ya HAKI.

**12. Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya majukumu ya msingi ya OR-TAMISEMI ni kama ilivyoainishwa kwenye Hati Idhini ya mgawanyo wa majukumu ya Wizara za Serikali ni; kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuuji Madaraka (D by D), na kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria; hivyo basi,

**13. Mheshimiwa Spika**, katika ugatuuji wa madaraka hatuwezi kuongelea jambo hilo bila ya kuangalia uwezo wa Halmashauri zetu kifedha, na nguvu ya kujitegemea katika muktadha mpana ambao msingi wake mkuu ni uwezo wake wa kujitegemea kifedha. Katika hili ni vyema tuangalie sheria zinazotoa mwanya wa kupata fedha (vyanzo vya mapato) na kwa jinsi gani uwezo wa kujitegemea unavyofifishwa kwa makusudi ili wananchi waendeleo kuwa masikini.

**14. Mheshimiwa Spika**, Vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimeainishwa katika vifungu Na. (6) hadi (9) vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 yaani The Local Government Finance Act, No. 9 of 1982. Kulingana na Sheria ya Fedha Na. 9 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na. 15 ya mwaka 2003 yaani The Finance Act No. 15 of 2003, Serikali za Mitaa hazitozi Kodi ya Mapato bali kodi hiyo hutozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Ni muhimu sana, tupewe tathmini ya hali za Halmashauri zetu katika kutimiza majukumu yake ya msingi kama ambavyo tumeyaaainisha hapo awali tangu Serikali ya awamu ya tano iinge madarakani. Thathmini hiyo



ni lazima ijibu swali la nia njema ya kupeleka madaraka kwa wananchi (d by d) iliyoanzishwa na Serikali ya awamu ya tatu na kuendelezwa na ile ya awamu ya nne.

**15. Mheshimiwa Spika**, ni vyema kwa ufupi tukaorodhesha vyanzo vya mapato kama vilivyokuwepo kabla ya vingine vikubwa kupokwa na Serikali Kuu, kwa sababu ambazo zilikuwa ni za kisiasa zaidi kuliko za kimaendeleo na dhana nzima ya uwepo wa Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Ibara za 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hali ilivyo sasa katika dhana nzima ya kuhakikisha Halmashauri zetu zinajitegemea nchi yetu ina utawala lakini inakosa uongozi.

#### **C. VYANZO VYA MAPATO KWA MUJIBU WA SHERIA**

**16. Mheshimiwa Spika**, ifuatayo ni orodha ya vyanzo vya mapato, ambavyo ni nguzo ya kuimarisha dhana nzima ya Ugatuzi wa Madaraka (D by D) mbali na kuwa na uwezo wa kumiliki rasilimali watu katika muktadha wa utawala na fedha.

#### **A. Taxes on Property**

i. Property rates.

#### **B. Taxes on Goods and Services**

- i. Crop cess (maximum 5% of farm gate price)
- ii. Forest produce cess

#### **C. Taxes on Specific Services**

i. Guest house levy

#### **D. Business and Professional Licenses**

- i. Commercial fishing license fees
- ii. Intoxicating liquor license fee
- iii. Private health facility license fee
- iv. Taxi license fee
- v. Plying permit fees
- vi. Other business licenses fees

#### **E. Motor Vehicles, Other Equipment and Ferry Licenses**

i. Vehicle license fees -

- ii. Fishing vessel license fees

#### **F. Other Taxes on the Use of Goods, Permission to Use Goods**

- i. Forest produce license fees
- ii. Building materials extraction license fee
- iii. Hunting licenses fees
- iv. Muzzle loading guns license fees
- v. Scaffolding / Hoarding permit fees

#### **G. Turnover Taxes**

- i. Service levy

#### **H. Entrepreneurial and Property Income**

- i. Dividends
- ii. Other Domestic Property Income
- iii. Interest
- iv. Land rent

#### **I. Administrative Fees and Charges**

- i. Market stalls / slabs dues
- ii. Magulio fees
- iii. Auction mart fees
- iv. Meat inspection charges
- v. Land survey service fee
- vi. Building permit fee
- vii. Permit fees for billboards, posters or hoarding
- viii. Tender fee
- ix. Abattoir slaughter service fee
- x. Artificial insemination service fee
- xi. Livestock dipping service fee
- xii. Livestock market fee
- xiii. Fish landing facilities fee
- xiv. Fish auction fee
- xv. Health facility user charges
- xvi. Clean water service fee
- xvii. Refuse collection service fee
- xviii. Cesspit emptying service fee
- xix. Clearing of blocked drains service fee
- xx. Revenue from sale of building plans
- xxi. Building valuation service fee

- xxii. Central bus stand fees
- xxiii. Sale of seedlings
- xxiv. Insurance commission service fee
- xxv. Revenue from renting of houses
- xxvi. Revenue from renting of assets
- xxvii. Parking fees-

## **J. Fines, Penalties and Forfeitures**

- i. Stray animals penalty
- ii. Share of fines imposed by Magistrates Court
- iii. Other fines and penalties

**17. Mheshimiwa Spika**, Maelezo au ufafanuzi wa utendaji kazi wa Serikali za Mitaa umetolewa katika sheria iliyotungwa na Bunge yaani Sheria ya “**The Local Government (District Authorities) Act, and The Local Government (Urban Authorities) Act**” ya mwaka mwaka 1982.

**18. Mheshimiwa Spika**, katika taarifa ya utafiti wa utekelezaji wa sheria hiyo, unaonyesha Serikali Kuu imeshindwa kuweka mkakati uliowazi na makini wa kufanikisha matakwa ya Kikatiba na Kisheria. Katika uchambuzi huo kwa ngazi ya mkakati wa utekelezaji umeleza kuwa hakuna mpango mahususi unaohusiana na ugatuaji madaraka unaonesha majukumu na mipaka ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. *“There is no explicit implementation plan regarding decentralisation. The separation between central government matters and local affairs is not established”<sup>1</sup>.*

**19. Mheshimiwa Spika**, Vigezo au viashiria vilivyoonyesha mkanganyiko kwa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa mujibu wa andiko hilo ni: ***Transfer of competencies and sector-based policies***: Serikali za Mitaa hapa nchini sio taasisi inayojitegemea kama inavyotakiwa kuwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Uhawilishwaji wa rasimali watu katika Serikali za Mitaa ni matakwa ya Serikali Kuu na si matakwa ya Serikali za Mitaa, pili uteuzi na ajira kwa watumishi hufanywa na

---

<sup>1</sup> Report on Local Government Decentralization Mandates

Serikali Kuu kupitia kwa kilinachoitwa-“**Local Government Service Commission**”. Hivyo jambo hilo husababisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokuwa na uwezo wa kuajiri au kufukuza mtumishi hadi pale mamlaka iliyofanya uteuzi au uajiri kufanya hivyo.

**20. Mheshimiwa Spika**, Mojawapo ya sababu za kushindwa kufanya vizuri katika utoaji wa huduma za msingi kwa wananchi kwa Halmashauri nyingi hapa nchini inatokana na kukosa au kutokuwa na uwezo kwenye utawala na fedha katika kutoa maamuzi yanayohusu maendeleo ya Halmashauri zao. Badala yake maamuzi mengi ya kiutawala na kifedha yanatolewa na Serikali Kuu, na utendaji wa Halmashauri nyingi kwa sehemu kubwa unaingiliwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

**21. Mheshimiwa Spika**, ni vizuri Serikali ya awamu ya tano ikatazama juhudi iliyofanywa na Serikali za awamu zilizotangulia hususan awamu ya tatu na ya nne ambazo zilifanikiwa kukaribia lengo na dhana nzima la ugatuaji wa madaraka kama linavyoelezwa katika Ibara ya 154 na 146 lakini kwa bahati mbaya tumerudi nyuma miaka takriban 25 iliyopita.

**22. Mheshimiwa Spika**, Nyenzo muhimu inayotumiwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa inazidi kuhodhi madaraka ya Serikali za Mitaa ni kuhodhi watumishi waandamizi (senior staffs) wa Serikali za Mitaa walio kwenye sekta za utawala, afya, fedha, kilimo na kadhalika, wote hawa huteuliwa kutoka Serikali Kuu.

**23. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Serikali za Mitaa baadhi ya majukumu yake ya msingi ili kuimarisha demokrasia na utawala bora ni pamoja na kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D); kuwezesha maandalizi na Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; kusimamia matumizi ya rasilimali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, lische na ustawi wa jamii

katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**24. Mheshimiwa Spika** shughuli hizo haziwezi kufanikiwa ikiwa kila kitu kinategemea kutoka Serikali Kuu, kutokana na ukweli kwamba Halmashauri zetu hazina vyanzo vya mapato vya uhakika kwani vimepokwa na Serikali Kuu.

**25. Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa uwezeshaji wa kweli utatokana na mapinduzi ya kidemokrasia (nguvu ya umma), uwezeshaji utaletwa na watu kwa ajili ya watu. Uwezeshaji hapa utaanzia kwa watu wenyewe kwa kuangalia watu wanataka nini na sio dola kuamua kwa niaba ya wananchi. Misaada toka kwenye taasisi na asasi za Serikali itasaidia pale tu ambapo jamii itakuwa tayari kwa misaada hiyo na tayari ina mipango yake ya maendeleo. Kinyume na hapo ni kupoteza rasilimali nyingi bila ya kuwepo matunda.

**26. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatakiwa ielewe kwamba vyanzo ilivyovipora kutoka Halmashauri ndio vilikuwa vyanzo vikubwa na nguzo imara ya kuzifikisha Halmashauri nyingi kufikia malengo ya kuondokana na utegemezi wa Serikali Kuu katika kutimiza majukumu yake ya msingi ya kuwahudumia wananchi.

**27. Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa ardhi ndiyo rasilimali pekee ambayo kila Halmashauri katika nchi inaimiliki. Ardhi ndiyo chanzo cha mapato cha uhakika kwa kila Halmashauri ya nchi hii, hivyo basi Serikali Kuu kujaribu kufifisha uwezo wa makusanyo ya chanzo hiki ni kuifanya Halmashauri kushindwa kabisa kutoa huduma za msingi kwa wananchi wake.

**28. Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zinatakiwa kuchukua 30% ya kodi ya ardhi, hivyo inapotokea kuwa Serikali Kuu inachukua fedha hizo na urejeshaji wake unakuwa ni pale itakapojiridhisha kuwa zinahitajika, hilo sio sahihi kwa maendeleo ya wananchi.

**29. Mheshimiwa Spika**, Chanzo hicho cha mapato ya Halmashauri kinachotokana na kodi ya ardhi kama makusanyo ya ndani (own source) ni muhimu sana katika kuzifanya Halmashauri zikabiliane na changamoto mbalimbali za kuhudumia wananchi.

**30. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ukusanyaji ufanywe na Halmashauri kama ambavyo ilikuwa inafanyika miaka yote na ziada au hitaji la fedha la Serikali lipelekwe na Halmashauri na sio kinyume chake.

**D. UTAWALA NA UENDESHAJI WA MABARAZA YA MADIWANI**

**31. Mheshimiwa Spika**, dhana nzima ya ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa inatoa madaraka kwa utawala na upangaji wa mipango kwenye Wilaya kwa Baraza la Madiwani.

**32. Mheshimiwa Spika**, TAMISEMI ndio mlezi wa Halmashauri ikihusishwa na Mabaraza ya Madiwani pia, lakini imeshindwa kukemea mambo ambayo yameshika kasi kwa siku za karibuni ya kuhakikisha wale wote waliopewa ridhaa na wananchi ya kuendesha Halmashauri hizo katika uchaguzi wa Oktoba 2015, hasa wale kutoka vyama nje ya CCM wanafanyiwa hila na kuondolewa.

**33. Mheshimiwa Spika**, ni aibu kubwa kwa Serikali inayojinasibu kuwa ni ya kidemokrasia na inafuata misingi ya utawala bora, kwa makusudi kushindwa hata kuona au kutekeleza dhana ndogo ya madaraka kwa umma, pale ambapo wananchi wanatoa ridhaa kwa chama cha Upinzani kutoa Mwenyekiti wa kuongoza Halmashauri, mara tu anaondolewa kwa hila.

**34. Mheshimiwa Spika**, hivi ni kweli kati ya Halmashauri takriban 134 zilizopo hapa nchini ni Wenyeviti au Mameya wanaotoka Vyama vya Upinzani tu ndio wenye shida na hivyo kuondolewa? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hizo hila zinazofanywa na Wakuu wa Mikoa za kuwaondoa Mameya au Wenyeviti wa Halmashauri ni kipimo kwa Waziri mwenye

dhamana kama kweli anawajibika kwa jamii na kufuata utekelezaji wa sera ya D by D au la. Tukumbuke kwamba Meya sio mtendaji kwa nafasi yake na stahili zake zote anazipata kwa Mkurugenzi (DED), hivyo kwa hali ya kawaida ubadhirifu wa Meya unatoka wapi na Mkurugenzi kubakia akiwa ni msafi na mchapa kazi?

**35. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, kwa mfumo huu ambao umeibuka katika Serikali ya awamu ya tano ya kuhakikisha inasigina Katiba na sheria zake ni ishara mbaya sana katika kufikia lengo la kuwa na Serikali za Mitaa zenye nguvu. Tukumbuke kwamba toka mfumo wa vyama vingi uanze hapa nchini, kuna Halmashauri kama vile Karatu, Kigoma, Ujiji, Bariadi, Moshi Mjini, Musoma Mjini, Tarime ambazo zilikuwa chini ya Upinzani katika Serikali za awamu ya tatu na ya nne lakini hatujawahi kusikia hiki kinachoitwa kuondolewa kwa Wenyeviti wa Halmashauri hizo eti kwa matumizi mabaya ya ofisi. Ni muhimu sana Serikali ya awamu ya tano iheshimu maamuzi ya wananchi hata wanapochagua wawakilishi wao kutoka vyama vya upinzani.

#### **E. UWEZO WA HALMASHAURI ZETU KUKABILIANA NA JANGA LA UGONJWA WA CORONA**

**36. Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ndizo zenye watu, na shughuli nyingi za kijamii na za kiuchumi zinafanyika zaidi kwenye maeneo yao. Shughuli za kiuchumi kama vile usafirishaji wa abiria kwa boda boda, bajaji, daladala, masoko katika maeneo mbalimbali na kadhalika na vituo vya kuabudia.

**37. Mheshimiwa Spika**, uhibiti wa ugonjwa huu kwa kiasi kikubwa kinga yake tunaambiwa ni usafi na kujitenga au kuzuia misongamano ya watu katika maeneo mbalimbali ya kijamii na kibiashara. Hoja yetu ya msingi ni kutaka kupata maelezo ni kwa vipi Halmashauri zetu zimejipanga kwa uwezo wa kifedha wa kuzuia maambukizi kuenea katika maeneo takriban yote yenye mkusanyiko wa watu?

**38. Mheshimiwa Spika**, ni kwa vipi pale itakapohitajika kuwapo na vituo vya “**isolation**”, matayarisho yake kwa sasa

yako vipi na kwa kila Halmashauri ina mkakati gani kuhakikisha inakabiliana na maambukizi badala ya kutegemea Serikali Kuu ambayo nayo uwezo wake unaweza kuwa ni mdogo. Ni kwa kiasi gani kila Halmashauri ina uwezo wa kuhakikisha vyakula kwenye masoko yake vinauwezo wa kuhimili kipindi ambacho eneo husika linaweza kuwa kwenye karantini?

**39. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa Serikali kwamba, ni vyema kujiandaa vilivyo kupambana ili kuepusha madhara makubwa pale mapambano yatakapoanza. Hivyo kinga ni bora kuliko tiba.

#### **F. HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI**

**40. Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa watu bilioni 4, ambao ni zaidi ya nusu ya idadi ya watu duniani, hawana huduma za msingi za afya. Changamoto hii ya afya duniani zinawakabili zaidi watu katika nchi za kipato cha chini na cha kati (Least and Middle Income Countries-LMICs). Mpango wa Afya Duniani unachangia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa kwa kutumia teknolojia ya Ada Global Health Initiative kwa manufaa ya dunia. Ushirikiano baina ya mashirika yasiyo ya kiSerikali (NGOs), Serikali za nchi za kipato cha chini na cha kati (LMICs), na mashirika ya kimataifa ya afya kwa lengo la kusaidia kuongeza upatikanaji wa taarifa za afya za kibinafsi na kuboresha utoaji wa huduma ya msingi ya afya kwa wale ambao wanahitaji zaidi inafanyika kwa njia ya kidigital chini ya taasisi ya Ada Global Health Initiative.

**41. Mheshimiwa Spika,** Ada Global Health Initiative katika mtandao wake inaonesha kuwa, watu bilioni nne wanakosa upatikanaji wa huduma za msingi za afya duniani. Kuna upungufu wa wahudumu wa afya milioni saba duniani ambapo asilimia sabini na tano ya upungufu huo unapatikana maeneo ya vijijini katika nchi zinazoendelea. Aidha kuna upungufu mkubwa wa madaktari wa magonjwa ya akili katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Takwimu zinaonesha kwamba uwiano ni madaktari 0.5 kwa wagonjwa



100,000. Takwimu hizo zinapaswa kutusukuma sisi Watanzania kuitathmini hali ya huduma ya afya za msingi katika nchi yetu.

**42. Mheshimiwa Spika**, huduma za afya ni msingi mkuu wa maendeleo katika uendeshaji wa Serikali za Mitaa na utoaji wa huduma hizo ni mojawapo ya jukumu la msingi la Halmashauri zetu. Vituo vya Afya na Zahanati ndizo ngazi za kwanza za afya zinazoigusa jamii moja kwa moja. Kwa sababu hii, wauguzi na wafanyakazi wengine wa vituo hivyo hujulikana kama Wahudumu wa Afya. Wahudumu hao ni wawakilishi wa mfumo mzima wa huduma za afya kwa jamii na ndiyo wanaojenga hisia za jamii kuhusu uwezo, huduma na ufanisi wa wafanyakazi wa afya. Vilevile ndiyo macho na masikio ya kada nyingine za afya katika jamii. Wahudumu hao ni viungo muhimu kwa mawasiliano na pia ni viungo muhimu katika utekelezaji.

**43. Mheshimiwa Spika**, katika mfumo wa utawala ulivyo sasa ni dhahiri kuwa kwa sasa kutokana na takwimu toka kwa asasi zinazojihusisha na afya ni kwamba ubora na upatikanaji wa huduma za afya kuna upungufu wa 52% ya wataalam wa sekta ya afya hapa nchini, jambo ambalo linaathiri utoaji wa huduma za msingi katika sekta ya afya. Iwekwe wazi kwamba ajira zilizotolewa na Serikali za takriban watumishi wa afya 7,680 sio kama inaondoa upungufu bali inaziba pengo ambalo lilitokea baada ya kuondoa takriban watumishi 7,300 katika zoezi lililoendeshwa la kuondoa vyeti fake. Nje ya upungufu huo bado kuna watumishi kuugua, vifo kwa watumishi na matatizo mengine ya kijamii yanayowakumba watumishi katika sekta ya afya, na hivyo kuzidisha upungufu na kupelekea utolewaji duni wa huduma za msingi katika afya. Huduma za afya katika maeneo ya vijijini hasa zahanati na vituo vya afya zimeathiriwa sana na upungufu mkubwa wa rasilimali watu -Human Resource in Health- (HRH)<sup>2</sup>.

**44. Mheshimiwa Spika**, tatizo la upungufu wa rasilimali watu

---

<sup>2</sup>Civil Society Organization's Statement during the Joint Annual Health Sector Review 2018 Policy Day Meeting, to be held on 26th November 2018, Dodoma

katika ngazi za chini limepelekea kuwepo kwa msongamano mkubwa wa wagonjwa kwenye Hospitali za Mikoa na Rufaa hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa madhara haya yote ni kutokana na Serikali kuu kuu kabisa mfumo wa kuzipa halmashauri uwezo wa kuajiri watendaji na badala yake ajira zote kuletwa Serikali Kuu. Vilevile ni matokeo ya upokaji wa vyanzo vya mapato katika ngazi ya Halmashauri na hivyo kuzifanya kukosa uwezo wa kutoa huduma za msingi kwa wananchi wake.

**45. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza na kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika kuboresha utoaji na upatikanaji wa huduma za afya mijini na vijijini ili kupunguza mzigo kwa Halmashauri zetu.

#### **G. ZAHANATI/KITUO CHA AFYA KILA KIJJI/ KATA**

**46. Mheshimiwa Spika**, azma ya Serikali kwa mujibu wa sera ya afya ya 2007 ni kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi. Kujenga ushirikiano kati ya sekta ya umma, sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kijamii na jamii katika kutoa huduma za afya na kuhakikisha kuwa huduma za afya ya msingi zinapatikana na kutolewa katika mfumo madhubuti na kushirikisha jamii, kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo.

**47. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha yote hayo kwa muktadha wa upatikanaji wa huduma bora za afya, Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha kuwa kila kijiji kina zahanati na kila kata ina kituo cha afya ili kuleta uwiano katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Jambo hili ni katika kukidhi matarajio ya wananchi kwa kuwa na huduma bora za afya.<sup>3</sup>

**48. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa sera hiyo ulianzishwa toka Bunge la Tisa na wananchi walipewa hamasa na wakajitoa sana kujenga maboma (vituo vya afya kila kata

---

<sup>3</sup>JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, SERA YA AFYA, 2007

ambavyo havikuezekwa) mengi sana. Lakini Serikali ilishindwa kutimiza ahadi yake ya kuezekwa na kumalizia matenegezo mengine ili vituo hivyo vianze kazi. Takwimu zinaonesha kuwa hadi sasa Serikali bado inadaiwa takriban shilingi 184,184,497,000.00 zikiwa na kumalizia maboma ya zahanati/vituo vya afya pamoja na shule. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata mchanganuo ni kiasi gani hasa ni kwa afya na shule? Hii ni ishara kubwa kabisa kuwa afya ya Watanzania sio kipaumbele kwa Serikali ya CCM, kwa hali ya kawaida kama wananchi wametimiza ahadi yao inakuwaje Serikali inashindwa kutimiza kulingana na makubaliano?

#### **H. ELIMU MSINGI NA SEKONDARI**

**49. Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu la TAMISEMI ni kusimamia na kuendesha elimu ya awali, msingi na Sekondari. Katika kusimamia huko ni kuhakikisha ubora wa elimu yetu unakuwa kwa kiwango ambacho kinakubalika kwa mazingira yetu ya ndani na pia kwa mazingira ya nje ya nchi, ubora au kiwango cha elimu kinachangiwa na mambo mengi, ambayo kwa muktadha wetu ni dhahiri kabisa tunashindwa, kwa kufahamu au kutokufahamu kuwa kufanya hivyo basi tunaporomosha wenyewe ubora au kiwango cha elimu hasa kwa shule zetu zinazosimamiwa na TAMISEMI.

**50. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa nchi ambayo inategemea kuwa bora duniani kwa kiwango kikubwa unategemea jinsi gani mfumo wake wa elimu ya awali hadi sekondari ulivyo imara na kuweza kutoa wahitimu ambao ni shindani na wabunifu kwa mazingira yanayowazunguka.

**51. Mheshimiwa Spika**, Ni kweli kuwa matokeo mabaya katika shule zetu za awali hadi sekondari kwa kulinganisha na yale ya shule binafsi, kwa kiwango kikubwa inatokana na uhaba na uduni wa miundombinu ya kufundishia wanafunzi, ukaguzi unaofanywa na wale wanaotakiwa kutimiza majukumu hayo na inakwenda mbele zaidi ya hapo ni kwa walimu kukosa furaha kutokana na kutopewa stahili zao za msingi na pia unyanyapaa wanaokutana nao kutoka kwa viongozi wa kisiasa kwenye maeneo yao ya kazi.

**52. Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha wa hotuba yetu tunaongelea kidogo kuhusu bajeti inayotolewa na Serikali Kuu kwenye kuboresha miundombinu ya kufundishia, ukaguzi na motisha kwa walimu. Kuna mambo mengi ikiwemo uwiano wa mwalimu na wanafunzi katika ufundishaji darasani, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia (*mazingira ya kufundishia na kujifunza kwa mwanafunzi n.k*)

**53. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kabisa kuwa ubora wa elimu kwa sasa unazidi kudidimia japokuwa tunaambiwa ufaulu unaongezeka, jambo hili linatia mashaka sana, kwani wanafunzi katika shule zetu za awali hadi sekondari wameongezeka sana na ufaulu kwa shule zetu unapangwa kulingana na namna matokeo wanavyotaka yawe na sio “pass mark point” za chini na za juu kwa kila somo ziwe ni ngapi ili mwanafunzi awe amefaulu kwa madaraja yaliyopangwa.

**54. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba wanafunzi bado wanajifunzia katika mazingira magumu (miundombinu ya kusomea) na hili linatokana na uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali ambao hauoneshi dhamira ya kweli ya kuipeleka nchi yetu kuwa taifa shindani katika medani za kimataifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni kwa nini hapo zamani wakaguzi walikuwa wanafanyakazi zao kwa umakini na umahiri na hivyo shule zetu ziliweza kufanya vyema, au ni kwa nini shule za binafsi zinafanya vyema kuliko za Serikali? Tuna uhakika majibu yatatolewa lakini ni majibu ya kuficha ukweli uliopo.

**55. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kuwa ubora wa jambo unaendana moja kwa moja na gharama inayotumika, hivyo ni lazima Serikali iwekeze vyema katika eneo hili la kuimarisha elimu yetu ya awali, msingi na sekondari, jambo hili la uwekezaji halitakiwi “kuwa-compromised” na uwekezaji kwenye maeneo mengine kama ambavyo Serikali ya awamu ya tano inafanya. Nia nje ya Tanzania njema ya kesho inatokana na maamuzi ya uwekezaji kwenye elimu ya juzi, jana na leo.

**56. Mheshimiwa Spika**, mfumo wetu wa elimu unaendana sana na mfumo wa uendeshaji wa Serikali, umegubikwa na usiri mkubwa katika mambo ya msingi ambayo yanaharibu kizazi chetu cha leo na kesho na hivyo kuifanya Tanzania ya kesho na kesho kutwa isiweze kutabirika. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa hatuwezi kuwa na elimu bora kama rasimali fedha na watu havitengwi kwa viwango toshelevu.

**57. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona dhana mpya ya elimu (*new concept on education is basing on competency based approach*) itakuwa suluhu kwa nchi yetu kwa kuanza kuitumia kuanzia shule za awali, msingi na sekondari, japokuwa sio mpya kwani zamani ilikuwa inatumika katika shule zetu lakini watawala wakaitupilia mbali. Nchi za Scandnavia na Asia zimepiga hatua kubwa katika sekta ya elimu kwa dhana hiyo.

**58. Mheshimiwa Spika**, Katika dhana mpya ya elimu ni kwamba inamtayarisha mwanafunzi kuelimika kwa kupata; kwanza uelewa (knowledge) wa kupata na kutumia taarifa mbalimbali, pili kuwa na uwezo(ability) wa kufanya tafakuri ya jambo; na tatu kupata ujuzi (skills) ujuzi wa kushiriki katika kutafuta suluhisho. Uwezesaji huo wa elimu ili aweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa jamii na uchumi wa nchi.

**59. Mheshimiwa Spika**, Aidha, dhana mpya ya malengo ya elimu kama inavyotumika kwa nchi za Scandnavia na Asia ni kumuandaa mwanafunzi kutumia mafundisho aliyopewa shuleni kuwa tayari katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayotokea duniani. *Competency based* inasisitiza elimu itakayotolewa iweze kutoa suluhisho kwenye matatizo (*problem solving skills*) katika ulimwengu tunaishi kama vile kuongezeka kwa idadi ya watu, kukua kwa teknolojia na matatizo mengine katika jamii. Aidha, katika kuwa na competency base katika elimu, ni muhimu kuangalia uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi.

**60. Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba katika elimu yetu kuna "mismatch" kati ya Mitaala na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira. Hoja ya msingi ni je kwa Tanzania elimu yetu ya

awali, msingi na sekondari inamuandaa mwanafunzi katika kupambana na matatizo na kutoa suluhisho kwa matatizo tuliyonayo katika jamii yetu na inamuwezesha kuishi bila kutegemea msaada wa mtu mwingine? Je, mhitimu huyo anachangiaje katika uchumi wetu mchanga? Ni muda mwafaka sasa kuangalia jinsi ya kuimarisha ubora wa elimu yetu ya msingi na sekondari

**61. Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 udhibiti ubora wa shule ulipangiwa shilingi bilioni 1.5 lakini hadi mwaka huo unamalizika fedha hizo hazikutolewa, vivo hivyo shilingi bilioni 25 zilitengwa kwa ajili ya kuimarisha ubora wa shule za sekondari (**Secondary Education quality Improvement Programme-SEQUIP**) na mradi huo haukupewa kiasi chochote cha fedha.

**62. Mheshimiwa Spika**, eneo la udhibiti ubora wa elimu limeathiri sana hali ya ukaguzi wa shule zetu, takwimu zilizotolewa na asasi inayojihusisha na elimu (Haki Elimu) zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 utafiti kwa shule za msingi 5,723 kati ya shule 17,174. Ni asilimia 33 tu ya shule ndizo zilizokaguliwa. Maana yake kwa mwaka huu wa 2020 kuna uwezekano mkubwa shule zilizokaguliwa zikawa ni chini au ikawa ni mara mbili ya zile zilizokaguliwa mwaka wa fedha 2018/19.

**63. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa shule za sekondari ni shule 1,185 kati ya shule zote 4,779 za sekondari. Hii ikiwa na maana kuwa ni asilimia 25 tu ndizo zilizokaguliwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza tena, ni vyema Serikali ikawekeza katika kuhakikisha ubora wa elimu na hilo ndio uwekezaji katika kupata Tanzania bora ya kesho na keshokutwa.

**64. Mheshimiwa Spika**, Katika suala la miundombinu nalo limekuwa kama kidonda ndugu kwani toka awamu ya nne kampeni ya ujenzi wa shule za kata ulipoanza, ni jambo jema na wananchi waliitikia na walijitolea sana kwa ujenzi wa mashule(maboma) ili Serikali imalizie ujenzi ambao nguvu za wananchi ziliishia, lakini hadi leo takwimu za TAMISEMI zinaonesha kuwa bado Serikali haijamalizia ujenzi wa

maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Jambo hili la Serikali kushindwa kukamilisha mkataba wake na wananchi ni kuwakatisha tamaa wananchi katika masuala ya kujitolea, takwimu za TAMISEMI zinaonesha kiasi cha shilingi 184,184,497,000/- bado hakijatolewa kwa ajili ya umaliziaji wa maboma ya shule na zahanati/ vituo vya afya. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu kati ya hizo, Maboma ya shule zinadaiwa kiasi gani na afya ni kiasi gani?

#### **I. WAKALA WA BARABARA MIJINI NA VIJIJINI (TARURA)**

**65. Mheshimiwa Spika**, kulingana na sheria iliyopitishwa na Bunge, ni kuwa Wakala huyu wa Barabara Mijini na Vijijini katika utendaji kazi wake hawajibiki kwa namna yoyote kwenye Baraza la Madiwani au kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Tukumbuke kwamba eneo la kazi la TARURA liko chini ya mamlaka ya Baraza la Madiwani na Mkurugenzi wa Halmashauri. Hivyo utendaji kazi wa TARURA kwa njia moja au nyingine unakosa chombo cha usimamizi wa kazi zake. TARURA kiutendaji inawajibika kwa chombo au mamlaka gani? Kwa vyovyote vile vile haiwezekani kuondoa madiwani katika kushauri na kusimamia matengenezo ya barabara zilizo ndani ya kata husika.

**66. Mheshimiwa Spika**, Baraza la Madiwani (kupitia Kamati yake ya Fedha) kabla ya uwepo wa TARURA linakuwa ziara kila mwezi ya kukagua miradi yote ambayo iko kwenye matengenezo. Lakini kutokana na TARURA kuzaliwa utaratibu huo wa kikanuni umekwisha na barabara za vijijini kwenye kata zimebakia bila ya kuwa na "mwenyewe" kwani Diwani hana tena uwezo wa kumsimamia makandarasi.

**67. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Waheshimiwa Madiwani pamoja na mambo mengine ndio wanaofahamu kwa undani ni barabara gani na umuhimu wake kwa wananchi kwenye kata husika na matengenezo yake yanaweza kufanyikaje kulingana na majira ya mwaka. Hivyo kutokuhusishwa kwa wananchi katika suala hili na kuachwa kuwa ni jukumu la TARURA badala ya kupunguza gharama na kujenga kwa ubora zaidi limeongeza gharama na ubora wa miundombinu inayojengwa umekuwa hafifu zaidi.

**68. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, tulifanya makosa katika sheria ya uanzishwaji wake kutokutambua uwepo wa Baraza la Madiwani na Mkurugenzi wa Halmashauri katika kile kinachoitwa “check and balance” ya TARURA, hivyo basi turekebishe Sheria ya TARURA ili pamoja na kazi zake ushirikishwaji na uwajibikaji wake uwe kwenye ngazi ya Halmashauri kupitia vyombo vyake.

**69. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa maduhuli yanayokusanywa na TARURA (ushuru wa maegesho) bado ni mdogo sana katika uendeshaji wake, japokuwa ni mdogo lakini bado TARURA inalazimika kuwasilisha maduhuli hayo moja kwa moja kwenye Mfuko wa Barabara (Tanzania Road Fund), na baadae aombe fedha kutoka kwenye mfuko huo ili kutekeleza majukumu yake.

**70. Mheshimiwa Spika**, katika utaratibu huu wa kupeleka kwenye Mfuko Mkuu, baadae unaomba tena kwenye Mfuko Mkuu ili uweze kutumia kulingana na bajeti ambayo tayari ipo, ni mfumo wa kiukiritimba mno na sheria ya Mfuko wa Barabara Namba 220 sehemu ya 2 kifungu cha 2 inatakiwa kufanyiwa marekebisha, kwani badala ya kwenda mbele tunarudishwa nyuma kwa sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe.

**71. Mheshimiwa Spika**, uhalisi ni kwamba wakala huyo ana majukumu makubwa mno yanayohitaji fedha za kutosha kutekeleza wajibu wake kulingana na hali halisi ya uharibikaji wa barabara zetu za vijijini na mijini hasa katika kipindi hiki cha mvua kubwa sana ambazo zinaendelea kunyesha nchi nzima(masika). Na ukweli ni kuwa wanaofahamu ni wapi barabara inahitaji matengenezo ya haraka ni madiwani pamoja na Mkurugenzi wao, sana nao hawana wajibu wowote kwa TARURA. Hii ni shida kubwa sana ambayo inatakiwa kutolewa ufumbuzi wa haraka.

**72. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/21 wakala umetengewa jumla ya shilingi 344,556,044,824.00 kati ya fedha hizo za ndani ni shilingi 275,034,159,00.00 na za nje ni shilingi 69,521,885,824.00. Lakini kulingana na hali halisi ya mvua



zilivyonyesha na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya ulifanyika kwa barabara zilizokuwa zinahudumiwa na Halmashauri ni dhahiri kuwa kiasi cha fedha kilichoombwa hakitaleta matokeo chanya yoyote katika kuifanya TARURA kutimiza majukumu yake.

**73. Mheshimiwa Spika**, Fedha ambazo TAMISEMI inaomba kuidhinishiwa shilingi 275,034,159,000.00 ni fedha za ndani kwa ajili ya kazi za TARURA, zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:-  
i) Ujenzi na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini zenye urefu wa kilomita 22,746.41 ambapo kilomita 13,450.43 ni matengenezo ya kawaida, kilomita 5,858.88 ni matengenezo ya maeneo korofi na kilomita 3,437.1 ni matengenezo maalum; na ii) Ujenzi na ukarabati wa madaraja 99, makalvati 256 na mifereji ya maji kilomita 78.

**74. Mheshimiwa Spika**, kama katika bajeti ya 2019/20 zilitengwa jumla ya shilingi 42,112,000,000.00 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa KM 86.6 tu, sasa hiyo bajeti iliyotengwa kutengeneza kilometa takriban KM 39633.94 pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja 99, makalavati 256 na mifereji ya maji yenye urefu wa KM 78? Huu ni utani ambao mwisho wake ni kuhakikisha wananchi wanashindwa kutoka huko waliko kwenda maeneo mengine ya nchi hii, fikiria pia mvua nyingi ambazo zimenyesha na zinaendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

**75. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo tumesema awali barabara zilizokuwa zinahudumiwa na Halmashauri zetu zinaweza kuhudumiwa pia na TARURA lakini kama ikiwa chini ya Baraza na vyanzo vya mapato ya ndani Halmashauri vikatumika kuiongezea nguvu.

**76. Mheshimiwa Spika**, kuna jambo lingine ambalo ni la ajabu na tunaona litakwaza utendaji wa TARURA, kwa hali halisi tuliyoieleza hapo awali, inakuwaje TARURA inapanga bajeti yake bila ushirikishwaji wa Baraza la Madiwani au ofisi ya Mkurugenzi? Inawezekana bajeti inayoombwa na TARURA

ni kwa ajili ya kulipata posho na mishahara na sio kwa lengo la kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara vijijini na mijini. Bajeti hiyo inayoombwa haina chembe ya ushirikishwaji wa wanufaikaji wa miundombinu inayotarajiwa kujengwa.

## J. WAKALA WA MAJI NA MAJI TAKA VIJIJINI-RUWASA

**77. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba idadi ya watu Tanzania imeongezeka na inazidi kupamba moto, toka watu milioni 12.3 mwaka 1967 hadi watu milioni 44.9 mwaka 2012, na sasa takriban watu milioni 55 mwaka 2019. Na kati ya hao asilimia 30 wanaishi mijini na asilimia takriban 70 wanaishi vijijini. Ina kadiriwa kwamba ifikapo 2050<sup>4</sup>, idadi ya watu kwa Tanzania itakuwa milioni 137 na asilimia 50 watakuwa wanaishi mijini. Hivyo basi ni vyema kuweka miundombinu inayoweza kukidhi mahitaji ya ukuaji wa idadi ya watu kwa muda uliopo na ujao.

**78. Mheshimiwa Spika**, changamoto iliyopo kwa RUWASA ni sawa na zingine, kwani kitendo cha kuondoa mfumo ambao ulikuwa unajaribu kubadilisha mtazamo wa wananchi katika kumiliki miradi yao ya maendeleo kuanzia ngazi za kubuni hadi kuendesha imeondoka, na hivyo miradi hii ya maji itaonekana sio ya wananchi bali ni mali ya Serikali. Hili ni kosa ambalo ni muendelezo wa makosa yanayofanywa na Serikali hii ya awamu ya tano kupoka mamlaka ya wananchi na kutarudisha Serikali Kuu.

**79. Mheshimiwa Spika**, Miradi ya maji na huduma zingine za kijamii zinatakiwa zibuniwe na wananchi, kujengwa kwa ushiriki wa wananchi na uendeshaji pia wananchi washirikishwe ili dhana nzima ya uendelevu iwepo. Kinyume cha hapo ni kuharibu rasilimali na fedha za walipa kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inatafakari sana kuhusu dhana hii mpya ya Serikali ya awamu ya tano ya kupora madaraka ya wananchi kupitia Baraza la Madiwani. Sasa kama huduma

---

<sup>4</sup> [www.nbs.g.tz](http://www.nbs.g.tz)

za maji zimeondolewa na huduma za barabara zimeondolewa, je bado kuna umuhimu wa kuwa na wawakilishi wa wananchi katika Baraza la Madiwani? Au uwepo wa Madiwani ni muhimu kama huduma zote muhimu ambazo utatuzi wake unahusisha wananchi wenyewe zinatwaliwa na Serikali Kuu?

**K. UTEKELEZAJI WA BAJETI 2019/20 NA MAOMBI YA FEDHA 2020/21**

**80. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha, 2019/20 TAMISEMI, kwa upande wa maendeleo zilitengwa jumla ya shilingi 496,563,123,910.00 na fedha za ndani zikiwa ni shilingi 286,738,400,000.00 na shilingi 209,824,723,910.00 zikiwa ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 fedha zilizokuwa zimetolewa kwa miradi ya maendeleo ni shilingi 196,078,940,851.00 sawa na asilimia 68.4 zikiwa ni fedha za ndani na shilingi 281,660,973,484.00 sawa na asilimia 86.6 zikiwa ni fedha za nje.

**81. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2020/21, OR – TAMISEMI inaomba kuidhinishiwa makadirio ya jumla ya shilingi 413,579,583,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pungufu ya shilingi 82,983,540,910.00 kwa kulinganisha na zile zilizoidhinishwa mwaka jana. Kati ya fedha hizo, shilingi 276,534,159,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 137,045,424,000.00 ni fedha za nje ikiwa ni pungufu ya shilingi 72,779,299,910.00 kulinganisha na zilizotengwa mwaka 2019/20.

**L. HITIMISHO**

**82. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli uliowazi kuwa TAMISEMI ni Wizara ambayo inahudumia Watanzania wote ikiwa na lengo la kuifanya kuwa na mamlaka kamili kwa mujibu wa Ibara ya 145 na 146 sambamba na sera ya ugatuuji wa madaraka.

**83. Mheshimiwa Spika**, kitendo chochote kitakachofanyika cha kuiondolea TAMISEMI hasa Mabaraza ya Halmashauri uhuru wao katika kuhakikisha yanatoa huduma kwa

wananchi, ni kitendo ambacho hakitoleta maendeleo kwa wananchi wengi, na hivyo kinapingana na dhana nzima ya wananchi kuwa ndio wenye mamlaka ya kuamua, kupanga na kushiriki katika mchakato mzima wa kujiletea maendeleo.

**84. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani mara zote imekuwa ikishauri na kutahadharisha juu ya azma ya Serikali inayopoka madaraka ya wananchi na kuyarudisha Serikali Kuu kuwa ni kuharibu kabisa mfumo wa kuipeleka nchi yetu kuwa nchi ya uchumi wa kati na nchi inayotegemea viwanda. Kwa bahati mbaya sana Serikali ya CCM imeshindwa kuelewa dhana hiyo ya wananchi kuwa wamiliki na wasimamizi wa mipango na miradi yao ya maendeleo.

**85. Mheshimiwa Spika**, jambo hilo la kupoka uhuru na vyanzo vikubwa vya mapato kwa Halmashauri, limesababisha Halmashauri nyingi kushindwa kujiendesha na hivyo kushindwa kutoa huduma za msingi kwa wananchi. Hivyo basi kuwa tegemezi na ombaomba kwa Serikali Kuu.

**86. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, tunawataka Watanzania ambao wametuelewa hasa katika dhana nzima ya kutoa uhuru kamili kwa Serikali za Mitaa kupitia Mabaraza ya Madiwani, tuungane wote kurejesha kile ambacho Serikali ya awamu ya tatu ilikianzisha cha kufanya maboresho ya Serikali za Mitaa ili kuwa imara katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

**87. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
**Japhary R. Michael (Mb)**

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Rais,  
TAMISEMI.  
08/04/2020**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge ndio mwisho wa mawasilisho sasa tutaanza na mchangiaji

ninayo majina hapa ya wachangiaji kutoka kwa wawakilishi wa vyama kama tulivyo humu ndani. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Gimbi Doto Masaba ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwanzi kabisa Mungu akubariki na naomba upeleke salamu zangu na shukurani kwa Mheshimiwa Spika kwa kusimamia Bunge letu vizuri na kwa fursa sawa kwetu wote. Ningependa vilevile kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa miaka hii na hii ni Bunge la mwisho kushirikiana kwa pamoja na kila mmoja akafika wakati huu Mungu atubariki wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais mwenye Wizara hii. Mheshimiwa Rais amesimamia Wizara hii na akisaidiwa na Waziri wetu na kwa kweli wengine wamesema na mimi nitakuwa nimekosa fadhila kama sitatambua miradi ile ya mkakati ambayo ametuwekea kwa manufaa ya nchi yetu na mikakati hiyo ndio itasaidia maendeleo ya wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutaja miradi hiyo kama *standard Gauge* ya *railway* ambayo itasaidia sana kubeba mizigo na kuongeza uchumi wetu, ufufuaji wa Shirika la Ndege ambayo itachochea sana maendeleo ya Utalii na usafiri wetu sisi wenyewe vilevile. Ya tatu ni ujenzi wa Bwawa la umeme la Mwalimu Julius Nyerere na ninyi mnajua kuwa na umeme wa uhakika maana yake ni kuwa na maendeleo ya hakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile afya ameichochea sana mpaka leo zahanati 1,198 jamani sio kazi ndogo katika miaka hii minne na miezi, vituo vya afya 487, hospitali 69, hospitali za rufaa 10 na Waziri leo ameelezea vituo vingapi, zahanati ngapi zitaongezeka ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais nina hakika hayo yote yanafanywa kwa ajili yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme vijijini na kuanzisha uwakala jamani kuwa na umeme vijijini maana yake na Miji ni kuletewa maendeleo vilevile, hili ni jambo kubwa kutoka vijiji 2118 leo 9000 na zaidi wana umeme jamani hili si jambo dogo na yote haya ni miradi ya mikakati ambayo ameanzisha Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi ndugu zangu ni wakala wa maji, wakala wa umeme na wakala wa barabara vijijini, wakala hizi zitasaidia sana barabara, maji ambayo ni jambo muhimu sana zitasaidia sana vilevile na umeme na kuleta maendeleo ya uhakika na ya haraka. Pamoja na hayo bila Mheshimiwa Jafo na Manaibu Waziri pamoja na Mtendaji Mkuu wa Wizara hiyo na watalaam wote nina hakika mengi yasingefanyika kwa hiyo nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Jafo na kila wakati tukiwa na jambo Mheshimiwa Waziri Jafo ukimuendea hajawahi kurudi nyuma ahsante sana wakisaidia na Manaibu Waziri pamoja na wataalam wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niseme kwamba jamani ningependa kusema machache ambayo yatasaidia sana vijiji vyetu na wilaya yangu. Kwanza ni sera ya barabara vijijini. Sera inasema kukarabati barabara ijijini haiongei kufungua barabara, ninaomba hii sera tuiangalie ili tuwe na kufungua na kukarabati barabara ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu tuna wakala wa *TARURA* ingawa wanapata fedha kidogo lakini tusibakie tu kukarabati kuna Wilaya ambazo hazina barabara nyingi, kuna Wilaya ambazo zina barabara nyingi lakini tukifungua tutawapa kipaumbele wale ambao hawana barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa mimi kwa wakala wa barabara, barabara ya kutoka Gisambarang kupitia Masusu, Milongori, Biroda mpaka Lalaji jamani ni mpakani halafu kuna msitu na kuna watu wengi sana, vilevile barabara nyingine ya kufungua ingekuwa barabara kutoka

Mascaroda kwenda Ng'arda, Lambo na kwenda Dareda ambako kuna hospitali kubwa pamoja na kwamba iko Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile ningependa kujiekeleza kwenye elimu ni muhimu sana na sasa elimu ya sayansi ndio muhimu nimefurahi, ninashukuru na ninampongeza Waziri kusema kwamba kila Wilaya zitajengwa barabara kwenye shule za sekondari, maabara zimeshajengwa zimefika mbali ninaomba sana tukamilishe ili watoto wetu wasome sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongea juu ya Watendaji wa vijiji na Kata. Kule kuna kata na vijiji ambavyo havina watendaji. Maana yake ni kwamba maendeleo na hata huduma za wananchi zinaomba muangalie umuhimu wa kuazisha ya kupeleka na kuajiri watendaji ili vijiji vyetu na kata zetu ziweze kuongozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kuongea kuongea habari ya *TASAF* ninajua itakuwa kwingine lakini ndio iko vijijini. Ninaishukuru Serikali namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Jafo na wengine wote kwamba sasa *TASAF* inaenda kwenye vijiji vyote *TASAF* ilikuwa inaenda kwenye vijiji vichache ikienda kwenye vijiji vyote wale masikini watapata namna ya kuweza kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapenda niseme kwamba kuhusu vituo vya afya niliomba kituo kwa ajili ya Basotu na Endasack lakini mmenipa vituo vya pembezoni ya Hilbadau au pamoja na Simbay sasa mmeniletea fedha kwa ajili ya Mogitu. Ninaomba usisahau kata hizo pamoja na kata zingine nakushukuru umesema kila kata, kila wilaya itapata vituo vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na vilevile nisipoongea juu ya mkopo ule wa asilimia 10 nitakuwa sijatenda haki. Jamani mikopo hii inainua wanawake, vijana na walemavu. Naishukuru na wilaya yangu kwamba wanatoa ingawa kuna deni ambalo huko nyuma hawakutoa

ninaomba kupitia msukumo wako madeni yale yaliyobaki wapewa wananchi lakini vilevile wanawake waendeleo sasa hivi naona msukumo umeongezeka tutaondoa umasikini wakisadiana na *TASAF* nina hakika tutakwenda mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Wizara hii ni Wizara muhimu sana ni *cross cutting* ni ya TAMISEMI ina maji na maji ni kitu muhimu sana. Wilaya kama ya Hanang iko kwenye *lift valley* hamna maji ninaomba jamani mshirikiane na Wizara ya Maji najua Wizara sasa hivi huu ni wakala hauko chini ya TAMISEMI lakini tuweze kuomba vijiji na kata zipate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana naomba niongee juu ya Corona, ni ugonjwa mbaya kuliko magonjwa mengine yote... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Desderius John Mipata atafuatiwa na Mheshimiwa Gimbi Doto Masaba, Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimshukuru pia Mwenyezi Mungu kutujaalia uzima na atujaalie atuvushe na janga hili la *corona* na naomba Watanzania wasikilize maagizo yaliyotolewa na Serikali pamoja na wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka mitano sasa, hii ndiyo bajeti ya miaka mitano tangu tumeingia hapa Bungeni. Mimi nilibahatika pia kuwepo katika miaka mitano iliyotangulia. Nimeona utumishi uliobadilika sana nikilinganisha na vipindi hivi viwili ambavyo nilikuwepo kwenye Bunge.



Katika kipindi hiki ni lazima niseme mambo yafuatayo ili Watanzania wajue na wananchi wajue kwamba mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika maeneo ya utumishi wa umma yameleta heshima kubwa sana kwa Taifa na sasa wananchi wanahudumiwa vizuri kupita wakati wowote ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeona ameo koa pesa nyingi sana katika fedha za umma kwa kufuta safari za nje, kwa kurekebisha Sheria ya Manunuzi ambayo ilikuwa inatumika vibaya, lakini vilevile amesaidia sana kuhakikisha kwamba rasilimali hizi zilizokuwa zinaokolewa zinakwenda kwenye uwekezaji wa wananchi kama vile madawa yameongezeka, shule nyingi zimejengwa na kwa uchache nitaelezea shule zangu zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba ipo pia miundombinu mingi na ya nguvu iliyojengwa kwa kipindi hiki. Kwa mfano, ujenzi wa reli katika kiwango cha *standard gauge*, ujenzi wa Bwawa la Nyerere ni miradi ya kimkakati ambayo ingeweza kujengwa katika Awamu ya Pili, ingeweza kujengwa katika Awamu ya Tatu, ingeweza kujengwa katika Awamu ya Nne lakini huyu Bwana kwa sababu ana maamuzi magumu na anachukua hatua za mara moja ameamua yeye mwenyewe. Ndiyo maana tunamuita sasa ni *Bulldozer* kwa sababu miradi yote hii Mungu akimsaidia sana atakaa miaka 10 tu kwenye nafasi hii lakini miradi hii itadumu kwa karne, Watanzania watakuwa wamepata Mtu wa pekee kwa sasa kuliko wakati wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Watanzania wajue, leo tuna Rais ambaye anatolewa mfano ndani ya Tanzania, nje ya Tanzania na duniani pia. Sasa ni wakati wa kumtumia vizuri na wakati mwingine kumpa nafasi zaidi na katika miradi amesema yeye mwenyewe kwamba katika suala la maendeleo hakuna siasa wala itikadi na wenzangu wa upande wa pili nimekuwa nikiwasikia wanasema amechukua ajenda zetu, sasa kiongozi afanye nini? Ameona kwenu kuna jambo zuri na ya kwake mazuri akayachukua, pamoja

akatekeleza. Kwa hiyo, ni nafasi sasa tumwache katika miaka mitano ijayo ili atende kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujio wa Mheshimiwa Magufuli kuwa Rais haukutarajiwa na watu wengi. Ni kama maongozi ya Mwenyezi Mungu kwa sababu tumekuta nchi yetu iko katika hali ngumu sana; rushwa, madawa ya kulevya na vitu vingine. Ameingia mtu ambaye amekuwa jasiri katika mambo hayo na ameyashughulikia sawasawa na sasa Taifa liko na Heshima. Tanzania imepata heshima miongoni mwa Mataifa, anasikika kila mahali. Kwa hiyo, kiongozi wa namna hiyo ukimpata, ni vizuri Watanzania kufikiri mara mbili. Ni wachache kupatikana hawa watu. Watu wanaothubutu, wenye uthubutu wa nguvu kama huu na kwa kweli watu wote mmeona madawa ya kulevya kwaheri, rushwa nchini kwaheri, maliasili zetu zimetunzwa vizuri, miundombinu inajengwa kwa nguvu zote. Kwa hiyo niseme tu kwamba miaka mitano hii iliyopita Serikali yetu imefanya jambo kubwa sana miongoni mwa Watanzania na miongoni mwa Mataifa yanayotuzunguka na ndiyo maana nchi zote ambazo zinatuzunguka wanasema tupate Magufuli wetu. Kwa hiyo tumepata kiongozi ambaye ni mfano katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, niseme tu kwamba, katika Jimbo langu nimepata pesa za kutosha katika elimu. Katika elimu tumepata pesa za kutosha, Shule ya Sekondari ya Milundikwa nilisimama hapa kuomba na kila mtu alisikia nimepata zaidi ya milioni 700 na ni shule ya mfano kabisa. Shule ya Sekondari ya Hundi tumepata zaidi ya milioni 130 na tumejenga, Chuo cha Maendeleo-Chala ambayo sasa ni VETA ambayo inapiganiwa tumepata milioni 636 na sasa tayari majengo yanaisha. Miundombinu, barabara yetu ya kutoka Sumbawanga kwenda Kanazi, kwenda Kibaoni imekwisha kuwekewa lami. Tunamaliza hivi, tumeanza Shule ya Sekondari mpya ya Myula na tumepata pesa, kwa hiyo kila mahali tumeweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kueleza matatizo yafuatayo yaliyopo Jimboni kwangu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa walizungumzia bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni changamoto, lazima yawepo hakuna wakati matatizo yote yatakwisha. Naomba fedha zaidi katika ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kasu ambacho tumekuwa tukikisema kila wakati, naomba fedha zaidi katika Kituo cha Afya cha Kala ili kiweze kufanikiwa.

Naomba vilevile niweze kupata fedha katika Kituo cha Afya cha Ninde ambacho tayari wametupatia pesa milioni 200 waongeze hela nyingine kiweze kukamilika lakini kwa vyovyote vile tumefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba matengenezo ya barabara ya Nkana-Kala, Milundikwa-Kisura, Namasi-Ninde, Kitosi-Wampembe, naomba umeme katika Kata ya Kala, Kata ya Wampembe, Kata ya Kizumbi na Kata ya Ninde. Kazi hii nzuri najua kwa maombi haya na Serikali yetu yote haya yatawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nawashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnaweza kuona sasa kwamba kweli Wabunge humu wamebobeza sasa, maana huu mchango kama unaweza kupigiwa makofi na Kambi zote siyo masihara. Mheshimiwa Mipata amefanya mambo mazito humu ndani. *(Kicheko)*

Haya nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kusimama katika Bunge lako hili ambalo naamini

kabisa kwamba tuko katika Bunge la mwisho kwa kipindi hiki na mkataba wetu unakwenda kuisha wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Chama cha Upinzani Kikuu hapa Nchini kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuongoza Chama hiki kwa umakini mzuri sana. Pia nimshukuru yeye pamoja na timu yake kuhakikisha kwamba yote yale ambayo yalikuwa yanapita katika nyuso zao, nawashukuru na kuwapongeza kwamba wameweza kuyashinda yote. Mungu awasimamie, tunaendelea kuwaombea, naamini katika harakati za kutafuta Dola yote hayo lazima tuyapatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeskiliza hotuba ya Waziri wa TAMISEMI; katika hotuba yake mambo mengi yamejikita sana kwenye kuboresha mambo mazuri, hakuna sehemu ambayo amezungumzia changamoto. Sasa nilikuwa najaribu kupata masikitiko pamoja na kwamba amezungumza kuhusu Halmashauri, makusanyo, mapato na mengine, lakini sikuona popote alikozungumza kwamba Halamshauri zetu ziko taabani. Leo nakwenda kuzungumza kwa mara ya mwisho kutetea Halmashauri hususani Halmashauri ninazotoka mimi. Kwa kweli inaleta masikitiko makubwa sana na nikirejea kauli ya Spika wakati juzi anabariki hotuba ya Waziri wakati anahitimisha Waziri Mkuu alisema; "ifikapo tarehe 30 Juni atahakikisha malipo ya Wabunge yote yako tayari".

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninasikitika kusema Mheshimiwa Jafo anapenda kufunga Halmashauri zake zikiwa zinaongoza kwa madeni makubwa kwenye Halmashauri zake kwa Madiwani kudai posho nyingi. Sasa sijajua wakati anahitimisha hotuba yake, nataka kusikia ni kauli gani ambayo ataitoa kuhusu madai ya Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Halmashauri ninayotoka Wilaya ya Itilima; Madiwani mpaka sasa hivi wanadai posho milioni 502. Madeni ya Benki hayalipiki, fedha za Bima hazilipiki, Madiwani hawawezi kutibiwa na Bima zao hakuna malipo yanayofanyika. Sasa ni ishara tosha kwamba

Mheshimiwa Jafo anaongoza idadi kubwa ya Watanzania waishio bila furaha yoyote katika Taifa hili. Haiwezekani Diwani akaitwa Diwani hana chochote, madai ya kuanzia Mwaka 2016 mpaka leo ninavyoongea madeni ni makubwa, ni makubwa. Sasa sijui tunakwenda wapi.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masaba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji; ni kwamba juzi tu tumetoka kumaliza kukagua hesabu za mikoa yote na halmashauri zote nchi nzima. Kamati yangu asilimia 96 ya madeni ya Waheshimiwa Madiwani wamekamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kumpa taarifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba umeipokea taarifa hiyo?

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei na ndiyo maana sikutaka kurejea kwenye halmashauri yoyote, zaidi ya halmashauri ninayoingia mimi, umenielewa? Kwa hiyo nimeongea hivyo nikiwa na uhakika na ukitaka *documents* za madai naweza kukabidhi kwenye meza yako. Hili jambo siyo ndiyo naanza kuliongea, nilishamfuata Naibu Waziri zaidi ya mara moja.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA. SALUM:** Taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masaba kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Saada Mkuya Salum.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tunamsikia mzungumzaji anavyosema na Makamu Mwenyekiti ambaye tuko Kamati moja ameelezea *situation* ilivyo. Sasa ikiwa anachukua

sehemu ndogo ya jambo lililokuwepo halafu analitapakanya inaonekana ndiyo *situation* ilivyo huo ni upotoshaji. Kwa hivyo, tunaomba wakati anachangia aji-*confine* katika sehemu ambayo yeye yupo na aweke *specific area* ya kile anachokizungumza kwa sababu sisi tuko kwenye Kamati na *situation* iko vizuri kama ambavyo Makamu Mwenyekiti ameelezea. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba uneipokea taarifa hiyo?

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei. Itilima siyo Zanzibar, kwa hiyo mimi nazungumza hapa kama Mwakilishi wa Itilima

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo. Naomba make, lakini Mheshimiwa Gimbi Masaba Wabunge wote humu ndani ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo nadhani hilo tulimalize kwa namna hiyo, kwa hiyo wewe endelea na mchango wako lakini Mheshimiwa Saada Mkuya Salum ni Mbunge wa Bunge hili kama wewe, kama Mbunge mwingine yoyote.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ninachokizungumza Kiti chako kinanielewa vizuri sana. Sauti niliyosimama hapa ndiyo sauti ya ninapotoka, sasa nisipozungumza matatizo ya maeneo niliyotoka nani azungumze? Mimi ndiyo Mwakilishi yeye kama ana mambo mazuri kule aendelee, naomba niendelee. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri nimepitia kwa ufupi kabisa, lakini sikuona mahali popote ambapo kuna ugatuzi wa Majimbo au Mamlaka ya Miji Midogo, sijaona popote pale. Hii ndiyo bajeti ya mwisho, tulitarajia hivi vitu tuvisikie lakini sijaona popote pale; na ni

kwa nini nilikuwa nafuatilia? Nilikuwa nafuatilia kule Mkoani Simiyu kuna Jimbo la Bariadi Mjini. Jimbo la Bariadi Mjini lina Halmashauri mbili, lakini Jimbo hili lina Mbunge mmoja. Sheria inamtaka Mbunge ahudumu Halmashauri moja sasa kama hili Jimbo lina Halmashauri mbili, lina Wakurugenzi wawili, lina Wenyeviti wa Halmashauri, lina Mabaraza ya Madiwani wote na haya Mabaraza lazima kuwe na Kamati za fedha. Mbunge anapaswa kuingia kwenye Kamati moja tu ya fedha, lakini sisi pale Bariadi kuna Mbunge ambaye ana ratibu Kamati mbili za Fedha ilihali wakijua kabisa kwamba Kamati ya fedha ni siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujua kwamba kwa nini ajenda ya ugatuzi wa madaraka haijaletwa wakati kuna Majimbo ambayo yana sifa kabisa ya mgawanyo. Ni nini kinachofanyika pale Bariadi, kuna siri gani katika Jimbo hili kutogawanywa? Kwa hiyo, nataka kauli ya Waziri atuambie ni kwa nini Jimbo hili haligawanywi wakati mamlaka zote linazo, kwa nini? Jimbo hili ni kubwa, lina Kata 31, kwa nini Mzee wangu anateseka na mamlaka mbili ambazo hazina sababu yoyote ya msingi? Kwa hiyo, naomba tafadhali sana watuambie siri ya kutogawanywa Jimbo hili, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nina ombi; hapo Mji wa Bariadi katika Mji wa Lamadi, huu mji unahitaji kufanywa kuwa mamlaka ya mji mdogo kutokana na kwamba sifa zote zipo za kufanywa kuwa Mji Mdogo wa Lamadi pale kwa sababu mapato yote yapo, sifa zote zipo, tuna kila kitu, tuna sekondari tatu, tuna shule za msingi saba, tuna vituo vya Polisi, tuna njia kama tatu zinazoingiza mapato katika Mji ule.

Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa atuambie *solution* ya Mji wa Lamadi kwa sababu yeye mwenyewe unafahamu ule mji ukifanywa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo utaleta manufaa makubwa sana. Pia utaleta shule kwa watu wengine kuhakikisha kwamba miji mingine inakua, sasa tunavyoendelea kuona miji inakua halafu tunaendelea kuifunga inakuwa siyo sawa. Kwa hiyo,

nimwombe sana Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha atueleze ni nini hatima ya Jimbo la Bariadi Mjini na Mji wa Lamadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu elimu bure; ni kweli kwamba Mbunge ambaye alisimama hapa akasema kwamba yapo mambo mengi waliyoyachukua yaliyotoka upinzani, nakubaliana naye kwa kauli hiyo, lakini namna yalivyochukuliwa sasa na elimu bure.

Waheshimiwa Wabunge hebu tujulize hivi elimu bure ni nini? Elimu bure tafsiri yake ni nini? Ni kitu gani tulichokuwa tunalipa kikubwa kwenye shule za msingi. Kama leo mwanafunzi anaenda shule amebeba *rim*, amebeba sijui nini, mita moja ya kitambaa cha *skirt* ni Sh.10,000 ili aweze kuvaa ni Sh.20,000 mita mbili, yaani yale mahitaji yote yako kwa mzazi. Nilitarajia kwamba, kama ni elimu bure haya majukumu makubwa yaondolewe kwa mzazi, lakini leo haya majukumu makubwa yote yamebaki kwa mzazi.

**MBUNGE FULANI:** *Ream*.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** *Ream*, mlinzi na kila kitu kwa mzazi sasa tafsiri ya elimu bure ni ipi wakati gharama zote ziko kwa mzazi?

## T A A R I F A

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mimi nilidhani kwamba mzazi huyu apunguziwe majukumu ili anavyotafuta fedha hizi zikasaidie maendeleo mengine. Sasa ni kitu gani tunachozungumza nafikiri hili limebaba ajenda nyingine ambayo ni ya uwongo kabisa jamani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masaba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha.



**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hakuna sehemu yoyote palipotamkwa elimu bure inaitwa elimu bila malipo. Miongozo ya Serikali ilikwishatoka kwamba wazazi watafanya hiki na Serikali itafanya hiki, hiyo elimu bure ilikuwa ya upande wa kule. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kuna wakati napata masikitiko sana hata Mbunge anavyosimama anapongeza kila kila kitu hii tuamini ni dhambi, kabisa! Huwezi kupongeza wananchi wako kule wanateseka, dakika saba zote unapongeza. Haiwezekani binadamu akakosa changamoto, kwa nini Serikali hii ina mambo mazuri tu? Huyu huyu Mbunge anayenipa taarifa mimi barabara zote hazipitiki, Serengeti haipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesema lazima tuijue tafsiri ya elimu bure; madawati mzazi, kila kitu mzazi halafu na sisi tumebeba kiholela hoja hii tunasema elimu bure, elimu bure tulikuwa tunalipa nini? Hata kipindi cha Kikwete ada ya sekondari tulikuwa tunalipa Sh.40,000, nani mzazi hana 40,000? Halafu mnaleta hapa *slogan* ya elimu bure, elimu bure, acheni utani jamani kwenye maisha ya Watanzania, siyo sawa. Eti elimu bure, elimu bure, ipi? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saada Mkuya Salum.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika Naibu, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo wako kutokana na maneno ambayo Mbunge aliyemaliza alivyokuwa akiyazungumza kama yanaruhusiwa katika Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ambayo Mbunge alikuwa anayatoa wakati nilipokuwa nikimpa taarifa kutokana na ukweli wa mambo yanavyokwenda jibu lake lilikuwa ni kwamba hapokei taarifa hiyo na kwamba Halmashauri ya Itilima siyo Zanzibar.

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** *It is true* kwamba Halmashauri haiwezi kuwa sawasawa na nchi ambayo imeunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba mwongozo kama maneno hayo yanaruhusiwa wakati Mbunge anaposimama na kutoa taarifa kwa mujibu wa Kanuni zilivyo na kulinganisha maeneo ambayo Mbunge anatoka *as if* kwamba Mbunge anayetoka Zanzibar hana haki ya kuzungumzia maeneo mengine na *specifically* ninaposimama mimi pia ni mjumbe wa Kamati hiyo ya TAMISEMI. Kwa hiyo, nilichokuwa nakizungumza ni kitu ambacho tumeki-*articulate* vizuri katika Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako ikiwa maelezo hayo yanaweza kuruhusiwa na yaendelee katika Bunge lako Tukufu na ikiwa sivyo basi tunaomba hiyo kauli ifutwe.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, Wanadhimu humu ndani inabidi wawe ni watu wenye, moja, uvumilivu lakini pia watulivu na wawe wanasikiliza hoja vizuri ili Kiti

kinapotoa maamuzi wajue namna ya kuongoza watu wao vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Saada Mkuya Salum akiomba kujua kama jambo ambalo amelizungumza Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba wakati akichangia linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Mheshimiwa Masaba wakati akichangia alipewa taarifa na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum ambaye alikuwa anaungana na Mheshimiwa Mwanne Mchemba kwenye hoja ya madeni ya Halmashauri hasa kuhusu posho za Madiwani.

Mheshimiwa Masaba alieleza namna ambavyo yeye Halmashauri yake, katika huo mchango mzima, siwezi kuzungumza kila neno lakini katika mchango wake alionyesha kwamba ni tatizo kubwa sana lakini baada ya kupewa taarifa akazungumzia Halmashauri anayotoka yeye ya Itilima. Kwa hiyo, wakati akipewa taarifa hiyo badala ya kujibu vile alivyoulizwa kwa sababu mimi nilimwongoza Kikanuni taarifa hiyo, je, unaipokea ama hauipokei? Yeye akasema pengine hali hiyo iko Zanzibar.

Mtakumbuka japokuwa sikuwa nimesimama kutoa huo mwongozo juu ya jambo hilo lakini nilitoa maelezo kwa kifupi kwamba jambo hilo alilolisema Mheshimiwa Masaba halikuwa sawasawa kwa sababu huyu anayezungumza hazungumzii Zanzibar. Kwa hiyo, kumhusisha yeye na hoja anayoisema na Zanzibar si sawasawa. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Saada Mkuya Salum kaamua kusimama na kuomba mwongozo wa Kiti kufahamu kama hilo jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi, haliruhusiwi na ndiyo maana wakati lilipotokea nililitolea maelezo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tuchunge kauli zetu na sisi wote humu ndani kiapo chetu ni kimoja Wabunge wote ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wote wana hadhi sawa na wanapochangia jambo popote linapotokea kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wako sawasawa.

Sasa niwaombe kwa sababu hii michango ya bajeti ndiyo imeanza ni vizuri sana kujipeleka kwenye ile hoja unayokuwa unaisemea. Sisi wote ni mashahidi kwa taarifa aliyoitoa Makamu Mwenyekiti ni wazi asilimia 96 madeni yamelipwa bado asilimia nne. Sasa kama Mbunge anataka kuzungumzia asilimia nne ile ikikaa hivyo hakuna mtu atampa taarifa mtu mwingine lakini ukionyesha kwamba asilimia 96 hazipo zipo tu hizi asilimia nne pia utakuwa hauweki huo usawa. Kwa hiyo, ni vizuri hata sisi tunapochangia tuyaone mambo haya kwa mapana hayo.

Kwa hiyo, mwongozo wangu kwa hili jambo alilouliza Mheshimiwa Saada Mkuya Salum ni kwamba jambo hilo haliruhusiwi Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Neema Mgaya atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Omary Mohamed Kigua ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na kutuweka hai ndani ya miaka yote mitano hadi hivi leo tukishirikiana vizuri Wabunge wote pamoja na Mawaziri na Mheshimiwa Spika katika kutekeleza majukumu ambayo tulipewa na wananchi wetu ili tuje kuwawakilisha humu ndani ya Bunge. Nichukue nafasi hii kumwomba Mungu aturudishe wote kwa umoja wetu ili tuendelee kuwatumika wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri iliyofanya ndani ya miaka mitano. Nampongeza Rais, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Vilevile, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Jafo pamoja na Manaibu wake Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waitara kwa

kazi nzuri waliyoifanya ndani ya Wizara hii. Nawaombea Mungu awarudishe tena na awarudishe kwenye nafasi zao ili waweze kukamilisha yale mambo mengine ambayo wamepanga kuwafanyia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe hususani akina mama kwa kujitoa kwa moyo wote katika kuchangia masuala mbalimbali ya maendeleo ili kuhakikisha kwamba mipango yote na kazi zote zilizopangwa na Wizara hii zinatekelezeka kwa urahisi. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipongezi tu bila kuwa na sababu, nina sababu za msingi. Naipongeza Serikali ndani ya miaka mitano imejenga vituo vya afya 433. Ndani ya Mkoa wetu wa Njombe tunaishukuru Serikali tumepata vituo vya afya zaidi ya 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niendeleo kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Magufuli kwa kazi nzuri waliyoifanya kuhakikisha kwamba wamejenga zahanati 368. Ndani ya Mkoa wetu wa Njombe tumejengewa zahanati zaidi ya 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali pamoja na Rais wetu mpendwa kwa kazi nzuri waliyoifanya ndani ya miaka mitano ya kujenga Hospitali za Wilaya 98. Ndani ya Mkoa wetu wa Njombe tumepata hospitali tatu, *Njombe DC, Makambako TC* na Halimashauri ya Wanging'ombe. Vilevile, tumeona kwamba kuna hela zimetegwa kwa ajili ya wodi zetu, Halmashauri ya Wanging'ombe tunashukuru tumepata, Halmashauri ya *Makambako TC* tumepata lakini sijui mmetusahau kidogo kule Njombe DC muweze kufanya mambo yaweze kukaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi kubwa sana ndani ya miaka mitano. Kusema kweli kwa kazi nzuri aliyofanya Mheshimiwa Rais naomba Watanzania wampe

nafasi tena aweze kukamilisha mambo yale ambayo amekusudia kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejenga madarasa 19,808, nina kila sababu ya kuipongeza Serikali. Serikali imejenga maabara 227 ndani ya miaka mitano na matundu ya vyoo 7,922. Hongera sana kwa Serikali, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile shule zetu zimeweza kupata madawati 5,070,896, hongera kwa Serikali. Serikali haikuishia hapo imefanya kazi kubwa ya kukarabati shule kongwe 73 zikiwepo baadhi ya shule ndani ya Mkoa wangu wa Njombe. Sisi watu wa Njombe ni wa shukrani, tunaishukuru Serikali na tunaahidi hatutafanya makosa Oktoba, 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Serikali imejitahidi, imejenga barabara kilometa 74,940. Hayo yote ni mambo mazuri ambayo yamefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Jemedari wetu, Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango mzuri ambao Serikali imeweka kwa ajili ya bajeti ya mwaka 2020/2021. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Jafo na Manaibu wake na timu nzima pale Wizarani kwa mkakati mzuri waliojiwekea wa kuhakikisha kwamba watakwenda kujenga maabara saba (7) na zahanati tatu (3) katika kila Halmashauri. Mimi sina cha kusema zaidi ya kuwatakia kheri Mawaziri hawa na Rais wetu na timu nzima, Mungu awape afya njema ili waje kutekeleza yale walioyokusudia kuyafanya. Kwa maana hiyo, namwombea Mheshimiwa Rais arudi, namuombea Mheshimiwa Waziri Jafo na Manaibu wake warudi Ubunge na kwenye nafasi zenu ili muweze kuifanya kazi hii vizuri na muikamilishe vizuri ndani ya miaka mitano mingine inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikutakie kheri wewe pamoja na Mheshimiwa Spika na Wabunge wote kila kheri turudi kukamilisha yale ambayo

wananchi wetu wametutuma tuje kuukamilisha kwa umoja wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru kina mama wa Mkoa wa Njombe kwa kuniadini na kwa kweli nimewatendea haki kama mnavyoniona na kila siku sichoki kuuzungumzia Mkoa wa Njombe. Kwa hiyo, nitumie pia nafasi hii kuwaomba ridhaa wanipe tena miaka mitano ili nije kukamilisha yale ambayo nilikuwa nimepanga kuja kuyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niungane na Wabunge wenzangu kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri anayowafanyia Watanzania kwa miradi mbalimbali ambayo imefanywa katika nchi yetu. Kazi zilizofanywa na Serikali hususani katika nchi yetu ni nyingi na ndiyo maana baadhi ya Wabunge wamesema na mimi naungana nao Mheshimiwa Rais huyu kwa kazi alizozifanya ndani ya miaka minne na zaidi, nadhani kwa sababu tuna ugonjwa huu wa *Corona*, tuna tatizo pia ambalo limeingia katika nchi yetu hasa miundombinu kuharibiwa na mvua ambazo zimenyesha nyingi sana, imevuruga mipango ya Rais ambayo alikuwa ameipanga katika miaka mitano na katika miaka mitano tena iwe kumi, kwa sababu mipango itakuwa imeharibika kutokana na haya mawili niliyoyataja, nadhani Bunge linalokuja iletwe Katiba hapa aongezewe miaka mitano

mingine mbele ili aweze kukamilisha ndoto za Watanzania ambazo amepanga ziweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija na ndugu yangu Mheshimiwa Jafo ambaye ndiye anasimamia Wizara hii, kwa kweli mdogo wangu Mheshimiwa Jafo amefanya kazi kubwa sana, pamoja na wanaokusaidia Naibu Mawaziri wawili, Katibu Mkuu na wataalam wote katika Wizara hii. Ukiangalia ukurasa wa 54 unasema tulikuwa na vituo 535 sasa tuna vituo 968 vikiwepo na vya Makambako. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo amefanya kazi kubwa sana. Kwa sababu amewafanyia kazi Watanzania naye tunamwomba kwenye Jimbo lake kule asitokee mpinzani upite bila kupingwa pamoja na wanaokusaidia nao wapite bila kupingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wapo wasaidizi wa Rais akiwepo Waziri Mkuu, kazi kubwa anayowafanyia Watanzania kwa kuzunguka, jana tu tumemwona alikuwa Zanzibar, anawazungukia Watanzania kutekeleza shughuli ambazo Rais amezipanga. Naye Waziri Mkuu kule Ruangwa, mimi na Wabunge tunakuomba upite bila kupingwa. *(Makofi/Vigelelele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile na dada yangu Mheshimiwa Jenista kwa kazi anazozifanya namwomba kule Peramiho apite bila kupingwa ili aendelee kuwatumikia Watanzania. Pia Spika wetu Job Ndugai kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya Bunge hili kuwatumikia Watanzania naye tunamuomba apite bila kupingwa. *(Makofi/Vigelelele)*

**MBUNGE FULANI:** Naibu Spika kule Mbeya.

**MHE. DEO K. SANGA:** Lakini na wewe Naibu Spika mdogo wangu, Mheshimiwa Tulia tunakuomba kule Mbeya upite bila kupingwa ili uweze kuwatumikia Watanzania. *(Makofi/Vigelelele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maombi haya, nirudi sasa kwenye Jimbo langu la Makambako.



**MBUNGE FULANI:** Na wewe upite bila kupingwa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Watanzania wakiwepo wa Jimbo la Makambako nawapenda sana, wanajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye Jimbo la Makambako. Miradi iliyotekelezwa kwenye jimbo langu ni mingi sana. Ombi langu ni dogo tu kwa Watanzania hususani Jimbo la Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, tuna mradi mkubwa ule wa fedha za kutoka Serikali ya India kwa mkopo nafuu. Mradi ule tumewaambia wananchi mara nyingi sana na kwa muda mrefu kwamba mradi utatekelezwa. Kwa sababu Wizara inayohusika wako hapa, naomba waone namna ya mradi ule kuweza kuanza katika mji wetu wa Makambako. Tunashukuru kwamba kuna miradi ipo inayoendelea ikiwepo pale Mawande, Lingala, Nyamande na pale Ikeru. Miradi hii inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Vituo vya Afya, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, pale kituo chetu kipya cha Lyamkena kimeshafikia asilimia 99. Tunaomba vifaa tiba pamoja na wataalam ili kituo hiki kianze kufanya kazi iliyokusudiwa ikiwepo pia na hospitali ya Halmashauri yetu ambayo imejengwa pale Mlowa na imefikia asilimia karibu 100. Tunaomba kupata vifaa tiba ili ianze iweze kuhudumia Wanamakambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile upande wa Kituo cha Afya cha Makambako cha zamani, nimemwambia Mheshimiwa Jafo mara nyingi kwamba hatuna wodi ya wanaume; na wanaume wanaugua. Kwa hiyo, ombi langu tuone namna ya kupata fedha tuwapelekee tuweze kujengewa wodi ya wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija upande wa umeme wa *REA*, Waziri mwenye dhamana, haki ya Mungu nitoe neno la shukrani kabisa. Kwenye Halmashauri yangu kimebaki kijiji kimoja tu kupata umeme. Naomba kwa sababu nacho ni

kimoja, kiweze kumalizwa. Nacho ni Mtanga. Vijiji vingine vyote tumeshapata umeme. Kwa hiyo, kilichobakia ni maeneo madogo madogo ya Vitongoji kuwapelekea. Kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa namna ambavyo mnatujali kupitia Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni watu wa *NIDA*, Waziri mwenye dhamana yuko hapa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, basi baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Omary Mohamed Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, ajjandae.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, ambaye ameniwezesha kusimama leo kuweza kuchangia bajeti iliyoko mbele yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo siyo upepo. Upepo huwa hauonekani, lakini yakifanyika mambo ambayo yana maslahi mapana na wananchi wa Tanzania na watu wanaona, hatuna budi kupongeza. Naomba tuipongeze Serikali katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo vibaya kupongeza kwa mambo ambayo yanaonekana. Nitoe mfano mdogo tu, hapa katika Mkoa wa Dodoma ambao sisi Waheshimiwa

Wabunge tupo. Leo hii Dodoma imebadilika sana; ukipita mitaani, barabarani huko unaona mabadiliko. Ila katika maeneo yetu tunakotoka tunaona namna ambavyo vituo vya afya, barabara, majengo ya shule yanavyokwenda. Sasa siyo vibaya hata kidogo Mheshimiwa Mbunge anaposimama na kuanza kusifia. Nadhani ni wajibu wetu Wabunge kuweza kusema yale mazuri ambayo yamefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imesheheneza mambo mengi sana. Imegusa kila eneo na hususan mambo ambayo yanagusa wananchi. Tukianza kwenye Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, yote yameonyeshwa hapa. Mimi nina ushauri ambao naomba Mheshimiwa Waziri auchukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mjumbe wa Kamati ya PAC na nilipata bahati ya kutembelea baadhi ya Hospitali za Wilaya ambayo Serikali ilitoa shilingi 1,500,000,000/=. Moja ya changamoto ambayo niliishuhudia na ni jirani tu hapa kwenye Hospitali ya Mtera; tuliona hospitali ile imejengwa kwa *force account*, jambo ambalo ni zuri kabisa, gharama ilikuwa ni ndogo, lakini kuna baandi ya mambo ambayo hayakuzingatiwa na pengine kama yangezingatiwa leo hii Hospitali hizo za Wilaya zingekuwa zimemaliza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmoja ni kwamba katika majengo yale hatukuzingatia nyumba za Madaktari, nyumba za kuweka maiti (*Mortuary*). Naomba sasa, maeneo yale ambayo yana Hospitali za Wilaya angalieni maeneo haya, hatuwezi kuwa na Hospitali ya Wilaya bila kuwa na Hospitali ya Mganga. Hili ni jambo la kuzingatia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia na nyumba za wahudumu ni jambo ambalo tulitakiwa tulizingatie. Kama Serikali Kuu hatuwezi kutoa fedha, basi tuangalie namna ambavyo Halmashauri zetu zinaweza zikatoa fedha ili Hospitali ya Wilaya ikikamilika, basi na nyumba za wahudumu ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la *TARURA*. Mwaka huu maeneo mengi Tanzania yamepata mvua za kutosha. Nichukulie mfano katika Wilaya yangu ya Kilindi mvua zilianza mwezi wa Kumi hadi leo hii, mvua zinaendelea kunyesha. Mvua ni baraka kwa Watanzania na mvua ni baraka kwa wakulima, lakini pia zimeharibu sana miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri mwenye dhamana kupitia *TARURA*, hebu angalieni maeneo ambayo mvua zimekuwa nyingi sana. Timu zipite kwenda kuangalia kwa sababu wakulima hawa watapata mazao ya kutosha, lakini mazao haya yatapita wapi kama barabara zitakuwa hazipitiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja. Ni kwamba nina barabara kubwa ambazo takribani miezi mitano sasa hivi hazipitiki. Kuna barabara ya Kwinji - Muungano hadi Kilindi Asilia. Ni eneo ambalo lina uzalishaji mkubwa sana, lakini ni eneo ambalo hata pikipiki haipitiki. Mheshimiwa Waziri aliniahidi akaniambia kwamba timu yako itapita Wilaya ya Kilindi kufanya tathmini kuona maeneo ambayo yameharibika. Hadi leo nazungumza hapa ni kwamba watu wake hawajafika. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwa heshima kubwa sana, najua Mheshimiwa Waziri ni msikivu, najua Serikali inasikia, maeneo hayo ambayo nimeyataja yaweze kupitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo eneo lingine ambalo pia ni muhimu sana, ni barabara ambayo inaunganisha Wilaya ya Kilindi na Simanjiro kwenye Kata Saunyi. Pia ni miezi sita haipitiki. Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu ina pori tengefu la Handeni, ni pori ambalo lina wanyama sana na eneo la utalii. Namwomba Mheshimiwa Waziri tuangalie namna ambavyo barabara hizi ni za kutengenezwa ili ziweze kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kwamba nilibahatika mwezi wa Tatu mwaka 2020, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya ziara

kwenye Jimbo langu la Kilindi. Katika maeneo ambayo alipita ilikuwa ni kwenye Kata ya Kwediboma ambayo Mheshimiwa Waziri alitupatia shilingi milioni 300. Ni kweli kabisa kwamba fedha zile zimefanya kazi nzuri lakini kituo kile hakijakamilika. Bahati mbaya zaidi, Wilaya ya Kilindi ina Vijiji 102, Vitongoji 611, Tarafa nne tuna Kituo cha Afya kimoja tu ambacho kinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu tuongezewe shilingi milioni 200 ili Kituo cha Afya cha kwenye boma kiweze kufanya kazi. Kama hiyo haitoshi, tuna Tarafa na Kata ya Tungule ambayo ina umbali takribani kilometa 200 wananchi hawa ili waweze kufika Kituo cha Afya cha Songwe ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya, ni umbali wa kilometa 240.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuna umuhimu wa hali ya juu sana kwamba Kata ya Tungule ambayo iko karibu kabisa na Wilaya ya Gairo tuweze kupatikwa Kituo cha Afya. Kwa mawazo yangu ukiniuliza, nitakwambia Vituo vya Afya ni bora zaidi kwa sababu vikijengwa katika ubora unaotakiwa kama ambavyo tunaona vilivyojengwa sasa hivi, tuna uhakika kabisa wa kuwasogezea wananchi huduma hii badala ya kujenga Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa sipingi kwamba Hospitali ya Wilaya ina umuhimu, lakini kwangu mimi ukiniuliza Mbunge wa Wilaya ya Kilindi, nahitaji zaidi Vituo vya Afya kwa sababu ndivyo ambavyo vinaweza vikahudumia wananchi wangu na kuweza kufika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ushauri juu ya watumishi katika Halmashauri zetu. Imejengeka kwamba watumishi wanatakiwa waweze kuhama baada ya kufikisha miaka mitano au sita, lakini kuna baadhi ya watumishi katika baadhi ya Halmashauri zetu wanakaa miaka hadi 20. Jambo hili halina afya hata kidogo. Halina afya kwa sababu wakati mwingine halimfanyi mtumishi aweze kufanya kazi wala kujifunza mambo mapya. Namwomba Mheshimiwa Waziri; angalia, pitia Halmashauri zako zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, tuna watumishi wamekaa miaka 18 mpaka 20 wilaya hiyo hiyo. Watumishi hawa hawajifunzi jambo lolote lile, hawapati changamoto mpya hususan katika sekta ya elimu. Wakati mwingine unaona kwamba elimu katika baadhi ya maeneo yetu, ufaulu wa wanafunzi hauendi sawa, kwa sababu mwalimu amekaa shule moja miaka 15 mpaka 20 hajajifunza jambo, anaona mazingira ni yale yale. Nashauri sana, namwomba sana hebu allangalie katika mtazamo ambao unaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine namwomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aangalie namna ambavyo *force account* inatumika. *Force account* ni nzuri lakini nadhani elimu haijaenda sawa sawa hususan kwa Wakurugenzi. Na sisi kama Wabunge tunao wajibu wa kueleza nini dhana ya *force account*, kwa sababu *force account* inatakiwa isaidie kupunguza gharama, lakini wananchi wanakuwa hawaelewi *force account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili pengine utengenezwe waraka maalum uende kwa Wakurugenzi waweze kuelezwa nini dhana ya *force account* kwa sababu wananchi hawaelewi.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana, shukrani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mheshimiwa Bonnah Kamoli ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa kibali sisi Wabunge wote na viongozi wote wa Bunge pamoja na Watumishi wa Bunge kuweza kufikisha Bunge hili la Kumi na Tisa, Mkutano huu wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa viongozi wote wa Bunge, viongozi wa Serikali, viongozi wa taasisi mbalimbali, viongozi wa vyama vya siasa, wanachama wote nchi nzima pamoja na wananchi wote walioungana nasi kipindi cha msiba wa Katibu wetu Mkuu aliyetutoka tarehe 30 Aprili, 2020 Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. Mungu awabariki sana kwa moyo wa upendo na Mungu aendelee kumweka mahali pema Peponi kiongozi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye Wilaya ya Kaliuwa. Hospitali yetu ya Wilaya ambayo kwa asilimia 80 imejengwa kwa fedha za wananchi wa Kaliuwa, kwa maana ya mapato ya ndani kwa asilimia 80, mwaka 2019 tulipata usajili wa muda kwa maelekezo kwamba tukamilishe baadhi ya majengo muhimu kama *theater* majengo ya wazazi ili tupate usajili wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 tulitengewa shilingi bilioni 1.5. Ninashukuru kwamba tumepata shilingi milioni 500 tu, mpaka sasa hivi shilingi bilioni moja hatujapata. Kwa kweli ninaiomba Serikali, kwa jicho la pekee waweze kukamilisha ile shilingi bilioni moja iliyobaki kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha ili hospitali ile ya Kaliuwa iweze kukamilika na kupata usajili wa kudumu, wananchi waache kuhangaika kwenda Hospitali za Kigoma, Urambo, Tabora na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba suala la watumishi wa afya kwa Wilaya ya Kaliuwa, tatizo sugu kubwa sana; mwaka 2018 nililia hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi akaniambia nilete maombi rasmi kwa Sekta ya Afya nikaleta maombi rasmi tuliokuwa na tatizo, lakini

tulipewa watumishi sita tu tangu mwaka 2018 na bado wengine wanahama. Kwa hiyo, bado kilio chetu kiko pale pale. Tunaomba Kaliuwa tuangaliwe kwa jicho la pekee kwa suala la watumishi wa Sekta ya Afya. Tumejenga Zahanati na Vituo vya Afya; Zahanati ina watumishi wawili na Kituo cha Afya kina watumishi watatu. Ni tatizo! Kwa hiyo, naomba suala la watumishi lipewe kipaumbele cha kutosha katika Wilaya ya Kaliuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Walimu wa Sayansi kwa Wilaya ya Kaliuwa ni tatizo. Tumehamasisha watoto wetu, wameanza kupenda kusoma sayansi, lakini pia tunaenda kwenye uchumi wa viwanda. Hatuwezi kwenda kwenye uchumi wa viwanda hatuna Walimu wa Sayansi. Walimu hawa ni wachache; shule inakuwa na Walimu wa Sayansi wawili, anachukuliwa mmoja anahamishiwa shule nyingine. Kwa hiyo, shule nzima inakuwa na Mwalimu wa Sayansi mmoja, ni tatizo. Tunaomba Serikali iangalie namna gani ya kuondoa changamoto kubwa ya Walimu wa Sayansi katika Wilaya yetu ya Kaliuwa na ninadhani pia ni suala la nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 Mheshimiwa Waziri wa Utumishi alitoa waraka kwa Halmashauri zote kuhakikisha kwamba walimu na watumishi wanapandishwa madaraja. Bado kupandisha watumishi madaraja ni tatizo. Wilaya ya Kaliuwa inaweza kuwa na tatizo kubwa zaidi, kwa sababu kuna walimu wamekaa tangu mwaka 2013 mpaka leo hajawahi kupanda daraja hata moja. Mwalimu huyu tunampa moyo gani wa kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018 kuna waliopewa barua za kupandishwa vyeo. Wameenda kusoma, tena wamejisomesha au wamesomesha na Serikali, lakini wamerudi hawajapandishwa cheo chochote; siyo mishahara wala siyo cheo. Bahati mbaya mwaka 2018 wamepewa barua mwaka 2019 wamenyang'anywa zile barua za kupandishwa vyeo. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwalimu kama huyu, mpaka wengine wameamua kuacha kazi kwa sababu hatuwatendei haki. Kwa nini Mtumishi wa Serikali apandishwe cheo kwa barua, halafu uje mnyang'anye ile barua ya kumpandisha cheo, ni Wilaya ya Kaliuwa tu au na wilaya nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifuatilie, ni kwa nini Wilaya ya Kaliuwa walimu hawapandishwi vyeo, hawapandishwi madaraja na kwa nini wale wengine walipewa barua za kupandishwa madaraja halafu wakaja wakanyang'anywa leo wana miaka mitano, wana miaka sita, wana miaka nane hawajapanda madaraja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la shule za Kata. Tunatambua shule za kata kiukweli zimesaida Taifa hili sana, kila mmoja ata-*acknowledge* hicho kitu. Watoto wetu hata wa maeneo ya vijijini wamepata elimu kwa mazingira hayo hayo, lakini angalau wamepata elimu. Tukumbuke waliosaidia shule hizi za kata 2007 ni walimu waliotelewa kwa mpango wa *crash program*; Walimu ambao walitolewa, wakaambiwa njooni mkafundishe watoto hawa. Wengine walikuwa na fani nyingine mbalimbali, wakaambiwa yeyote mwenye kutaka kuja kufundisha, aje akafundishwe kwenye *crash program*, wakafundishwa, wakaja kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, 2007 wamefanya kazi miaka 10, mwaka 2017 wakaondolewa kama wezi, bila chochote. Kwa kweli Serikali hatukutenda haki. Hata kama kulikuwa na makosa, waliambiwa wajiendeleze, wengine walikuwa vyuoni wanasoma, wengine washajiendeleza, wengine walikuwa hawajachukua hatua yoyote; walioko mashuleni wametoka, wameshaondolewa kazini; waliokuwa wanajiendeleza wamefika *degree*, wengine wamefika mwaka wa pili ameondolewa kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Serikali iangalie namna ya kuona juhudi walizofanya kuendeleza Shule za Kata kwa *10 years* wanaondolewa kama vile wameiba,

hawakutendewa haki. Wana familia, wamehudumu katika Taifa hili kwa moyo wao wote, wengine walitaka kuwa wafanyabiashara, wakaamua kuwa walimu. Tuwaangalie kwa namna ya pekee. Ninaiomba Serikali iangalie namna gani kuwatia moyo angalau wamalizie masomo yao waone jinsi ya kuweza kuwarudisha kazini waendeleo kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni la *TARURA*. Napongeza kazi nzuri ya *TARURA* wanayoifanya, lakini barabara zetu zimebomoka sana, sana na fedha wanayopewa *TARURA* haitoshi. Kwa hiyo, bado tatizo ni kubwa. Wilaya ya Kaliuwa peke yake tuna mzunguko wa ndani barabara za udongo, barabara za *TARURA* 1,370.5, tunapata kwa mwaka mzima shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 tulipata shilingi milioni 675, mwaka huu tumepata shilingi milioni 625, inazidi kupungua, lakini mvua ni nyingi na barabara zimekatika. Kwa hiyo, bado wananchi wanashindwa kupitisha mazao yao kwenye barabara mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaomba mara nyingi Bungeni namna gani *TARURA* iongezewe fedha, kiukweli wanafanya kazi bila kupewa fedha. Shida ni kwamba fedha hawapewi, ni kidogo sana na mzunguko wa barabara ni mkubwa. Kwa hiyo, wanashindwa kutekeleza wajibu sawa sawa na ile kazi ambayo wamepewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala lingine. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi Wilaya ya Kaliuwa ya kilometa saba za lami katikati ya mji. Natambua ahadi za Mheshimiwa Rais zinatekelezwa na TAMISEMI. Kaliuwa huu ni mwaka wa tano, Mheshimiwa Rais anaenda kumaliza muda wake, hata robo kilometa hatujawahi kupata. Ninaiomba Serikali iangalie, kilometa saba, hata moja kweli! Hivi Rais anavyokuja wakati mwingine kuja kuomba ridhaa ya wananchi wale, atawaambia hata kilometa moja ameshindwa kuwapa kweli jamani! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie ahadi za Mheshimiwa Rais ambazo wengine wamepata angalau kilometa mbili, kilometa moja; Kaliuwa na wananchi wake nao wana haki ya kupatiwa japo kilometa chache ili angalau anapokuja Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuomba kura kwa wakati mwingine awe na cha kusema kwa wale wananchi ambao aliahidi hadharani na nina imani kabisa kwamba watakuwa wanamhoji maswali mengi kuhusiana na suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda nilioupata Naendelea kuwashukuru wananchi wa Kaliuwa kwa kunitia moyo na kuendelea kuniadini na kuwatumikia. Nami nina imani kwa kipindi hiki tukimaliza na Serikali isaidie kutekeleza ahadi ambazo ilikuwa imeahidi ili angalau tunapokwenda kwenye kampeni tuwe na ya kusema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa, tunapoelekea kwenye uchaguzi hii sauti ya Mheshimiwa Sakaya inabidi watu tukajifunze maana hakuna maji wala kituo mahali. *(Makofi/Kicheko)*

Inaonekana huko kazi ipo, mtihani inaitwa! Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad ajiandae.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu ni mchango wangu wa mwisho kwa Wizara hii ya TAMISEMI, hususan kwa Bunge hili la Kumi na Moja, ninaomba nisajili mchango wangu wa ushawishi wa leo, ushawishi wa kesho mwezi Oktoba na kwa matumizi ya vijana wa karne hii na karne inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi wa Tanzania mpya imefanywa na Mawaziri wengi. Lakini kipekee kabisa Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetimiza ndoto za ujenzi wa taifa jipya kifkra na kimtazamo. Wizara hii imefanikisha ujenzi wa Tanzania katika Sekta ya Elimu, Sekta ya Afya, Sekta ya

Miundombinu na katika maeneo mbalimbali. Wizara hii haikujenga tu Tanzania, haikujenga tu Taifa, bali imejenga na imeimarisha mitazamo chanya ya kifikra na kimantiki ya wazalendo wapya hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuona Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kuwa ni kiongozi wa pili wa Taifa letu hili ambaye amefanikisha na anafanikiwa sasa kuzalisha wazalendo wapya hapa nchini. Na hii inajidhihirisha kwa mitazamo yake ya kielimu kama mwalimu, mitazamo yake ya kifikra kama mwanafalsafa wa Hapa Kazi Tu, na anatendea haki mitazamo yake hii ya Hapa Kazi Tu kwa kuwataka Watanzania wote kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu ni kiongozi mwenye misimamo isiyoyumba katika kufanya maamuzi. Na katika wazalendo ambao ninawaona Mheshimiwa Rais amefanikiwa kuwatengeneza, si mwingine bali ni wengi isipokuwa kipekee nimtaje Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo. Amekuwa mkweli, hodari na mchapakazi mwenye kufika kila eneo, hasubiri Mheshimiwa Rais anapokwenda, yeye anatangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunampongeza sana na kumtakia kila la heri katika wajibu wake. Na tunaamini wananchi wa Kisarawe watamchagua kwa wingi sana na pia hakutakuwa na ushindani katika jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, pamoja na mapambano tunayoendelea nayo ya Ugonjwa huu wa Corona, niombe sasa Ofisi hii ya Rais, TAMISEMI kutoa maelekezo ya makini kabisa kwa watendaji wote wa kata na vitongoji kutoa maelekezo kwa wenyeviti wote wa vijiji na vitongoji pamoja na wenyeviti wa mitaa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 9 ya Katiba yetu ambayo inatambua misingi ya uendeshaji wa nchi yetu kwamba ni misingi ya kijamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwa viongozi wote hawa ofisi ya Rais TAMISEMI sasa itoe maelekezo kwa kuwataka viongozi hawa kufanya kazi kama mchwa ili kuweza kutambua katika maeneo yao wale wageni wanaoingia, wenyeji waliopo, wagonjwa waliopo, lakini pia kutambua wale wahalifu katika maeneo yao. Hii ni misingi ambayo tunaitambua nchi yetu inafuata iliyopo katika Ibara ya 9 ya Katiba yetu, misingi ya ujamaa na kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi na shukrani sana kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa namna ya kipekee kabisa Waziri wa TAMISEMI ametambua kwamba Rufiji ilizaliwa miaka 600 iliyopita, na kwa kutambua hilo amegundua kwamba wafanyakazi wa Halmashauri ya Rufiji wanafanya kazi katika jengo lililojengwa mwaka 1889, akaona ni bora wafanyakazi hawa awafikirie na kukubali kutoa fedha za ujenzi wa jengo jipya la Halmashari ya Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakupongeza sana na tukuombe Mheshimiwa Waziri sasa wataalam wako wanaoandaa michoro na *BOQ* kutuharakishia sana kwa sababu wananchi wa Rufiji wana kiu kubwa ya kupata jengo jipya kutokana na jengo lao hili kudumu zaidi ya miaka 100 iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hiyo, niombe sasa Ofisi ya Rais TAMISEMI kuangalia uwezekano wa ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya ya Rufiji kwa kuwa hospitali iliyopo ilijengwa mwaka 1960 ikihudumia Wilaya za Kilwa na Rufiji pamoja na wilaya ziliopo karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na athari za mafuriko ambayo Rufiji imepata nimuombe Mheshimiwa Waziri Jafo, miaka kadhaa iliyopita niliomba fedha za ununuzi wa boti, mafuriko yametuletea shida kiasi kwamba hatukuwa na boti katika maeneo yetu. Kwa hiyo, kuna fedha Mheshimiwa Waziri alishatoa shilingi milioni 200, kwa bahati mbaya sana fedha hizi zilirudishwa tena TAMISEMI. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja kufunga hapa watangazie wananchi wa Rufiji kwamba sasa ile milioni 200 umeirudisha

Rufiji ili tuweze kununua boti kuwasaidia wananchi wetu ambao watapata maafa ya mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za mafuriko zimekumba baadhi ya vituo vyetu vya afya ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya cha Muhoro. Muhoro kuna watu takribani 25,000 lakini sasa hivi wanakosa huduma za afya kutokana na athari kubwa ya mafuriko ambayo tumeipata. Nikuombe Mheshimiwa Waziri ukiwa unafunga hapa sasa utuambie zile fedha za dharura zilizopo katika Wizara yako muweze kuzitenga kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Muhoro pamoja na ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ngorongo ambao leo hii hawawezi kwenda Kata ya Kipugira kwa ajili ya kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara ya *TARURA*, barabara ya kutoka Utete kwenda Ngarambe. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aangelie uwezekano wa kukarabati barabara hii. Barabara hii iwapo itakarabatiwa basi itawezesha mizigo inayotoka kule Dangote inayokwenda kwenye mradi wa Rufiji kwa kuwa mradi huu ni kipaumbele cha Mheshimiwa Rais namba mbili kabisa baada ya Mradi wa *SGR*, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kutambua kazi kubwa Mheshimiwa Waziri anayofanya, tunatambua leo hii anajenga Daraja la Mbuchi kule Muhoro. Lakini anapojenga Daraja la Mbuchi pale Muhoro mafuriko yamekomba Daraja la Muhoro kwa hiyo nimuombe kwa fedha zile anazoanza kule Mbuchi aanze sasa kujenga Daraja la Muhoro ili wananchi waweze kupita Muhoro waweze kwenda Mbuchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunatambua kiasi cha fedha nyingi ambacho Wizara yake imetoa katika eneo la elimu, eneo la afya, zaidi ya shilingi bilioni tano imeingia katika eneo la elimu na eneo la afya. Kwa Mtanzania asiyetambua mchango huu atakuwa na matatizo kichwani mwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Pascal Haonga ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwanza kukushuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika nchi yetu ya Tanzania katika hiki kipindi cha miaka minne ambacho tunaendelea sasa kumaliza na kuwa kipindi cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda tu kupongeza kwamba tulikuwa tuna mambo mengi ambayo tuliomba au tuliyaweka kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi 2015-2020 na mambo hayo tukiangalia mpaka sasa asilimia 90 au asilimia 88 yote yameshatekelezwa. Kwa uchache tu ninapenda kutaja barabara ambazo zimejengwa, barabara ambazo ni kubwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam; tuna *flyover* ambayo iko pale *TAZARA* imejengwa kipindi cha Awamu ya Tano, lakini pia tuna barabara ya Ubungo ambayo ni *interchange* imejengwa kipindi cha Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuna barabara sita ambazo zinatoka Dar es Salaam mpaka Pwani ambazo zimejengwa kipindi cha Awamu ya Tano. Lakini pia tuna barabara nyingine ambayo inajengwa Nakanazi pamoja na Kasulu ambazo zinajengwa kwa bilioni 260; zimejengwa Awamu ya Tano. Tuna Daraja la Busisi ambalo linajengwa kwa miezi 48, Mheshimiwa Rais ameshalizindua kwa hiyo tuna vitu vingi ambavyo tunaweza kujivunia katika Serikali ya Awamu ya Tano au Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ambayo imeweza kuvitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, pamoja na Manaibu wake wote kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika Nchi ya Tanzania, hususani kwenye Jimbo langu la Segerea ambapo kwa sasa

tuna barabara nyingi za lami ambazo zimejengwa katika kata mbili zilikuwa chini ya Mradi wa *DMDP* lakini najua ziko chini ya TAMISEMI, barabara za kilometa 16 na masoko sita lakini pia na bustani mbalimbali ambazo wameweza kubadilisha mazingira ya hizi kata mbili. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa kwa kazi kubwa aliyofanya kwa kuleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nampongeza kwa kusimamia na kuangalia suala zima la elimu bure ambapo mpaka sasa hivi tumekuwa na ongezeko kubwa la watoto shuleni, ni kwa sababu wamekuja kwa sababu ya elimu bure. Kwa hiyo, nipende kutumia nafasi hii kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jafo kwa mambo makubwa ambayo anayafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka kuliongelea ni kuhusiana na barabara zetu za ndani. Pamoja na pongezi hizo lakini bado tunamuomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jafo, aweze kufanya kazi kubwa kwa kuangalia barabara za Mkoa wa Dar es Salaam lakini pia na mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kama barabara za Mkoa wa Dar es Salaam katika Jimbo la Segerea, Jimbo la Ukonga na Jimbo la Ilala, barabara sasa hivi zina hali mbaya sana, na zina hali mbaya sana kwa sababu ya mvua. Mvua imekuwa kubwa na mvua imeharibu miundombinu na imeharibu miundombinu ni kwa sababu kuna mifereji na barabara nyingi ambazo hazijaweza kutengenezwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninataka nimuombe Mheshimiwa Jafo; *TARURA* haiwezi kubadilisha mazingira yaliyopo sasa hivi kwa bajeti ambayo tumekuwa tukipanga. Kwa kweli barabara ni mbovu sana na ninajua *TARURA* wanataka kufanya kazi lakini bajeti yao ni ndogo.

Katika Jimbo la Segerea tuna mafuriko makubwa, mafuriko yamechukua sehemu kubwa. Kama unavyojua



Mheshimiwa Jafo kwenye jimbo letu ndiyo umepita Mto Msimbazi, kwa hiyo, katika ule mto umepita sasa hivi unaingia, sio kwamba wananchi wameufuata Mto Msimbazi, sasa hivi maji ndiyo yanawafuata watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Vingunguti kuna makaburi ambayo sasa hivi yanaondoka na maji. Unakuta makaburi mengi sana, makaburi kama 200 ya Kata ya Vingunguti yameondoka na maji na hayo makaburi zamani yalipokuwa yamepangiwa hayakupangiwa kwenye mto lakini kutokana na uchakavu wa miundombinu, kutokana na uchakavu wa mifereji hayo maji yameacha njia yake na yameshaenda sasa kwenye nyumba za watu na hatimaye kusababisha hayo makaburi kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuna mradi mkakati ambao mmeujenga Kata ya Vingunguti, machinjio ya kisasa. Mheshimiwa Jafo machinjio ya kisasa tunakupongeza sana, ni machinjio mazuri ambayo yatawasaidia wafanyabiashara wadogowadogo hata kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri barabara ya kukufikisha kwenye hayo machinjio ni barabara mbovu sana, imeharibika kutokana na miundombinu ya mvua na kutokukarabatiwa kwa muda mrefu. Kwa hiyo ninakuomba sana katika bajeti yako hii ya 2020/2021, naomba utuangalie katika hizo barabara ambazo tumezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinelele ninachotaka kuongelea ni kuhusiana na Ugonjwa wa Corona. Nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy, pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wanaifanya. Nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa, Paul Makonda, pamoja na Mkuu wangu wa Wilaya, Dkt. Sophia Mjema, ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa kwa ajili ya uhamasishaji wa watu jinsi gani ya kujikinga na huu ugonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze Wizara kwa kazi kubwa ambayo imefanya kwa ajili ya kutoa utaratibu kwanza wa utoaji taarifa kwamba ni Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio watakaohusika kutoa taarifa nani ana Corona na wagonjwa wangapi wapo. Hiyo inatusaidia sisi kutokupata taarifa ambazo sio makini au sio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa ushauri kutokana na huo Ugonjwa wa Corona. Kuna wananchi wetu wengi ambao walikuwa wanafanya biashara mfano kama hizi biashara za mamantilie au biashara za kupika, biashara nyingi tu ambazo zimeathiriwa na Ugonjwa wa Corona. Sasa wananchi wengi wamechukua mikopo benki kwa sasa hivi kwa kuwa biashara hakuna na hawa wananchi wako nyumbani.

Ninaomba kupitia Wizara ya Fedha kuongea na Benki Kuu ili waangalie hizi benki ndogondogo kama wanaweza kuwasaidia hawa wananchi ambao walikuwa wanalipa labda kwa mwaka mmoja, waweze kuongezewa mwaka mmoja mbele. Kwa sababu sasa hivi kama watawaacha waendeleo hivi ina maana wananchi wengi wanaweza wakauziwa vitu vyao. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara ya Fedha ifanye kitu kama hicho ili kuweza kuona kwamba hawa wananchi wetu tunawakinga na janga hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wetu, kwa sababu kila kata kuna bwana afya, sasa hawa mabwana afya kwa wakati huu tunamuona tu Mheshimiwa Makonda anatoa taarifa au anahamasisha pamoja na yeye kuhamasisha lakini bado tuna watendaji wa afya ambao tayari wana utaalim wa afya ambao wanaweza kwenda mitaani waweze kuwaelekeza watu jinsi ya kujikinga na Ugonjwa wa Corona. Kwa hiyo, ninaomba hawa watendaji wa afya kwa kipindi hiki waweze kutembea na kuweza kuwaambia watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine...

*(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Bonnah, ahsante sana.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia ajandae.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenijalia afya na uzima na hatimaye nimeweza kusimama ndani ya ukumbi huu kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na anaendelea kuifanya katika kuwatumikia Watanzania. Niwapongeze pia wasaidizi wake wa karibu; Makamu wa Rais mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, wamekuwa karibu sana na Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba masuala yote ambayo wanakuwa wamekusudia kuyafanya yanafanyika kikamilifu na yanaonekana mbele za Watanzania, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, Manaibu wako na watendaji wote wa TAMISEMI, hakika mmeitendea haki Wizara hii; hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kushukuru kwa yale makubwa ambayo yamefanyika ndani ya Mkoa wa Shinyanga. Ninaanza kwa kushukuru kwa sababu kuna mambo ambayo niliyasema sana ndani ya Bunge hili, lakini kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali sikivu inayoongozwa na Jemedari, Dkt. John Pombe Magufuli, wamekwenda kuyafanya kikamilifu na wananchi wa Shinyanga wanayaona, naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali na kumshukuru sana Rais wetu kipenzi, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga unaendelea na uko katika hatua nzuri; ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga umekwishakamilika, hospitali ambayo nimeipigia kelele toka nimeingia mwaka 2010 ndani ya ukumbi huu, sasa hivi imekwishakamilika. Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu umekwishakamilika, ujenzi wa mabweni katika shule zetu za sekondani, nizitaje baadhi ya shule hizo; Shule ya Sekondari Saba Sabini, Ulowa, Kinamapula, Nyashimbi, Bukamba, Busoka Sekondari. Hiyo yote ni kazi ya Serikali ya Awamu ya Tano ndani ya kipindi cha miaka minne; hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa vituo vya afya sita katika Mkoa wa Shinyanga. Vituo hivyo vimekamilika na vinafanya kazi na wananchi wetu wanapata huduma kwa ukaribu zaidi, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie katika sekta ya elimu, nilikuwa najaribu kusikiliza hotuba ya Kambi ya Upinzani; wanasema miundombinu haitoshi hawajaona chochote, miundombinu haitoshi; lakini niwapitishe tu kwa harakahara. Kwenye suala la miundombinu katika shule za msingi Mheshimiwa Waziri Jafo hapa amesema vyumba vya madarasa 19,808 vimejengwa ndani ya miaka mine; vyumba vya maabara 227 vimejengwa ndani ya miaka mine; vifaa vya maabara shule 1,258 vimesambazwa katika shule zetu; matundu ya vyoo 7,922 yamejengwa katika shule zetu; na

ukarabari wa shule kongwe 73 umefanyika kwa kiasi kikubwa kwa kiwango cha juu katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda tu Mkoa wa Shinyanga vyumba vya madarasa 276 vimejengwa; matundu ya vyoo 155; nyumba za Walimu 23; maabara 10; na mabweni 16. Kwa nini nisiseme hongera Daktari John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo umeifanya ya kuwatumikia Watanzania na kutekeleza ahadi ambazo umekuwa ukizitoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Azza kuna Taarifa.

**MHE. FRANK G, MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa Taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Azza kwamba, kwa mujibu wa taarifa ya tafiti ya Haki Elimu baada ya tangazo la elimu bure ongezeko la watoto kujiandikisha ni 17%, lakini ongezeko la miundombinu katika nchi hii ni 1% peke yake.

Kwa hiyo, ni kweli anazungumza kwamba, yamefanyika na Mheshimiwa Waziri ameonesha kwenye bajeti, lakini ukweli ni kwamba, bado tuna upungufu mkubwa na ndio maana bado hawakuweka mahitaji na upungufu uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri Mbunge ajue kabisa kwamba, bado tuna upungufu mkubwa na tumshauri tu Mheshimiwa Jafo aendelee kuhakikisha kwamba, wanaongeza vyumba kwa kasi na wapange fedha nyingi kwa ajili ya kuongeza vyumba vya madarasa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu ushauri kwenye hiyo taarifa utatoa wakati wako wa kuchangia, lakini pale ulipoishia kwenye Taarifa, ndio nitakapomuuliza Mheshimiwa Azza kama anaikubali hiyo Taarifa au anaikataa?

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa yake siipokei na wala siikubali. Namwambia kwamba, maendeleo ni hatua kwa hatua, huwezi ukafanya mambo yako yote ukayakamilisha kwa wakati mmoja. Hata sisi humu ndani leo hii ukipewa pesa begi zima hutamaliza yale yote ambayo umeyakusudia katika nafsi yako. Kwa hiyo, Serikali inafanya awamu kwa awamu, infanya hatua kwa hatua, hongera Daktari John Joseph Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ambayo ameisoma Mheshimiwa Jafo leo nimeangalia na nimeskiliza kwa makini kwa mwaka huu wa fedha Mkoa wetu wa Shinyanga tumetengewa shilingi milioni 840 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa. Taarifa hiyo iko ukurasa wa 339, kwa nini nisiseme maendeleo ni hatua kwa hatua? Hatua moja huanzisha hatua nyingine. Hongereni sana. Ukamilishaji wa maabara. Mkoa wa Shinyanga peke yake tumetengewa shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara 44 ndani ya Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi upande wa afya katika kazi ambazo zimefanyika ndani ya miaka hii minne. Ujenzi na ukarabati wa hospitali za Halmashauri zetu umefanyika kwa Halmashauri 98. Vituo vya afya 433, zahanati 368 ambazo zimejengwa na kufanyiwa ukarabati, lakini kwa Mkoa wa Shinyanga pekee vituo vya afya sita vimejengwa vyenye thamani ya shilingi bilioni 7.4, tunashukuru sana wananchi wa Shinyanga kwa kazi kubwa ambayo imefanywa. Hospitali za Halmashauri katika Mkoa wetu zimejengwa hospitali tatu ambazo ni Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Hospitali ya Wilaya ya Ushetu na Hospitali ya Halmashauri ya Msalala ambayo bado haijakamilika na mwaka huu nimeona imetengewa tena bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa afya ukamilishaji wa zahanati nimeona Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa katika bajeti ya mwaka huu kila Halmashauri itapata zahanati tatu. Kwa Mkoa wa Shinyanga peke yake tuna bilioni 3.9 kwa ajili ya zahanati, sina sababu ya kukaa hapa kuanza kutaja kwamba, naomba zahanati

fulani, naomba zahanati fulani, naamini hizi bilioni 3.9 zitakwenda kukamilisha zile zahanati zetu ambazo zimeanzishwa na wananchi na wananchi sasa kwenda kupata huduma ambayo inastahili, tunawashukuru sana; lakini pia nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala tumetengewa bilioni moja kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali ya Halmashauri ya Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika bajeti ya mwaka huu katika ujenzi wa nyumba za watumishi na majengo ya utawala. Nitumie fursa hii tena kusema kwa Mkoa wa Shinyanga tuna bilioni 2.5 ambazo zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala na majengo haya yanakwenda kujengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Naishukuru Serikali kwa kuona kwamba, watumishi wetu wanatakiwa sasa kuwa na sehemu nzuri ya kufanyia kazi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Shinyanga na Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kwani kwa muda wote wameniamini na kuweza kufanya nao kazi ndani ya miaka minne.

Nawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa, lakini pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ambayo ndio Halmashauri Mama ninayoishi kwa kuweza kunilea na kunifikisha hapa nilipofika. Niko pamoja na ninyi na nitaendelea kuwa pamoja na ninyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona unanitazama kengele imegonga, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Dkt. Saada Salum Mkuya ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hii bajeti ya Wizara ya TAMISEMI. Awali ya yote naomba kwanza kuwashukuru viongozi wangu wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo ngazi ya Taifa, kwa kuendelea kuwa imara licha ya changamoto mbalimbali ambazo wameendelea kupitia na wafahamu kwamba, siku zote ili dhahabu ing'ae lazima ipite kwenye moto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja ambazo nimezipanga kuzitungumza siku ya leo na hoja ya kwanza naomba nianze kwenye eneo lile la *TARURA*:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* ni chombo ambacho kiliundwa, lakini chombo hiki kimekuwa sasa ni kama pambo tu kwa sababu, chombo hiki hakipewi fedha. Nchi hii ina vijiji zaidi ya elfu 12, leo *TARURA* inayosimamia barabara zote za vijiji zaidi ya elfu 12, barabara zote za mijini, eti inapewa fedha 30% tu, lakini fedha hizo nazo wakati mwingine haziendi kama ambavyo tumezidhinisha kwenye Bunge hili. Kwa hiyo, nashauri kwamba kwenye *TARURA* hapa yafanyike mabadiliko kidogo kwenye sheria, angalau iwe asilimia 50 kwa 50 ili mwisho wa siku *TARURA* iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha *TARURA* bila kuwapa fedha maana yake hamna kitu ambacho tumekifanya. Watu wanalipwa mishahara pale *TARURA*, lakini fedha haziendi kama ambavyo zimeidhinishwa na Bunge. Kwa hiyo, nishauri tu kwamba, licha ya fedha kidogo hizo ambazo hazipeleki kwanza ziwe zinapelekiwa, lakini zaidi ili kuweza kwenda vizuri ni jambo jema kama tutaenda kubadilisha sheria ili iwe asilimia 50 kwa 50 ili mwisho wa siku *TARURA* iweze kuwa na fungu la kutosha, vijiji zaidi ya elfu 12 ni vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, hii mvua iliyonyesha kuanzia mwaka jana na inaendelea, katika



maeneo mengi nchini karibu barabara nyingi za vijijini na za mijini zimekatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu kuna barabara ya kutoka pale Kijiji cha Ivwanga kwenda *Mbozi Mission, Mbozi Mission* kule kuna hospitali kubwa ya *mission*, lakini pia kuna Chuo cha *Nursing* pale cha Serikali, lakini kuna soko kubwa, lakini barabara hiyo pia inaenda hadi Jimbo la Mheshimiwa Hasunga, Kijiji cha Iganduka. Sasa barabara hii ina hali mbaya sana kuliko Waziri anavyofikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara nyingine ya kutoka Mloo kwenda Isansa Kituo cha Afya, imekatika, ina hali mbaya kwelikweli, lakini yote haya ni kwa sababu hizi barabara zinasimamiwa na *TARURA* na *TARURA* inapewa pesa kidogo, kwa hiyo, mambo yamekuwa ni mabaya kweli na yamekuwa ni magumu. Madaraja mengi yameharibika kwa hiyo, nashauri sheria hapo iweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine nadhani pamoja na mapambano ambayo yanaendelea kuhusu ugonjwa wa *corona* nashauri kwamba, pia Serikali ingeangalia kutenga fedha kama dharura kwa ajili ya kuweza kurudisha hali ya miundombinu ya barabara ambayo imeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nizungumze suala la kuhusu vituo vya afya. Ukurasa ule wa 54 limezungumzwa suala la vituo vya afya na tumeambiwa kwamba, vituo vya afya vimefikia sasa 968; unapozungumza kutoka mwaka 1961 tangu nchi hii ipate uhuru unazungumza vituo vya afya 968 na kata ambazo tunazo kwenye nchi hii ni zaidi ya kata elfu nne na kitu, maana yake tuna upungufu; ukienda kwenye Sera ya Afya, tuna upungufu wa vituo vya afya zaidi ya elfu tatu na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Afya inasema kituo kimoja cha afya kwenye kila kata, leo unazungumza vituo 968. Yaani leo tukisema tuongeze miaka mingine ya Serikali hii ya CCM kukaa madarakani miaka mingine 59 kwa *speed*

hii ambayo inaenda, maana yake unazungumza kutakuwa na vituo elfu moja mia nane na kitu vya afya, kama ndio watakuwa wanaenda hivi, ambapo maana yake miaka 59 ni mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vituo vya afya ni vichache kweli, wakati mwingine watu wanakaa wanampongeza Mheshimiwa Jafo tunakupongeza unafanya nini, wakati mwingine mnamharibia Mheshimiwa Jafo kwa sababu mnatakiwa mmwambie kwamba, kosa liko hapa, ili Mheshimiwa Jafo aweze kusonga mbele. Leo vituo 968 ni vichache mno, yaani tuwaongeze miaka mingine 59 au 60 ndio muwe na 1800, bado hamuwezi kukamilisha vituo vyote kwenye kata zote zaidi ya elfu nne na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huu ni mwendo wa kinyonga, siwezi nikaendelea kumdanganya rafiki yangu Mheshimiwa Jafo, kaka yangu kwamba, anafanya kazi nzuri wakati naona *speed* ni ndogo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, ni vizuri Sera ya Afya iweze kutekelezwa, kituo kimoja cha afya kwenye kila kata ili mwisho wa siku nchi hii tuweze kuwa na vituo vya afya kwenye kila kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni jambo ambalo linashangaza sana. Mimi kwangu pale nina kata moja inaitwa Mlowo. Hii kata ina wakazi karibu laki moja, kuna zahanati ya kijiji kwenye kata hiyo; zahanati ya kijiji tu, wakazi zaidi ya laki moja.

Sasa kwa mazingira kama haya unaweza ukawa ni Mbunge mwendawazimu pekee ambaye unaweza ukaanza kupongeza mambo kama haya, wakati watu zaidi ya laki moja hawana kituo cha afya wana zahanati; kwa hiyo, nishauri jambo, Sera ya Afya itekelezwe, kituo cha afya kwenye kila kata, hapo nadhani tutakuwa tumetatua tatizo la vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa ule wa 141 wa hotuba ya Waziri amezungumza kuhusu kwamba, mwaka huu wa fedha 2020/2021 TAMISEMI imepanga kusimamia shughuli

za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na kadhalika. Kwenye nchi hii kumetokea tatizo kubwa sana, leo wale Mameya au Wenyeviti wa Halmashauri waliochaguliwa kidemokrasia kabisa hasa kupitia Vyama vya Upinzani wanaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Meya mmoja wa Iringa pale anaitwa Alex Kimbe ameondolewa kinyume kabisa na utaratibu. Sheria inasema ili kumwondoa huyu Meya inatakiwa angalao 2/3 ya kura iweze kupigwa; Manispaa ya Iringa yenye Madiwani wote kama 24 ilitakiwa wafikie angalau Madiwani 17 kumwondoa Meya wa Iringa. Wameingia madiwani wa CCM 14, walihitajika Madiwani angalao wafike 17 ndio waweze kumuondoa Meya, leo Madiwani 14 wamevunja sheria, wamemwondoa meya kisa anatoka CHADEMA, hilo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini tu kwamba, yote haya, huu mpango wa Serikali kwamba, wanataka kusimamia shughuli za utawala bora, hilo jambo haliwezekani. Nimwambie jambo Mheshimiwa Jafo rafiki yangu kwamba, ameshawahi kuongea Desmond Tutu, ameshawahi kusema naomba nimnukuu: *“if you are neutral in situation of injustice you have chosen the side of the oppressor.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kinachofanyika kwenye nchi hii hawa watu wanaondoolewa kinyume na utaratibu kwa kweli, huku ni kunyanyaswa na huo ni uonevu na Mheshimiwa Jafo kama amenyamazia uonevu huu, maana yake na yeye anaungana na Wakuu wa Mikoa wote wanaosababisha uonevu uendeleo kwenye nchi hii. Ninapozungumza hapa Meya wa Dar es Salaam, Isaya Mwita, aliondolewa kinyume na utaratibu. Kabisa wanaingia kupiga kura hawana 2/3 wamemwondoa kinyume kabisa, kihuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwambieni ukweli kabisa mambo haya yanaumiza na Mheshimiwa Jafo kunyamazia mambo haya maana yake naye anaungana na yule ambaye anaenda kufanya matendo ya uovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme tu kwamba, haya mambo yanaumiza sana. Nchi hii hata siku moja haitakaa kikae Chama cha Mapinduzi peke yake, lazima vyama vya upinzani viwepo na vitaendelea kuwepo tu. Sasa mazingira kama haya ni mazingira ambayo yanatia hofu sana na utawala bora kwenye nchi hii umeingia katika majaribu makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine pia, hapa ambalo naomba nizingumze kidogo kuhusu suala la ahadi ya milioni 50 kwenye kila kijiji. Nawakumbusha tuambieni kijiji gani ambacho milioni 50 imepelekwa? Kwa sababu, hapa tumeona watu wanajigamba, wametekeleza, vituo vya afya, sijui vitu gani, lakini milioni 50 iliyokuwa imeahidiwa kwenye kila kijiji wamepeleka shilingi ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu nina vijiji karibu 121 na nahitaji bilioni sita karibu na milioni 50, maana katika vijiji 121 vya Halmashauri ya Mbozi hawajapeleka kwenye kijiji hata kimoja. Watekeleze ahadi hiyo na ahadi ya *laptop* kwa kila Mwalimu; wamepeleka *laptop* ngapi kwa Walimu wa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagongwa Mheshimiwa, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum na Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia katika bajeti hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Napenda kwanza kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi

kubwa sana aliyoifanya katika kipindi cha miaka mitano. Sina wasiwasi kabisa miaka mitano mingine ijayo tutaona mapinduzi makubwa sana ya kimaendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze kuchangia katika sekta ya afya na kabla sijaanza kuchangia sekta ya afya nimpongeze Makamu wa Rais, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Manaibu wake Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Mwita pamoja na Katibu Mkuu na Manaibu wake kwa kazi kubwa sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa upande wa sekta ya afya ndani ya kipindi cha miaka mine, tayari Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano imeanza kujenga na kukarabati hospitali za halmashauri 98, kati ya hizo 77 zimekamilika. Zitakapokamilika zote mwezi Juni, 2020 tutakuwa na hospitali za Halmashauri za Wilaya 175, ndio kusema tutabakiwa na Halmashauri tisa tu kujenga hospitali za wilaya ambazo nina uhakika kwa *speed* ambayo tunayo ndani ya mwaka mmoja wa mwaka 2020/2021 tutakuwa tumemaliza kabisa zoezi la kujenga hospitali za wilaya na hivyo kuifanya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhamia kwenye ujenzi wa vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu ambaye anasema tangu tumepata Uhuru mpaka sasa hivi tumejenga vituo vya afya 900. Tanzania tuna kata 3,956 mpaka sasa hivi tumeshajenga vituo vya afya zaidi ya 900, ndiyo kusema kwamba tunahitaji chini ya miaka 10 kukamilisha ujenzi huu. Kwa sababu kama tumeweza kujenga vituo vya afya 433 ndani ya kipindi cha miaka 5, tunahitaji chini ya miaka 10 kukamilisha vituo vya afya 3,956. Kwa hiyo, yule aliyekuwa anasema tutahitaji zaidi ya miaka 20, hebu arudi kwa mwalimu wake wa hesabu na akazipitie tena zile hesabu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

## T A A R I F A

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia, kuna taarifa, Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa, nimkumbushe tu kwamba tunamshukuru Jafo angalau kajitahidi, yeye alikuwa Waziri wa Wizara hii na alikuwa ni mwanachama wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, labda kama anatuambia anaomba msamaha kwa kwenda taratibu, hakufikia malengo. Nakupongeza Mheshimiwa Jafo kwa kufanya kazi nzuri. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunapotaka kutoa taarifa tutumie zile Kanuni zetu vizuri. Hii siyo taarifa, Mheshimiwa Hawa Ghasia, endelea na mchango wako.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, anajifurahisha kwa sababu nimesema tumeongeza kutoka vituo vya afya 535 kwenda 968. Ndiyo kusema kuna kazi iliyofanyika siku za nyuma na tunaendeleza. Ndiyo maana nikasema tukikamilisha Hospitali za Halmashauri 98 tutakuwa na Hospitali za Halmashauri 175. Maana yake kuna kazi imefanyika siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokisema *speed* imeongezeka na ndiyo maana nikasema kwa *speed* ambayo Mheshimiwa Jafo anayo, kwa *speed* ambayo Mheshimiwa Magufuli anayo...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** ... tunahitaji chini ya miaka 10 kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya katika nchi yetu. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, ungempa muda azungumze maana umeingia sasa hivi, umeshamsikia na mchango na taarifa unayo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. Hadi nimesimama maana yake nimemsikia kuna kitu nataka nimpe taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia, endelea na mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wataelewa tu, naona wanaelewa kidogo kidogo na wanachangamka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiacha hospitali za wilaya, Serikali ya Awamu ya Tano iko katika mchakato mpaka kufikia Juni, 2020 itakuwa kwa zaidi ya asilimia 60 imekamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini. Hata anayezungumza anafahamu kwamba katika Mkoa wake wa Mara kuna Hospitali ya Rufaa inajengwa na Chato pia inajengwa na zikikamilika hizo ndiyo kusema kwa maana ya Kanda tutakuwa tumekamilisha ujenzi wa Hospitali za Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokea kule juu kwenye rufaa tunakuja kwenye hospitali za halmashauri, hospitali za mkoa, katika sekta ya afya, Mheshimiwa Magufuli akiingia awamu ya pili ana-*deal* na vituo vya afya na zahanati tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale ambao wanasema kwamba hakuna kilichofanyika, hebu warudi waangalie tulikotoka, tulipo na tunakokwenda. Watakubaliana na mimi kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza Ilani yake kwa *speed* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Jafo kwa kusimamia vizuri elimu bila ada. Kama ambavyo tumesema, hili ni wazo la Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli la kuhakikisha kwamba watoto wote wa maskini wanakwenda shule na kuondoa ada katika shule zetu. Jambo hili limeongeza watoto wanaoandikishwa darasa la kwanza na hata wanaokwenda sekondari na imesaidia sana wazazi kujikita katika kuwapatia wanafunzi mahitaji mengine ambayo zamani ilikuwa wachangie ada na pia watafute na sare na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongeza ujenzi wa vyumba za madarasa na ujenzi wa mabweni. Mimi ninayezungumza katika halmashauri yangu tunayo mabweni mawili ambayo yanaendelea kujengwa, tumepata pesa za kukamilisha maboma katika halmashauri yangu na miundombinu katika elimu ya sekondari na msingi imeboreshwa kwa kiasi kikubwa. Nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Blasius Byakanwa kwa ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Serikali Kuu ilipojikita katika kukamilisha vyumba vya madarasa, kujenga nyumba za walimu yeye akaja na wazo la shule ni choo na akahamasisha wananchi, viongozi mbalimbali katika mkoa wetu na sasa hivi tunafanya vizuri sana katika kuhakikisha kwamba tunasaidiana na Serikali Kuu. Si kila kitu kuiachia Serikali, tunakuja tunasimama hapa tunasema kitu fulani hakijakamilika, sisi kama sisi na wananchi wetu tumefanya nini?

Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa kuja na wazo la shule ni choo pamoja na mengine yale ambayo yako katika mchakato mzuri sana, nina imani kabisa tutamsaidia katika kupitisha sheria ili gongo sasa ikawe *sanitizer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuanzisha Mamlaka ya



Wakala wa Barabara Vijijini (*TARURA*). *TARURA* imefanya kazi nyingi sana na kubwa sana. Nachoiomba Serikali ni kuiongezea vyanzo vya mapato. Pesa wanayopewa *TARURA* na kazi waliyonayo ni tofauti. Tunaomba tuwaongeze na tuwatafutie vyanzo vya uhakika vya mapato ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Jafo pamoja na Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimentaja Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma ajiandae.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, natoa shukrani zangu sana kwa Mwenyezi Mungu kuweza kutupa neema yake ya uhai tukasimama leo hapa katika kazi zetu. Pili, nitoe pongezi nyingi sana kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na jitihada zake. Anafanya kazi kubwa sana katika kusukuma gurudumu la maendeleo la Tanzania ikiwa ni pamoja na wasaidizi wake. Sijapata nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu lakini nitumie fursa hii kumpongeza sana kwa usaidizi wake kwa Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wakiwemo Mawaziri wa Ofisi yake ya Waziri Mkuu na Naibu Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Jafo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati na nadhani katika Kamati ambayo imepata bahati kubwa ni Kamati yetu kutokana na kufanya kazi na Mheshimiwa Jafo pamoja na Naibu wake. Tunapata ushirikiano mkubwa sana katika Kamati yetu na kila hoja ambayo Kamati imekuwa iki-

*raise* Mheshimiwa Jafo na wasaizidi wake walikuwa wanaifanyia kazi vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati yetu sisi tuna bahati nyingine kwamba Wabunge wengi na tofauti walikuwa wakihudhuria wakati tunapitia mafungu ya mkoa. Tulichokuwa tukikiona ni kwamba Wabunge wengi wakija pale wanakuwa pamoja na Wakuu wa Mkoa yaani ile *agenda* inakuwa ni moja kwamba sisi sasa tunakuwa hatuna namna. Mara nyingine hata wale Wabunge wao wanatoa *clarity* katika hoja mbalimbali ambazo sisi Kamati tunakuwa tumezi-*raise*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelisema hili ili tuone kwamba inapotokea hoja mtu inamuuma, inam-*burn* wakati yeye ni mmoja wa Wabunge katika Bunge letu na alikuwa kama linamuuma kweli kulikuwa kuna ratiba imetolewa *publicly* kila mtu anajua kwamba wengi walikuwa wanakuja na kuona kama kutakuwa kuna hoja basi hoja ile inazungumzwa pale na inatolewa maelezo na kama kulikuwa kuna *issue* ya kuchukuliwa, Mheshimiwa Jafo na wasaidizi wake hata pamoja na Wakurugenzi walikuwa wanachukua. Kwa hivyo, hizi hoja ambazo ziko *petty*, nadhani hazina msingi, tusichukue *resource* ya muda sana kwa ajili ya ...

## TAARIFA

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saada kuna taarifa, Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa anayezungumza. Hiki anachokizungumza tayari umeshakitolea maamuzi lakini pia ambacho nataka kukizungumza ni kwamba si kila Mbunge analazimika kwenda kwenye Kamati na Mbunge ambaye hajaenda kwenye Kamati pia ana mamlaka ya kuzungumza ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kitendo cha kusema kwamba angekuja kwenye Kamati ili aweze kupata ufafanuzi wakati ana nafasi kubwa ya kutoa hoja ndani ya Bunge anakuwa anamkosea Mheshimiwa Mbunge ambaye ametoa hoja za namna hiyo.

Kwa hiyo, nafikiri aendelee kuchangia tu mchango wake lakini asiseme tu kwamba angekuja kwenye Kamati, hiyo siyo hoja kabisa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, jambo ulilolizungumza si kati ya taarifa mtu anazoweza kupewa. Unatumia Kanuni tofauti kama kuna jambo alilolisema ambalo hukubaliani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane ili tujue namna ya kwenda vizuri. Hapa haizungumziwi hoja ya Mbunge mmoja, Wabunge waliochangia ni wengi na wameonesha kwamba kwenye maeneo yao wana hoja ambazo wangependa zisikilizwe.

Mheshimiwa Saada anachofanya ni kuwakumbusha wajibu wetu. Kama una jambo ambalo ungetaka liingie huko kwa Mheshimiwa Jafo sasa hivi ulitakiwa kuwa umeshafanya huko. Hapa tunajadili sawa lakini hapa ni kwa ujumla lakini kila Mbunge ambaye ana hoja mahsus alishaenda huko, ndiyo utaratibu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitunzie muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya na kuna msemo wa Kiingereza unasema: "*Life is not about duration, it is about donation*". Hii inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba mtu kadri unavyoishi, unaweza ukaishi miaka 5, 100, hakuna kitu ambacho wewe utakumbukwa nacho kama hujaleta

mabadiliko chanya katika jamii ambayo wewe unaishi.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, Mheshimiwa Rais ameongoza katika kipindi cha miaka minne lakini *donation* yake katika maendeleo ya nchi hii ni kubwa mno. Nataka nilizungumze hili kwa sababu hata kule Zanzibar sasa hivi tuna Magufuli *effect* kwamba hata utendaji wa kazi umebadilika. Kwa hiyo, *life is not about duration*, tunaweza tukakaa Bungeni miaka mitano lakini kama hujaleta mabadiliko yoyote hata katika Bunge yaani umekuwepo wewe tu kama Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona *impact* kubwa katika kipindi cha miaka minne katika maeneo mengi; huduma za jamii, afya, elimu, maji na hata kwenye *financial infrastructures*. Kwenye hili nampongeza sana Mheshimiwa Jafo kwa ubunifu ule wa kuwapa Wakurugenzi wetu mamlaka ya kununua *Point of Sales (POS)* umeleta *impact* kubwa kwamba hata wao sasa hivi wanajua wajibu wao katika masuala haya ya *financial resources*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili nataka nimsisitize Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba sasa hata Wakuu wetu wa Mikoa wanakuwa na ubunifu mkubwa zaidi wa vyanzo vya mapato. Maana masuala ya kusema kwamba fedha hazijapelekwa kutoka Hazina au zimechelewa isiwe ndiyo kikwazo cha kutotekeleza wajibu wao katika mikoa. Kwa sababu wao ndiyo wasimamizi wa mikoa lakini wajue wao ndiyo wasimamizi wa uchumi na maeneo ya mikoa husika, hata kama *performance* ya mkoa itakuwa ndogo, wanaowajibika ni wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile kusema fedha hazijaletwa, kwa sababu hata fedha kukusanywa kwake kunategemea sana msingi wa nchi, eneo au tunasema *regional intergration* na hata uchumi mkubwa wa dunia. Kwa hiyo, ukiwa na *excuse* kwamba fedha hazijapelekwa *it's simply* kwa sababu kunakuwa na *effect* tu ya dunia au *region* imetokea ambayo nchi tunakuwa hatuna *control* nayo.

Nataka kusisitiza kwamba Wakuu wetu wa Mikoa wawe wabunifu na hili nali-*echo* jambo ambalo tumelizungumza katika Kamati, wawe wabunifu wa kuleta maendeleo ya uchumi katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kulisema, katika mipango yetu ya maendeleo kuna vipengele vile vya mikoa wana *components* zile za afya na mara nyingi fedha zake tumezi-*peg* kutoka nje. Hata hivyo, tunajua kwa hili janga la *Corona* zile fedha *it's likely* kwamba zinaweza zikapungua kwa kiasi kikubwa kwa sababu wachangiaji wa fedha zile ambazo ziko katika mfumo wa *basket fund* ni wale *bilateral donors* ambao wengi wameathiriwa na maradhi haya ya *Covid 19*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumesikia mwongozo na mikakati ambayo Waziri wa Fedha siku ya Jumatatu aliutoa vizuri lakini tuone kwamba afya ni jambo la msingi. Kwa maana hiyo ni lazima tuweke mkakati mahsusili ili *activities* zile ambazo tumezipanga kutokana na fedha zile zinazotokana na *bilateral development partners* zinatekelezwa kwa fedha zetu. Nina maana kwamba tujiweke tayari kuhakikisha kwamba tunaweza kutekeleza zile *activities* ambazo tumezipanga hususan kwenye sehemu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu mwaka jana tulibadilisha sheria, zile asilimia 10 za mikopo ilikuwa hakuna walemavu ilikuwa ni wanawake na vijana lakini tulibadilisha ili tui-*include component* ya walemavu. Hata hivyo, wakati tunapitia bajeti za mikoa na *progress they have made* katika mwaka 2019/2020 tumeona kwamba fedha zinazokwenda kwa walemavu zimekuwa na changamoto. Changamoto kubwa ni kujitokeza kwa walemavu kuchukua mikopo na kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, tunasisitiza kwamba hili jambo tuliangalie tena ili watu wenye mahitaji maalum wakiwemo walemavu tunaweza kuwa-*accommodate* vipi, aidha, wao wenyewe wasimame au

tuweke misingi ambayo wale ambao hawako katika mahitaji maalum, wanawa-*accommodate* wale wenye mahitaji maalum kuona hii mikopo inakwenda vizuri kama vile ambavyo tumetarajia. Hili nadhani tulitafakari zaidi kuona kwamba vipi tutaweza kuwa-*accommodate* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, kuna vikundi vimejiendeleza vizuri sana. Nilikuwa nikiongea na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi *the other day*, kuna kikundi ambacho kimekuwa *model* kimetoka Mwanza katika eneo lake, wamefanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunasisitiza tena, hebu tuangalie ile *model* ambayo wao wameifanya tuweze kuona wanawake na vijana wengine wanaiga ule mfano kupata uzalishaji zaidi na hivyo kuleta tija ili mifuko yetu iwe endelevu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pendekezo kwa Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi ambao tunakwenda kugombea, hivi vikundi vinazalisha na wanatutegemea sisi sana. Kwa hiyo, zile harakati zetu wakati wa uchaguzi tuone kwamba zile tenda tunatoa kwa vile vikundi waweze kufaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *otherwise* nakushukuru sana kwa wakati wako na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma na Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika hoja hii iliyopo mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, lakini pia nawashukuru sana wapiga kura wa Urambo ambao wananipa ushirikiano wa hali ya juu. Nawashukuru, nawaomba waendeleo kuniunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Rais na Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. Hii siyo mara ya kwanza, nimeshasema mara nyingi na ninaomba nirudie hapa, katika mambo ambayo nimejifunza kwa Rais huyu, kwanza nikuthubutu. Anathubutu; pili, anaamua, anafanya maamuzi na tatu, anatekeleza. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia na Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao wote kwa pamoja kwa kweli wametusaikia katika awamu hii kuleta maendeleo makubwa sana wakisaidiana na Waheshimiwa Mawaziri na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitumie nafasi hii pia kuwashukuru sana viongozi wote waliopo TAMISEMI. TAMISEMI kazi mnaifanya, hongereni sana. Mheshimiwa Jafo unafanya kazi kubwa sana ukisaidiwa na Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Waitara, Mtendaji Mkuu, Nyamhanga; wote akina Dkt. Gwajima; Dkt. Bakari na *Engineer* Seif, wote tunawajua wanafanya kazi, hongereni sana. Mheshimiwa Jafo endelea kuchapa kazi na kundi lako lote unalofanya nalo kazi. Kazi wanaiweza; ukiiangalia *TARURA*, Afya, wote wanafanya kazi kubwa sana upande wa Afya na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi Urambo tumenufaika, tunashukuru. Tumepata Vituo vya Afya viwili, lakini naomba na hapo hapo mtuongezee tupate na cha tatu tupate kwa sababu tuna Kata 18. Kwa kweli mmefanya kazi kubwa sana. Barabara tumeziona, maji tunategemea kutoka *Lake Victoria*; mambo mengi tumeyaona lakini tunategemea kutakuwa na mengi yanayokuja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nilete maombi yafuatayo: la kwanza kabisa naomba mwaangalie wafanyakazi. Ndugu zangu wafanyakazi wana tatizo moja kubwa ambalo naiomba Serikali inayoongozwa na Chama

cha Mapinduzi, wafanyakazi kupanda madaraja sasa hivi ni kazi. Wakipanda madaraja, kuwarekebishia mishahara ni tatizo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba waangaliwe sana wafanyakazi ambao wako karibu na kustaafu. Hakuna ambacho Serikali yetu haiwezi kukifanya. Naomba Utumishi na waajiri ambao ni Wakurugenzi na mfuko ule unaohudumia walimu pamoja na wafanyakazi wa afya, ule unaoitwa *PSSSF* wakae pamoja waone jinsi gani ya ku-*coordinate* ili wafanyakazi wanapopandishwa mishahara, basi na mishahara yao irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi nina walimu 30 ambao wamestaafu, lakini mishahara yao haikurekebishwa baada ya kupanda madaraja, wamepata matatizo. Jambo hili linaweza kufanyiwa kazi kwa kuhusisha hayo maeneo matatu kama nilivyosema; Waajiri, Mfuko na Utumishi mkaweka utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kama walivyoongea wenzangu, kuna uhamisho mwingine kwa kweli ni wa lazima. Naomba suala la uhamisho kwa wafanyakazi liangaliwe. Kwa mfano, mtu mume wake amestaafu, amekwenda Tanga. Unamwambia wewe mwalimu tafuta mtu wa Tanga anayekuja Urambo, ambayo ni kazi kubwa sana. Kwa hiyo, kuna uhamisho mwingine kwa kweli kuna haja ya Serikali kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie; Utumishi na Wakurugenzi jambo gani ambalo mnaweza kufanya likawasaidia walimu wanaotaka kuhama kwa *genuine issues*? Kuna wengine ambao kwa kweli ni *genuine*, kwa mfano, anafuata familia yake na mambo ya namna hiyo au maradhi. Naomba masuala haya mawili yaangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, naomba tuangalie suala la upungufu wa wafanyakazi. Sisi kwa mfano Urambo tuna upungufu wa Walimu wa Sayansi 230, walimu wa Msingi



458 na wafanyakazi katika sekta ya afya 124. Naomba masuala haya pia yaangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia itakumbukwa kwamba Serikali yetu ilikuwa na nia nzuri, ilipeleka fedha za maboma katika Halmashauri zote. Kwa bahati mbaya sana, sijui *computer* ili-*skip* Urambo! Tunaomba Mheshimiwa Waziri ukaangalie Urambo peke yake sijui ilifanyaje yenyewe ikarukwa hatukupata fedha za maboma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo, tuna shule nzuri na kubwa sana inaitwa *Uyumbu High School*, ni ya sayansi, inachukua wanafunzi kutoka nchi nzima, lakini kwa bahati mbaya sana hali yake siyo nzuri, ina upungufu wa mabweni na madarasa. Naomba Uyumbu iangaliwe kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo nirudi kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tulicheza ngoma kwa ajili ya vyoo. Vyoo ambavyo ni vya mfano wa chumba kuwahifadhi watoto wa kike, lakini pia chumba cha kuhifadhi watoto wenye ulemavu. Kazi tuliifanya, lakini kwa ubunifu uliotokea baadaye tukaamua kwamba basi tuje na Shule ya Sekondari. Mmeona kwenye magazeti. Karibuni mkaone shule ambayo tunategemea itaitwa *Bunge Girls High School*, mkipata nafasi mkaione. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wanawake tupige makofi kazi tulifanya kubwa tukaungwa mkono na wanaume. Naomba sana siku tukipanga mkaangalie *Bunge High School* ambayo natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika na ofisi yake na Mheshimiwa Naibu Spika, ambao wanaisimamia ile shule. Sasa hivi imefikia hatua ya kuwekwa mabati. Basi tumuunge mkono Mheshimiwa Spika, tukipata nafasi tukaone kule kazi kubwa inayofanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, msifikiri tulipoteza muda, hatukupoteza muda. Kwa taarifa iliyoletwa na Mheshimiwa Jafo kwenye Kamati yetu imesema kwamba sasa hivi

TAMISEMI wamechukua zile ramani na tayari wameshajenga majengo 1,233 kwa kufuata yale maelekezo ambayo tuliwaomba wayafuate. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Jafo na uongozi mzima wa TAMISEMI, mmefikia 1,233; tunajua mnaweza kufanya zaidi ili watoto wetu wa kike na wenye ulemavu wapate hifadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama mnakumbuka *TWPG*, yaani Wabunge Wanawake kwa kusaidiana na *ofcourse* Wabunge wanaume wakiwemo akina Mheshimiwa Mwalongo na wengine, tulizungumzia sana umuhimu wa taulo za kike. Kama alivyoongea Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Rweikiza kwenye taarifa yake, amepongeza Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha unaoisha 2019/2020 tayari wameshatoa taulo za kike 33,000 na mwaka huu 2020/2021 wameweka lengo la kutoa taulo za kike 43,000 kwa kutumia fedha zao za ndani. Ni jambo la kupongeza sana TAMISEMI. Mheshimiwa Jafo umehimiza Wakuu wa Mikoa wamelihimiza hili, naomba tu uendelee kwa kweli kwa sababu watoto wa kike kwa taarifa ya *UNICEF* ya mwaka 2008 ni kwamba tunapoteza watoto wa kike asilimia 10 kwa kutokwenda shule kwa kuogopa kutokupata hifadhi wanapokuwa shuleni. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nakupongeza Mheshimiwa Jafo, mnachapa kazi, endeleeni kuchapa kazi na niseme tu, kwa kweli lipo hili jambo ambalo wenzangu wameongea sana, *TARURA* inafanya kazi kubwa. Mwaka huu ndiyo mvua imetuadhiri, nakwambia barabara huko kwetu zinahitaja makalavati. Wananchi wanaweza kujitolea kwa kusaidiana na *TARURA*, lakini wanahitaji makalavati. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli *TARURA* iangaliwe kwa jicho la huruma, iongezewe fedha. Tunajua *TANROAD* wanafanya kazi nzuri sana lakini pia na *TARURA* waongezewe fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, narudia tena kuwapongeza sana TAMISEMI kwa kazi kubwa wanayoifanya na tunaomba mwendeleo kufanya kazi kubwa sana chini ya

Jemedari wetu Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ambaye kama nilivyosema ni mtu anayetufundisha sisi tuige viongozi kuthubutu, ubunifu na kutekeleza. Naogopa kuishia kusema CCM oyee! (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata na Mheshimiwa Angelina Malembeka ajjandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nichangie bajeti hii ya Wizara hii muhimu ya TAMISEMI kwa kuanza na maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala* anasema kwenye kitabu chake kitakatifu cha *Quran*, "*antum shuadaau fil-ardhwi.*" Kwamba wenyewe nyie binadamu hapa hapa duniani mnajuana na mnafahamiana kwamba huyu anafanya nini na huyu yupo vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila anayesimama ndani ya Bunge hili anaanza kwa kupongeza. Sisi Wabunge tunafahamiana, nani anayepongeza kwa dhati na nani anayepongeza kwa ajili ya kutaka kuonekana kwamba naye anaiunga mkono Serikali, lakini kinafsi tunafahamiana sisi binadamu wenyewe humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumza kwa dhati kabisa kwamba Mheshimiwa Jafo mimi ninampongeza. Pongezi zangu hizi ni za dhati kabisa kwa sababu sinaga unafiki siku zote. Ninalozungumza, kama kuna ukweli nazungumza ukweli kwamba hapa natakiwa nizungumze ukweli, kama kwenye kukosoa ninakosoa ukweli. Mimi ni miongoni mwa watu ndani ya Bunge hili ambao tunazungumza ukweli panapotakiwa kuzungumza ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jafo tunakushukuru sana kwamba uliweza kuleta fedha pale

Mtwara shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Mtwara ikiwemo ujenzi wa baadhi ya barabara pale Manispaa ya Mtwara Mikindani ambapo Mbunge wake ndio mimi ninayezungumza, Mbunge wa Mjini Kanda ya Kusini pale. Zile fedha zimefanya kazi ile ambayo Mheshimiwa Jafo ulikusudia iweze kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba wakati tunapitisha wale Waheshimiwa Madiwani, wameenda kusaini ule mkataba, walienda kusainia Dar es Salaam na yule Mkandarasi ambaye anafanya kazi ya ujenzi wa ule mkataba. Sasa sijui kulikuwa na nini? Niliwahi kuuliza hapa ndani ya Bunge Mheshimiwa Jafo nikamweleza kwamba kwa nini wale wahusika walikwenda kusainia ule mkataba Dar es Salaam? Kwa sababu taarifa tulizokuwa nazo ni kwamba kulikuwa na ujanja ujanja kidogo ulifanyika ili baadhi ya fedha ziweze kuchotwa na kutumika kwa maslahi mengine ambayo siyo ya ule ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kwenye hizi fedha, ujenzi unaendelea vizuri, lakini unachelewa kukamilika, sasa hatujui tatizo ni nini? Tatizo ni wewe TAMISEMI au tatizo ni yule Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya Kichina? Barabara kadhaa zimejengwa, nyingi bado hazijakamilika pale Mtwara Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba msukumo wako Mheshimiwa Jafo, kwa sababu ni mtu ambaye unasikia tukikueleza, tunaomba umsukume yule Mkandarasi, barabara zile za Mtwara Mjini eneo la kupumzikia wananchi wa Mtwara pale Mashujaa, tunajenga pale *Hide Park*, eneo la kupumzika lile, paishe, pakamilike kwa wakati ili vijana wetu waweze kupumzika siku za *weekend* na sisi wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. Kwa hiyo, tunaomba huu mradi ufuatilie uweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni hili suala la ugonjwa huu ambao Mheshimiwa Jafo ameugusia, ugonjwa wa *Corona*, ni ugonjwa ambao ni hatari sana. Ugonjwa huu hasa kwenye Halmashauri hizi ambazo zipo pembezoni huko

kwa mfano Mtwara, kule Kitaya maeneo ya Masasi, Nanyumbu na wapi ambapo tumepakana na nchi ya *Mozambique* wananchi wanaingiliana sana na sijaona utaratibu wa Serikali kwamba inawapima wale watu wanaokuja kupitia zile njia za panya. Kwa sababu maeneo yale ya Kitaya, Mahurunga na Kivava watu wanapita usiku na mchana kutoka Msumbiji kuja Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri Wizara ya TAMISEMI iweke mpango maalum wa kuhakikisha kwamba mipaka ile (njia zote za panya) zinazibwa na wale watu wanaoingia wanapimwa sawa sawa. Hiki kitendo ambacho kinafanywa na Serikali kwa kumulika tu, unachukua kitu kama tunavyofika hapa Bungeni unamulikwa usoni, halafu joto lako sijui likiwa 32 wewe hauna *Corona*. Wenzetu nchi za nje ukienda Kenya hawapimi kwa kipimo hicho tu kimoja wakaweza kugundua kwamba huyu mtu anaumwa *Corona*, wanapima damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, weka fedha za dharura kwa ajili ya kushughulikia watu wote wanaoingia Tanzania na Watanzania kila Halmashauri waweze kupimwa damu tuweze kugundua ugonjwa huu wa *Corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo cha kumulika joto tu kwamba joto limepanda au halijapanda, mtu mwingine anaweza akapanda joto lake kwa sababu ya mazoezi, ametembea sana kwenye jua, joto lake likapanda. Ili tuweze kugundua kweli kuna wagonjwa wa *Corona* Tanzania, tufuate nchi za wenzetu; majirani zetu hapa Kenya na Uganda wanatumia vipimo maalum, kila mwananchi anapimwa kipimo cha damu ili aweze kugundulika kama ana *Corona* au hana vimelea hivi vya *Corona*. Tunaiomba Serikali ichuke suala hili *seriously*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna suala hili la Hospitali za Wilaya. Niliwahi kusema mwaka 2019 kwamba maeneo mengi wenzetu wamepewa Hospitali za

Wilaya, Manispaa ya Mtwara Mikindani sina Hospitali ya Wilaya na niliongea na Mheshimiwa Jafo tukakubaliana kwamba atatenga fedha kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Mtwara Mikindani, lakini mpaka leo zile fedha hazijaletwa na tulishatenga eneo pale Kata ya Ufukoni ambapo kuna wakazi wengi sana, nikazungumza na Mheshimiwa Waziri Kata ya Ufukoni ina wakazi wengi sana, hatuna Kituo cha Afya lakini pia Manispaa nzima haina Hospitali ya Wilaya. Tunaomba itengwe fedha tujengewe Hospitali za Wilaya, pale Mtwara Mikindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, hii ni bajeti yangu ya mwisho kuzungumzia suala la TAMISEMI mwaka huu 2020. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa uliniahidi kwamba Mtwara Mjini utaleta fedha tujenge Hospitali ya Wilaya, naomba basi mwaka huu utuletee zile fedha, wananchi wa Mtwara nilishawaeleza kwamba tayari Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameahidi na ameiandika kwenye *diary* yake kwamba miongoni mwa maeneo ambayo Hospitali za Kanda zitapelekewa fedha kujengwa ikiwemo ni Manispaa ya Mtwara Mikindani, mwaka huu tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tulipata zile fedha kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Afya cha Likombe. Tulipata shilingi milioni 500 pale Mtwara. Sasa kituo kile kinatumika sasa kama Hospitali ya Wilaya kwa sababu hatuna Hospitali ya Wilaya. Wananchi wa maeneo mengi hata maeneo ya vijijini kule Mtwara Vijijini, Jimbo la Nanyamba na wengine wanatoka *Mozambique* wanakuja kujitibu kwenye Hospitali ile ya Likombe, lakini ile hospitali haina *capacity* kubwa ya kuweza kupokea wagonjwa wengi kwa kiasi hicho ambacho wanafika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado tunaomba kile kituo kama mpango wa Hospitali ya Wilaya bado unachelewa, basi kipewe vitendea kazi maalum; kiwekewe *X-Ray*, kiongezewe watabibu na kipelekewe madaktari bingwa kwa sababu kile kituo kinafanya kazi kama Hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Jafo kwa kuwa ni msikivu sana

tunaamini na wananchi wa Mtwara wanaamini kwamba haya yote ambayo wamenituma kuja kukueleza utayafanyia kazi mwaka huu 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala hili la fedha, Kamati ya TAMISEMI imezungumza na imeshauri Serikali kwamba fedha ambazo zinatengwa na Halmashauri ambazo sisi wabunge tulipitisha hapa kwenye Bunge hili ikawa ni sheria sasa kwamba ile asilimia 10 ni lazima iende kwa wahusika; walemavu na vijana waweze kupata ile fedha, lakini Kamati imeeleza hapa kwamba zipo baadhi ya Halmashauri hazipeleki zile fedha. Nyingine zinapeleka 3% tu. Imetajwa hapa Halmashauri ya Simiyu na Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huku ni kulidharau Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo ndiyo tulipitisha hii sheria kwamba ile asilimia 10 itengwe na kila Halmashauri itenge kwa mapato ya ndani kwa ajili ya kuhudumia hawa watu wenye ulemavu na vijana. Tunaomba sana Halmashauri ambazo hazitengi hizi fedha, Serikali, Mheshimiwa Jafo aje atueleze anazichukulia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukua hatua gani kwa Halmashauri ambazo hazitengi fedha hizi asilimia 10 kwa ajili ya kuwagharamia, kuwapa hawa vijana na watu wenye ulemavu kwa sababu ni sheria ambayo tulipitisha sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Kutokuitekeleza hii sheria maana yake ni kulidharau Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mtaani kuna walimu wengi sana ambao wame-*graduate* takribani miaka mitatu, minne hivi sasa na hawana ajira. Ukipitia shule za sekondari na msingi ambazo Serikali inajinasibu kwamba tumeweka elimu bure, wanafunzi wamekuwa ni wengi, ikama ya walimu imekuwa ni ndogo. Yaani ukilinganisha walimu na masomo, walimu ni wachache masomo yaliyoko na pia wanafunzi ni wengi kuliko walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba ile *ratio* sasa ya walimu kwa masomo iweze kuzingatiwa. Hili haliwezi kupatikana kama Serikali inawaacha walimu mtaani wanahangaika, hawana ajira. Shule hazina walimu, lakini walimu wanahangaika, wanatembea mitaani, Serikali haitaki kuwaajiri. Tunaomba kasi ya kuajiri ambayo Serikali imekuwa inadonoadonoa iweke utaratibu maalum wa kuwaajiri hawa walimu ambao wapo mitaani, shule zetu ziondokane na upungufu wa walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wapo wengi sana Mheshimiwa Jafo unawajua huko mitaani. Ukitembelea shule hata hapa Dodoma, nenda kaangalie ikama ya walimu kwa masomo, bado walimu hawatoshi wakati Serikali imesomesha walimu wengi wapo mitaani. Shule za *private* huko, nazo zimejaa. Kwa hiyo, hawa walimu tumewafundisha kwa kazi gani? Wamesoma kwa gharama kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri kwenye ule mkopo wa Serikali hawa walimu wote wanasomeshwa na wanakopeshwa, wengine wanapewa *grant*, walimu wa sayansi wanasomeshwa bure na Serikali. Leo tunawasomesha, tunaenda kuwaacha mtaani. naomba Wizara ya TAMISEMI, kwa sababu tuna uhitaji wa walimu, shule zetu za msingi na sekondari hazina walimu, tuongeze walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, nizungumze kidogo suala hili la *TARURA*. Wenzangu wamezungumza kwamba *TARURA* ina maeneo mengi ya kufanyia kazi ikiwezekana kuliko hata *TANROADS* kwa sababu miji yote, vijijini huko na mijini wamepewa usimamizi wa *TARURA*. Fedha wanazopewa ni asilimia 30, *TANROADS* wanapewa asilimia 70. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunaomba *atleast* iweze kuongezwa hii fedha asilimia 30 ifike asilimia 50 angalau iwe nusu kwa nusu kati ya *TANROADS* na watu wa *TARURA* ili hawa watu wa *TARURA* waweze kujenga barabara zetu. Barabara zetu ni mbovu na mafuriko ndiyo hivyo kama



unavyoona tena na ofisi ambayo inashughulikia suala la maafa mwaka 2019 haijapewa hata senti tano. Ofisi ya Mheshimiwa Jenista hapa haijapewa hata senti tano kwenye suala la maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba, ili kuokoa barabara zetu, maafa haya ambayo yanatokea mijini na vijijini, *TARURA* ipewe fedha itasaidiana na Wizara ya Mheshimiwa Jenista ili kujenga barabara ambazo zimebomoka huko mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maftah Waheshimiwa nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata atafatiwa na Mheshimiwa Angelina Malembeka tutamalizia na Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya TAMISEMI Ofisi ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na afya tumeweza kuendelea kushiriki kujadili hoja zetu muhimu katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Jemedari wetu tingatinga, burudoza namba moja yetu si mwingine tena bali ni namba moja yetu Dkt John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri Mkuu niwapongeze Mawaziri wote, niwapongeze Naibu Mawaziri wote, niwapongeze Makatibu Wakuu wote, niipongeze Serikali yote kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri walizofanya ndani ya kipindi cha miaka minne kazi zenye weledi kazi zinazoonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzisoma kazi zilizofanywa na Serikali yetu sikivu Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndani ya miaka minne imeweza kuleta elimu bure bila malipo kuanzia shule ya msingi na sekondari watoto wanasoma bure na ndiyo maana watoto wengi wameweza kujitokeza kwenda shule kwa sababu kabla ya hapo watoto walikuwa wanabaki nyumbani wazazi walikuwa wanashindwa kulipa hiyo elfu 10, elfu 40, elfu 50. Lakini baada ya kuleta elimu bila ada watoto wamekuwa ni wengi wamejitokeza kwa wingi, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya miaka minne na ushee imeweza kuboresha upatikanaji wa madawa mahospitalini, ndani ya kipindi cha miaka minne imeweza kukarabati na kujenga vituo vya afya takriban 433 si kazi ndogo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa sana kwa watazania imeweza kuleta mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu imeweza kununua ndege takriban nane na zingine zinaendelea kuja tuseme nini mbele ya macho ya Mungu? Mungu atupe nini atupe kidonda bado watu wanasema hawaoni kilichofanyika bado watu wanasema hiyo elimu bure haina maana kwa kweli Mwenyezi Mungu anawaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kazi kubwa lakini nikupongeze wewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa ya kuliendesha Bunge hili kwa utulivu mpaka tunaenda kumaliza kipindi chetu cha miaka mitano nakupongezeni sana wewe pamoja na Spika wetu wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi ninaenda sasa kwenye hoja zangu za msingi nianze na *TARURA*. *TARURA* imefanya kazi nzuri sana *TARURA* imefanya kazi nzuri sana lakini kutokana na changamoto ya mvua

nyingi za mwaka huu barabara nyingi zimeweza kuharibika na madaraja mengi yameweza kuharibika kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuongeza zile 30% iweze kuwa 50 na TANROADS pia iweze kupewa fungu la kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado barabara nataka niiongelee barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga. Barabara ile ina mabonde ni barabara nzuri sana lakini ina *bumps* nyingi sana kiasi kwamba wanaume wanaoendesha magari kwenye barabara ile na wanawake viuno vyao sasa hivi wanaumwa. Barabara ile imezidi sana zile *bumps* ni kilo mita zaidi 280, 300 lakini ma-*bumps* yamekuwa mengi matuta ni makubwa yamekuwa karibu karibu kiasi kwamba mabasi yanayokwenda kule yanaharibika yanayobeba abiria yanaharibika hata magari madogo madogo na yenyewe kila wakati yanaharibika kutokana na matuta makubwa yaliyokithiri kwenye ile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuja Mheshimiwa Rais kwenye Mkoa wa Rukwa alitamka mbele ya mkutano wa hadhara kwamba matuta yatapunguzwa sasa ninaomba atakapokuja kuhitimisha atuambie ni lini matuta hayo yatapunguzwa hata kama siyo kuyamaliza yote basi yapunguzwe yanaharibu sana magari lakini binadamu pia wanarushwa sana wanaposafiri kwenye ile barabara wanaumwa ninavyosema hivyo ukiwapima wanaume wanaosafiri safiri kwenda kule viuno vyao haviko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee tena suala la ukubwa wa Jimbo ukumbwa wa Majimbo. Mkoa wa Rukwa umebarikiwa sana kuwa na Majimbo makubwa Jimbo la Kwela maarufu kama Sumbawanga DC ni kubwa sana tunamshukuru Mheshimiwa Rais alipokuja alirudisha halmashauri ikapelekwa kwenye mji mdogo wa Laela tunamshukuru. Lakini bado kuna changamoto kubwa lile Jimbo limegawanyika katika sehemu mbili Ufipa wa Juu na Ufipa wa Chini, lile Jimbo lina kata 28 sasa Ufipa wa chini huku sasa hivi madaraja yamebomoka na Mwenyezi Mungu

aliligawa *automatically* lile Jimbo aliligawa katika sehemu mbili upande wa chini, ziwani kuna kata 14 na upande wa juu kuna kata 13 kwa hiyo, wananchi wanapata tabu sana kufuata huduma wanapata shida kufuata huduma huku juu ambako halmashauri imepelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba na kule wapelekewe mamlaka ili waweze kujitegemea kwasababu kipindi hiki wakati wa mvua hakuna mawasiliano kabisa madaraja yamebomoka hakuna kabisa watu wanapata tabu kwenda kufuata huduma ufipa wa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana suala hili ni kilio kikubwa sana cha wananchi wa Jimbo la Kwela, wanaomba mamlaka igawanywe aidha Jimbo ligawanyike katika sehemu mbili na wenyewe huku chini wapate mamlaka na huku juu iendelee mamlaka kama Mheshimiwa Rais alivyotupelekea halmashauri yetu pale mji mdogo wa Laela.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Angelina Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema alotuwezesha Wabunge sisi wote mpaka leo hii kuwepo hapa kujadili haya ambayo tunayazungumza.

Nitoe pongezi kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya yeye na timu yake yote Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa ujumla. Lakini

kipekee nimpongeze Mheshimiwa Jafo kama yeye hongera sana Mheshimiwa Jafo umefanyakazi nzuri kwenye Wizara yako wewe na wasaidizi wako lakini kazi hii hujaifanya tu vizuri kwenye nchi, lakini pia umeifanya vizuri katika Jimbo lako Mwenyezi Mungu atakusaidia utarudi tena *In Shaa Allah*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pia pongezi zangu kwa Makamu wa Rais mama Samia Suluhu, kwa Waziri Mkuu, kwa Rais wa Zanzibar, Makamu wa pili wa Rais Zanzibar kwa jinsi wanavyoweza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuweza kutufanya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tusimame tukijidai kwamba kazi imetekelezeka. Kipekee pia niwashukuru na niwapongeze Wabunge wote ambao Awamu zote Nne walikuwa wanasema ndiyo ili kazi ifanyike na ninaomba mwaka huu tusisite tena tupige ndiyo ili kazi iliyobaki ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kuhusiana na suala zima la uwezeshaji kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri hadi sasa hivi bilioni 93.3 zimekopeshwa bila riba kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Vikundi 915 vya watu wenye ulamavu vikundi 4266 vya vijana na vikundi 8207 vimepata mikopo hiyo hapo ninachoomba wale waliokopeshwa warudishe lakini hapo hapo halmashauri ziendelee kutoa mikopo hii kwa wananchi kwa sababu hii ni ahadi iliyotolewa na Chama cha Mapinduzi ni lazima itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia ujenzi wa majengo ya utawala majengo ya utawala yamejengwa 86 kati ya hayo 29 yamekamilika na 57 yako katika hatua za mwisho za kukamilika ili Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa wakae katika maeneo mazuri. Niipongeze sana Serikali yangu kwa kujali watumishi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameeleze katika sekta ya elimu madarasa 19,808 yamekamilika, napenda niongezee kwamba madarasa 1313 yanaendelea yako katika ujenzi yatakamilika wakati wowote. Lakini kuna

maabara 227 zimejengwa nipende tu kuongezea kwamba katika maabara hizo vifaa vya maabara vimeshatolewa katika sekondari 1258 ni jambo zuri sana ambalo Serikali imelifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la matundu ya vyoo ambalo 7922 yamekamilika na mengine 571 yako katika ujenzi na yako katika hatua za mwisho ambazo wanategemea kukamilisha muda si mrefu. Shule kongwe zimetajwa 73 zimekarabatiwa vizuri lakini nilizungumzia masuala ya mabweni mabweni yamekarabatiwa kiasi kwamba yanaonekana ni mapya ile ni kazi nzuri sana ambayo imeonyesha jinsi gani TAMISEMI imeweza kuokoa kwa sababu bila kukarabati yale majengo yangeharibika kabisa na tungepata hasara mpya ya kujenga majengo mapya. (*Makofi*)

Suala la hospitali zimeelezwa hapo hospitali 98 kuna vituo vya afya kadhaa kuna zahanati kadhaa mchango wangu hapa nilitaka niongeze kwamba Chama Cha Mapinduzi kupitia utekelezaji wa Ilani imeweza kuwezesha upatikanaji wa dawa na vifaa vya tiba kwa 92% hayo ni maendeleo makubwa sana. Lakini kwa kuwa kuna watu ambao roho zao hazina sifa za kusifia hatuwezi kuwalaumu lakini mwenye macho anaona mwenye masikio anasikia na wengine ndiyo huko huko wanaenda kujifungua wanaona zile hospitali wengine ndiyo huko huko watoto wao wanasoma lakini wanashindwa kusifia sisi tumuombe Mwenyezi Mungu tu amuwezeshe Rais wetu na Mawaziri wake wafanye kazi vizuri Mwenyezi Mungu uko pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *corona* suala la *corona* limekuja ghafla na kwa kazi kwenye suala hili nimpongeze Waziri wa Afya na timu yake pamoja na Waziri Mkuu lakini pia kipekee niwapongeze watumishi wote wa sekta ya afya popote nchini. Kwa sababu kila mtu anaogopa kufa lakini wale wenzetu inabidi watoke waende kule kuhudumia watu ninawapongeza sana sana sana na ninaomba tufate maelekezo ya wauguzi, madaktari na viongozi wetu. Kwa mfano hapa Ofisi ya Bunge tumejitahidi

sana kujilinda kwa namna yoyote lakini je hivi tunavyojilinda tukitoka nje ya Bunge na sisi tunaendelea kujilinda? Kule Chako ni chako tunaacha kwenda? Huku na huku tunaacha kwenda? Naomba hilo tuliangalie kwasababu vinginevyo tutakuwa tunatunzwa vizuri hapa Bungeni halafu tukitoka nje tunabeba ya kule nje tunaleta humu Bungeni inakuwa sawa sawa na bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine pia huko kwa wananchi wetu tusaidiane pia kuendelea kutoa elimu isije ikaonekana sisi huku tunatunzwa halafu wananchi wetu wanapata tatu. Kwa hiyo, Wabunge tukitoka hapa tukirudi na sisi tuwajibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tusaidiane na Serikali kwa sababu hili suala lilikuwa haliko kwenye bajeti Mbunge ambaye anaweza kujitolea kwa ajili ya kusaidia visafisha mikono na vitu vingine aendelee kutoa ili muda ukipita basi tujue na Wabunge nao tuliwajibika isije ikawa hapa 90% tunawasema tu Mawaziri, sijui nani hawajafanya nini, je sisi kama Wabunge tumefanya nini? Hilo nalo tujipime na sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa uchaguzi dakika za mwisho tusitafutiane fitna na maneno yapo maneno ya kuudhi ambayo yanatugusa sisi wengine hatupendi kuyasema tuombeane dua. Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ina wajumbe kutoka Zanzibar sita na wanazunguka nchi nzima kufanya kazi sasa mtu anaposema huku siyo Zanzibar hatuendi hivyo tufanye kazi na tuheshimiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NABU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutamalizia na Mheshimiwa Sikudhani Yasin Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kusimama katika Bunge lako hili ninaamini

hii ni bajeti ya tano na kwa lugha nyingine ni bajeti ya mwisho kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu wenzangu wengi wamempongeza Mheshimiwa Rais na wamesema sababu mbalimbali. Lakini naamini kwamba ili awe Rais lazima kuna michakato ilianza mchakato wa kwanza Rais alitokana na Chama cha Mapinduzi. Mwaka 2015 Mheshimiwa Rais alikabidhiwa Ilani kutoka kwenye Chama chake cha Mapinduzi, Ilani ambayo ilikuwa imeainisha mambo mbalimbali ambayo yatatekelezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano. Naomba niseme kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu nampongeza kwa dhiti Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya yote Mheshimiwa Rais ni binadamu kama binadamu wengine anapofanya vizuri ni lazima tumpongeze na kumpongeza ni kumtia moyo ili aendelee kufanya vizuri naomba niungane na wote ambao wanampongeza tulioko ndani ya Bunge lakini na wale walioko nje ya Bunge kwa sababu sote tunaona kazi nzuri ambayo inafanyika na Mheshimiwa Rais hakika tunampongeza na tunaendelea kumuomba kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwatumikia wananchi katika taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nikupongeze wewe ambaye leo umekalia kiti lakini ninaamini kabla ya wewe yupo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii taasisi ambayo umeisimamia ni taasisi kubwa sana mmetusimamia watu wengi wenye tabia tofauti tumekuwa tukiona katika taasisi zingine mbalimbali watu hawamalizi wakiwa wamoja lakini naendelea kuamini kwamba tunamaliza Bunge tukiwa wamoja hongereni sana na *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu aendelee kuwaweka ili mushike nafasi hizo katika kipindi kijacho. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme mambo machache kupitia Wizara hii ya TAMISEMI nafahamu kwamba



tunajadili mapato na matumizi katika Wizara hii ya TAMISEMI lakini kabla sijasema yale ambayo nayakusudiwa pia naomba nimpongeze kaka yangu Jafo. Watu wamemsema kwa sifa mbalimbali. Naomba niseme sifa moja miongoni mwa sifa alizokuwa nazo Mheshimiwa Jafo ni msikivu hana unyanyapaa kwa Wabunge wenzake ukitoka ukienda kumpelekea hoja yako anakusikiliza na amekuwa akitusaidia katika kutekeleza mambo mbalimbali katika Majimbo yetu nakuombea kaka yangu endelea kufanya vizuri na In Shaa Allah wananchi katika Jimbo lako watakuona utarudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mikopo ya 10% nafahamu kwamba tunazungumza mikopo ya 10% ni pesa ambazo zinatokana na mapato ya ndani katika halmashauri zetu. Hizi 10% tumezitenga katika maeneo matatu 4% vijana, 4% wakinamama na 2% ya walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba niseme katika eneo la walemavu mikopo hii inatolewa kwa kuunda vikundi mbalimbali sasa nilikuwa naomba nishauri kupitia Wizara hii kwamba katika uundaji na utoaji wa mikopo hii ya 2% kwa upande wa walemavu, ziko changamoto zingine ambazo zinajitokeza katika utekelezaji inawezekana kabisa walemavu wapo katika maeneo mbalimbali unaweza ukakuta kijiji kimoja kina mlemavu lakini kijiji X hakina mlemavu ndani ya kata lakini sifa mojawapo ya hawa walemavu kupata mikopo ni kujiunga katika vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba jambo hili liangaliwe kwasababu tumeweka jambo hili mahususi kwa upande wa walemavu ikiwezekana wakopeshwe hata mlemavu mmoja mmoja siyo lazima wakopeshwe kupitia vikundi. Nafahamu kwamba wanapounda kikundi mara nyingi kinatakiwa kikundi cha watu wanaoaminiana sasa huwezi kutoka kwenye kijiji X ukaenda kumpata kwenye kijiji B mlemavu mwingine ili muungane watu ambao hamfahamiani inakuwa haipendezi na kwa namna nyingine inaweka ugumu katika kuwasaidia hawa walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana sana tuwaangalie sana katika kuwasaidia hawa walemavu kulingana na ile dhamira ya Serikali tupunguze masharti kwa upande wa walemavu. Ikionekana kwamba kuna mlemavu ambaye yuko kwenye kijiji X amekidhi vigezo vya kukopeshwa bila kujali yuko katika kikundi basi ni vizuri Serikali ikamuangalia na nafahamu hili Mheshimiwa Jafo analiweza kwasababu liko ndani ya utekelezaji wake tuendeleo kuzishauri halmashauri zetu ili na wale walemavu waweze kupata hii mikopo bila kuwa na masharti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwa sababu mwisho wa siku wakipata mikopo wanatakiwa warudishe sasa kama hawatakuwa watu wanaoaminiana inakuwa ngumu katika kuwafuatilia. Naomba nilisisitize hilo kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu tuwasaidie walemavu kwa kupunguza masharti kama nilivyosema Mheshimiwa kaka Jafo unaliweza liko ndani ya uwezo wako. *(Makofi)*

Jambo lingine naomba nipongeze Serikali kwa suala la ukarabati wa vituo vya afya. Vimeelezwa hapa vituo vya afya 433 ninaamini ni miongoni mwa vituo ambavyo vipo katika mkoa wangu wa Ruvuma, tumekarabati baadhi ya vituo vya afya na nafahamu kwamba lengo la kukarabati vituo vya afya ni kuweka huduma karibu kwa wananchi na sote tunafahamu tulikotoka ilikuwa siyo rahisi kuona kwamba kituo cha afya kinaweza kutoa hata huduma ya upasuaji kwa mama mjamzito. Lakini kwa vituo hivi vya afya ambavyo kwa sasa vinakarabatiwa vina lengo la kuokoa maisha ya akinamama wajawazito na watoto. Nasema hongera sana kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine pia naomba nizungumzie kwenye suala la ukamilishaji baadhi ya zahanati kaka Jafo umesema kwenye taarifa yako kwamba ni milioni 150 katika kila halmashauri nafahamu ziko halmashauri mpaka ziko zahanati mpaka leo hatujafanya vizuri na kuna maboma, kwa hiyo, ni vizuri tukaziangalia zile zahanati ambazo tayari tulishaanza kuzikarabati lakini zimesimama kwa ukosefu wa pesa, kwa hiyo, pesa hizi zielekeze kwenye

kukarabati katika zile zahanati ambazo tayari Serikali ilishapeleka pesa lakini zimesimama kwa ajili ya kukosa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimeona mambo mbalimbali ambayo yanaendelea katika mkoa wangu ikiwemo ujenzi wa hospitali katika Jimbo la Madaba ambapo bilioni 1 imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali. Naona umewasha taa naomba nimalizie suala dogo tu kwa ridhaa yako na unafhamu kwamba katika uchangiaji huu mimi ni mtoto wa mwisho. Kwa hiyo, naomba na mtoto wa mwisho anahitaji kuvumiliwa naomba univumilie kama dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala moja suala la milioni 140 kukamilisha maboma katika shule za msingi nasema niliseme hili kwa sababu nafahamu yako maboma mengi yamejengwa kwa nguvu za wananchi, wananchi walifyatua tofali wananchi walisomba mchanga wananchi walikusanya mawe lakini maboma yale hayajakamilika naishukuru sana Serikali niombe pesa hizi ziende zikafanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunivumilia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ambayo naamini Mheshimiwa Jafo na watendaji kazi wake wataifanyia kazi.

Lakini nilete kwenu tangazo moja kutoka kwa Mheshimiwa Spika kwa mamlaka aliyonayo chini ya Kanuni ya 5(1) ameagiza siku ya kesho Bunge litakuwa kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa saba mchana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge baada ya tangazo hilo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa tatu kamili asubuhi kesho. *(Makofi)*

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Aprili, 2020 Saa Tatu Kamili Asubuhi)*